

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA TISA**

**Kikao cha Tisa – Tarehe 15 Aprili, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Nane Mchana)*

**D U A**

*Spika (Mhe. Job Y. Ndugai) Alisoma Dua*

**SPIKA:** Mheshimiwa Wabunge, tukae, Katibu!

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI:-**

Hati zifuatazo ziliwasilishwa mezani:-

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI UTUMISHI  
NA UTAWALA BORA:**

Hotuba ya Bajeti ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA - MAKAMU MWENYEKITI  
WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI  
ZA MITAA:**

Maoni ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa kuhusu Utekelezaji wa Majukumu ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2019/2020 pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MHE. RUTH H. MOLLEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI BUNGENI KWA OFISI YA RAIS UTUMISHI NA UTAWALA BORA:**

Maoni ya Kambi Rasmi ya Bungeni kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**MASWALI NA MAJIBU**

*(Maswali yafuatayo yameulizwa na kujibiwa kwa njia ya mtandao)*

Na. 74

**Idadi ya Watu Wenye Ulemavu wa Ngozi Nchini**

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO** aliuliza:-

Je, kuna watu wangapi wenye ulemavu wa ngozi nchini na ni Wilaya gani inaongoza kwa kuwa na idadi kubwa zaidi?

**WAZIRI MKUU** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa taarifa ya Sensa ya Watu na Makazi iliyofanyika nchini mwaka 2012, idadi ya watu wenye ulemavu wa ngozi nchini ni 16,127 ambapo wanaume ni 8,872 na wanawake ni 7,255.

Aidha, kwa mujibu wa taarifa hiyo, mikoa yenye idadi kubwa ya watu wenye ulemavu wa ngozi ni Dar es Salaam yenye watu 1,637; Mwanza 1,063; na Dodoma 1,034. Hata hivyo, taarifa inayoonesha mchanganuo wa watu wenye ulemavu wakiwemo wenye ulemavu wa ngozi kiwilaya haikuandaliwa.

Na. 75

### **Hitaji la Vifaa Tiba Kituo cha Afya Igoma**

**MHE. KEMILEMBE J. LWOTA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, Serikali imefanya jitihada kubwa katika ujenzi na uboreshaji wa Sekta ya Afya kwa kujenga Vituo vya Afya kikiwemo Kituo cha Afya Igoma:-

Je, ni lini Serikali itapeleka vifaa tiba kama vile *X-ray*, *Ultrasound* na vifaa vingine vya kiuchunguzi kama ilivyoahidi?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kemileembe Julius Lwota, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Kituo cha Afya Igoma kilipatiwa kiasi cha shilingi milioni 400 kwa ajili ya ukarabati na upanuzi na kazi hiyo imekamilika. Serikali inaendelea kuvipatia vifaa tiba Vituo vya Afya vilivyokamilika ambapo hadi sasa jumla ya shilingi bilioni 27.11 zimetumika. Kituo cha Afya Igoma kitapewa kipaumbele cha kupatiwa vifaa katika awamu zinazofuata ili kukiwezesha kutoa huduma.

Na. 76

### **Kupandisha Hadhi Barabara ya Getifonga, Mabogini, Chekereni na Kahe**

**MHE. ANTONY C. KOMU** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, barabara ya kutoka Gatefonga, Mabogini, Chekereni, Kahe mpaka Wilaya ya Mwanga ni muhimu kwa uchumi wa Mkoa wa Kilimanjaro lakini haipitiki kipindi cha mvua.

Je, ni kwa nini Serikali haikubaliani na mapendekezo ya *RCC* Kilimanjaro ya kuipandisha hadhi barabara hii kwa kuwa chini ya *TANROADS*?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Antony Calist Komu, Mbunge wa Moshi Vijijini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia Sheria ya Barabara Na.13 ya mwaka 2007 Kifungu cha 12(2)- (3), barabara ya Gatefonga, Mabogini, Chekereni na Kahe haina sifa ya kusimamiwa na *TANROADS*. Hivyo, barabara hiyo itaendelea kufanyiwa matengenezo kupitia Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini (*TARURA*) ili kuhakikisha inapitika wakati wote.

Na. 77

**Ujenzi wa Barabara ya Itoni - Lusitu**

**MHE. EDWARD F. MWALONGO** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itatekeleza ahadi yake ya kujenga kwa kiwango cha lami barabara ya Itoni – Lusitu?

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Edward Franz Mwalongo, Mbunge wa Njombe Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Upembuzi yakinifu, usanifu wa kina na uandaaji wa nyaraka za zabuni za Barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (kilomita 211.42) umekamilika tangu mwaka 2016 kwa barabara yote.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua umuhimu wa barabara hii, na kwa vile barabara ya Itoni – Ludewa – Manda (kilomita 211.42) ni ndefu, Serikali iliamua kuijenga kwa awamu. Awamu ya kwanza ni sehemu ya Lusitu – Mawengi (kilomita 50) ambayo ni sehemu korofi. Sehemu hii inajengwa kwa kiwango cha zege la saruji na ujenzi umefikia asilimia 42. Mradi huu wa kilomita 50 za kwanza umepangwa kukamilika tarehe 30 Oktoba, 2020.

Mheshimiwa Spika, awamu inayofuata ni ujenzi wa sehemu ya Itoni – Lusitu (kilomita 50) kwa kiwango cha lami. Katika mwaka wa fedha 2020/2021, mradi huu umeombewa shilingi bilioni sita kwa ajili ya kuanza ujenzi.

Na. 78

### **Hitaji la Mahakama ya Wilaya – Mkalama**

**MHE. ALLAN J. KIULA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, wananchi wa Jimbo la Iramba Mashariki wanasafiri umbali mrefu na pia kutumia gharama kubwa kufuata huduma ya Mahakama ya Wilaya iliyopo Kiomboi na baadhi yao hukata tamaa na hivyo hupoteza haki zao:-

Je, ni lini Mahakama ya Wilaya itajengwa Mkalama kama ilivyoahidiwa Bungeni mwaka 2019?

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Allan Joseph Kiula, Mbunge wa Iramba Mashariki kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, uhaba wa majengo ni moja ya changamoto inayoikabili Mahakama ya Tanzania. Mahitaji ya majengo ya kuendeshea shughuli za Mahakama hapa nchini ni makubwa. Kwa msingi huo, Mahakama imejiwekea

utaratibu wa kujenga majengo haya kwa awamu kulingana na mpango wa ujenzi na upatikanaji wa fedha.

Mheshimiwa Spika, ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya Mkalama ni miongoni mwa Majengo ya Mahakama za Wilaya 33 ambayo yatajumuisha Mahakama za Mwanzo katika jengo moja. Ujenzi wa majengo haya umepangwa kuanza mwezi Juni na kukamilika mwezi Disemba, 2020 kwa ufadhili wa Benki ya Dunia. Kwa sasa Mahakama ipo katika hatua za mwisho kukamilisha taratibu za awali ili ujenzi wa majengo hayo uanze kwa muda kama ilivyo katika mpango wa Mahakama.

Mheshimiwa Spika, tayari Mshauri Elekezi amefanya mapitio ya michoro na ujenzi unatarajiwa kuanza kama ilivyopangwa. Hivyo, naendelea kumwomba Mheshimiwa Mbunge kuwa na subira ili jengo hili likamilike ambalo litatatua changamoto alizozitaja kwenye swali lake la msingi.

Na. 79

### **Tatizo la Ugonjwa wa Figo**

**MHE. MGENI J. KADIKA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa figo unakua kwa kasi kubwa sana katika nchi yetu ya Tanzania:-

Je, ni mkoa gani katika Mikoa yote Tanzania Bara na Visiwani unaongoza kwa kuwa na wagonjwa wengi wa figo?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mgeni Jadi Kadika, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ugonjwa wa figo husababishwa kwa kiasi kikubwa na magonjwa yasiyoambukiza. Kulingana

na Utafiti ulioitwa *Community Base Survey to assess prevalence of kidney diseases* wa mwaka 2013 uliofanyika katika maeneo ya Kaskazini Mashariki ambayo ilihusisha Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Morogoro pamoja na Utafiti uliofanyika mwaka 2015 ulihusisha Mkoa wa Pwani na Dar es Salaam ulionesha asilimia 44 unasababishwa na ugonjwa wa kisukari na shinikizo la damu linachangia asilimia 34.

Mheshimiwa Spika, utafiti huo uliofanyika katika Mikoa ya Kilimanjaro, Arusha, Tanga na Morogoro mwaka 2013 ulionyesha tatizo kuwa kubwa asilimia saba na takwimu za utafiti kwenye jamii uliofanyika Kisarawe na Dar es Salaam mwaka 2015 ulionesha tatizo kuwa kubwa kwa asilimia 12.4.

Mheshimiwa Spika, magonjwa yasioambukiza husababishwa na mtindo usio bora wa maisha ikiwa ni pamoja na matumizi ya pombe kupita kiasi, matumizi ya tumbaku na bidhaa zake, matumizi ya chumvi ya mezani, kutokufanya mazoezi na kwa ujumla na lishe mbaya, mfano matumizi ya mafuta kupita kiasi. Viashiria vyote hivi huchangia kupata magonjwa ya shinikizo la damu na kisukari ambayo ndio husababisha zaidi ugonjwa wa figo.

Mheshimiwa Spika, mtindo usiofaa wa maisha upo mjini na vijijini pamoja na mikoa yote ya Tanzania Bara na Visiwani. Tatizo hilo ni kubwa kwa Mkoa wa Dar es Salaam ambako takwimu za kitabibu zinaonyesha kuwa na wagonjwa 1,234 na mkoa wa pili kuwa na tatizo la wagonjwa wa figo wengi ni Mkoa wa Arusha wenye idadi ya wagonjwa 563 na Mkoa ambao una takwimu chache za wagonjwa wa Figo ni Simiyu wagonjwa 113.

Mheshimiwa Spika, nitoe wito kwa wananchi kuendelea kufanya mazoezi kuepukana na magonjwa yasiyoambukiza.

Na. 80

## **Chanjo ya Saratani ya Shingo ya Kizazi**

**MHE. MWATUM DAU HAJI** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni Serikali ilianzisha mpango wa chanjo ya Saratani ya Shingo ya Kizazi kwa wasichana kuanzia umri wa miaka kumi na mbili:-

Je, mafanikio gani yamepatikana kwenye mpango huo?

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mwatum Dau Haji, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara ilianzisha chanjo ya *HPV* dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi mwezi Aprili, 2018 kwa wasichana wa miaka tisa hadi 14. Katika kipindi hicho, chanjo hii ililenga kuhakikisha kuwa wasichana 643,383 wenye umri wa miaka 14, ambao wote ni walengwa wa huduma hii, wanapata chanjo kwa wakati. Aidha, kwa kipindi cha mwaka 2019, walengwa wa chanjo hii walikuwa wasichana wapatao 685,580.

Mheshimiwa Spika, mwaka 2018 chanjo hii ilianzishwa na jumla ya wasichana 383,683 walifikiwa kwa dozi ya kwanza ya chanjo hii, sawa na asilimia 60 ya lengo la wasichana 643,383. Aidha, jumla ya wasichana 128,021 walifikiwa kwa dozi ya pili ya chanjo hii katika kipindi tajwa, sawa na asilimia 33 ya lengo la wasichana 383,683 walifikiwa chanjo ya kwanza. Vilevile, mwaka 2019, jumla ya wasichana 533,615 sawa na asilimia 78 walifikiwa kwa dozi ya kwanza na wasichana 334,014 sawa na asilimia 63 ya lengo la wasichana walifikiwa na kupatiwa dozi ya pili.



Mheshimiwa Spika, idadi ya wasichana waliofikiwa kwa chanjo hiyo ni kiashiria kwamba wamepata kinga dhidi ya saratani ya mlango wa kizazi.

Aidha, kwa kuzingatia umuhimu wa chanjo hii katika kukinga maradhi na vifo, pamoja na ukweli kuwa chanjo ni uwekezaji katika uchumi wa Taifa, Serikali hutoa chanjo hizi bila malipo katika vituo vinavyotoa huduma za chanjo vya Serikali, Mashirika ya Dini na Binafsi na mashuleni.

Mheshimiwa Spika, wizara inaendelea kuwahimiza wananchi hasa wazazi/walezi wenye watoto wa umri wa kupata chanjo hii (miaka 14) kuwapeleka mara moja watoto wote ambao hawakupata au hawajakamilisha chanjo kulingana na ratiba ili waweze kukamilisha chanjo zao. Aidha, Wizara inawahakikishia wananchi wote kwamba huduma za afya zikiwemo chanjo zinaendelea kutolewa nchini na hutolewa bila malipo. Wananchi waendeleo kutumia huduma hizi wakati wote, kwani chanjo ni haki ya msingi kwa kila mtoto.

Na. 81

### **Mbegu Bora za Alizeti kwa Wakulima Serengeti**

**MHE. MARWA R. CHACHA** aliuliza:-

Mheshimiwa Spika, baada ya zao la tumbaku kukosa soko na mwelekeo, wananchi wa Wilaya ya Serengeti wameamua kuanzisha kilimo cha alizeti:-

Je, Serikali iko tayari kuwapa mbegu bora za kisasa zinazotoa mafuta mengi?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Marwa Ryoba Chacha, Mbunge wa Jimbo la Serengeti kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ni kweli wakulima wa tumbaku katika Wilaya ya Serengeti pamoja na uzalishaji wa zao la tumbaku wamejikita pia katika uzalishaji wa zao la alizeti ili kuongeza kipato na kuwa na zao la biashara zaidi ya tumbaku.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imenunua mbegu za alizeti kilo 400 aina ya *Hysun 33* zenye thamani ya Sh.12,000,000 na kuwanufaisha wakulima 400 katika kata kumi (10). Aidha, mbegu hizo zina uwezo wa kuzalisha kilo 800 hadi 1,000 kwa ekari.

Mheshimiwa Spika, katika mwaka 2019/2020, halmashauri hiyo pia imetenga jumla ya Sh.10,000,000 kwa ajili ya kununua kilo 300 za mbegu bora za alizeti ambapo taratibu za manunuzi zimekamilika na mbegu hiyo itasambazwa kwa wakulima.

Mheshimiwa Spika, vilevile msimu wa mwaka 2020/2021, Halmashauri ya Serengeti imetega jumla ya Sh.25,150,000 kwa ajili ya ununuzi wa mbegu za alizeti kilo 838. Aidha, uhamasishaji wa sekta binafsi kushiriki katika kununua na kusambaza mbegu bora za alizeti kwa bei nafuu unaendelea sambamba na uwekezaji katika viwanda vya kusindika alizeti ambapo hadi Machi, 2020 kuna jumla ya viwanda sita vya kusindika alizeti vinavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, katika kuongeza uzalishaji wa mbegu za alizeti mwezi Desemba, 2019 Serikali imeidhinisha aina mpya tisa mpya za mbegu za alizeti zenye sifa ya kutoa mafuta mengi kati ya asilimia 32 hadi 42, mavuno kati tani mbili (2) hadi tano (5) kwa hekta na kuhimili magonjwa na ukame.

Aidha, wizara kupitia ASA na makampuni binafsi itaendelea kuzalisha mbegu hizo pamoja na mbegu aina ya *RECORD* kwa ajili ya kuongeza upatikanaji wa mbegu za alizeti nchini.

Na. 82

**Uhakiki wa Wananchi Waliozalisha Miche ya Korosho na Kusambaza Pembejeo**

**MHE. DKT. RASHID M. CHUACHUA** aliuliza:-

Uhakiki wa wananchi waliozalisha miche ya korosho kwa mwaka 2017/2018 pamoja na uhakiki wa waliosambaza pembejeo kwa mwaka wa fedha 2015/2016 bado haujakamilika:-

(a) Je, ni lini uhakiki huo endelevu utakwisha?

(b) Je, wanaodai pesa zao watalipwa lini?

**WAZIRI WA KILIMO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dkt. Rashid Mohamed Chuachua, Mbunge wa Jimbo la Masasi lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, awamu ya kwanza ya uhakiki wa wazalishaji miche ya korosho ilifanyika katika Mikoa ya Mtwara, Lindi, Ruvuma, Singida, Dodoma na Tabora na jumla ya wazalishaji 419 walihakikiwa. Hadi kufikia tarehe 30 Machi, 2019, jumla ya vikundi 407 kati ya vikundi 419 vilivyohakikiwa katika mikoa hiyo vimelipwa jumla ya Sh.2,371,523,877.00. Aidha, wazalishaji wanne hawajalipwa kutokana na akaunti zao kusinzia na kuwa na majina tofauti na akaunti za malipo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imepanga kukamilisha uhakiki wa wazalishaji wa miche ya korosho katika Mikoa ya Pwani, Morogoro, Tanga, Kilimanjaro, Mbeya, Iringa, Njombe, Songwe na Wilaya ya Masasi (Mtwara) kabla ya mwezi Julai, 2020.

Mheshimiwa Spika, mawakala waliosambaza pembejeo za mbolea na mbegu kwa msimu wa 2016/2017

kwa ujumla wao waliwasilisha madeni yenye thamani ya Sh.65,444,665,000.00, ambapo Serikali ilifanya uhakiki ili kujiridhisha na uhalali wa deni hilo. Aidha, matokeo ya uhakiki huo yalibaini udanganyifu mkubwa katika usambazaji wa pembejeo na hivyo Serikali kukabidhi vyombo vya dola kufanya uchunguzi wa kina ili kuiwezesha Serikali kuchukua hatua stahiki.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa pembejeo za zao la korosho, wazabuni saba waliosambaza pembejeo katika msimu wa mwaka 2015/2016 walikwishalipwa kiasi cha Sh.1,399,289,000.00 ambacho ni sawa na thamani ya pembejeo walizosambaza. Aidha, endapo kuna msambazaji wa pembejeo za zao la korosho ambaye alisambaza pembejeo katika msimu huo wa kilimo na bado hajalipwa, tunaomba kupatiwa taarifa hizo ili tuweze kufuatilia na kuchukua hatua.

Na. 83

### **Kutangaza Kiswahili na Utalii Nje ya Nchi**

**MHE. MARYAM SALUM MSABAHA** aliuliza:-

Je, Balozi zetu zinazowakilisha nchi yetu katika nchi mbalimbali zimetangazaje Tanzania katika Sekta ya Utalii na Kiswahili?

**WAZIRI WA MAMBO YA NJE NA USHIRIKIANO WA AFRIKA MASHARIKI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maryam Salum Msabaha, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Wizara kupitia Balozi zake imeendelea kuitangaza Tanzania katika Sekta ya Utalii na Kiswahili kwa kutekeleza diplomasia ya uchumi inayoweka msisitizo katika kuvutia watalii kutembelea vivutio vya utalii vilivyopo nchini pamoja na kufanikisha ushirikiano katika

masuala ya utamaduni hususan kutangaza na kukuza matumizi ya lugha ya Kiswahili. Baadhi ya hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Kuandaa kampeni mbalimbali za kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini. Kwa mfano Ubalози wa Tanzania Moscow, Urusi uliwezesha Tanzania kushinda tuzo ya kuwa Eneo Bora zaidi la Utalii duniani iliyotolewa na Jarida la Kirusi la *National Geographical Traveller (NGT)* mwaka 2018;

(ii) Kuratibu ziara maalum za makundi mbalimbali kama vile Watu Mashuhuri, Wanahabari kutoka vituo maarufu duniani, na mafunzo ya utalii. Kwa mfano ziara ya Waandishi wa Habari kutoka kituo maarufu cha runinga cha China kijulikanacho kama *Travel Channel* mwezi Oktoba, 2018 na ziara ya mafunzo ya utalii kwa washiriki 20 ambao ni wadau wa Sekta ya Utalii kutoka nchi nne za Kusini Mashariki mwa Asia ambazo ni Malaysia, Thailand, Indonesia na Ufilipino mwezi Aprili, 2019;

(iii) Kuratibu kusainiwa kwa makubaliano mbalimbali yanayolenga katika kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini ili kuvutia watalii wengi zaidi pamoja na kukuza Lugha ya Kiswahili. Kwa mfano, kuwezesha Tanzania kusaini Hati ya Makubaliano na Kampuni ya *Touchroad International Holding Group (TIHG)* ya nchini China iliyowezesha ujio wa watalii 450 waliotembelea sehemu ya historia ya Masalia ya Binadamu wa Kale Olduvai Gorge, Mbuga za Wanyama za Serengeti na Ngorongoro katika kipindi cha mwezi Mei, 2019 na Julai, 2019;

(iv) Kuratibu ushiriki wa nchi katika maonesho na makongamano mbalimbali ya kimataifa ambayo yaliwezesha Tanzania kutangaza vivutio vya utalii, Lugha ya Kiswahili, sanaa na utamaduni wa Mtanzania. Kwa mfano Ubalози wa Tanzania nchini Israel uliratibu ushiriki wa kampuni za kitalii, mashirika ya ndege, wamiliki wa hoteli pamoja na kampuni za usafirishaji katika maonesho ya kimataifa ya utalii nchini Israel mwezi Februari, 2019. Hatua hii iliwezesha

Tanzania kupokea jumla ya watalii 1,050 kutoka Israel katika kipindi cha mwezi Desemba, 2019 na Februari, 2020;

(v) Balozi kuendelea kuwa kituo cha matangazo ya bidhaa za utalii, kukuza Lugha ya Kiswahili pamoja na kushawishi mashirika ya ndege kuanzisha safari za kuja Tanzania na kutafuta fursa za Shirika la Ndege Tanzania kwenda nje ili kuchochea Sekta ya Utalii na kukuza uchumi wa nchi kwa ujumla; na

(vi) Kuendelea kuzishawishi kampuni za ndege kuweka video fupi katika ndege zao zinazoonesha vivutio vya utalii vya Tanzania kwa lengo la kutangaza vivutio vya utalii vilivyopo nchini kwa wasafiri wanaotumia ndege hizo. Kwa mfano Ubalozi wa Tanzania nchini Malaysia umefanikiwa kuishawishi Kampuni ya Ndege ya *Lion Group Air* ya nchini Indonesia inayomiliki Zaidi ya ndege 350 kuweka video hizo kwenye ndege zao.

Mheshimiwa Spika, kwa maelezo hayo ni dhahiri kuwa Balozi zetu katika nchi mbalimbali zimeendelea kuchukua hatua mbalimbali katika kuhakikisha zinaitangaza vyema Tanzania Kimataifa ili kuchochea ujio wa watalii wengi nchini na kukuza lugha ya Kiswahili.

**SPIKA:** Katibu.

**NDG. LAWRENCE MAKIGI - KATIBU MEZANI:**

### **HOJA ZA SERIKALI**

#### **Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora**

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora), Mheshimiwa Capt. (Mst.) George Mkuchika karibu tafadhali, una nusu saa. (*Makofi*)

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja kwamba kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais - Ikulu na mafungu yaliyoandikwa kwenye kitabu chetu, kwa sababu ya kunusuru muda mtayaona. Aidha, naomba Bunge lako Tukufu likubali kupitia Mpango wa Utekelezaji wa Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia amani na utulivu katika nchi yetu ambavyo vimetuwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuwahudumia wananchi. Aidha, napenda kumshukuru sana Mheshimiwa Rais, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa aliyoionyesha kwangu na kuniteua nimsaidie kufanya kazi katika Ofisi yake. Ahadi yangu kwake Mheshimiwa Rais ni kutekeleza kazi zangu kwa juhudi, uadilifu, utii na uaminifu ili kukidhi matarajio ya wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru sana Naibu wangu, Mheshimiwa Dkt. Mary M. Mwanjelwa, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kunisaidia kazi zangu za kila siku za kuiongoza ofisi hii. Kwa namna ya pekee, namshukuru Mungu kuwa tumepata nafasi nyingine ya kukutana tena kupokea utekelezaji wa ofisi yangu na kutafakari malengo yajayo katika Mkutano huu wa Kumi na Tisa na wa mwisho wa Bunge. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee, naishukuru sana Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti mahiri Mheshimiwa Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Makamu Mwenyekiti wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum (Tabora) kwa ushirikiano,

maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/2020 na Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha maandalizi ya utendaji kazi wa ofisi yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kamati hii imekuwa inatoa ushauri sana kwetu. Kwa mfano, Kamati hii ndiyo iliishauri Wizara yangu kwamba sasa Serikali Mtandao tuibadilishe iwe Mamlaka ya Serikali Mtandao. Lile ni agizo la Kamati na mimi na wenzangu katika Wizara tukalifanyia kazi, Waheshimiwa Wabunge tunawashukuru sana mkatuunga mkono leo tunayo Mamlaka ya Serikali Mtandao. Huo ni mfano mmojawapo tu katika mifano ambayo Kamati hii imetushauri, tunashukuru na kupokea ushauri wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba pia kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa tangu alipochaguliwa mwaka 2015. Sote tumeshuhudia utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya mwaka 2015 na ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa kampeni ya uchaguzi. Uongozi wake mahiri umedhihirika kwa jinsi anavyopambana na rushwa, ufisadi na ubadhirifu wa rasilimali za umma.

Aidha, Mheshimiwa Rais nyakati zote amekuwa akihimiza uadilifu, uwajibikaji, uchapakazi na utendaji wenye matokeo katika utumishi wa umma hali ambayo sote ni mashahidi kuwa utumishi wa umma umeimarika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii popote alipo kila mtumishi wa umma kuwapongeza na kuwaambia kwamba Serikali yetu inaona ufahari kuwa na ninyi watumishi wa umma mliochujwa na mliobaki mko makini. Tunaposema kwamba makusanyo ya Serikali yameongezeka maana yake kazi ile imefanywa na watumishi wa umma. Bila watumishi wa umma kukusanya mapato kwa wingi kiasi hicho, yale



mengi tunayoyafanya katika Serikali ya Awamu ya Tano tusingefanya. Hongereni sana watumishi wa umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kumpongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa jinsi anavyomsaidia Mheshimiwa Rais wetu. Tunashuhudia anavyokutuma kwenda maeneo mbalimbali wakati yeye anatengeneza mambo hapa nyumbani, tunakupongeza sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo kwa wananchi wa Zanzibar. Aidha, nampongeza kwa hatua anazochukua kuimarisha muungano wetu, amani na utulivu katika nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile nampongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote wa kizalendo. Shughuli za *TASAF* kule ziko chini ya ofisi yake, namshukuru sana anavyosimamia masuala ya *TASAF* akisaidiwa na Waziri wa Nchi, ndugu yangu Mheshimiwa Mohammed Aboud Mohammed. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya usimamizi na uratibu wa kazi za kila siku za Serikali Bungeni. Kwa kipindi chote cha Bunge la Kumi na Moja amedhihirisha umahiri mkubwa wa uongozi na matokeo yake tumeyaona hapa Bungeni, hili litaendelea kukumbukwa. Ndiyo maana pamoja na kwamba humu ndani tuko watu wa vyama vingi, Mheshimiwa Majaliwa anatumvumilia sisi sote na ndiyo maana tumefika hapa kwa sababu ana moyo wa kutuweka pamoja tufanye kazi bila kujali itikadi za vyama vyetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umakini, busara na hekima kubwa. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa ustadi wa kazi wanayoifanya ya kuliongoza Bunge letu wakikusaidia wewe, hakika wamekuwa msaada mkubwa sana katika uendeshaji wa Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, watu walileta masihara hapa sijui ndiyo tuseme leo kwa sababu upo, walisema Mheshimiwa Spika wetu kwa tabia yake kila Bunge likianza anatupeleka Jangwani na Msimbazi, mbona leo kimya? Wakasema aaa, kama yeye amenyamza amekuachia wewe. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kuwapongeza vijana wangu wa Jangwani wa Yanga. Kucheza na Simba ukarudisha magoli mawili ndani ya dakika tatu haijapata kutokea. Kucheza na Simba Morrison akapiga kamoja chwaa, akaenda kupumzika, haijapata kutokea. Tunaelekea kukosakosa ubingwa lakini kwa tabia na mila zetu za Yanga afadhali ukose ubingwa kuliko kutomfunga Simba. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, nawapongeza pia Waheshimiwa Mawaziri wenzangu wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio makubwa wanayoendelea kuyaleta kwa wananchi wa Tanzania kupitia usimamizi wao mahiri wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi. Mawazi wenzangu nataka kuwaambia naona fahari kuwa mmoja wa mchezaji katika timu hiyo ambayo ameiunda Mheshimiwa Rais. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kipekee, napenda kumshukuru Mheshimiwa Waziri mwenzangu Ofisi ya Rais, Waziri pacha, Mheshimiwa Selemani Jafo, anayeshughulika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano mkubwa anaonipa pamoja na viongozi wengine wa wizara yake. Kusema kweli shughuli za TAMISEMI na shughuli za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora zinategemeana sana.

Mimi siwezi kukamilisha mambo yangu bila yeye na yeye hakamilishi shughuli zake bila mimi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Jumanne Mtaturu kwa kuchaguliwa tena bila kupingwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki katika uchaguzi mdogo uliofanyika. Mmekaa muda mrefu hamna mwakilishi sasa mmempata mwakilishi makini, atawawakilisheni vizuri na mandhali alikuwa anamaliziamalizia basi mpeni tena mitano hiyo afanye vitu vyake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, vilevile, kwa masikitiko makubwa sana natoa pole kwa msiba wa Mheshimiwa Rashid Akbar Ajali aliyekuwa Mbunge mwenzangu Wilaya ya Newala; yeye akiwa Jimbo la Newala Vijijini uliotokea tarehe 15 Januari, 2020. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, amina.

Mheshimiwa Spika, naomba kuchukua fursa hii pia kumpongeza somo yangu na mdogo wangu, Mheshimiwa George Simbachawene, Mbunge wa Kibakwe kwa kuchaguliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi. Ndugu yangu wa Msimbazi kule anaitwa Mheshimiwa Mussa Azzan Zungu, Mbunge wa Ilala, naye nampongeza kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira. Muungano wa nchi hii upo mikononi mwako, wewe ndiye utakayetuongoza na sisi tupo nyuma yako kuhakikisha kwamba tunaimarisha Muungano wa nchi yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nawashukuru Balozi Mhandisi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Dkt. Moses Kusiluka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi na Utawala Bora; Naibu Katibu Mkuu na Wataalamu wote katika ofisi yangu ambao shughuli zao walizozifanya zinanipa mimi kiburi cha kusimama hapa kusoma hotuba ya Wizara yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru sana nchi wahisani na washirika wa maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi lakini pia kuimarisha utawala bora katika nchi yetu. Kwa kutambua mchango wao mkubwa, niruhusu niwasome.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kushukuru nchi zifuatazo: Jamhuri ya Watu wa China (makomredi); Japan; Uingereza; India; Jamhuri ya Korea; Canada; Marekani; Sweden; Australia; Umoja wa Ulaya; Denmark; Norway; Uholanzi; Finland; Uswisi; Italia; Malaysia; Misri; Singapore; Cuba; Thailand; na Ireland. Vilevile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa kama vile Benki ya Dunia; Benki ya Maendeleo ya Afrika (*African Development Bank*); *OFID-OPEC Fund for International Development*; *DFID, KOICA; GIZ; USAID; SIDA; UNDP*; Jumuiya ya Madola; *DANIDA; JICA; UNICEF; ILO; WFP; UN Women; Global Fund*; Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (*International Monetary Fund*); na Taasisi ya *Bill and Melinda Gates*. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, natumia fursa hii kuwashukuru sana wananchi wa Jimbo la Newala Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Ahadi yangu kwao ni kutowaangusha katika kuliendeleza Jimbo letu jipya la Newala Mjini. Vile vile naishukuru sana familia yangu ikiongozwa na mke wangu Anna kwa ushirikiano wanaonipa na kwa maombi yao wakati wote ninapoendelea kutekeleza majukumu ya Kitaifa na kuwaacha wao wakiwa peke yao. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa masikitiko makubwa, natoa pole sana kwa Watanzania wenzangu, viongozi na Watumishi wa Umma waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki. Sote tumeshuhudia majanga yaliyoikumba nchi yetu ikiwemo ajali ya moto, mafuta kule Morogoro mwezi Agosti, 2019 ambako ilileta simanzi kubwa katika Taifa letu. Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu takribani 104 na wengine kuachwa na ulemavu.

Mheshimiwa Spika, majanga mengine yaliyotokea mwaka huu, ajali ya treni ya uokoaji na kiberenge iliyotokea mwezi Machi, 2020 katika reli iliyotoka *Ruvu Junction* ambapo ilisababisha vifo vya watumishi watano na kujeruhi mtumishi mmoja. Vilevile wanajeshi wetu 10, wenzangu wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania vilivyotokea mwezi Februari, 2020 Msata, mkoani Pwani wakati wakiwa kwenye mazoezi ya kujiweka imara kijeshi na Askari watatu wa Jeshi la Polisi waliofariki kwa ajali ya gari mkoani Njombe.

Mheshimiwa Spika, vilevile athari za mvua za majanga watu wamepoteza maisha. Tunamwomba Mwenyezi Mungu mvua tunazoziomba ziwe mvua za kiasi za kututusha, zisiwe mvua za gharika. Halikadhalika mvua hizi zimeleta uharibufu mkubwa kama nilivyosema kwa mali, miundombinu na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, tunatambua kwamba dunia sasa inakumbwa na mlipuko wa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya *Corona*. Mawaziri wenzangu walionitangulia, Kamati mbalimbali zilizotangulia, wachangiaji mbalimbali mpaka na ndugu yangu Mheshimiwa Lema, Mbunge wa Arusha Mjini walichangia kuwasahi Watanzania tuwe wakali zaidi katika kusimamia ili madhara haya yasiwe makubwa. Nami naungana nao mkono, nasi kila mmoja kwa dini yake tumwombe Mwenyezi Mungu atuepushe na balaa hili ili nchi yetu irejee kwa amani kama ilivyokuwa siku za nyuma. *(Makoff)*

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako Tukufu maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango kazi iliyokuwa imewasilishwa. Mwaka wa fedha 2019/2020 tumeeleza tumefanya nini.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mapitio ya utekezaji wa Mpango wa mwaka wa fedha. Nitaongea kwa kifupi sana kwa haya mafungu kutokana na muda tuliyonao. Ofisi ya Rais, Ikulu katika mwaka wa fedha Fungu 20; Ofisi ya Rais Ikulu iliidhinishwa shilingi bilioni 23.14 kwa ajili ya Matumizi ya

Kawaida na hadi kufikia Machi, 2020 shilingi bilioni 17 zilikuwa zimepokelewa.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza majukumu, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri tumeeleza fedha tuliomba kiasi gani, tumeeleza fedha ambazo zimetumika.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais Ikulu imeendelea kuongoza kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, kazi zilizofanyika tumezieleza ikiwa namba moja pale, huduma zimetolewa kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake na kutoa ushauri na kazi tulizozifanya tumezieleza. Hizo kazi tulizozifanya ni kwa mujibu wa mgawanyo wa majukumu ambayo Mheshimiwa Rais ameipangia Ofisi yangu.

Mheshimiwa Spika, tumezungumza kwa kifupi juu ya Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa, kama alivyosema Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ni moja ya Taasisi zilizo chini ya Ofisi yangu. Hii imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza sana Brigedia Jenerali Mbung'o kwa Mheshimiwa Rais kumthibitisha kwamba badala ya kuwa Kaimu Mkurugenzi Mkuu, sasa ndio Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa na Rais amemthibitisha baada ya kuona utendaji wake umekuwa wa kuridhisha, mahiri, ikiwemo pamoja na kurudisha hela walizokuwa wameibiwa wakulima katika vyama vya msingi. Hongera sana afande wangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, matokeo ya tafiti mbalimbali zilizofanywa tumeeleza. Viko vyombo vya Kimataifa vimefanya utafiti juu ya hali ya utawala bora katika Tanzania, hali ya rushwa katika Tanzania; vyombo vyote vya nje na ndani vinakubali kwamba Watanzania sasa wako mbioni

kupambana na rushwa na wamepata mafanikio makubwa.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha mwaka wa fedha 2019/2020 baadhi ya shughuli zilizotekelezwa tumeziorodhesha pale ambazo nazo zinatokana na mgawanyo wa Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Spika, Taasisi ya Uongozi, hiki ni kituo kinatoa taaluma, kinatoa mafunzo mbalimbali. Nataka nipongeze *Uongozi Institute* katika kipindi hiki, wao wameshirikiana na Rais Mstaafu, Mheshimiwa Benjamin William Mkapa mpaka ametoa kitabu kile ambacho sisi wananchi Watanzania tunaona kwamba ni zawadi kubwa sana Mzee Mkapa ameipa Taifa letu. Nachukua nafasi hii kumpongeza Mzee Mkapa kwa kitabu chake, tunakisoma, tunatafakari, wajukuu wanasoma kitabu chake. Bado nikishauriwa na Mheshimiwa Halima Mdee nami nitaandika na wajukuu zangu wasome. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, Mpango wa Kusimamia Rasilimali na Biashara za Wanyonge, tumeeleza tumefanya nini katika kipindi hiki. Nami nataka niwapongeze sana wananchi wa Singida. Tulikwenda na Kamati Singida, Mkoa wa Singida, tulikwenda na Kamati pale Singida Manispaa, tumekuta *One Stop Center* ya kuwasaidia wanaorasimisha biashara za wanyonge Tanzania kwa kazi nzuri wanayofanya. Wamewarahisishia kazi. Ukifika pale unajandikisha, *NIDA* pale, benki pale na kila kitu kiko pale. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, upande wa Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (*TASAF*), tumeeza shughuli zilizofanywa. Jambo kubwa hapa kwenye *TASAF* ninalotaka kulisema kuwaambia Watanzania wenzangu ni kwamba awamu iliyopita tulikuwa tumefika tu asilimia 70 ya walengwa. Juzi Serikali ya Rais, Mheshimiwa John Pombe Joseph Magufuli imekopa hela Benki ya Dunia shilingi trilioni moja na ushee kwa ajili ya kuendeleza mpango wa *TASAF*; na safari hii tunawafikia walengwa wa *TASAF* wote, tunazifikia vijiji vyote, Halmashauri zote na Shehia zote Tanzania Bara, Unguja na Pemba.

Mheshimiwa Spika, Wakala wa Ndege za Serikali hapa tumeeleza shughuli zinafanywa na Wakala wa Ndege za Serikali. Mwaka huu ni mara kwanza mimi kuiombea fedha baada ya Wakala wa Ndege za Serikali kuhamishiwa Ofisini kwangu. Tunasimamia suala la manunuzi ya ndege, masuala ya ukodishaji wa ndege, sisi ndiyo tunadai kwa niada wa Watanzania kuhakikisha kwamba waliokodi ndege zetu wanalipa kama mkataba unavyosema. Tumeanza vizuri, nataka niwatoe hofu Watanzania wenzangu kwamba ndege zenu zinafanya kazi nzuri na wanatulipa kwa wakati. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi, kwa hapa kubwa jipya tu ni kwamba Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi pamoja na kazi zao za kila siku sasa hivi katika siku zijazo tutakuwa tunajaza fomu kupitia mtandao. Kwa hiyo, hili suala la kwamba tunakwenda Ofisi pale unakuta makaratasi mengi yamelundikana, wamerekebisha hayo.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Taasisi zake, hapa kuna taasisi nyingi; nasema ndani ya nusu saa tumeeleza kiasi gani tumeomba, kiasi gani tulipewa, tumeeleza na kazi gani ambazo zimefanyika katika taasisi zile zote ambazo ziko chini ya Katibu Mkuu Menejimenti Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Kubwa ambalo tayari nimeshalieleza huko ni kwamba tumesimamia utungwaji wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Mheshimiwa Spika, zamani mtu alikuwa aliyemo ndani ya Serikali alikuwa anaweza kukodi huduma za mtandao kwa watu binafsi, anaacha Serikali mtandao au anaingia mkataba na watu huko bila kuushauri Serikali mtandao. Leo hilo haliwezi kufanyika, watafanya shughuli zote kwa maelekezo na ushauri wa Serikali mtandao.

**SPIKA:** Sasa omba fedha Mheshimiwa Waziri.



**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, niombe fedha, ahsante.

Mheshimiwa Spika, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na mipango ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi ya Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninaomba sasa kuwasilisha rasmi mapendekezo ya maombi ya fedha kwa ofisi yangu kwa mwaka wa fedha 2020/2021 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Fungu 20 - Ofisi ya Rais Ikulu, jumla ya shilingi 24,049,003,000/=; Fungu 30 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, shilingi 608,155,446,000/=; Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretariei ya Maadili ya Viongozi wa Umma, shilingi 9,471,110,000/=; Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma, jumla ya shilingi 43,878,828,000/=; Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira shilingi 3,360,526,000/=; Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma, shilingi 5,231,094,000/=; Fungu 9 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma, jumla ya shilingi 1,445,945,000/=; Fungu 4 - Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, jumla ya shilingi 4,564,368,000/=.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge wenzangu, jumla kuu ya bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Matumizi ya Kawaida shilingi 517,131,499,000/=. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo, shilingi 183,024,821,000/=. Jumla kuu ninayoomba Bunge lako kwa unyenyekevu, itupatie leo watumishi wa Ofisi hii ni jumla ya shilingi bilioni 700,156,320,000/=.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**HOTUBA YA WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA KAPT. (MST.) GEORGE H. MKUCHIKA (MB) KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2020/21 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

UTANGULIZI

**1. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja kwamba, kutokana na taarifa iliyowasilishwa ndani ya Bunge lako Tukufu na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa iliyochambua bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu (Fungu 20 na 30); Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma (Fungu 33); Menejimenti ya Utumishi wa Umma (Fungu 32); Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (Fungu 67); Tume ya Utumishi wa Umma (Fungu 94); Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09); na Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa (Fungu 04); Bunge lako Tukufu sasa lipokee na kujadili Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20. Aidha, naliomba Bunge lako Tukufu likubali kupitisha Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Fedha kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

**2. Mheshimiwa Spika**, Awali ya yote, namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuendelea kutujalia amani na utulivu ambavyo vimetuwezesha kutekeleza majukumu ya kuongoza Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora na kuwahudumia wananchi. Aidha napenda kumshukuru Mheshimiwa Rais Dkt. John Pombe Joseph Magufuli kwa imani kubwa aliyonayo kwangu na kuniteua nimsaidie kufanya kazi katika Ofisi yake. Ahadi yangu kwake ni kutekeleza kazi zangu kwa juhudi, uadilifu, utii na uaminifu ili

kukidhi matarajio ya Wananchi. Vile vile, napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Dkt. Mary M. Mwanjelwa (Mb.) kwa kunisaidia katika kazi za kila siku za kuiongoza Ofisi yangu. Kwa namna ya pekee namshukuru Mungu kuwa tumepata nafasi nyingine ya kukutana tena kupokea utekelezaji wa Ofisi yangu na kutafakari malengo yajayo katika mkutano huu wa 19 na wa mwisho wa Bunge la 11.

**3. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee naishukuru Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa chini ya Mwenyekiti wake Mheshimiwa Jasson Samson Rweikiza, Mbunge wa Jimbo la Bukoba Vijijini na Makamu wake Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba, Mbunge wa Viti Maalum Tabora kwa ushirikiano, maelekezo na ushauri mzuri walioutoa wakati wa kupitia Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti ya Mwaka wa Fedha 2019/20 na Mapendekezo ya Mpango wa Utekelezaji na Makadirio ya Mapato na Matumizi ya fedha kwa Mwaka wa Fedha 2020/21. Maoni, ushauri na ushirikiano wa Kamati umetuwezesha kuboresha maandalizi na utendaji kazi wa Ofisi yangu.

**4. Mheshimiwa Spika**, naomba pia, kutumia nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuendelea kuiongoza nchi yetu kwa ufanisi na mafanikio makubwa tangu alipochaguliwa Mwaka 2015. Sote tumeshuhudia utekelezaji wa malengo ya Ilani ya Uchaguzi ya CCM ya Mwaka 2015 na ahadi alizozitoa kwa wananchi wakati wa uchaguzi. Uongozi wake mahiri umedhihirika kwa jinsi anavyopambana na rushwa, ufisadi na ubadhirifu wa rasilimali za Umma. Aidha, Mheshimiwa Rais nyakati zote amekuwa akihimiza uadilifu, uwajibikaji, uchapakazi na utendaji wenye matokeo katika Utumishi wa Umma hali ambayo sote ni mashahidi kuwa Utumishi wa Umma umeimarika. Vile vile, usimamiaji mahiri wa miradi mikuu ya kimkakati kwa Taifa ni jambo ambalo kila mmoja wetu ameliona na hatuna budi kujivunia. Pili, nampongeza Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa

Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa namna anavyomsaidia Mheshimiwa Rais katika utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi.

**5. Mheshimiwa Spika**, Pia napenda kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Ali Mohamed Shein, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa uongozi wake shupavu na nia yake thabiti ya kuleta maendeleo Zanzibar na kuimarisha muungano, amani na utulivu. Vile vile, nampongeza Mheshimiwa Balozi Seif Ali Iddi, Makamu wa Pili wa Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kuendelea kuwatumikia wananchi wa Zanzibar kwa moyo wake wote.

**6. Mheshimiwa Spika**, napenda kuchukua fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, kwa kuendelea kuwa nguzo muhimu ya usimamizi na uratibu wa kazi za kila siku za Serikali Bungeni. Kwa kipindi chote cha Bunge la 11 amedhihirisha umahiri mkubwa wa uongozi na matokeo yake Bunge hili litaendelea kumkumbuka.

**7. Mheshimiwa Spika**, naomba nikupongeze wewe binafsi na Naibu Spika, kwa kuliongoza Bunge letu Tukufu kwa umakini, busara na hekima kubwa. Nawapongeza pia Wenyeviti wa Bunge kwa ustadi wa kazi wanayoifanya ya kuliongoza Bunge letu, hakika wamekuwa msaada mkubwa sana katika uendeshaji wa Bunge kwa ujumla.

**8. Mheshimiwa Spika**, Nawapongeza pia Mawaziri wote wa Serikali ya Awamu ya Tano kwa mafanikio makubwa wanayoendelea kuyaleta kwa wananchi wa Tanzania kupitia usimamizi wao mahiri wa utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi ya CCM na Dira ya Maendeleo ya Mwaka 2025. Kipekee napenda kumshukuru Waziri mwenzangu katika Ofisi ya Rais, Mheshimiwa Selemani Jafo (Mb) anayeshughulika na Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa kwa ushirikiano mkubwa anaonipa pamoja na Viongozi wenzake wa Ofisi ya Rais TAMISEMI maana shughuli zetu zinategemeana sana.

**9. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. Jumanne Mtaturu (Mb.) kwa kuchaguliwa bila kupingwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Singida Mashariki katika uchaguzi mdogo uliofanyika. Vile vile, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa msiba wa Mhe. Rashid Ajali Akbar aliyekuwa Mbunge wa Jimbo la Newala Vijijini uliotokea tarehe 15 Januari, 2020. Tunaomba Mwenyezi Mungu aiweke roho ya marehemu mahali pema peponi, Amina!

**10. Mheshimiwa Spika**, naomba kuchukua fursa hii kumpongeza Mhe. George Boniface Simbachawene (Mbunge wa Kibakwe) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi na Mhe. Mussa Azzan Zungu (Mbunge wa Ilala) kwa kuteuliwa kuwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais anayeshughulikia Muungano na Mazingira. Nawatakia mafanikio katika nafasi hizi walizopewa na Mheshimiwa Rais.

**11. Mheshimiwa Spika**, nawashukuru Balozi Mhandisi John William Kijazi, Katibu Mkuu Kiongozi; Dkt Moses Kusiluka, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Ikulu; Dkt. Laurean J. Ndumbaro, Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma; Dkt Francis Michael, Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Makamishna, Watendaji Wakuu wa Taasisi; Wakurugenzi na Watumishi wote wa Ofisi ya Rais Ikulu na Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya katika kutekeleza majukumu yanayoiwezesha Ofisi kufikia malengo yake, ikiwa ni pamoja na kukamilisha Hotuba hii kwa wakati. Aidha, napenda kuwashukuru waajiri na watumishi wote wa Umma kwa kutekeleza wajibu wao kwa ufanisi, uzalendo na imani yao kwa uongozi wa Serikali ya Awamu ya Tano ambao umeiwezesha Serikali kutekeleza majukumu yake ya kuwahudumia wananchi.

**12. Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee napenda kuzishukuru Nchi Wahisani na Washirika wa Maendeleo ambao wamechangia jitihada zetu za kuleta maendeleo kwa wananchi. Hivyo, nachukua fursa hii kuwashukuru na kuwataja wachache ambao ni:- Jamhuri ya Watu wa China,

Japan, Uingereza, India, Jamhuri ya Korea, Canada, Marekani, Sweden, Australia, Umoja wa Ulaya, Denmark, Norway, Uholanzi, Finland, Uswisi, Italia, Malaysia, Misri, Singapore, Cuba, Thailand na Ireland. Vile vile, nayashukuru Mashirika ya Maendeleo ya Kimataifa ambayo ni: Benki ya Maendeleo ya Afrika (AfDB), Benki ya Dunia (WB), OFID-OPEC Fund for International Development, DfID, KOICA, GIZ, USAID, SIDA, UNDP, Jumuiya ya Madola, DANIDA, JICA, UNICEF, ILO, WFP, UN Women, Global Fund, Mfuko wa Fedha wa Kimataifa (IMF) na Taasisi ya Bill and Melinda Gates Foundation.

**13. Mheshimiwa Spika**, natumia fursa hii kuwashukuru wananchi wa Jimbo la Newala Mjini kwa kuendelea kunipa ushirikiano wakati wote ninapoendelea kuwawakilisha. Ahadi yangu kwao ni kutowaangusha katika kulijenga na kuliletea maendeleo Jimbo letu. Vile vile, naishukuru familia yangu kwa ushirikiano wanaonipa na kwa maombi yao wakati wote ninapotekeleza majukumu ya Kitaifa.

**14. Mheshimiwa Spika**, kwa masikitiko makubwa natoa pole kwa Watanzania wenzetu, Viongozi na Watumishi wa Umma waliopotelewa na ndugu zao kutokana na majanga mbalimbali yaliyotokea katika kipindi hiki. Sote tumeshuhudia majanga yaliyoikumba nchi yetu ikiwemo ajali ya lori la mafuta iliyotokea mwezi Agosti 2019 Mjini Morogoro ambayo ilileta simanzi kubwa katika Taifa letu. Ajali hiyo ilisababisha vifo vya watu takriban 104 na wengine kuachwa na ulemavu. Majanga mengine yaliyotokea ni: ajali ya Treni ya Uokoaji na Kiberenge iliyotokea mwezi Machi, 2020 katika reli inayotoka Ruvu Junction ambayo ilisababisha vifo vya watumishi watano na kujeruhi mtumishi mmoja; vifo vya wanajeshi wetu 10 wa Jeshi la Wananchi wa Tanzania vilivyotokea mwezi Februari 2020 Msata, mkoani Pwani wakati wakishiriki mazoezi ya Kijeshi na Askari watatu wa Jeshi la Polisi waliofariki kwa ajali ya gari mkoani Njombe. Vile vile, athari za mvua kubwa zinazoendelea kunyesha katika maeneo mbalimbali nchini ambazo zimesababisha vifo na wengine kubaki majeruhi. Hali kadhalika, mvua hizi zimeleta uharibifu mkubwa wa mali na miundombinu ya barabara

na madaraja. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awaponye waliojeruhiwa ili waendeele kujenga taifa letu na kwa waliofariki dunia, Mwenyezi mungu aziweke roho zao mahala pema peponi.

**15. Mheshimiwa Spika**, tunatambua kwamba Dunia kwa sasa imekumbwa na mlipuko wa ugonjwa unaosababishwa na virusi vya Corona - COVID 19. Ugonjwa huu umeshababisha vifo katika nchi mbali mbali na wagonjwa wengine wanaendelea kupata matibabu. COVID 19 iliripotiwa kuingia nchini mwetu mwezi Machi, 2020 ambapo Mheshimiwa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu na Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Wazee, Jinsia na Watoto wameendelea kuelekeza na kuchukua hatua mbali mbali ili kukabiliana na janga hili. Nikiwa Waziri mwenye dhamana na Utumishi wa Umma, natoa rai kwa watumishi wote nchini kufuata na kuzingatia maelekezo yanayotolewa na Viongozi pamoja na Wataalam wa afya ili kujikinga na ugonjwa huu na kuzuia kusambaa kwa maambukizi ya virusi vya Corona. Tunamuomba Mwenyezi Mungu awaponye wote waliothibitika kupatwa na ugonjwa huu na pia atukinge na janga hili.

**16. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/20 tuliwasilisha mbele ya Bunge lako tukufu maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza mipango kazi inayoweza Ofisi yangu kwa mazingatio ya kisera na kimkakati. Kwa mara nyingine tupo mbele ya Bunge lako tukufu ili kutoa Taarifa ya Utekelezaji wa shughuli tulizoombea fedha kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 pamoja na kuwasilisha mapendekezo ya Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21.

#### **A. MAPITIO YA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MWAKA WA FEDHA 2019/20**

**17. Mheshimiwa Spika**, utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 ulizingatia, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21) na Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya Mwaka 2015 pamoja na Dira ya Taifa ya Maendeleo ya 2025. Shughuli zilizotekelezwa na kila taasisi ni kama ifuatavyo:-

OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

**18. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Fungu: 20 Ofisi ya Rais, Ikulu iliidhinishiwa **Shilingi 23,144,913,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2020 **Shilingi 17,044,246,000** zilipokelewa na kutumika.

**19. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza majukumu yake, katika Mwaka wa Fedha 2019/20, Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri (Fungu 30) inayojumuisha Taasisi zilizo chini ya Ikulu, iliidhinishiwa **Shilingi 564,312,423,717**. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 410,123,039,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 154,189,384,717** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020, **Shilingi 429,371,669,447.57** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 335,850,018,390.56** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 93,521,588,057.01** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Yafuatayo ni maelezo kwa kila Taasisi:-

**a. OFISI YA RAIS - IKULU**

**20. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Ikulu imeendelea kuongoza, kufuatilia na kusimamia utekelezaji wa shughuli za Serikali. Katika kipindi cha Mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020, kazi zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Huduma ziliendelea kutolewa kwa Mheshimiwa Rais na familia yake;

(ii) Ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;

(iii) Ushauri umetolewa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya na kufikia maamuzi sahihi;

(iv) Mikutano 31 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri ilifanyika, ambapo nyaraka 68 zilichambuliwa. Mikutano 15 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika na nyaraka 35



zilichambuliwa na ushauri kutolewa. Mikutano 15 ya kazi ya Kamati Maalum na Makatibu Wakuu (IMTC) ilifanyika ambapo mada 45 ziliwasilishwa na kujadiliwa. Mikutano sita (6) ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo nyaraka 29 zilijadiliwa na kufanyiwa maamuzi. Aidha, mikutano mitatu (3) ya Kamati ya Katiba na Bunge ya Baraza la Mawaziri ilifanyika ambapo miswada 12 ilijadiliwa;

(v) Kumbukumbu za Mikutano ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu na Baraza la Mawaziri ziliandaliwa na kusambazwa kwa wakati kwa wahusika. Aidha, ufuatiliaji na tathmini ya Maamuzi ya Baraza la Mawaziri ulifanyika na taarifa ya utekelezaji wake iliandaliwa;

(vi) Ziara ya Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri kutembelea migodi ya madini na masoko ya madini katika Mikoa ya Arusha, Shinyanga, Geita, Mwanza na Mara ilifanyika tarehe 19 – 30 Februari, 2020 ili kuona hali halisi ya utekelezaji na kushauri ipasavyo;

(vii) Ziara ya Maafisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu kutembelea na kukagua utekelezaji wa Miradi ya Kimkakati ya Ujenzi wa Reli kwa Kiwango cha Kimataifa (SGR) na Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Julius Nyerere ilifanyika tarehe 2 – 4 Machi, 2020;

(viii) Uratibu wa utekelezaji wa Programu ya Kujenga Uwezo wa taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT) inayotekelezwa na taasisi nufaika 9 nchini ulifanyika;

(ix) Ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) umefanyika kwa kupitia Taarifa za utekelezaji kutoka kwenye Wizara, Wakala, Idara za Serikali Zinazojitegemea, na Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(x) Elimu kwa umma kuhusu Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa imetolewa kwa wawakilishi wa Wamiliki wa Vyombo vya

Habari, Viongozi wa Madhehebu ya Dini na katika Mkutano wa Mwaka wa Jumuiya ya Tawala za Mitaa Jijini Dar es salaam, Mwanza na Dodoma;

(xi) Mafunzo kuhusu maudhui na usimamizi wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa, Awamu ya Tatu yalitolewa kwa Viongozi na Wajumbe wa Kamati ya Kudhibiti Uadilifu kwa Vyuo Vikuu vya Sokoine, Mzumbe na Dodoma, Mamlaka ya Mapato Tanzania, Mamlaka ya Mawasiliano, Mamlaka ya Usimamizi wa Huduma za Bima, Watumishi wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Shirika la Umeme Tanzania;

(xii) Mafunzo ya majaribio ya mfumo wa kieletroniki wa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa yametolewa kwa wawakilishi wa Wajumbe wa Kamati za Kudhibiti Uadilifu katika Wizara, Mikoa na Halmashauri za Mwanza na Dodoma;

(xiii) Rufaa 151 za Watumishi wa Umma, Mamlaka ya Nidhamu na Waajiri zilichambuliwa na kutolewa uamuzi na Rais na Katibu Mkuu Kiongozi ambapo wahusika walijulishwa. Aidha, malalamiko 459 ya Watumishi wa Umma na wananchi wengine yalichambuliwa na kutolewa maelekezo;

(xiv) Ufuatiliaji wa uzingatiaji wa sheria na maelekezo yanayotolewa na Katibu Mkuu Kiongozi na Mkuu wa Utumishi wa Umma ulifanyika katika mikoa ya Kagera, Geita na Dar es Salaam;

(xv) Majibu na ushahidi kwenye kesi za madai 16 zinazohusu watumishi wa Umma na wananchi wengine zilizoko Mahakama Kuu zinazopinga uamuzi wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania au Katibu Mkuu Kiongozi yalitolewa kwa kushirikiana na Ofisi ya Wakili Mkuu wa Serikali;

(xvi) Mikutano mitatu (3) ya uratibu na uendeshaji wa maboresho ilifanyika kujadili mafanikio, changamoto na mipango ya baadae ya maboresho; na

(xvii) Ujenzi na ukarabati wa majengo katika Ikulu ya Chamwino umefanyika.

**b. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)**

**21. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa imeendelea kutekeleza majukumu yake kwa kuzingatia Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Sura ya 329. Majukumu hayo ni pamoja na kuelimisha Umma kuhusu athari za rushwa, kuchunguza tuhuma za makosa ya rushwa, kuwafikisha watuhumiwa mbele ya vyombo vya sheria na kuishauri Serikali kuhusu masuala mbalimbali ya mapambano dhidi ya rushwa.

**22. Mheshimiwa Spika**, Juhudi zinazochukuliwa na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inayoongozwa na Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli katika kukabiliana na vitendo vya rushwa nchini zimeleta mafanikio makubwa kwa kuongeza nidhamu, uadilifu na uwajibikaji katika nyanja mbalimbali zikiwemo za utumishi wa umma, biashara, ukusanyaji mapato na matumizi ya fedha za umma. Mafanikio haya yameijengea Serikali msingi/uwezo imara wa kukuza uchumi na kuongeza kasi ya utoaji huduma za kijamii kwa wananchi.

**23. Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya utafiti uliofanywa na taasisi mbalimbali za kimataifa na za kitaifa kuhusu hatua zinazochukuliwa na Serikali katika kupambana na rushwa nchini zimedhihirisha kuwa Tanzania inafanya vizuri katika kudhibiti vitendo vya rushwa na ufisadi nchini.

**24. Mheshimiwa Spika**, Kiashiria cha Corruption Perception Index (CPI) cha Taasisi ya Kimataifa ya Transparency International ambacho kinapima hali ya rushwa kwa kutumia mzani wa 0-100 ambapo nchi inayopata alama (0) ndiyo imekithiri kwa rushwa na inayopata alama 100 ndiyo inafanya vizuri zaidi, kimeonesha kuwa katika utafiti wa mwaka 2019, kuwa Tanzania imeendelea kufanya vizuri kwa kufikia kiwango cha asilimia 37 na kushika nafasi ya 96 kati ya nchi 180 duniani ikiwa ni kupanda kwa nafasi 23 ikilinganishwa

na kiwango cha asilimia 30 katika nafasi ya 119 ya mwaka 2015. Aidha, kwa kutumia kiashiria cha Mo Ibrahim taarifa ya mwaka 2018, inaonesha kuwa kwa kipindi cha miaka kumi kuanzia mwaka 2008 hadi 2017, Tanzania ilipiga hatua katika nyanja ya Utawala Bora kwa kupata asilimia 58.5 na kuwa nchi ya 14 kati ya nchi 54 za Afrika. Kwa mujibu wa taarifa hiyo Tanzania ni miongoni mwa nchi sita za Afrika zinazopiga hatua katika nyanja ya uwazi na uwajibikaji mwaka hadi mwaka.

**25. Mheshimiwa Spika**, Utafiti uliofanywa na AFROBAROMETER mwaka 2014 ulionesha kuwa asilimia 66 ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimeongezeka. Hata hivyo, matokeo ya utafiti uliofanyika wa mwaka 2017 yanaonesha kuwa asilimia 72 ya waliohojiwa walisema kuwa kiwango cha rushwa kimepungua. Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa na TWaweza mwaka 2017 nao umebainisha kuwa asilimia 85 ya wananchi waliohojiwa walieleza kuwa rushwa imepungua ukilinganisha na asilimia 11 ya waliohojiwa mwaka 2014.

**26. Mheshimiwa Spika**, Matokeo ya utafiti uliofanywa na Transparency International's Global Corruption Barometer for Africa na ripoti yake kutolewa Julai, 2019 juu ya mtazamo na uzoefu wa wananchi kuhusu rushwa, katika kipengele cha juhudi za Serikali katika mapambano dhidi ya rushwa yanaonesha Tanzania imefanya vizuri kwa kuwa ya kwanza kati ya nchi 35 za Afrika zilizofanyiwa utafiti.

**27. Mheshimiwa Spika**, Aidha, matokeo ya utafiti uliofanywa mwaka 2019 na World Economic Forum kuhusu ufanisi katika matumizi ya umma (efficiency of Government spending) yamebainisha kuwa Tanzania imeshika nafasi ya 28 kati ya nchi 136 duniani zilizofanyiwa utafiti huo.

**28. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Uchunguzi wa majalada 183 ulikamilika na kuwasilishwa kwa Mkurugenzi wa Mashtaka kuombewa kibali ambapo Majalada 47 yalipata kibali cha kuwafikisha watuhumiwa mahakamani. Aidha, majalada mengine yanaendelea kufanyiwa kazi;

(ii) Kesi mpya 352 zilifunguliwa mahakamani katika kipindi hiki na kufanya jumla ya kesi zilizoendeshwa mahakamani kufikia 762. Katika kipindi hiki, kesi 339 ziliamuliwa mahakamani ambapo kesi 143 watuhumiwa wake waliachiwa huru na kesi 196 watuhumiwa wake walipatikana na hatia na kuhukumiwa kifungo au kulipa faini. Kesi 649 zinaendelea mahakamani;

(iii) **Shilingi bilioni 50.8** zimeokolewa kutokana na operesheni mbalimbali za uchunguzi na ufuatiliaji wa miradi ya maendeleo unaofanyika kote nchini ambapo **Shilingi bilioni 6.7** ni fedha taslimu zilizorejeshwa Serikalini, **Shilingi bilioni 11.2** ni thamani ya mali zilizotaifishwa ambazo ni nyumba tatu (3) na viwanja vinne (4), **Shilingi bilioni 30.0** ziliokolewa baada ya uchunguzi kufanyika na kubaini mzabuni aliongeza bei kwenye huduma aliyotoa serikalini na **Shilingi bilioni 2.9** zilidhibitiwa au kurejeshwa kwa wananchi. Aidha, kiasi cha fedha na mali zilizowekewa zuio kusubiria kukamilika kwa taratibu za kisheria za utafishaji ni: **Shilingi bilioni 7.0; dola za kimarekani milioni 5.26**; magari 14 yenye thamani ya **Shilingi milioni 635**, nyumba 14 zenye thamani ya **Shilingi bilioni 13.0** na nyumba moja (1) yenye thamani ya **Dola za Marekani 410,000**;

(iv) Utafiti wenye lengo la kuimarisha mifumo ya udhibiti wa mianya ya rushwa umefanyika katika maeneo ya ukusanyaji mapato unaofanywa na Halmashauri, Ukadiriaji wa kodi unaofanywa na TRA na manunuzi ya umma. Matokeo na mapendekezo ya kuziba mianya ya rushwa katika maeneo haya yamewasilishwa kwa mamlaka husika ili hatua stahiki zichukuliwe;

(v) Kazi 275 za uchambuzi wa mifumo zilifanyika katika sekta mbalimbali zikiwemo Vyama vya Ushirika na masoko ya

mazao ya kilimo (AMCOS), uwekezaji na mapato, ambapo kutokana na kazi hizo, hatua zimechukuliwa ikiwemo kuanzisha uchunguzi kutoa elimu kwa umma na kushauri mamlaka husika namna ya kudhibiti mianya ya rushwa katika vyama hivyo;

(vi) Ufuatiliaji wa matumizi ya fedha za umma katika Miradi ya maendeleo nchini umefanyika ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana. Miradi 244 ya maendeleo yenye thamani ya **Shilingi bilioni 9,860** katika sekta za kipaumbele za Afya, Elimu, Maji, Ujenzi na Nishati ilifuatiliwa. Kati ya miradi hiyo, miradi 34 yenye thamani ya **Shilingi bilioni 8.90** ilionekana kuwa na kasoro mbalimbali na inaendelea kufanyiwa uchunguzi;

(vii) Utafiti wa kitaifa wa hali ya rushwa na utawala bora (National Governance and Corruption Survey) unaendelea. Utafiti huu unatarajiwa kukusanya taarifa kuhusu kiwango cha rushwa, aina za rushwa na tabia/mbinu mpya za vitendo vya rushwa kwa lengo la kuisaidia Serikali kuweka msingi wa kisayansi ili kuendelea kukabiliana na tatizo la rushwa nchini;

(viii) Warsha/vikao 294 vya Wadau kujadili matokeo ya kazi za utafiti na uchambuzi wa mifumo kwa lengo la kuweka mikakati ya kudhibiti rushwa vilifanyika katika maeneo ya ujenzi wa hospitali za wilaya, usambazaji wa umeme vijijini na sekta ya Elimu (fedha za Ruzuku kwa shule za msingi);

(ix) Kazi 196 za ufuatiliaji wa utekelezaji wa maazimio yatokanayo na mapendekezo ya uchambuzi wa mifumo zilifanyika ili kuziba mianya ya rushwa katika maeneo ya ukusanyaji wa mapato kwa kutumia POS (Point of Sales) na EFDs; udhibiti wa rushwa katika ukusanyaji wa kodi ya majengo; miradi ya maji; huduma za utoaji Hati za Kusafirira na ukusanyaji wa mapato katika Jiji la Dar es Salaam;

(x) Elimu kuhusu athari za rushwa na juhudi za Serikali za kuidhibiti ili kupata uungwaji mkono ilitolewa kwa umma kupitia njia mbalimbali zikiwemo semina 3,296, mikutano ya hadhara/mijadala 3,186, vipindi vya redio na televisheni 511,

maonesho 291 na taarifa kwa umma 179 zilitolewa kupitia vyombo vya habari. Aidha, habari/makala 370 ziliandaliwa kwa ajili ya wavuti na jarida la TAKUKURU na matangazo manne yaliandaliwa kwa ajili ya kuelimisha umma;

(xi) Elimu kuhusu rushwa ilitolewa kwa vijana walio shuleni na vyuoni ambapo Klabu za wapinga rushwa 5,418 ziliimarishwa ili kujenga kizazi cha vijana wenye maadili na wanaochukia rushwa;

(xii) Kampeni ya UTATU inayoshirikisha TAKUKURU, POLISI na Wadau ilizinduliwa ikiwa na mfumo wa kielektroniki wa kunasa na kuripoti matukio ya vitendo vya rushwa barabarani na sehemu nyingine;

(xiii) TAKUKURU imepokea malalamiko na taarifa kutoka kwa wananchi saa 24 kwa siku ambapo wananchi 166,643 wameweza kuifikia TAKUKURU kwa simu namba 113 ambapo walipata fursa ya kutoa maoni, ushauri, kuuliza maswali na kutoa taarifa za vitendo vya rushwa;

(xiv) Kampeni ya “Vunja Ukimya” inayolenga kudhibiti rushwa ya ngono iliendeshwa katika mikoa yote. Lengo kubwa likiwa ni kuwahamasisha wanaokumbana na vitendo hivyo na wananchi kwa ujumla kutoa taarifa TAKUKURU ili hatua dhidi ya wahusika zichukuliwe;

(xv) Elimu kwa umma imetolewa kupitia vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ambapo jumla ya matangazo 19 yaliandaliwa na kusambazwa kwa njia ya “Whatsup”, taarifa mbalimbali zimeendelea kutolewa kwenye mitandao ya “Twitter”, “WhatsApp” na “Instagram”. Aidha, TAKUKURU imepata usajili wa TAKUKURU Online TV ili kuwashirikisha wananchi wengi kwa gharama nafuu;

(xvi) Mfumo wa TEHAMA ndani ya TAKUKURU umeimarishwa kwa kuunganisha Ofisi za wilaya 58 kwenye mtandao wa taasisi na kuboresha njia za mawasiliano katika mikoa 17 kwa lengo la kurahisisha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na

mawasiliano kutoka ngazi za Wilaya, Mikoa na Makao Makuu;

(xvii) Huduma za TAKUKURU zimesogezwa kwa wananchi kwa kufungua Ofisi kwenye Wilaya mpya 21 na hivyo kufanya Takukuru kuwa na Ofisi katika Mikoa na Wilaya zote Tanzania Bara. Ofisi hizi zimepatiwa watumishi na vitendea kazi ikiwemo magari; na

(xviii) Watumishi 234 walipatiwa mafunzo ili kuwajengea uwezo wa kumudu majukumu kwa ufanisi.

### c. TAASISI YA UONGOZI

**29. Mheshimiwa Spika**, Taasisi ya UONGOZI imeendelea kusimamia malengo yake ya kuwa Kituo cha Utaalam wa Hali ya Juu cha kuendeleza Viongozi Barani Afrika kwa kuanzia na Tanzania, Ukanda wa Afrika Mashariki na hatimaye Afrika kwa ujumla. Walengwa ni Viongozi Waandamizi waliopo na wanaojitokeza wakiwemo wanasiasa, watumishi wa Serikali na Mahakama.

**30. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha mwezi Julai, 2019 hadi Machi, 2020 shughuli zifuatazo zilitekelezwa:-

(i) Programu ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi iliendelea kutekelezwa. Stashahada hii inalenga kuwajengea viongozi uwezo wa kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kujenga sifa binafsi za kiongozi. Stashahada hii yenye moduli 10 inatekelezwa kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Aalto kilichoko Helsinki, nchini Finland. Katika kipindi hiki, awamu ya tatu ya mafunzo inayojumuisha Maafisa Waandamizi 33 kutoka Wizara, Taasisi na Mashirika ya Umma iliendelea kutekelezwa;

(ii) Viongozi wa Umma 628 wamepata mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 17 kwa lengo la kuimarisha utendaji na kupanua uelewa katika masuala ya kiuongozi. Kozi zilizotolewa zilihusu maeneo ya Uongozi; Uongozi wa Kimkakati; Uongozi Wenye Maadili; Mapambano Dhidi ya



Rushwa, Uongozi Binafsi na Akili Hisia, Matumizi Sahihi ya Muda kama rasilimali ya umma; Uongozi na Usimamizi wa Mabadiliko ndani ya taasisi na Usimamizi wa Sekta Binafsi;

(iii) Kwa kushirikiana na taasisi za ndani na nje ya nchi, makongamano matano (5) ya Kimataifa, Kikanda na Kitaifa yalifanyika kwa lengo la kukutanisha viongozi ili kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu na kuwaongezea uelewa wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Jumla ya viongozi 1,479 walishiriki kutoka Tanzania na nchi mbalimbali ndani na nje ya Afrika. Mikutano ifuatayo ilifanyika:-

(a) Kongamano la Kikanda la Viongozi wa Afrika kuhusu "Usimamizi bora wa Rasilimali kwa Maendeleo Endelevu Barani Afrika", lilifanyika tarehe 26 na 27 Julai, 2019. Kongamano liliandaliwa kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Mstaafu Benjamin William Mkapa. Kongamano lilihudhuriwa na Viongozi 161 kutoka nchi 21, wakiwemo Mhe. Dkt. John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Marais Wastaafu kutoka Tanzania, Afrika ya Kusini, Nigeria, Madagascar, na Somalia; Wakuu wa Taasisi za Kimataifa na Kikanda za FAO, UNEP, UNU-Institute for Natural Resources, SADC, EAC, AfDB, AGRA na WWF, wafanyabiashara maarufu, Wakuu wa Taasisi za Kiraia, na wanataaluma;

(b) Kongamano la Kikanda juu ya "Kuimarisha Ushirikiano ndani ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika (SADC)" lilifanyika ambapo mada kuu ilitolewa na Mhe. Benjamin William Mkapa, Rais Mstaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kongamano liliandaliwa kwa kushirikiana na Sekretarieti ya Jumuiya ya Maendeleo Kusini mwa Afrika na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na kuhudhuriwa na Viongozi 515 kutoka nchi za SADC akiwemo Mhe. Netumbo Nandi-Ndaitwah, Naibu Makamu wa Rais na Waziri wa Mahusiano ya Kimataifa wa Namibia, Mhe. Harrison Mwakyembe, aliyemwakilisha Waziri wa Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki na Dkt. Stergomena Tax, Katibu Mtendaji wa Sekretarieti ya SADC;

(c) Kongamano la kitaifa kuhusu “Usimamizi wa Misitu kwa Lengo la Kukuza Rasilimali Maji” lilifanyika kama sehemu ya Jukwaa la Maendeleo Endelevu. Kongamano lilifunguliwa na Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, ambaye pia ni mlezi wa Jukwaa. Kongamano hili lilihudhuriwa na viongozi 99 kutoka Wizara na Idara za Serikali, Asasi za kiraia, na Sekta Binafsi;

(d) Kongamano la Kumbukizi ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere juu ya: “Tanzania Miaka 20 baada ya Mwalimu” liliandaliwa kwa kushirikiana na Kigoda cha Mwalimu Nyerere na kuhudhuriwa na washiriki 585, wakiwemo viongozi waliopo madarakani, wastaafu na wanafunzi wa Vyuo na Sekondari; na

(e) Kongamano la Kitaifa kuhusu “Ushiriki wa Watanzania katika Miradi ya Kimkakati: Mafanikio, Fursa na Changamoto” lilifanyika kwa kushirikiana na Baraza la Taifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi. Kongamano hili liliambatana na uzinduzi wa Miongozo ya Kitaifa na Kisekta ya Ushiriki wa Watanzania na uzinduzi wa Tovuti ya Miradi ya Kimkakati ambapo Washiriki 175 walihudhuria kongamano hilo.

(iv) Vipindi vitano (5) vya mahojiano na viongozi waandamizi na wataalam wa masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu viliandaliwa na kurushwa kwenye runinga na kuwekwa kwenye tovuti ya Taasisi ya UONGOZI na mitandao ya kijamii kwa lengo la kubadilishana taarifa, maarifa na uzoefu. Vipindi hivi vinaonekana Bara zima la Afrika;

(v) Kwa kushirikiana na Taasisi ya Umoja wa Mataifa; UNU-WIDER, iliyoko Finland tafiti 22 zinafanyika kwenye maeneo ya uchumi wa Viwanda, Uchumi Mpana, Fedha, Usimamizi wa Mikopo endelevu, pamoja na maeneo mengine;

(vi) Kitabu kinachoelezea maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Tatu Mhe. Benjamin William Mkapa kilichapishwa na kuzinduliwa tarehe 12 Novemba, 2019 na Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Uzinduzi huu ulihudhuriwa na washiriki 545 wakiwemo marais wastaafu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Spika wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na viongozi wengine kutoka serikalini na mashirika mbalimbali. Aidha, chapisho la maisha ya Rais Mstaafu wa Awamu ya Pili Mhe. Ali Hassan Mwinyi linaendelea kuandaliwa; na

(vii) Chapisho kuhusu masuala ya Maendeleo Endelevu lilitolewa.

#### **d. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)**

**31. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) umeendelea kutekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa Kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa Biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, MKURABITA imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Wakulima 180 na viongozi 22 wa Vyama vya wakulima wamejengewa uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata Mitaji katika Benki na Taasisi zingine za Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa katika Vijiji vya Mvumi na Magubike. Aidha, mafunzo yalipotolewa yamewezesha Wakulima 48 kufungua akaunti katika benki;

(ii) Huduma za Urasimishaji wa Biashara zimesogezwa kwa wananchi kwa kuanzisha Vituo vya Huduma kwa Pamoja katika Manispaa ya Tabora na Mji wa Babati ambapo huduma muhimu za utoaji leseni za biashara, utoaji wa Namba ya Utambulisho wa Mlipa kodi (TIN) kupitia TRA, usajili wa jina la biashara kupitia BRELA, huduma za benki na mifuko ya hifadhi ya jamii zinapatikana sehemu moja. Aidha,

wafanyabiashara 1,529 wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara. Katika kipindi husika Vituo vimesajili biashara 396 na wafanyabiashara 420 wamefungua akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kujiongezea mitaji. Uwekaji wa huduma za Urasimishaji wa Biashara kwa wananchi kwa kuanzisha vituo katika Halmashauri ya Manispaa ya Nyamagana pamoja na Miji ya Kahama na Songea umeanza;

(iii) Zoezi la Urasimishaji wa Ardhi Mijini kwa dhana ya Mfuko Endelevu wa Wilaya limeanza kwa kufanya utambuzi wa milki 200 kati ya 1,000 zilizopangwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa;

(iv) Hati za Haki Milki za Kimila 159 katika kijiji cha Inzomvu kilichopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Mpwapa zimetolewa;

(v) Elimu kwa umma kuhusu utekelezaji wa shughuli za urasimishaji imetolewa kupitia vipindi 14 vya redio na runinga za TBC. Maudhui ya vipindi yalihusu maeneo yaliyofanyiwa urasimishaji katika Halmashauri za Wilaya za Mbarali, Kilombero, Kilosa, Urambo, Misungwi, Manispaa za I l a l a , Mtwara, Singida, Morogoro, Jiji la Tanga, na Halmashauri za Miji ya Njombe, Geita na Bariadi; na

(vi) Ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa shughuli za urasimishaji umefanyika katika Halmashauri ya Wilaya ya Itigi katika Vijiji vya Sanjaranda na Kitopeni.

#### e. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

**32. Mheshimiwa Spika**, Mfuko wa Maendeleo ya Jamii umeendelea kutekeleza Awamu ya Tatu ya TASAF kwa kuyapa kipaumbele maeneo ya Ukuzaji wa uchumi na kupunguza umaskini wa kipato; Kuinua ubora wa maisha na ustawi wa jamii; na Utawala bora na uwajibikaji. Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mfuko wa Maendeleo Jamii (TASAF) umetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Ruzuku ya **Shilingi bilioni 35.6** ilihawilishwa kwa kaya masikini zilizopo kwenye Mpango ambazo zina watu 4,920,344 kwa Tanzania Bara na Zanzibar katika Vijiji/Mitaa/Shehia 9,867. Kaya hizo zimeweza kupata ruzuku hiyo kwa masharti ya lishe, afya na elimu;

(ii) Mpango wa kutoa ajira za muda umetekeleza miradi 1,521 kutoka katika Vijiji, Mitaa na Shehia zipatazo 1,212 ambapo kaya za walengwa 161,416 zilipata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar. Miradi hiyo ina thamani ya **Shilingi bilioni 6.4**. Miradi iliyotekelezwa ni pamoja na ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji, uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti, uchimbaji wa visima vifupi, uboreshaji wa barabara, uhifadhi wa vyanzo vya maji na hifadhi ya mazingira;

(iii) Miradi 119 ya miundombinu ya elimu, afya na maji yenye thamani ya **Shilingi bilioni 11.23** imetekelezwa katika Halmashauri 11 za Mikoa ya Arusha, Njombe, Tanga, Mtwara na Tabora. Aidha, mafunzo kuhusu taratibu za utekelezaji na usimamizi wa miradi katika maeneo husika yalitolewa kwa wawezeshaji wa ngazi ya Halmashauri na wajumbe wa Kamati za Usimamizi za Jamii;

(iv) Mfumo wa malipo kwa Walengwa kwa njia za kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki) umeandaliwa na majaribio yamefanyika katika Mamlaka ya Maeneo ya utekelezaji 16 ambayo ni; Jiji la Arusha, Manispaa ya Ilala, Manispaa ya Kinondoni, Manispaa ya Temeke, Halmashauri ya Bahi, Mpanda Mji, Halmashauri ya Siha, Halmashauri ya Kilwa, Halmashauri ya Bagamoyo, Halmashauri ya Kisarawe, Manispaa ya Kigoma – Ujiji, Halmashauri ya Mkuranga, Manispaa ya Songea, Halmashauri ya Urambo, Halmashauri ya Muheza, na Halmashauri zote za Unguja kwa upande wa Zanzibar. Hadi kufikia Februari, 2020 Walengwa 55,087 walinufaika na **Shilingi bilioni 2.14** zimelipwa kwa kutumia njia hiyo;

(v) Vikundi 22,303 vya Kuweka Akiba na Kukuza Uchumi wa Kaya vyenye jumla ya walengwa 311,114 vimeundwa katika

Mamlaka ya Maeneo ya Utekelezaji 44. Vikundi hivyo vimeweka akiba ya Jumla ya **Shilingi bilioni 2.5** na kukopeshana **Shilingi bilioni 1.6**;

(vi) Mfumo wa Teknolojia, Habari na Mawasiliano (TEHAMA) wa utunzaji wa kumbukumbu za Walengwa, uendeshaji na utoaji taarifa umeimarishwa. Aidha, Mfumo wa kuwasilisha na kupokea malalamiko umekamilika na umeanza kutumika katika Maeneo yote ya Utekelezaji 161. Mifumo ya TASAF imeunganishwa na mifumo mingine ya kitaifa kama vile NIDA na GePG. Aidha, Kituo cha huduma kwa wateja kimeanzishwa TASAF Makao Makuu na kinafanya kazi;

(vii) Mfumo wa ukusanyaji takwimu kwa njia ya kielektroniki kwa kutumia kishikwambi (tablet) kwa ajili ya utambuzi wa kaya maskini na ufuatiliaji wa utekelezaji wa miradi umekamilika na kufanyiwa majaribio katika Halmashauri tatu za Mtwara Vijijini, Nanyamba na Siha na kaya 5,219 zilitambuliwa katika vijiji 98. Hadi kufikia Januari 31, 2020, masjala ya walengwa ilikuwa na jumla ya kaya milioni 1.1 zilizoandikishwa zenye watu milioni 5.2. Aidha, utengenezaji wa kanzidata mpya ya fedha umekamilika na kuanza kufanya kazi;

(viii) Mapitio ya pamoja ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu utekelezaji wa shughuli za Mpango yamefanyika katika vipindi sita vya Julai, 2019 mpaka Februari, 2020. Taarifa zote za mapitio zimeonesha utekelezaji wa Mpango unaendelea vizuri na unawasaidia Walengwa kuondokana na umaskini na kuwajengea uwezo wa kiuchumi na kuwaendeleza watoto katika afya na elimu bora;

(ix) Mafunzo ya kuwajengea uelewa kuhusu Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini yametolewa kwa Waheshimiwa madiwani 57, Waheshimiwa Masheha 154, Wajumbe wa Kamati za Mradi 220, Waheshimiwa Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa 30, Wawezeshaji wa Halmashauri 200, Walengwa wa Vikundi vya Kuweka Akiba na Kuwekeza 892 na Wajumbe wa Kamati

ya Baraza la Wawakilishi inayosimamia Viongozi Wakuu wa kitaifa Zanzibar 22;

(x) Mafunzo maalum kuhusu usimamizi wa rasilimali za mpango, ufuatiliaji wa utekelezaji, tathmini za shughuli za mpango, utoaji wa taarifa pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango yalifanyika kwa wasimamizi wa Mpango katika Mikoa ya Dar es salaam na Pwani pamoja na Unguja kwa upande wa Zanzibar; na

(xi) Uzinduzi rasmi wa Kipindi cha Pili cha Awamu ya Tatu ya TASAF umefanywa na Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania tarehe 17 Februari, 2020, Dar es Salaam. Uzinduzi huo utafuatiwa na utekelezaji wa Mpango baada ya taratibu zote kukamilika.

#### f. WAKALA WA NDEGE ZA SERIKALI

**33. Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Ndege za Serikali ina jukumu la kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Viongozi wengine Wakuu wa Kitaifa. Wakala ilianzishwa ili kuboresha huduma na kuimarisha usalama wa usafiri wa ndege kwa viongozi wanaotumia huduma hizo. Aidha, Wakala imeongezewa jukumu lingine la kuratibu kwa niaba ya Serikali, ununuzi wa ndege, kuzikodisha kwa Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kusimamia mikataba ya ukodishwaji wa ndege hizo.

**34. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Wakala wa Ndege za Serikali ilitokeleza kazi zifuatazo:-

(i) Huduma za usafiri wa anga zimetolewa kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa ambapo jumla ya safari 117 za ndani na tano za nje ya nchi zilifanyika;

(ii) Wanahewa 34 wamepatiwa mafunzo ya kisheria ya uhuishaji wa leseni zao;

(iii) Matengenezo madogo ya ndege tatu zinazowahudumia Viongozi Wakuu wa Kitaifa yalifanyika. Aidha, mafuta ya ndege na vipuri vilinunuliwa kadri ya mahitaji;

(iv) Gharama za bima za ndege pamoja na bima za Wanahewa zililipwa;

(v) Ukarabati na upanuzi wa karakana za ndege za Serikali umeanza kufanyika;

(vi) Ndege mbili mpya zilipokelewa ambapo moja ni aina ya Boeing 787- 8 (Dreamliner) na nyingine aina ya De – Havilland (Bombardier) Dash 8 - Q400. Aidha, Wakala imeingia mkataba wa ununuzi wa ndege tatu ambapo moja ni aina ya De - Havilland (Bombardier) Dash 8 - Q400 ambayo inatarajiwa kuwasili nchini mwaka 2020 na mbili ni aina ya Airbus A220 – 300 zinazotarajiwa kuwasili nchini mwaka 2021; na

(vii) Wakala ya Ndege za Serikali imeingia mikataba miwili ya ukodishaji ndege na Kampuni ya Ndege Tanzania (ATCL) na kufanya mikataba iliyosainiwa kufikia nane.

## OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

**35. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitengewa **Shilingi 9,999,946,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 7,382,075,100** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,617,870,900** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020 **Shilingi 4,649,426,253.26** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 4,352,256,344.93** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 297,169,908.33** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**36. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ilitekeleza shughuli zifuatazo:-



(i) Malalamiko 113 ya ukiukwaji wa maadili dhidi ya Viongozi wa Umma yalipokelewa na kuchambuliwa. Kati ya malalamiko hayo, malalamiko 58 yalihusu Sheria ya Maadili ya Viongozi na malalamiko 55 hayakuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma. Uchunguzi kwa malalamiko 15 yanayohusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma umekamilika na uchunguzi wa malalamiko 43 unaendelea. Aidha, malalamiko 55 ambayo hayakuhusu ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma walalamikaji walipewa ushauri na mengine yalielekezwa kwenye mamlaka zinazohusika;

(ii) Jumla ya Viongozi wa Umma 14,878 ambao ni sawa na asilimia 96 kati ya Viongozi 15,470 wamarejesha Fomu za Tamko la Rasilmali na Madeni kwa kipindi kilichoishia tarehe 31 Desemba, 2019 ikilinganishwa na Viongozi 15,391 waliorejesha kipindi kama hicho mwaka 2018. Viongozi 592 sawa na asilimia 4 ya Viongozi wote bado hawajarejesha Tamko kufikia Februari, 2020;

(iii) Uhakiki maalum kuhusu Mgongano wa maslahi ulifanyika kwa Waheshimiwa Wabunge na Majaji. Jumla ya Viongozi 203 (Wanaume 120 na wanawake 83) walihojiwa ikiwa ni sawa na asilimia 89 ya viongozi waliotarajiwa. Kati ya viongozi 203 waliohojiwa, asilimia 14 walionekana kuwa na viashiria vya mgongano wa maslahi katika mchanganuo ufuatao: asilimia 3 ya viongozi walikuwa ni *hisia ya mgongano wa maslahi*, asilimia 10 walikuwa ni *uwezekano wa kuingia katika mgongano* na asilimia moja ya viongozi walibainika kuwa na *mgongano halisi*. Aidha, uhakiki ulibaini udhaifu wa kimfumo unaoweza kuwaingiza viongozi kwenye migongano ya maslahi wakati wakitekeleza majukumu yao;

(iv) Elimu kwa umma ilitolewa kwa viongozi wa Umma 2,732, Watumishi wa Umma 5,552 na wananchi 3,545 kuhusu jinsi ya kujiepusha na mgongano wa maslahi na kuishi kwa kuzingatia kiapo cha Ahadi ya Uadilifu. Vipindi 52 vya redio vilitolewa kupitia vyombo mbalimbali vya habari. Aidha, Klabu 32 za Maadili zenye wanachama 1,065 zilianzishwa katika shule za Msingi, Sekondari na Vyuho. Klabu 154

zilitembelewa kwa lengo la kukuza na kuendeleza maadili miongoni mwa wanafunzi na wanachama wa klabu. Hadi sasa, Sekretarieti ina zaidi ya klabu 500 za Maadili katika Mikoa mbalimbali nchini zenye wanachama 6,000;

(v) Siku ya Maadili Kitaifa iliadhimishwa Kitaifa Mkoani Dodoma tarehe 10 Desemba, 2019 kwa kushirikiana na Taasisi za Serikali zinazosimamia masuala ya utawala bora, uwajibikaji, haki za binadamu, mapambano dhidi ya rushwa na maadili. Maadhimisho ya Siku hii yalihusisha pia mijadala na midahalo ya maadili Kikanda na Kimataifa;

(vi) Nyenzo za ufuatiliaji na udhibiti wa tatizo la Mgongano wa Maslahi kwa Viongozi wa Umma zimeandaliwa kupitia kikao kazi kilichoshirikisha Taasisi mbalimbali za Umma;

(vii) Ujenzi wa Ofisi za Sekretarieti ya Maadili Makao Makuu Dodoma umeanza;

(viii) Mfumo wa Ujazaji Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao umejengwa na kuunganishwa na Mfumo wa Mamlaka za Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA). Mfumo huu utawezesha Viongozi wa Umma kutuma Tamko la Rasilimali na Madeni kwa njia ya mtandao na kuliwasilisha wakiwa mahali popote kwa kutumia TEHAMA bila kuhitaji kufika katika ofisi za Maadili; na

(ix) Kanuni za mgongano wa maslahi zimeandaliwa na tayari zimeanza kutumika.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI ZAKE

#### **a. Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

**37. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha wa 2019/20, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma: Fungu 32 inayojumuisha taasisi zilizo chini yake iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 72,572,322,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Mpango wa mwaka. Kati ya fedha hizo, **Shilingi 31,512,322,000**

ziliidhinishwa kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 41,060,000,000** kwa ajili ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020 **Shilingi 29,437,330,955.89** zilipokelewa na kutumika. Kati ya fedha hizo **Shilingi 24,666,078,876.93** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 4,771,252,078.96** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

**38. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Taasisi zake ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Uandaaji wa Nyaraka za kisera katika Wizara 15 ulifanyiwa uchambuzi ili kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji na kuimarisha uzingatiaji wa mipaka ya utekelezaji;

(ii) Kanuni za Utumishi wa Umma zimefanyiwa mapitio ili kukidhi mahitaji ya sasa ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Kanuni hizo zitaanza kutumika baada ya kuidhinishwa;

(iii) Miundo ya Maendeleo ya Utumishi ya taasisi 54 ilihuishwa ili kuwianisha na kuoanisha mishahara katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia matokeo ya zoezi la Tathmini ya Kazi. Kati ya miundo ya taasisi hizo, miundo ya taasisi 22 iliidhinishwa na Miundo ya taasisi 18 tayari imeanza kutekelezwa;

(iv) Taasisi za Umma 26 zilifanyiwa ufuatiliaji ambao umebaini kuongezeka kwa utekelezaji bora wa afua za UKIMWI. Vile vile, taasisi hizo zilihamasishwa kuhusu ujumuishwaji zaidi wa masuala ya Anuai za Jamii (Jinsia, UKIMWI na Ulemavu) katika Utumishi wa Umma ili kutoa huduma jumuishi kwa wananchi;

(v) Nyaraka nne za Kiutumishi zilitolewa ili kuimarisha Menejimenti ya Utumishi wa Umma. Nyaraka hizo ni Waraka wa Matumizi ya magari ya Serikali; Waraka wa Utumishi kuhusu ufafanuzi wa utaratibu wa Mawasiliano Serikalini; Waraka wa Utumishi kuhusu Utaratibu wa Kutekeleza Maelekezo/Maagizo yanayotolewa na Viongozi kwa njia ya mdomo; Waraka wa Watumishi wa Umma kuhusu Utaratibu wa Kukopesha Fedha Taslimu Watumishi wa Umma kwa ajili

ya Kununulia Magari/Pikipiki, Samani au Matengenezo ya Magari/Pikipiki;

(vi) Nyumba 477 kwa ajili ya watumishi wa umma, sekta binafsi na wanachama wa mifuko ya hifadhi ya jamii zilijengwa kupitia Watumishi Housing katika maeneo ya Dodoma (100), Dar es Salaam (268), Morogoro (50) na Mwanza (59) na kuziua kwa masharti nafuu.

(vii) Uwekaji wa miundombinu ya barabara, umeme na maji kwenye nyumba 68 zilizoengwa Dar-es- salaam na Watumishi Housing umefanyika;

(viii) Miundo na Mgawanyo wa Majukumu 114 iliuhishwa na kuidhinishwa na Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, miundo hiyo ni ya Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma;

(ix) Taasisi za Umma sita zimewezeshwa kuandaa Maelezo na Orodha ya Kazi kwa Taasisi;

(x) Uainishaji wa aina ya mafunzo ya ufuatiliaji na tathmini yanayohitajika kwa watumishi wa Umma kwa kila ngazi ya Serikali umeratibiwa na kutambua mahitaji kwa kushirikisha wadau wa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini;

(xi) Vikao viwili vya Wadau wa Ufuatiliaji na Tathmini viliratibiwa na kufanyika ili kupata maoni ya namna bora ya kuunda na kutekeleza Mifumo ya Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini;

(xii) Miongozo ya viwango mbalimbali vya kuboresha utendaji kazi serikalini imeandaliwa na kusambazwa katika taasisi za Umma. Miongozo hiyo ni pamoja na Mwongozo wa Uandishi wa Nyaraka mbalimbali za Serikali; Mwongozo wa Karatasi Maalum ya Barua yenye Anwani (Letter Heads) na Mwongozo wa Kitambulisho cha Mtumishi wa Umma;

(xiii) Mifumo ya Utendaji Kazi katika taasisi za Umma imehushwa ambayo ni Mpango Mkakati wa Taasisi (Taasisi

sita); Mkataba wa Huduma kwa Mteja (Taasisi sita) na Nyenzo ya kufanya Tafiti ya Utoaji Huduma (Taasisi moja);

(xiv) Watumishi wa Umma 290,625 wa Kada mbalimbali walipandishwa vyeo. Aidha, Vibali vya ajira mpya na mbadala katika utumishi wa umma vyenye nafasi 6,975 kwa kada mbalimbali vimetolewa ili kuimarisha utendaji katika utumishi wa umma;

(xv) Taasisi za Umma zote zimewezeshwa kuandaa makadirio ya mishahara ya watumishi wake kwa kutumia Mwongozo wa Ikama na Bajeti ya Mishahara ya watumishi wa Umma kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021;

(xvi) Madai ya malimbikizo ya mishahara kwa watumishi wa Umma **14,761** yenye thamani ya **Shilingi 33,326,487,212.05** yalilipwa, hivyo kufanya idadi ya watumishi waliolipwa madai yao tangu Serikali ya Awamu ya Tano iingie madarakani kufikia **100,684** ambao wallilipwa kiasi cha **Shilingi 130,426,656,606.14**. Vile vile, madai ya watumishi **13,058** yenye thamani ya **Shilingi 33,715,291,606.05** yamehakikiwa na kuwasilishwa Hazina kwa uhakiki na malipo. Aidha, madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa umma **23,923** yenye thamani ya **Shilingi 54,673,930,534.96** yanaendelea kuhakikiwa na OR-MUU;

(xvii) Ukaguzi wa Matumizi na usimamizi sahihi wa Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) umefanyika katika Wizara, Idara Zinazojitegemea, Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa na Taasisi za Umma;

(xviii) Usafishaji (uwekaji wa taarifa za kila mtumishi kwa usahihi) na Uboreshaji wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara za watumishi kwa waajiri wote wanaotumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS) umefanyika;

(xix) Utoaji huduma kwa waajiri mbalimbali uliwezesha kwa kutoa vibali vya uhamisho vya watumishi wa umma 4,144, kuazimwa 650, kushikizwa 26 na likizo bila malipo 180;

(xx) Katika kuwezesha waajiri kujaza nafasi za uongozi kwenye taasisi zao, mapendekezo ya nafasi za uteuzi 1,374 yalipokelewa, kati ya hayo 1,183 sawa na asilimia 86 yalirejeshwa kwa waajiri kwa utekelezaji. Aidha, vibali vya uteuzi 116 vimetolewa kwa nafasi za uongozi ambazo zilipendekezwa kwa afisa zaidi ya mmoja, mikataba ya ajira 94 imeshughulikiwa na vibali 263 vya kukaimu nafasi za uongozi vimetolewa;

(xxi) Watumishi wa Umma 885 walijengewa uwezo kwa kupewa nafasi za mafunzo nje ya nchi katika fani mbalimbali zikiwemo Kilimo, Madini, Afya, Nishati, Elimu na TEHAMA. Fursa hizo za mafunzo zilitolewa kwa Ufadhili wa Serikali na Wadau wa Maendeleo ambao ni Serikali ya Jamhuri ya Korea (64); Serikali ya India (229); Serikali ya Japan (85); Serikali ya Jamhuri ya Watu wa China (465); na Serikali ya Australia (42);

(xxii) Viongozi 16 wa Serikali waliwezesha kubadilishana uzoefu wa utendaji kazi miongoni mwa nchi zao. Viongozi 10 wa Serikali walihudhuria Mkutano wa 4 wa Jumuiya ya Utawala wa Utumishi wa Umma na Usimamizi Barani Afrika uliofanyika Cairo-Misri. Vile vile, Viongozi sita walihudhuria Mkutano wa sita wa Mtandao wa Mameneja wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma uliofanyika Rabbat – Morocco;

(xxiii) Mamlaka ya Udhhibiti wa Bima Tanzania na Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu itakayoziwezesha taasisi hizo kufikia malengo ya mipango mkakati iliyojiwekea;

(xxiv) Taasisi za Umma Sita zimewezeshwa kuandaa Mipango ya Urithishanaji Madaraka ili kuwaandaa na kuwajengea uwezo watumishi waweze kumudu majukumu ya nafasi za uongozi na kufanya taasisi ziendeele kutoa huduma bora. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Vitambulishio vya Taifa; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania; Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya; Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam; na Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki;

(xxv) Taasisi saba zilijengewa uwezo wa namna ya kufanya Tathmini ya Mahitaji ya Mafunzo na kuandaa mipango ya mafunzo. Taasisi hizo ni Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga; Wakala wa Huduma za Misitu Tanzania; Chuo cha Teknolojia Dar es Salaam; Tume ya Kurekebisha Sheria Tanzania; Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania; Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya; na Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa;

(xxvi) Ufuatiliaji wa uzingatiaji wa Maadili ulifanyika kwenye taasisi za Umma 29 kati ya 31 zilizokusudiwa. Aidha, matokeo ya Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika taasisi 13 kwa mwaka 2018/19 yalionyesha kiwango cha uzingatiaji wa Maadili kilifikia asilimia 79 ikiwa ni ongezeko la asilimia 4 kutoka tathmini ya mwaka uliotangulia;

(xxvii) Ufuatiliaji wa ushughulikiaji wa malalamiko ya wananchi katika taasisi za Umma umeonesha kiwango cha ushughulikiaji kimefikia asilimia 84 ambapo jumla ya malalamiko 588 yalishughulikiwa kati ya 698 yaliyopokelewa. Kiwango hiki ni ongezeko la asilimia 26.7 ikilinganishwa na mwaka uliotangulia;

(xxviii) Kampeni za ukuzaji maadili katika menejimenti za taasisi za Umma zilifanyika kupitia mafunzo ya maadili ya utendaji kwa menejimenti na watumishi 266 kutoka Sekretarieti ya Mkoa wa Katavi na Ofisi za Wakuu wa Wilaya tano na Mamlaka za Serikali za Mitaa sita;

(xxix) Uhamasishaji wa uadilifu katika Utumishi wa Umma ulifanyika katika Wiki ya Uadilifu na kuhitimishwa Kitaifa tarehe 11/12/2019 kwa kushirikiana na taasisi saba zinazosimamia Maadili katika Utumishi wa Umma;

(xxx) Uhamasishaji wa ukuzaji wa maadili umeendelea kufanyika ambapo watumishi 2,654 kutoka taasisi 22 za Umma wamepatiwa mafunzo ya maadili. Vile vile, vipindi 10 vya redio na vipindi nane vya runinga vinavyohusu Ukuzaji wa Maadili na Uzingatiaji wa Maadili katika Utumishi wa Umma vimeendelea kurushwa katika Redio na Rungina mbalimbali nchini;

(xxx) Uimarishaji wa usimamizi wa TEHAMA Serikalini umefanyika kwa kuwezesha utungwaji wa sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao. Maandalizi ya msingi ya utekelezaji wa Mamlaka hiyo yamekamilika;

(xxxii) Maandalizi ya uanzishwaji wa vituo vya Huduma Pamoja yamefanyika ambapo Mshauri Mwelekezi wa kutathmini huduma zinazotolewa na Serikali na miundombinu iliyopo kwa ajili hiyo ameanza kazi kwa kutembelea wadau mbalimbali Dodoma, Dar es Salaam na Zanzibar;

(xxxiii) Ujenzi wa mfumo mpya wa HCMIS kwa kutumia wataalam na fedha za ndani umekamilika na kufanyiwa majaribio ndani ya taasisi. Mfumo huu una uwezo mkubwa wa kusimamia masuala ya kiutumishi ikilinganishwa na Mfumo unaotumika sasa. Aidha, zoezi la kuhamisha taarifa kutoka mfumo wa sasa kwenda mfumo mpya na mpango wa mafunzo kwa watumiaji wa mfumo mpya unaendelea. Vile vile, mfumo huu utaunganishwa na mifumo mingine kama e-OPRAS, Mahudhurio ya Kielektroniki na Vitambulisho vya Taifa;

(xxxiv) Mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS – Lawson) ili kuwa na uendelevu wa utoaji huduma yametolewa kwa Maafisa Utumishi/Tawala 220 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xxxv) Taasisi za Umma 34 zilijengewa uwezo kuhusu mfumo wa Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini ili kuimarisha utoaji huduma kwa ngazi ya taasisi. Aidha, taasisi za Umma tano ziliwezesha kuandaa Mikataba ya Utendaji Kazi kwa Mtumishi mmoja mmoja. Taasisi hizo ni Tume ya Nguvu za Atomiki Tanzania (TaEC), OR-TAMISEMI, Shirika la Bima la Taifa, TAKUKURU na Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi;

(xxxvi) Maandalizi ya Mfumo wa Wazi na Mapitio ya Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki (e- OPRAS) ambao utatumika kupima utendaji kazi wa watumishi wa Umma yamekamilika;



(xxxvii) Maandalizi ya kustaafu kwa watumishi wa umma yametolewa ambapo watumishi watano wa Ofisi waliwezesha kuhudhuria mafunzo ya wiki moja ya kujiandaa kustaafu yaliyotolewa na Chuo cha Utumishi wa Umma mkoani Morogoro;

(xxxviii) Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma imeandaliwa na kukamilika. Hatua inayoendelea ni kutafuta rasilimalifedha za utekelezaji. Hata hivyo, Ofisi kupitia fedha za ndani imeanzisha utekelezaji wa baadhi ya maeneo ya matokeo ya programu hiyo yanayojumuisha ujenzi wa Mifumo ya kielektroniki na kuingizwa katika michakato ya utekelezaji wa utoaji huduma kwa Umma;

(xxxix) Makala kuhusu mafanikio ya miaka minne ya Serikali ya Awamu ya Tano katika eneo la Utumishi wa Umma iliandaliwa na kuchapishwa katika jarida maalum la Nchi Yetu Toleo Na. 232 la Novemba, 2019 linalotolewa na Idara ya Habari MAELEZO;

(xl) Umma umehabarishwa kuhusu ajira zilizotolewa na Serikali kwa wahitimu wa mafunzo ya JKT "Operesheni Magufuli" waliojitolea kwa kipindi cha kuanzia miaka miwili, ambapo wahitimu 1,500 walijitokeza kuomba ajira ili wawe sehemu ya kuimarisha utendaji kazi katika taasisi za Umma; na

(xli) Huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 5) zimetolewa kwa mujibu wa Sheria.

## **b. Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**39. Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kilianzishwa ili kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za Uongozi, Menejimenti na Utawala. Aidha, Chuo kinaendesha kozi za kitaaluma kwa ngazi za Cheti, Stashahada na Shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Rasilimali Watu, Utawala na Ununuzi wa Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo katika Kampasi sita zilizoko

kwenye Mikoa ya Dar es Salaam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya.

**40. Mheshimiwa Spika**, utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa Umma umeendelea kuimarishwa ili kuwajengea uwezo katika utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi. Katika kuhakikisha kuwa mafunzo yanayotolewa kwa watumishi wa Umma yanaimarisha utendaji kazi wao, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) iliunganishwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kupitia Tangazo la Serikali Na. 63 lilitolewa katika Gazeti la Serikali la Tarehe 31 Januari, 2020. Hivyo, kwenye Wasilisho la Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, majukumu ya TaGLA yataonekana katika majukumu ya Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania.

**41. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Chuo cha Utumishi wa Umma kimetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Watumishi wa Umma 1,014 walipatiwa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma ambayo yamelenga kuimarisha uwezo wa utendaji kazi, hiyo ni sawa na asilimia 105 ya Watumishi waliolengwa;

(ii) Watumishi wa Umma 2,805 wamepatiwa Mafunzo ya Uongozi na Maendeleo pamoja na Menejimenti na Usimamizi wa Ofisi katika Taasisi za umma, hiyo ikiwa ni sawa na asilimia 83 ya lengo la mwaka;

(iii) Mafunzo ya Awali yalitolewa kwa Watumishi wa Umma wapya 2,116 ili kujenga uelewa wa utendaji kazi wa Serikali;

(iv) Wanafunzi 10,902 sawa na asilimia 109 walidahiliwa katika ngazi ya Shahada ya Kwanza, Stashahada na Cheti, kwa ajili ya mafunzo ya muda mrefu katika fani za utunzaji wa kumbukumbu, uhazili, TEHAMA, utunzaji wa fedha za umma, na Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Usimamizi wa Ununuzi wa Umma na Uongozi na Utawala Bora;

(v) Maandiko ya ushauri katika maeneo sita ya kitaalamu yameandaliwa na kuwasilishwa kwa wateja. Aidha, ushauri katika maeneo manne ya kitaalamu katika Menejimenti ya Utumishi wa Umma ulitolewa;

(vi) Utafiti katika maeneo mawili yanayolenga kuboresha Utumishi wa Umma umeanzishwa;

(vii) Makala tano za kitaalamu katika Utumishi wa Ummazimechapishwa katika majarida mbalimbali ndani na nje ya nchi. Aidha, Jarida moja la Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC Journal) lipo katika hatua za uchapishaji;

(viii) Watumishi 81 wa Chuo cha Utumishi wa Umma wamejengewa uwezo katika taaluma mbalimbali, kama ifuatavyo: Shahada ya Uzamivu (sita), Shahada ya uzamili (watatu) na mafunzo ya muda mfupi watumishi (72);

(ix) Ujenzi wa awamu ya pili wa jengo la madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi ya Tabora lenye ghorofa mbili umekamilika. Aidha, ukarabati wa paa za njia kwenda kwenye madarasa na Hostel iitwayo Oysterbay umekamilika;

(x) Uandaaji wa michoro ya usanifu majengo kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya Kampasi ya Dodoma umeanzishwa; na

(xi) Eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Tanga limepatikana na mchakato wa umilikishwaji umeanzishwa.

#### c. Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA)

**42. Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (TaGLA) ina jukumu la kuwajengea uwezo Watumishi wa Umma na Sekta binafsi kwenye maeneo mbalimbali kwa kuratibu na kuendesha mafunzo na midahalo maalum ya muda mfupi kwa kutumia Teknolojia ya Habari na Mawasiliano ili kuhimili kasi ya mabadiliko ya utoaji wa huduma kwa wananchi.

**43. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha kuanzia Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao imetekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Huduma za maunganisho ya kuwezesha mafunzo kwa njia ya mtandao kwa washiriki 1,640 kutoka Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na sekta binafsi zimetolewa. Mafunzo haya yalitolewa katika maeneo ya Uongozi na Menejimenti, Utawala Bora, Maadili, Anuai za Jamii, Mazingira, TEHEMA, Afya na Stadi za utendaji kazi;

(ii) Mafunzo yametolewa kwa washiriki 516 kwa njia ya video ndani na nje ya nchi. Midahalo hiyo ilijumuisha kubadilishana uzoefu wa Mfumo wa Upimaji wa Wafanyakazi na Usimamizi wa Bajeti kutoka Serikali ya Korea kwa kushirikiana na Chuo cha Maendeleo cha Korea Kusini (KDI). Pia midahalo 24 ya ndani na nje ya nchi imeratibiwa na kufanyika. Midahalo hii ni pamoja na Majiji Endelevu, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza, Midahalo ya Jumuiya ya Wanasheria Tanganyika (TLS), matumizi ya TEHAMA serikalini na midahalo ya Afya na Mazingira;

(iii) Matumizi ya vifaa vya mawasiliano kwa njia ya video na mfumo wa mawasiliano ndani na nje ya nchi vya Wakala yamesimamiwa na kufanyiwa matengenezo;

(iv) Elimu kwa wadau ilitolewa juu ya manufaa ya kutumia Teknolojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA) kwa njia ya mtandao wa video. Wadau hao ni Chuo Kikuu Huria cha Tanzania, NIMRI, African Legal Support Facility (ALSF), DAWASA, Wizara ya Mawasiliano ya Lesotho, Tume ya Utumishi wa Umma ya Zimbabwe, Shirika la Posta Tanzania na Jumuiya ya Wanasheria Tanganyika;

(v) Wigo wa huduma za Wakala uliongezwa kwa wateja 287 katika Kituo cha Wakala cha Morogoro. Aidha, Wakala imewajengea uwezo watumishi wake ili kuimarisha utendaji wa kazi. Watumishi sita walipata mafunzo ya muda mfupi, kati yao hao watumishi wanne wamepata mafunzo ya ndani ya nchi na watumishi wawili wamepata mafunzo nje ya

nchi. Aidha, mtumishi mmoja amemaliza mafunzo ya Shahada ya Uzamili katika fani ya Usimamizi wa Rasilimaliwatu kutoka Chuo Kikuu cha Mzumbe; na

(vi) Elimu juu ya jinsi ya kuratibu mikutano, midahalo na mafunzo ilitolewa. Aidha, Ushauri ulitolewa juu ya Ufungaji Bora wa Vifaa, sifa zake, mazingira ya chumba kwa ajili ya mikutano au mafunzo na mitambo stahiki ya mawasiliano kwa njia mtandao wa video. Vile vile, ushauri wa kitaalamu na kubadilishana uzoefu ulitolewa kwa taasisi nne za Serikali zikiwepo Wizara, Idara Zinazojitegemea na Wakala za Serikali (MDA).

**d. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)**

**44. Mheshimiwa Spika**, Wakala ya Serikali Mtandao imebadilika na kuwa Mamlaka ya Serikali Mtandao kwa mujibu Sheria ya Serikali Mtandao Na. 10 ya Mwaka 2019 ambayo imeanza rasmi tarehe 15/12/2019 kwa Tangazo la Serikali Na. 964 la tarehe 6/12/2019. Sheria hii inaipa Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA) majukumu na nguvu ya kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za serikali mtandao.

**45. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi hiki cha Awamu ya Tano, Mamlaka ya Serikali Mtandao, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, imeimarisha na kujenga mifumo imara ya kusimamia ukusanyaji wa mapato katika Taasisi za Serikali zikiwemo Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mifumo hiyo imesaidia sana kurahisisha ukusanyaji wa mapato, kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma na kuwezesha ongezeko la ukusanyaji wa mapato katika sekta mbalimbali za Serikali kuanzia Serikali Kuu hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hadi sasa Taasisi za Umma 631 na watoa huduma za malipo 19 zikiwemo Benki na Kampuni za Simu zimeunganishwa katika Mfumo Mkuu wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini "Government e-Payment Gateway – GePG".

**46. Mheshimiwa Spika**, Mamlaka pia imejenga uwezo wa wataalam wa TEHAMA serikalini na kuwezesha mifumo ya

TEHAMA ya Serikali kujengwa kwa kutumia wataalam wa ndani tofauti na awali ambapo mifumo hiyo ilikuwa inanunuliwa. Hatua hii imesaidia kuokoa gharama za ubunifu, ujenzi na uendeshaji wa mifumo hiyo pamoja na kuimarisha usalama wa mifumo husika.

**47. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Mamlaka imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Mamlaka imeunganisha taasisi za Umma zilizopo Dodoma kwenye Mtandao wa Mawasiliano Serikalini ili kuwezesha mawasiliano miongoni mwa taasisi za Serikali, pamoja na kuongeza na kuboresha usalama wa taarifa na kupunguza gharama za mawasiliano. Aidha, Mamlaka imekamilisha ukarabati wa Kituo cha Utafiti, Ubunifu na Maendeleo ya Serikali Mtandao katika eneo la Chuo Kikuu cha Dodoma, ambapo wanafunzi 33 kutoka UDOM, UDSM, NM-Aist, DIT, Chuo Kikuu cha St. Joseph, na MUCE wameshiriki katika kazi mbali mbali za utafiti na ubunifu;

(ii) Uboreshaji wa utoaji wa huduma kwa wananchi umefanyika kwa kuandaa na kusimamia uendeshaji wa Mifumo na Miundombinu Shirikishi ya TEHAMA ikiwemo; Mtandao wa Mawasiliano Serikalini (Govnet), ambapo taasisi mpya 27 zimeunganishwa hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa kufikia 245; Mfumo wa Kutoa Huduma kwa Njia ya Simu za Mkononi ambapo taasisi mpya 13 zimeunganishwa na hivyo kufanya jumla ya taasisi zilizounganishwa kufikia 160; Mfumo wa Ofisi Mtandao ambapo taasisi mpya 18 zimeunganishwa na kufanya jumla ya taasisi zote kufikia 77; Mfumo wa Mawasiliano kwa Njia ya Barua Pepe ambapo taasisi mpya 30 zimeunganishwa na kufanya jumla ya taasisi zote kufikia 426;

(iii) Taasisi mpya 26 zimeunganishwa na kutumia huduma ya vituo vya kisasa na mahsus (Data Centres) kwa ajili kuhifadhi Mifumo ya Serikali Mtandao na taarifa ili kuboresha mazingira, kuongeza usalama na kupunguza gharama ya kuhifadhi rasilimali shirikishi miongoni mwa taasisi za umma na kufanya jumla ya taasisi zinazotumia huduma hiyo kufikia

75. Aidha, Mamlaka imeanza ujenzi wa Mfumo Maalum utakaowezesha Mifumo mbalimbali ya TEHAMA Serikalini kubadilishana tarifa;

(iv) Usimamizi wa shughuli za taasisi umeboreshwa kwa kutengeneza Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi. Mfumo huo unafanya kazi kupitia moduli zinazowasiliana na kuunganisha shughuli za Idara na Vitengo kielektroniki. Hadi sasa mfumo huu unatumiwa na taasisi 19;

(v) Mamlaka imeshirikiana na taasisi za umma katika kubuni na kutengeneza mifumo mbalimbali kama vile; Mfumo wa Kukusanya Ushuru wa Magari Daraja la Kigamboni; Mfumo wa Tiketi wa Kielekroniki wa Kampuni ya Huduma za Meli; Mfumo wa Kielektroniki wa Dirisha Moja; Mfumo wa Usimamizi wa Miradi ya TEHAMA Serikalini; Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili unaotumiwa na Baraza la Kiswahili; Mfumo Maalum wa Kusimamia Mafunzo na Semina; Mfumo wa Bodi ya Taifa ya Wahasibu na Wakaguzi wa Mahesabu; Mfumo wa Bodi ya Wahandisi; Mfumo wa Bodi ya Wataalamu wa Ununuzi; Mfumo wa kuingiza taarifa na nyaraka kwa Sekta ya Afya; Mfumo wa Usimamizi wa Rasilimaliwatu Serikalini; Mfumo wa Sekta ya Maji utakaotumika na Mamlaka zote za Maji nchini; Mfumo wa Idara ya Wakili Mkuu wa Serikali; Mfumo wa Kuhifadhi Taarifa za Vifaa vya Maktaba ya Bunge na Mfumo wa Bunge Mtandao. Ubunifu huu, umesaidia Serikali ya awamu ya Tano kuokoa fedha nyingi ambazo zingetumika, iwapo mifumo hiyo ingejengwa na wakandarasi;

(vi) Mafunzo kwa taasisi 92 yametolewa katika maeneo ya usimamizi wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini ikiwemo, Mfumo wa Barua Pepe; Mfumo wa Ofisi Mtandao; Mfumo wa Vibali vya Kusafiri Nje ya Nchi; Mfumo wa Kusimamia Rasilimali za Taasisi; Utoaji wa huduma mtandao kwa umma; na usimamizi wa tovuti;

(vii) Huduma za ushauri kuhusu uhakiki wa Mifumo ya TEHAMA, Tathmini ya Usalama, Utayarishaji wa Mpango wa Kukabili Majanga, Utayarishaji wa Sera na Mikakati ya TEHAMA ya taasisi, Usanifu wa Shughuli na Tathmini ya Miradi ya TEHAMA

zimetolewa kwa taasisi 35 ili kuhakikisha uwekezaji unaofanywa na Serikali kwenye TEHAMA unaleta matokeo yaliyokusudiwa;

(viii) Msaada wa kiufundi na ushauri umetolewa kwenye taasisi za umma kupitia Dawati la Msaada wa Huduma kwa Wateja;

(ix) Usimamizi wa viwango na miongozo ya matumizi ya TEHAMA Serikalini umefanyika ili kuondoa urudufu, kupunguza gharama, kuongeza ubora wa huduma zinazotolewa kwa umma na kuhakikisha usalama wa mawasiliano;

(x) Watumishi 73 wamewezeshwa kuhudhuria mafunzo ya kitaalam ya muda mfupi na muda mrefu yanayoendeshwa na Bodi mbali mbali za kitaaluma; na

(xi) Ujenzi wa Kituo cha Usaidizi wa masuala ya Serikali Mtandao kwenye Mji wa Serikali Mtumba - Dodoma umekamilika na kuweka vifaa vitakavyoimarisha mawasiliano katika mji huo unaendelea

OFISI YA RAIS, SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**48. Mheshimiwa Spika**, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma (imeanzishwa kwa mujibu wa Kifungu 29 (1) cha Sheria ya Utumishi wa Umma Sura 298.

**49. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 2,376,443,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2020, kiasi cha **Shilingi 1,676,457,590** za Matumizi ya Kawaida zilitolewa na kutumika.

**50. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020, Sekretarieti imetekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Matangazo 51 ya nafasi za ajira yaliandaliwa na kutolewa kwa niaba ya waajiri 83 katika Utumishi wa Umma ambao



ni Wizara tano, Idara Zinazojitegemea sita, Mashirika ya Umma 12, Wakala za Serikali sita, Mamlaka sita, Taasisi 25 na Vyuo vya Elimu ya Juu 23;

(ii) Usimamizi na uendeshaji wa michakato ya ajira umefanyika mara sita kwa niaba ya waajiri 83 ambapo wasailiwa 2,968 waliofaulu usaili walipangwa katika vituo vya kazi vifuatavyo: Mamlaka za Serikali (932), Mashirika ya Umma (1,097), Wakala za Serikali (235), Wizara (158), Mamlaka za Serikali za Mitaa (271), Taasisi za Elimu (175), Idara Zinazojitegemea (watano) na Sekretarieti za Mikoa (95). Aidha, kati ya waajiriwa hao 17 ni wenye mahitaji maalum, kati ya hao wanawake ni saba na wanaume ni kumi;

(iii) Utaalam wa masuala ya uendeshaji wa mchakato wa ajira ulitolewa kwenye usaili uliofanyika mara 14 kwenye taasisi zilizokasimiwa kuendesha usaili kwa mujibu wa Tangazo la Serikali Na. 922 la Tarehe 29 Novemba, 2019. Mamlaka zilizohusika ni Halmashauri ya Manispaa ya Sumbawanga, Halmashauri za Wilaya za Biharamulo (usaili mara mbili), Bukoba, Kondo, Dodoma, Busega, Kaliua, Tanga Muheza, Meru na Mbulu, Bagamoyo na Ileje. Taarifa za usaili uliofanyika zimeandaliwa na kuhifadhiwa kwa ajili ya kumbukumbu na rejea.

Aidha, usaidizi wa utaalam ulitolewa kwenye usaili wa taasisi za elimu ya juu uliofanyika mara sita. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Chuo Kikuu Mzumbe, Chuo Kikuu Huria Cha Tanzania, Chuo cha Uhasibu Tanzania, Chuo Kikuu cha Kilimo Sokoine na Chuo Kikuu Kishiriki Cha Elimu Mkwawa;

(iv) Usimamizi na uendeshaji wa mchakato wa kumpata mwakilishi wa kanda ya Afrika kugombea nafasi ya Katibu wa Bunge la Jumuiya ya Madola ulifanyika kwa kushirikiana na Ofisi ya Bunge la Tanzania;

(v) Mfumo wa maombi ya kazi kwa njia ya kielektroniki 'Recruitment Portal' umekamilika. Mfumo huo umeunganishwa na mifumo ya Serikali ikiwemo ya NIDA, NECTA, NACTE na OR-MUUUB;

(vi) Mfumo wa Mawasiliano ya Ndani (intranet) umekamilika na kuanza kutumika. Mfumo huu umeboresha mawasiliano ndani ya Sekretarieti ya Ajira;

(vii) Ukaguzi wa vyeti 8,079 vya waombaji ulifanyika ili kuhakiki usahihi wa taarifa za waombaji kazi ambapo vyeti 58 viligundulika kuwa ni vya kugushi;

(viii) Usimamizi wa mitihani ya mchujo na ya vitendo kwa kada mbalimbali ulifanyika;

(ix) Huduma za kiutawala na kiutumishi kwa Ofisi ya Zanzibar zilitolewa;

(x) Usambazaji wa Kanuni za Uendeshaji za Sekretarieti ya Ajira kwa Halmashauri za Tanzania Bara umefanyika;

(xi) Utatuzi wa changamoto za kada ya udereva zilijadiliwa baina ya Sekretarieti na wadau wa usafirishaji ambao ni Chuo Cha Taifa cha Usafirishaji, Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi na Chama cha Wamiliki wa Shule Binafsi za Udereva; na

(xii) Elimu kwa Umma kuhusu shughuli za Sekretarieti ya Ajira ilitolewa kupitia Makala na vipeperushi mbalimbali pamoja na mikutano sita ya vyombo vya habari. Aidha, taarifa za maboresho ya mifumo ya ajira zimekuwa zikiuhishwa katika tovuti ya taasisi na mitandao ya kijamii.

OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

**51. Mheshimiwa Spika,** Tume ni chombo rekebu na inayo mamlaka na wajibu wa kuhakikisha kuwa masuala ya Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma yanasimamiwa na kuendeshwa kwa kuzingatia Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu mbalimbali kama inavyotolewa na Mamlaka. Wajibu huu wa Tume una lengo la kuimarisha Utawala Bora unaozingatia matokeo. Katika kutekeleza wajibu huu pamoja mambo mengine Tume imeendelea kufanya ukaguzi wa Rasilimaliwatu kwa Mamlaka za Ajira na Nidhamu. Aidha,

Tume ya Utumishi wa Umma ni Mamlaka ya Rufaa kwa Watumishi wa Umma dhidi ya Uamuzi unaotolewa na mamlaka zao za nidhamu.

**52. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2019/20 Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma iliidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 4,889,515,606** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia Machi, 2020 kiasi cha **Shilingi 3,279,257,786.98** za Matumizi ya Kawaida zilitolewa na kutumika.

**53. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020 Tume imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Uzingatiaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu katika usimamizi wa Utumishi wa Umma umesimamiwa kwa kufanya ukaguzi katika taasisi 77;

(ii) Maamuzi ya rufaa 138 yalifanyika na malalamiko 504 yalishughulikiwa kupitia mikutano mitatu ya Tume iliyofanyika;

(iii) Elimu kwa wadau kuhusu majukumu ya Tume na Utekelezaji wa Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma ilitolewa kwa taasisi za umma 21. Aidha, kupitia ziara ya Makamishna wa Tume, elimu ilitolewa kuhusu Sheria ya Utumishi wa Umma Sura ya 298 na haki na wajibu wao kwa watumishi wa umma 1,070 wakiwemo Viongozi wa Taasisi za Umma ambao ni Wakuu wa Mikoa (Mwanza na Simiyu), Makatibu Tawala wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi wa Halmashauri, Makatibu Tawala wa Wilaya, Watendaji Wakuu wa Wakala za Serikali, Taasisi za Umma na Watumishi wa Sekretarieti za Mikoa na Halmashauri.

Vilevile elimu ilitolewa kupitia kurusha vipindi sita hewani vya Runinga na vipindi sita vya Redio. Pia, kupitia maadhimisho ya Wiki ya Maadili na Haki za Binadamu wadau wa Tume walipatiwa elimu kuhusu Sheria Na. 8 na Kanuni zake;

(iv) Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume ya Mwaka 2018/19 iliandaliwa na

kuwasilishwa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(v) Utekelezaji wa mahitaji ya anuai za jamii katika utumishi wa umma ulifanyika kwa kuwapatia huduma watumishi wa Tume wenye uhitaji maalum kulingana na Miongozo iliyopo; na

(vi) Watumishi 209 wa Tume wamewezeshwa kupata mafunzo ambapo watumishi 17 walihudhuria mafunzo ya muda mrefu, watumishi 100 walihudhuria mafunzo ya muda mfupi katika maeneo ya uadilifu na OPRAS. Vile vile, watumishi 92 walipatiwa mafunzo maalum ya Uchambuzi wa Rufaa na Ukaguzi wa Rasilimali Watu.

#### BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**54. Mheshimiwa Spika**, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma ina jukumu la kufanya mapitio ya mara kwa mara na kupendekeza viwango vya mishahara na masilahi mengine; na kuzishauri mamlaka kuhusu misingi ya miundo ya mishahara katika Utumishi wa Umma.

**55. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa fedha 2019/20, Bodi iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 1,474,241,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Hadi kufikia mwezi Machi, 2020, **Shilingi 1,040,580,328** zilipokelewa na kutumia.

**56. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai 2019 hadi Machi, 2020, Bodi imetekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Maandalizi kwa ajili ya ushauri kuhusu masilahi kwa watumishi wa Umma yamefanyika kwa kufanya utafiti wa mapitio ya Mipango ya Motisha katika Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa kukusanya taarifa kutoka taasisi 94 za Umma na uchambuzi wa taarifa hiyo unaendelea;

(ii) Mapitio ya mwenendo wa bajeti ya mishahara ya watumishi wa umma kwa kipindi cha miaka 10 yamefanyika.

Aidha, rasimu ya taarifa hiyo imeandaliwa na kujadiliwa na wadau kabla ya kuiwasilisha Serikalini; na

(iii) Taarifa kuhusu gharama za maisha kama msingi wa kukadiria kiwango cha mshahara wenye staha kwa watumishi wa Umma imeandaliwa na kuwasilishwa kwenye mamlaka husika; na

(iv) Mkutano wa wadau kuhusu uboreshaji wa utendaji kazi na kuongeza tija katika utumishi wa Umma ulifanyika. Maoni yaliyotolewa yalichambuliwa na mapendekezo yamewasilishwa serikalini.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

**57. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma.

Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

**58. Mheshimiwa Spika**, Katika mwaka wa fedha 2019/20, Fungu 4: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa, iliidhinishiwa jumla ya **Shilingi 4,774,066,000**, kati ya fedha hizo **Shilingi 2,774,066,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa Miradi ya Maendeleo. Hadi kufikia Machi, 2020, **Shilingi 1,836,345,500** za Matumizi ya Kawaida zilipokelewa na kutumika.

**59. Mheshimiwa Spika**, katika kipindi cha Julai, 2019 hadi Machi, 2020 Idara ya Kumbukumbu ilitekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Nyaraka za kihistoria zimeendelea kuchambuliwa na kukusanywa ka lengo la kutunza historia ya nchi yetu. Idara imekusanya nyaraka na machapisho 728 kutoka Taasisi za Umma nne na kuhifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha kumbukumbu Dodoma. Taasisi hizo ni Halmashauri ya Jiji la Arusha (161), Ofisi ya Katibu Tawala Mkoa wa Dar es Salaam (117) na Ofisi za Wakuu wa Wilaya ya Lushoto (365) na Korogwe (85);

(ii) Ukarabati wa nyaraka zilizohifadhiwa katika Ghala Kuu la Nyaraka umefanyika ambapo nyaraka kongwe 197 zimefanyiwa ukarabati ikiwemo nyaraka zinazomhusu Baba wa Taifa Mwl. Julius K. Nyerere 109, Hansards 32, Ripoti za ukaguzi 22, Mikataba 32 na Act Supplement mbili;

(iii) Uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka katika mifumo ya kidijitali ili kuweza kudumu muda mrefu, kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi umefanyika ambapo majalada 490 yameingizwa kwenye mfumo huo;

(iv) Mifumo bora ya Utunzaji Kumbukumbu za Kiutendaji imewekwa katika Wizara na taasisi za Umma 25. Aidha, Mfumo wa Kielektroniki wa Masijala umewekwa katika taasisi za Umma saba kwa kushirikiana na Mamlaka ya Serikali Mtandao. Taasisi hizo ni Mamlaka ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali, Msajili wa Hazina, Wakala wa Vipimo, Bodi ya Manunuzi na Ugavi na Shirika la Reli Tanzania, Wakala wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) na Wakala wa Usalama na Afya Mahala pa Kazi (OSHA);

(v) Mafunzo ya utunzaji wa kumbukumbu yametolewa katika taasisi za Umma 17 ambazo ni Ofisi ya Rais, Ikulu, Wizara ya Ulinzi na Jeshi la Kujenga Taifa, Shirika la Bima la Taifa, Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi, Wakala wa Barabara Tanzania, Tume ya Vyuo Vikuu, Tume ya Taifa ya UNESCO, Shirika la Umeme Tanzania, Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Pwani, Ofisi za Wilaya ya Kisarawe, Chalinze, Kibaha, Mtwara, Mbinga na Moshi na Ofisi za Halmashauri ya Manispaa ya Singida na Iringa;

(vi) Kumbukumbu tuli za taasisi za Umma tatu ambazo ni Baraza la Mitihani la Taifa, Tume ya Utumishi wa Umma na Chuo cha Uhasibu Tawi la Dar es Salaam zimechambuliwa na kubaini zile zinazostahili kuhifadhiwa na zile ambazo zinastahili kuteketezwa kwa mujibu wa Sheria na Taratibu;

(vii) Kumbukumbu za Ubalozi wa Tanzania Nchini Kenya zimechambuliwa na kuhamishwa kutoka Nairobi kwenda Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma ambapo jumla ya majalada 1,059 yenye umuhimu wa kudumu yamehamishwa. Aidha, Majalada yaliyofungwa 21,985 ya mashauri ya Mahakama Kuu Kanda ya Mwanza yakiwemo majalada ya madai 12,128 na jinai 9,857 yalilihamishiwa katika Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa Mwanza;

(viii) Huduma ya utaaalam wa kuandaa miongozo ya kutunza na kuteketeza kumbukumbu imetolewa katika taasisi za umma mbili ambazo ni Tume ya Vyuo Vikuu Tanzania na Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi. Aidha, huduma hiyo inaendelea katika Shirika la Viwango Tanzania;

(ix) Kumbukumbu na nyaraka 3,318 za Waasisi wa Taifa zimechambuliwa na kukusanywa kutoka katika maeneo mbalimbali nchini wakiwemo watu binafsi waliyofanya kazi kwa karibu na Waasisi wa Taifa kwa lengo la kuhifadhi historia ya Nchi yetu;

(x) Elimu kwa umma kuhusu umuhimu wa kutunza kumbukumbu na nyaraka imetolewa kupitia njia mbalimbali ikiwemo kipindi cha televisheni ya Taifa (TBC) na mitandao ya kijamii. Aidha, Jumla ya wanafunzi 74 kutoka katika Taasisi za Elimu ya Juu walipatiwa mafunzo kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Idara. Vyuo hivyo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam wanafunzi wanne, Chuo Kikuu Mzumbe wanafunzi 62, Chuo cha Ukutubi Bagamoyo wanafunzi watatu na Chuo cha Kumbukumbu ya Mwl. Nyerere wanafunzi watano;

(xi) Uwezo wa watumishi umeimarishwa kwa kuwawezesha waajiriwa wapya saba kupata mafunzo ya awali. Aidha, mtumishi mmoja amewezeshwa kuhudhuria Shahada ya

Uzamili. Vile vile, mafunzo ya UKIMWI na Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza yametolewa kwa watumishi wote wa Idara;

(xii) Uwezo wa Idara katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka katika ofisi za Kanda umeongezwa kwa kukamilisha ujenzi wa Kituo cha Kumbukumbu cha Kanda ya Ziwa-Mwanza; na

(xiii) Ukarabati wa jengo la Idara lililopo Dar es Salaam umekamilika. Aidha, ukarabati wa Ghala la Taifa la kuhifadhi nyaraka unaendelea.

## **B. MPANGO WA UTEKELEZAJI KWA MWAKA 2020/21 NA MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIWA**

**60. Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 umezingatia, Mpango wa Maendeleo wa Miaka Mitano (2016/17 – 2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015; Maelekezo ya Serikali yaliyoainishwa na Mheshimiwa Rais wakati wa uzinduzi rasmi wa Bunge la 11 Mwezi Novemba, 2015; Sheria ya Bajeti, Sura 439 pamoja na kanuni zake; na Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya III.

**61. Mheshimiwa Spika**, Mpango na Bajeti kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 imezingatia utatuzi wa changamoto katika utoaji huduma kwa umma kwa kadri inavyowezekana. Kwa ujumla changamoto hizo ni kama ifuatavyo: Baadhi ya ofisi za utoaji huduma kutokuwepo katika mikoa yote ya Tanzania; Bado kumekuwepo na malalamiko kutoka kwa wananchi kuhusu upatikanaji wa huduma zitolewazo na Taasisi za Umma, kuendelea kuwepo na kaya maskini, ushirikiano mdogo wa wananchi katika suala la utoaji wa ushahidi mahakamani dhidi ya watuhumiwa wa rushwa; kukosekana kwa sheria ya kuwabana wahusika wanaoshindwa kutekeleza ushauri wa TAKUKURU kuziba mianya ya rushwa katika maeneo yao; na Mabadiliko ya TEHAMA yamekuwa yakiibua changamoto katika upelelezi.



OFISI YA RAIS, IKULU NA TAASISI ZAKE

**a. Ofisi ya Rais - Ikulu**

**62. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Ikulu imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;

(ii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuhusu ratiba ya kila siku;

(iii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;

(iv) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

(v) Kuandaa mkutano wa tathmini wa mwaka kati ya Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na wadau wengine;

(vi) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa Shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

(vii) Kuratibu utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu kwa kushirikisha wadau wa Sekta ya Umma na Sekta Binafsi;

(viii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) na

Programu za Maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;

(ix) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu, na kukamilisha mfumo wa kielektroniki wa Ufuatiliaji na Tathmini wa utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III);

(x) Kupokea, kupitia na kuchambua rufaa na malalamiko ya watumishi wa umma na wananchi;

(xi) Kuendesha mikutano miwili ya Watendaji na Maafisa wa Serikali kuhusu utaratibu wa kushughulikia malalamiko na rufaa pamoja nakufuatilia utekelezaji wa maagizo mbalimbali ya Katibu Mkuu Kiongozi;

(xii) Kuratibu na kuendesha mikutano sita ya uratibu wa Maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa Maboresho katika Sekta ya Umma nchini;

(xiii) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Programu ya Kujenga Uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT);

(xiv) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino; na

(xv) Kukarabati majengo ya Ikulu ya Dar es salaam na Ikulu Ndogo za Mwanza, Arusha, Lushoto, Tabora na Shinyanga na nyumba za wafanyakazi zilizopo Dodoma.

#### **b. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANANA RUSHWA (TAKUKURU)**

**63. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, TAKUKURU imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

- (i) Kukamilisha uchunguzi wa majalada ya tuhuma za rushwa unaoendelea pamoja na tuhuma mpya zitakazojitokeza;
- (ii) Kuendesha kesi 649 zinazoendelea na kesi mpya zitakazofunguliwa Mahakamani;
- (iii) Kufuatilia na kudhibiti vitendo vya rushwa kabla, wakati na baada ya Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 2020 ili kuwadhibiti wagombea wote ambao sio waadilifu kwa kuhakikisha kuwa hawatumii fedha kuwarubuni wananchi kupata uongozi;
- (iv) Kuhuisha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Na. 11 ya Mwaka 2007;
- (v) Kufanya utafiti kuhusu mianya ya rushwa katika sekta za umma na binafsi;
- (vi) Kufanya uchambuzi wa mifumo katika sekta na idara mbalimbali katika ngazi ya mkoa na wilaya;
- (vii) Kuweka mikakati kwa kushirikiana na wadau ili kudhibiti mianya ya rushwa na kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa mikakati hiyo;
- (viii) Kufuatilia matumizi ya fedha za umma katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo ili kuhakikisha utekelezaji wake unazingatia thamani halisi ya fedha;
- (ix) Kutekeleza Mkakati wa Mawasiliano wa TAKUKURU ili kujenga uwezo na uelewa kuhusu rushwa, ufisadi na juhudi za Serikali katika kupambana na rushwa kwa makundi mbalimbali katika jamii kwa kutumia njia mbalimbali za mawasiliano kuyashawishi makundi haya kuunga mkono na kushiriki katika mapambano dhidi ya rushwa nchini;
- (x) Kutumia njia za mawasiliano za kimkakati kulifikia kundi la vijana ili washiriki katika shughuli zinazowajenga kimaadili na kushiriki kupambana na rushwa ili kuwa na jamii inayochukia rushwa;

(xi) Kutumia vyombo vya habari na mtandao ya kijamii kubeba agenda ya mapambano dhidi ya rushwa ili kuushirikisha umma katika mapambano hayo;

(xii) Kujenga majengo ya ofisi za TAKUKURU katika mikoa na wilaya;

(xiii) Kujenga karakana kwa ajili ya kutengeneza magari ya taasisi ili kupunguza gharama za uendeshaji zinazotumika katika kutengeneza magari hayo;

(xiv) Kuimarisha mfumo wa TEHAMA katika taasisi ili kurahisisha na kuwezesha mtiririko mzuri wa majalada, takwimu na mawasiliano kutoka ngazi za wilaya, mkoa na makao makuu; na

(xv) Kutoa mafunzo ya weledi kwa watumishi ili kuongeza ufanisi.

#### c. TAASISI YA UONGOZI

**64. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Taasisi ya UONGOZI imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uzamili ya Uongozi kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi 35 katika maeneo ya kufanya maamuzi ya kimkakati, kusimamia rasilimaliwatu na rasilimali nyingine na kuimarisha sifa binafsi za kiongozi;

(ii) Kutoa mafunzo ya Stashahada ya Uongozi kwa njia ya mtandao kwa Viongozi 30;

(iii) Kutoa mafunzo ya muda mfupi kupitia kozi 30 kwa lengo la kuwajengea uwezo Viongozi 765 katika maeneo ya Uongozi na Maendeleo Endelevu, kutokana na mahitaji na maombi ya walengwa;

(iv) Kuandaa mkutano wa kimataifa na kikanda na mikutano saba ya kitaifa katika masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

(v) Kuandaa vipindi 12 vya runinga vitakavyoshirikisha viongozi waandamizi na wataalam mbalimbali ndani na nje ya nchi, juu ya Uongozi na Maendeleo Endelevu. Vipindi hivi vitarushwa kwenye runinga, tovuti na mitandao yaki jamaa na kuonekana katika Bara zima la Afrika;

(vi) Kufanya utafiti kwenye maeneo manne kuhusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu; na

(vii) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo yanayohusu masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu pale utakapohitajika.

#### **d. MPANGO WA KURASIMISHA RASILIMALI NA BIASHARA ZA WANYONGE TANZANIA (MKURABITA)**

**65. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, MKURABITA imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kuanzisha vituo saba vya urasimishaji na uendelezaji biashara ili kuwawezesha wafanyabishara kupata huduma muhimu sehemu moja katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Ilala, Mbeya, Iringa, Tunduma, Arusha, Musoma na Chato. Aidha, mafunzo ya kurasimisha na kuendesha biashara yatatolewa kwa wafanyabishara 4,900 kwa lengo la kuwawezesha kusajili biashara zao;

(ii) Kuanzisha vituo vitatu vya urasimishaji wa biashara Zanzibar, katika Manispaa ya Chakechake, Mkoani na Kaskazini B ili kuwawezesha wafanyabiashara kupata huduma muhimu sehemu moja ambapo wafanyabiashara 1,500 watapata mafunzo na kusajili biashara zao;

(iii) Kutoa mafunzo kuhusu fursa na matumizi bora ya Hati za Haki Milki za Kimila kwa wakulima 1,500 waliorasimisha ardhi zao na viongozi 60 wa vyama vya wakulima katika Halmashauri za Wilaya Tatu za Chamwino, Kilolo na Kilosa. Aidha, kwa upande wa Zanzibar mafunzo yatatolewa kwa wamiliki 2,000 wa ardhi katika maeneo ya Nungwi, Welezo, Chokocho na Kiungoni;

(iv) Kukamilisha urasimishaji wa ardhi mjini katika Mamlaka za Serikali za Mitaa za Miji ya Morogoro, Tunduma, Babati, Iringa, Arusha, Njombe na Miji Midogo ya Tandala na Ikonda Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, urasimishaji wa ardhi mjini utafanyika Chakechake na Unguja Mjini. Jumla ya Hati Milki 6,500 zitaandaliwa na kutolewa;

(v) Kukamilisha uandaaji na utoaji Hati za Haki milki za Kimila 11,700 kwa wananchi katika Halmashauri za Wilaya za Rufiji, Kibiti, Musoma, Butiama, Chamwino, Nyang'wale, Makete, Bukoba Vijijini na Newala za Tanzania Bara. Aidha, kwa upande wa Zanzibar Hati Milki 2,000 zitatolewa katika maeneo ya Chanjamjawiri Wilaya ya Chakechake Pemba na Mahonda Wilaya ya Kaskazini B Unguja;

(vi) Kukamilisha ujenzi wa Masjala za Ardhi za Vijiji katika Halmashauri za Wilaya nne za Chamwino (vijiji viwili), Itigi (kijiji kimoja), Mbinga (kijiji kimoja), Mvomero (kijiji kimoja). Aidha, ujenzi wa Masjala za Ardhi za vijiji utaanza katika Halmashauri za Wilaya ya Newala (kijiji kimoja) na Mbalali (kijiji kimoja);

(vii) Kuendelea na urasimishaji wa Wachimbaji Wadogo wa Madini katika Mkoa wa Geita;

(viii) Kufanya Ufuatiliaji na Tathmini ya Utekelezaji wa shughuli za Urasimishaji ardhi katika Halmashauri za Mtwara, Magu, Mvomero, Chamwino, Korogwe, Serengeti, Uyui, Sikonge, Unguja na Pemba. Aidha, ufuatiliaji na tathmini utafanyika kwa ajili ya urasimishaji wa biashara katika Halmashauri za Mtwara, Geita, Morogoro, Tanga, Babati, Tabora na Singida;

(ix) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo ya maboresho ya sheria za ardhi na biashara katika Wizara za Kisekta; na

(x) Kuandaa vipindi 20 vya redio na runinga kuhusu utekelezaji wa Shughuli za urasimishaji Tanzania Bara na Zanzibar.

e. MFUKO WA MAENDELEO YA JAMII (TASAF)

**66. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, TASAF imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kufanya utambuzi na uandikishaji wa kaya maskini katika maeneo ya Vijiji 2,072 na Mitaa 1,264 ambayo haikufikiwa katika kipindi cha kwanza cha Mpango. Zoezi hili linategemea kuzifikia kaya za walengwa zipatazo 235,647;

(ii) Kufanya utambuzi na uhakiki wa hali za ustawi wa maisha ya walengwa wa Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini iwapo zimeboreka. Zoezi hili litatoa fursa ya kuwaondoa wale watakaobainika kuwa sio maskini tena kwa vigezo vitakavyotumika kupitia utaratibu wa wazi utakaoandaliwa na kukubalika na wadau katika maeneo husika;

(iii) Kuhawilisha ruzuku kwa kaya maskini ambazo hazitakuwa na uwezo wa kufanya kazi katika Halmashauri 185 Tanzania Bara na wilaya zote Zanzibar;

(iv) Kutoa ajira za muda kwa jumla ya kaya za walengwa 230,000 ambazo zitahusika katika utekelezaji wa miradi 2,500 ya kutoa ajira za muda itakayoibuliwa na jamii. Walengwa hawa watatoka katika Halmashauri 44 pamoja na Unguja na Pemba;

(v) Kuendeleza utekelezaji wa Mkakati na Miongozo ya Kuweka Akiba na Kuwekeza Katika maeneo ya utekelezaji. Wawezeshaji 1,800 katika Halmashauri 72 watapatiwa mafunzo ya kuunda vikundi endelevu vya kuweka akiba kwa kaya za walengwa. Jumla ya vikundi 21,600 vya walengwa vitaundwa, kupewa mafunzo na vitendea kazi;

(vi) Miradi 2,390 katika sekta ya afya, elimu, maji, ujasiriamali na barabara za vijijini itatekelezwa chini ya mpango wa kutoa ajira za muda katika Halmashauri 42 pamoja na Unguja na Pemba;

(vii) Kutoa mafunzo ya namna ya kutekeleza na kusimamia miradi kwa wafanyakazi 6,984 wa Halmashauri na viongozi wa vijiji pamoja na kamati za usimamizi za jamii 24,444;

(viii) Kuongeza wigo kwenye mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya Kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki). Njia hii ya malipo itawezesha fedha kutumwa moja kwa moja kwa mlengwa na kumfikia kwa haraka ambapo gharama za uendeshaji zitapungua kwa kiasi kikubwa;

(ix) Kuimarisha mifumo ya TEHAMA ya utunzaji wa kumbukumbu za walengwa, uendeshaji na utoaji wa taarifa ili kuwezesha utekelezaji wa shughuli za Mpango hususan kuimarisha mawasiliano kati ya maeneo ya utekelezaji na TASAF Makao Makuu Dodoma;

(x) Kujenga uwezo wa watumishi katika ngazi mbalimbali za utekelezaji ikiwa ni pamoja na TASAF Makao Makuu, wataalam wa sekta kutoka kwenye wizara, mikoa, halmashauri na jamii ili kuweza kusimamia na kutekeleza shughuli za Mpango kwa ufanisi;

(xi) Kuimarisha usimamizi, ufuatiliaji na tathmini ya shughuli za Mpango pamoja na matumizi ya rasilimali ili kuongeza ufanisi na uwajibikaji katika ngazi zote za utekelezaji wa Mpango; na

(xii) Kufanya mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na Wadau wa Maendeleo kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini.

#### f. WAKALA YA NDEGE ZA SERIKALI

**67. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Wakala ya Ndege za Serikali imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;



- (ii) Kusimamia mikataba ya ukodishaji wa ndege kwa Kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL);
- (iii) Kufanya matengenezo makubwa ya ndege zinazowahudumia viongozi wakuu wa kitaifa na ununuzi wa vipuri vya ndege za Serikali;
- (iv) Kufanya ukarabati wa karakana ya ndege za Serikali;
- (v) Kulipia gharama za bima za ndege;
- (vi) Kugharamia uendeshaji wa Ofisi na kulipia gharama za mafuta ya ndege; na
- (vii) Kutoa mafunzo kwa wanahewa yanayohusu uhuishaji wa leseni zao.

**68. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 20 Ofisi ya Rais, Ikulu inaomba kiasi cha **Shilingi 24,049,003,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida. Aidha, Fungu 30: Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri inaomba kiasi cha **Shilingi 608,155,446,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 439,935,875,000** ni Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 168,219,571,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### SEKRETARIETI YA MAADILI YA VIONGOZI WA UMMA

**69. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, shughuli zilizopangwa kutekelezwa ni kama ifuatavyo:-

- (i) Kupokea Matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- (ii) Kupokea na kushughulikia malalamiko na taarifa za ukiukwaji wa maadili kutoka kwa wananchi kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma;

(iii) Kuchunguza tuhuma za ukiukwaji wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma dhidi ya Viongozi wa Umma;

(iv) Kufanya uhakiki wa matamko ya Rasilimali na Madeni kwa Viongozi wa Umma 2,000;

(v) Kuratibu na kuwezesha utekelezaji wa majukumu ya Baraza la Maadili ya Viongozi wa Umma;

(vi) Kutoa elimu kwa Viongozi wa Umma na wananchi kuhusu Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma na Hati ya Ahadi ya Uadilifu;

(vii) Kuandaa taarifa ya mwaka ya utekelezaji wa shughuli za Sekretarieti na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(viii) Kufanya utafiti kuhusu hali ya Mgongano wa Maslahi miongoni mwa Viongozi wa Umma;

(ix) Kuanzisha na kuendeleza Klabu za Maadili katika shule na vyuo nchini;

(x) Kuendelea na ujenzi wa Ofisi ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma Makao Makuu Dodoma; na

(xi) Kuimarisha mifumo ya mawasiliano katika kutumia mfumo wa ujazaji wa fomu za matamko ya rasilimali na madeni kwa viongozi wa umma kwa njia ya mtandao kwa kuunganisha mfumo na mifumo mingine ya Serikali.

**70. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inaomba kuidhinishiwa **Shilingi 9,471,110,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 7,621,110,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 1,850,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA TAASISI  
ZILIZO CHINI YAKE

**a. Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

**71. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma katika Mwaka wa Fedha 2020/21 itaendelea kutekeleza majukumu yake ya msingi ya kuhakikisha kuwa Utumishi wa Umma unaendeshwa kwa kuzingatia misingi ya utawala bora na kwamba Sera, Sheria, Kanuni na Taratibu mbalimbali za Utumishi wa Umma zinazingatiwa. Aidha, Ofisi itahakikisha watumishi wa Umma wanawajibika na kuwa wasikivu kwa wananchi wanapotoa huduma mbalimbali.

**72. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma imepanga kutekeleza kazi zifuatazo:-

(i) Kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali katika kuandaa Sera za Kisekta zinazozingatia utafiti ili kuziwianisha na kuondoa migongano na urudufu wakati wa utekelezaji;

(ii) Kufanya mapitio ya Sheria na Miongozo ya kiutumishi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazi;

(iii) Kuhuisha miundo ya Maendeleo ya Utumishi na kuwianisha na kuoanisha viwango vya mishahara katika Utumishi wa Umma kwa kuzingatia matokeo ya zoezi la Tathmini ya Kazi;

(iv) Kufanya ufuatiliaji na kuhamasisha ujumuishwaji wa masuala ya Anuai za Jamii katika Utumishi wa Umma ili kutoa huduma bora kwa wananchi;

(v) Kutoa miongozo ya kuimarisha Menejimenti ya Utumishi Umma kupitia Nyaraka za Kiutumishi;

(vi) Kushughulikia mahitaji ya vibali vya uhamisho, kushikizwa, kuazimwa na likizo bila malipo kwa watumishi na baina ya waajiri mbalimbali katika Utumishi wa Umma;

(vii) Kupokea na kushughulikia mapendekezo ya nafasi za uteuzi, mikataba ya ajira na vibali vya kukaimu nafasi za uongozi kadiri maombi hayo yatakavyokuwa yanawasilishwa na waajiri mbalimbali;

(viii) Kuelimisha watumishi wa Umma na waajiri kuhusu umuhimu wa kupunguza malalamiko ya wateja na kushughulikia ipasavyo malalamiko yanayowasilishwa;

(ix) Kuimarisha upatikanaji wa taarifa (Kanzi data) za Viongozi wa Serikali, Maafisa Waandamizi na Maafisa Daraja I;

(x) Kusimamia ajira za watumishi wa Umma ambapo katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Serikali inatarajia kuajiri watumishi wapya 44,811 wakiwemo wa Kada ya Elimu (13,529), Afya (10,467), Kilimo, Mifugo na Uvuvi (2,145) Jeshi la Polisi (2,725), Magezea (685), Jeshi la Zimamoto (501), Uhamiaji (495) na Hospitali za Mashirika ya Kidini na hiari (1,262).

Aidha, Serikali inatarajia kuajiri watumishi 13,002 wa Kada nyinginezo wakiwemo wahadhiri wa vyuo vikuu vya Umma nchini;

(xi) Kupandisha vyeo watumishi 222,290 wa Kada mbalimbali kulingana na maelekezo yatakayotolewa;

(xii) Kuchambua na kuhakiki madai ya malimbikizo ya mishahara ya watumishi wa Umma 20,027 yenye thamani ya **Shilingi 45,743,803,190.79** na kuchukua hatua ipasavyo;

(xiii) Kuidhinisha taarifa za kiutumishi na mishahara kwenye Mfumo wa Taarifa za Kiutumishi na Mishahara (HCMIS);

(xiv) Kufanya uhakiki wa watumishi kwenye Sekretarieti za Mikoa ili kuhakikisha kunakuwa na matumizi bora ya rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(xv) Kuhakikisha kuwa taarifa za watumishi zinakuwa sahihi na kuboresha taarifa za kiutumishi na mishahara kupitia HCMIS;

(xvi) Kuendesha mafunzo ya namna ya kutumia Mfumo mpya wa HCMIS kwa watumishi wa umma;

(xvii) Kuhuisha miundo na mgawanyo wa majukumu ya Ofisi/Wizara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 100 na kuziwasilisha kwa Mheshimiwa Rais kwa ajili ya kupata idhini ya utekelezaji. Lengo la shughuli hii ni kuongeza ufanisi katika utoaji huduma pamoja na kupunguza ukubwa na matumizi ya Serikali ili fedha zitakazopatikana zielekezwe kwenye miradi ya maendeleo;

(xviii) Kuwezesha Wizara, Idara Zinazojitegemea, Wakala za Serikali na Mashirika ya Umma 20 kuandaa Orodha ya Kazi na Maelezo ya Kazi ili kupata uwiano mzuri wa watumishi katika kutekeleza majukumu ya Taasisi husika;

(xix) Kuboresha michakato ya utoaji huduma na kuimarisha usimamizi wa Mifumo na Viwango vya utendaji kazi kwa kufanya ufuatiliaji pamoja na kutoa ushauri wa kitaalam katika Taasisi za Serikali ili kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma kwa wananchi;

(xx) Kuandaa Mkakati wa Ufuatiliaji na Tathmini wa Kitaifa na kuwezesha utekelezaji wake;

(xxi) Kuandaa Mfumo Jumuishi wa Ufuatiliaji na Tathmini Serikalini kwa kushirikiana na wadau mbalimbali ambao utaunganisha Mifumo ya ufuatiliaji na Tathmini iliyopo katika Taasisi zote za Umma;

(xxii) Kuratibu fursa za mafunzo yanayotolewa na Serikali na Wadau wa Maendeleo;

(xxiii) Kuwezesha Taasisi za Umma 10 kuandaa Mipango ya Rasilimaliwatu, Mipango ya Mafunzo na Urithishanaji wa madaraka;

(xxiv) Kukamilisha na kusambaza Mwongozo wa Kuwezesha Taasisi za Umma Kuandaa Mpango wa Rasilimaliwatu wa muda wa kati na muda mrefu;

(xxv) Kuandaa Mfumo wa Kielektroniki wa Mpango wa Rasilimaliwatu;

(xxvi) Kukamilisha mapitio ya Kanuni za Maadili ya Utumishi wa Umma na kujenga uelewa wa Kanuni hizo kwa wadau;

(xxvii) Kufanya Ufuatiliaji wa Uzingatiaji wa Maadili katika Sekretarieti za Mikoa miwili, Mamlaka za Serikali za Mitaa 10 na Taasisi nyingine za Umma tano;

(xxviii) Kuwezesha uanzishwaji wa Mfumo wa Kushughulikia Malalamiko ya Wananchi katika Utumishi wa Umma kwenye Sekretarieti za Mikoa, Mamlaka za Serikali za Mitaa pamoja na Taasisi nyingine za Umma;

(xxix) Kufanya kampeni za kimaadili kwenye Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xxx) Kufanya uhamasishaji wa uzingatiaji wa maadili kupitia vyombo vya habari;

(xxxi) Kushughulikia malalamiko ya wananchi yanayohusu ukiukwaji wa maadili katika Utumishi wa Umma;

(xxxii) Kuhimiza na kusimamia uanzishwaji wa Kamati za Uadilifu katika Taasisi za Umma;

(xxxiii) Kuratibu uanzishwaji wa vituo vya HUDUMA PAMOJA kwa ajili ya kutolea Huduma za Serikali sehemu moja;

(xxxiv) Kufanya tathmini na kuwajengea uwezo wataalamu wa TEHAMA katika taasisi za Serikali ili kuwawezesha kujenga, kusimamia na kuendeleza mifumo ya TEHAMA ya Serikali;

(xxxv) Kufuatilia uzingatiaji wa mwongozo wa kusimamia utekelezaji wa Serikali Mtandao ya Mwaka 2017 katika taasisi za Serikali;

(xxxvi) Kufanya ukaguzi wa usalama wa mifumo ya HCMIS na e-OPRAS;

(xxxvii) Kujenga uwezo kwa Maafisa TEHAMA na watumishi wengine kuhusiana na Mkakati wa Matumizi ya TEHAMA;

(xxxviii) Kukamilisha maandalizi ya Mpango Mkakati wa Taifa wa utekelezaji wa Serikali Mtandao;

(xxxix) Kuratibu maandalizi ya Kanuni mbalimbali za utekelezaji wa Sheria inayotungwa ya Serikali Mtandao;

(xl) Kuratibu maandalizi na utekelezaji wa Programu ya Dijitali Tanzania;

(xli) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Sera ya Usalama ya Kielektroniki;

(xlii) Kufanya Tathmini ya kina ya Utendaji kazi wa Wakala za Serikali;

(xliii) Kujenga uelewa wa Viongozi wa Kisiasa na Watendaji katika Taasisi za Umma, Menejimenti na watumishi kuhusu Mikataba ya Utendaji Kazi Serikalini;

(xliv) Kuziwezesha Taasisi za Umma kuandaa na kutekeleza Mikataba ya Utendaji Kazi;

(xlv) Kufanya ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi (OPRAS) kwenye Taasisi za Umma;

(xlvi) Kufanya mkutano wa ufuatiliaji na wadau kuhusu majaribio ya utekelezaji wa Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki (e - OPRAS);

(xlvii) Kuwezesha usimamizi, uwekaji na mafunzo ya Mfumo wa Wazi wa Mapitio na Tathmini ya Utendaji Kazi wa Kielektroniki (e - OPRAS) kwa taasisi za umma;

(xlviii) Kuendelea kutoa huduma za kitaalamu katika Usimamizi wa Mikataba ya Utendaji kazi kwa Wizara, Idara

Zinazojitegemea, Mashirika ya Umma, Wakala za Serikali, Sekretarieti za Mikoa na Mamlaka za Serikali za Mitaa;

(xlix) Kutekeleza shughuli za Programu ya Maboresho katika Utumishi wa Umma kwenye maeneo ya matokeo ya Motisha na Uwajibikaji; Michakato ya Utoaji Huduma; na Menejimenti ya Rasimaliwatu;

(l) Kutoa elimu kuhusu majukumu ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora;

(li) Kutoa mafunzo kwa Watumishi wa Umma wanaotarajiwa kustaafu mwaka 2020/21 ili kuwaandaa kwa maisha ya baada ya miaka ya ajira katika Utumishi wa Umma;

(lii) Kujenga nyumba 500 katika mikoa mbalimbali ikiwemo nyumba 300 jijini Dodoma;

(liii) Kuanzisha Mfuko wa Uwekezaji wa “Faida Fund” ambao utawawezesha wafanyakazi, wakulima, wavuvi, wafugaji, wafanya biashara wadogo na wanafunzi kuweka akiba kwa njia ya kununua vipande na kukuza mitaji yao kupitia uwekezaji wenye faida;

(liv) Kutoa huduma ya upimaji ardhi kwa kushirikiana na halmashauri na taasisi za Serikali zenye uhitaji; na

(lv) Kutoa huduma kwa Viongozi Wakuu wa Kitaifa (Wastaafu 11 na wajane 5) kwa mujibu wa sheria.

**b. Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**73. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21 Chuo kinatarajia kutekeleza malengo yafuatayo:-

(i) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya mitihani ya Utumishi wa Umma kwa watumishi 1,115;

(ii) Kutoa mafunzo ya lazima na yanayoombwa na Taasisi za Umma katika kukidhi mahitaji halisi ya watumishi wa umma kulingana na kada zao;



(iii) Kutoa mafunzo yanayoendeleza stadi, weledi na ujuzi wa watumishi wa umma katika masuala ya Uongozi, Menejimenti, Utawala na uendeshaji wa ofisi za Umma kwa Watumishi wa Umma 3,920;

(iv) Kutoa Mafunzo ya Awali katika Utumishi wa Umma kwa watumishi wa Umma 2,540;

(v) Kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa washiriki 13,014 katika fani za Utunzaji wa Kumbukumbu, Uhazili, Kompyuta, Utunzaji wa Fedha za Umma, Menejimenti ya Rasilimaliwatu, Usimamizi wa Ununuzi wa Umma na Uongozi na Utawala Bora;

(vi) Kutoa ushauri wa kitaalam katika maeneo 12 yatakayotoa fursa kwa watumishi wa umma kuboresha mifumo na mbinu za utekelezaji wa majukumu yao kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa umma na wadau mbalimbali kwa lengo la kukuza na kuendeleza uchumi wa Taifa letu;

(vii) Kufanya utafiti wa mahitaji halisi ya Menejimenti ya Utumishi wa Umma na kusambaza matokeo ya utafiti huo kwa lengo la kukuza weledi na ufanisi wa utendaji kazi kwa watumishi wa umma;

(viii) Kuwezesha mafunzo ya muda mrefu kwa watumishi nane wa Chuo cha Utumishi wa Umma katika ngazi zifuatazo; watumishi watano Shahada ya Uzamivu na watatu Shahada ya Uzamili;

(ix) Kuanza ujenzi wa majengo yatakayotumika kwa ajili ya madarasa, maktaba na ofisi katika Kampasi za Singida na Tanga;

(x) Kuandaa michoro ya usanifu majengo kwa ajili ya mradi wa ujenzi wa majengo ya Kampasi ya Mwanza eneo la Lucheleele;

(xi) Kutafuta eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kampasi ya Mbeya;

(xii) Kutoa mafunzo yanayotoa fursa kwa watumishi wa Umma kuongeza stadi, weledi na ujuzi katika matumizi ya Teknolojia;

(xiii) Kutoa mafunzo yanayolenga kubadilishana uzoefu kuhusu utawala na menejimenti ya utumishi wa Umma kwa mujibu wa mahitaji halisi ya utumishi wa Umma na wadau wengineo;

(xiv) Kutoa mafunzo kwa watumishi wa Umma yanayolenga kuwaunganisha na kubadilishana uzoefu wa wataalamu wa kimataifa katika matumizi ya mifumo ya mawasiliano kwa njia ya mtandao katika utoaji wa huduma ndani na nje ya nchi;

(xv) Kuendesha mafunzo kwa njia ya mtandao ili kusaidia Serikali kupunguza gharama, kuwa na mazingira rafiki katika kujifunza, kutoa fursa ya kuepuka muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi, kupunguza safari nje ya mahali pa kazi na kuepuka kuwa mbali na familia; na

(xvi) Kukuza Sera za Serikali za utamaduni wa kujifunza na kusaidia utumiaji wa Teknolojia miongoni mwa watendaji katika kutelekeza majukumu yao kwa lengo la kukuza uchumi na kuleta maendeleo nchini.

#### c. Mamlaka ya Serikali Mtandao (e-GA)

**74. Mheshimiwa Spika**, Katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Mamlaka ya Serikali Mtandao inatarajia kutelekeza kazi zifuatazo:-

(i) Kusanikisha katika taasisi za umma, Mfumo Shirikishi wa Kusimamia Shughuli na Rasilimali za Taasisi;

(ii) Kuhuisha na kutelekeza Mifumo Shirikishi ya TEHAMA ikiwemo Mfumo wa Kutoa Huduma kwa Njia ya Simu za Mkononi kwa Taasisi za Umma; Mfumo wa Vibali vya Kusafiria Nje ya Nchi, Mfumo wa Masijala na Mfumo wa Barua Pepe wa Serikali;

(iii) Kuendelea na uimarishaji wa usalama wa mifumo ya TEHAMA;

(iv) Kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kubadilishana taarifa;

(v) Kuimarisha Vituo vya Kuhifadhi Taarifa na Mifumo ya TEHAMA ya Serikali na Kujikinga na Majanga ili kuongeza usalama wa mifumo na taarifa za Serikali na kupunguza gharama ya kuhifadhi rasilimali shirikishi miongoni mwa Taasisi za Umma;

(vi) Kusimamia na kuimarisha usalama wa Mtandao wa Mawasiliano Serikalini;

(vii) Kutoa mafunzo ya Serikali Mtandao kwa Viongozi, Wasimamizi wa TEHAMA na watumiaji wa huduma za Serikali Mtandao kwa Taasisi za Serikali ili kuongeza uelewa na uwezo wa Taasisi za Umma katika kutumia TEHAMA na kuongeza ufanisi wa kiutendaji na utoaji wa huduma kwa wananchi;

(viii) Kutoa ushauri wa kitaalam na msaada wa kiufundi kwa taasisi za Umma katika utekelezaji wa serikali mtandao;

(ix) Kutoa elimu kwa Umma kuhusu utekelezaji wa sheria ya serikali mtandao pamoja na sheria na kanuni zake; na

(x) Kuwajengea uwezo watumishi wa mamlaka kwa kuwapatia mafunzo mbalimbali yanayoendana na taaluma zao ili kuboresha utekelezaji wa majukumu yao ya kazi.

**75. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 32 Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma inaomba kiasi cha **Shilingi 43,878,828,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 32,923,578,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 10,955,250,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

SEKRETARIETI YA AJIRA KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**76. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma, imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

(ii) Kushiriki kama wataalam waalikwa kwenye usaili unaoendeshwa na taasisi zinazotumia Sheria zilizokasimiwa kwa taasisi husika;

(iii) Kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar ili kurahisisha michakato ya ajira kwa ajira za Muungano;

(iv) Kuhamisha watumishi wa Ofisi kutoka Dar es Salaam kwenda Makao Makuu Dodoma;

(v) Kufanya utafiti kwa waajiri na wadau mbalimbali ikiwa ni hatua ya kupata mrejesho wa utekelezaji wa shughuli za uendeshaji wa michakato ya ajira pamoja na utendaji kazi wa Ofisi;

(vi) Kuimarisha utendaji kazi wa taasisi kwa kutumia TEHAMA;

(vii) Kuboresha mifumo ya uendeshaji wa usaili kwa kutumia mbinu za kisasa, ikiwemo matumizi ya "psychometric test";

(viii) Kutoa taarifa na elimu kwa Umma ili kukuza uelewa kuhusu shughuli zinazotekelezwa na Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;

(ix) Kuhakiki vyeti vya waombaji kazi na kupata taarifa nyingine muhimu ili kupunguza kesi zinazotokana na kugushiwa kwa vyeti; na

(x) Ununuzi wa vitendea kazi hususani magari ili kusaidia utekelezaji wa majukumu ya Taasisi kwa wakati.

**77. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha wa 2020/21, Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 3,360,526,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

#### OFISI YA RAIS, TUME YA UTUMISHI WA UMMA

**78. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Tume imepanga kutekeleza majukumu yafuatayo:-

(i) Kukagua taasisi (Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu) 160 katika Ukaguzi wa Kawaida na Ukaguzi Maalum kwa taasisi 10 ili kuangalia uzingatiaji wa Sheria, Kanuni, Miongozo na Taratibu za usimamizi wa Rasilimaliwatu katika Utumishi wa Umma;

(ii) Kufanya mikutano ya Kisheria ya Tume ili kujadili na kutolea uamuzi rufaa na malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakvoyopokelewa;

(iii) Kuhuisha Miongozo ya Tume ya uzingatiaji wa masuala ya Ajira na Nidhamu na kuisambaza kwa Waajiri, Mamlaka za Ajira na Nidhamu;

(iv) Kuelimisha taasisi za Umma na watumishi wa Umma kuhusu majukumu ya Tume na utekelezaji wa Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya Utumishi wa Umma kupitia, ziara za Makamishna, vikao vya kazi, vyombo vya habari, machapisho na Tovuti;

(v) Kuandaa Taarifa ya Hali ya Utumishi wa Umma na Utekelezaji wa Majukumu ya Tume kwa kipindi cha Mwaka wa Fedha 2019/20 na kuiwasilisha kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania;

(vi) Kutoa huduma kwa watumishi wa Tume wenye mahitaji maalum; na

(vii) Kutoa elimu kwa watumishi wa Tume kuhusu VVU, UKIMWI, Magonjwa Sugu Yasiyoambukiza na mapambano dhidi ya rushwa.

**79. Mheshimiwa Spika**, ili kutekeleza Mpango wa Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 94, Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 5,231,094,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

BODI YA MISHAHARA NA MASILAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA

**80. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma (Fungu 09) inatarajia kutekeleza majukumu kama ifuatavyo:-

(i) Kufanya utafiti kuhusu utekelezaji wa Mfumo wa Jumla wa Kimenejimenti wa Motisha katika Utumishi wa Umma ili kuishauri Serikali juu ya mfumo huo;

(ii) Kufanya utafiti kuhusu mazingira magumu ya kazi;

(iii) Kuandaa taarifa ya gharama ya maisha kila robo mwaka na kushauri juu ya gharama za chini za maisha;

(iv) Kukusanya na kuchambua taarifa za misingi ya kuzingatiwa katika kutoa masilahi na ushauri wa mwongozo wa kuzingatiwa wakati wa kutoa masilahi.

**81. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 9: Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 1,445,945,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida.

OFISI YA RAIS, IDARA YA KUMBUKUMBU NA NYARAKA ZA TAIFA

**82. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Sheria ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa Na. 3 ya mwaka 2002, Idara ya Kumbukumbu ya Nyaraka za Taifa imepewa jukumu la kusimamia na kuratibu utekelezaji wa Sera, Sheria, Kanuni

na Taratibu za utunzaji kumbukumbu na nyaraka katika Taasisi za Umma. Aidha, Idara ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa Sheria ya Kuwaenzi Waasisi wa Taifa Na. 18 ya Mwaka 2004 katika kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa letu (Mwalimu Julius Kambarage Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume).

**83. Mheshimiwa Spika**, katika Mwaka wa Fedha 2020/21, Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa itatekeleza shughuli zifuatazo:-

(i) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya Nchi yetu kutoka taasisi za Umma, taasisi na watu binafsi;

(ii) Kutambua, kukusanya, kutunza na kuhifadhi kumbukumbu na vitu vya Waasisi wa Taifa;

(iii) Kuimarisha Vituo vya Kanda kwa lengo la kuongeza uwezo wa Idara katika ukusanyaji na utunzaji wa kumbukumbu na nyaraka;

(iv) Kuweka na kuhuisha mifumo ya utunzaji wa kumbukumbu katika Taasisi za Umma ili kuongeza ufanisi na tija katika utoaji wa huduma Serikalini;

(v) Kuimarisha mifumo ya kielektroniki katika usimamizi wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za taifa kwa ajili ya kuhifadhi kumbukumbu na nyaraka katika teknolojia ya kisasa ili kurahisisha upatikanaji na kulinda nakala halisi;

(vi) Kusaidia taasisi za umma kutengeneza miongozo ya kuhifadhi na kuteketeza kumbukumbu pamoja na kufanya tathmini ya kumbukumbu tuli za taasisi za umma zilizohifadhiwa katika Kituo cha Taifa cha Kumbukumbu Dodoma;

(vii) Kujenga uwezo wa taasisi za Umma katika usimamizi wa kumbukumbu na nyaraka za Serikali kwa kuandaa mikutano kazi kwa menejimenti za taasisi za Umma na mafunzo kazi

kwa Waratibu na Watunza kumbukumbu kuhusu Sheria, Kanuni, Taratibu na Miongozo ya utunzaji wa taarifa, kumbukumbu na nyaraka za Serikali;

(viii) Kutoa elimu kwa wananchi kuhusiana na umuhimu wa utunzaji na uhifadhi wa kumbukumbu na nyaraka za Taifa pamoja na shughuli za Idara; na

(ix) Kuimarisha uwezo wa utendaji wa Watumishi wa Idara.

**84. Mheshimiwa Spika**, katika kutekeleza majukumu yake kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, Fungu 4: Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa inaomba kuidhinishiwa kiasi cha **Shilingi 4,564,368,000** kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na Miradi ya Maendeleo. Kati ya fedha hizi, **Shilingi 2,564,368,000** ni kwa ajili ya Matumizi ya Kawaida na **Shilingi 2,000,000,000** kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo.

#### C. MAJUMUISHO

**85. Mheshimiwa Spika**, Kwa kuwa hii ni bajeti ya mwisho ya kipindi cha Awamu ya Tano, hatuna budi kujivunia mafanikio ambayo Ofisi yangu imeyapata. Miongoni mwa masuala ambayo Serikali ya Awamu ya Tano iliahidi kuyashughulikia ni suala la watumishi hewa na wenye vyeti feki ambapo watumishi wapatao 19,708 waliondolewa na kiasi cha **Shilingi Bilioni 19.84** kwa mwezi kuokolewa.

**86. Mheshimiwa Spika**, Katika kipindi hiki, kodi ya Mshahara kwa watumishi wa Umma (PAYE) ilipunguzwa hadi tarakimu moja kwa kima cha chini kutoka asilimia 11 hadi asilimia 9 ikiwa ni utekelezaji wa ahadi za Ilani ya CCM ya Uchaguzi ya Mwaka 2015. Ofisi yangu pia, ilihakikisha kuwa nidhamu ya utendaji kazi na maadili ya watumishi wa Umma vinaimarishwa. Vile vile, watanzania wameshuhudia jinsi masuala ya rushwa na uhujumu uchumi yalivyoshughulikiwa kwa mafanikio makubwa ili kulinda rasilimali za Umma.

**87. Mheshimiwa Spika**, Suala jingine ambalo Serikali ya Awamu ya Tano iliahidi kulisimamia ni suala la ukusanyaji wa



mapato ya Serikali. Ofisi yangu, kwa kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango, imeimarisha na kujenga mifumo ukiwemo Mfumo Mkuu wa Kielektroniki wa Ukusanyaji wa Mapato Serikalini "Government e-Payment Gateway – GePG". Mifumo hii imesaidia sana kurahisisha ukusanyaji wa mapato, kuziba mianya ya upotevu wa fedha za umma na kuwezesha ongezeko la ukusanyaji wa mapato katika sekta mbalimbali za Serikali kuanzia Serikali Kuu hadi Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**88. Mheshimiwa Spika,** Katika kufanikisha ongezeko la matumizi ya Serikali Mtandao isiyokuwa na urudufu na kufanikisha azma ya Serikali ya kutumia Serikali Mtandao kwa asilimia 100 ifikapo Mwaka 2025, Ofisi yangu imewezesha utungwaji wa Sheria ya Mamlaka ya Serikali Mtandao ili kuipa nguvu taasisi ya awali katika kuratibu, kusimamia na kukuza jitihada za Serikali mtandao.

**89. Mheshimiwa Spika,** Baada ya kueleza baadhi ya mafanikio turejee kuwa Utumishi wa Umma ni mtambuka na endelevu kwa maana ya menejimenti yake na utawala bora hivyo unatarajiwa kuendelea kuwa nguzo muhimu katika uendeshaji wa nchi katika kipindi cha mwaka 2020/21 na hivyo kutoa mchango mkubwa sana katika utulivu wa nchi yetu na maendeleo tunayodhamiria kuelekea kwenye nchi ya uchumi wa kipato cha kati ifikapo mwaka 2025. Aidha, maendeleo hayo yanatarajiwa kupatikana kwa kuimarisha uchumi wa viwanda kama inavyowekwa wazi katika Mpango wa Pili wa Maendeleo wa Miaka Mitano.

**90. Mheshimiwa Spika,** kama nilivyoeleza katika utangulizi wa Hotuba yangu, mwaka huu wa 2019/20, tunakamilisha kipindi cha Bunge la 11, hivyo hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutupa nguvu na afya katika kutekeleza majukumu yetu kwa kipindi chote. Aidha, sote tunatambua kuwa mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi Mkuu ambapo wengi wetu tunatarajia kwenda kwa wananchi kuomba ridhaa yao ya kuwawakilisha kwa miaka mingine mitano. Ninawaomba nyote kwa Mwenyezi Mungu ili sote tutakaogombea tena tushinde katika majimbo yetu kwa

kishindo na hatimaye tuendelee kukamilisha kazi iliyoanzishwa na Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais Dkt. John Joseph Pombe Magufuli.

**91. Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa miundo na mgawanyo wa majukumu kwa mawaziri, utekelezaji wa Ofisi yangu kwa ujumla unajumuisha, Ofisi ya Rais Ikulu; Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora; Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma; Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma; Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na Ofisi ya Rais, Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa.

**92. Mheshimiwa Spika**, Mipango na Bajeti kwa Mafungu niliyoyataja yamezingatia vipaumbele vya Serikali ya Awamu ya Tano kwenye eneo la kuimarisha utendaji kazi wa Utumishi wa Umma na kuifanya nchi yetu iondokane na matumizi mabaya ya rasilimali fedha, ukiukwaji wa maadili ya uongozi na kupunguza urasimu usio wa lazima katika utoaji huduma na hivyo kuongeza tija katika kutekeleza masuala yenye masilahi mapana kwa Taifa letu.

**93. Mheshimiwa Spika**, Bajeti ya Mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora imelenga kuwa na Utumishi wa Umma unaotoa huduma bora kwa haraka na staha, kuzingatia Katiba, Sera, Sheria, Kanuni, Miongozo na taratibu ili kujenga imani zaidi kwa wananchi. Katika kuendana na wakati jitihada zaidi zitawekwa kwenye kujenga uwezo na mifumo ya kimenejimenti na utoaji huduma ikiwemo matumizi sahihi na salama ya fursa zinazopatikana katika utoaji huduma kwa TEHAMA ndani ya Serikali.

**94. Mheshimiwa Spika**, baada ya kueleza kwa kina utekelezaji wa majukumu kwa Mwaka wa Fedha 2019/20 na Mipango na Bajeti ya Ofisi ya Rais, Ikulu na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, naomba sasa, kuwasilisha rasmi

mapendekezo ya maombi ya Ofisi yangu kwa Mwaka wa Fedha 2020/21 kwa muhtasari kama ifuatavyo:-

**a. Fungu 20: Ofisi ya Rais, Ikulu**

i. Matumizi ya Kawaida Sh. 24,049,003,000  
Jumla Sh. 24,049,003,000

**b. Fungu 30: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri**

i. Matumizi ya Kawaida Sh. 439,935,875,000  
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 168,219,571,000  
Jumla Sh. 608,155,446,000

**c. Fungu 33: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma**

i. Matumizi ya Kawaida Sh. 7,621,110,000  
ii. Matumizi ya Miradi ya Maeneleo Sh. 1,850,000,000  
Jumla Sh. 9,471,110,000

**d. Fungu 32: Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma**

i. Matumizi ya Kawaida Sh. 32,923,578,000  
ii. Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 10,955,250,000  
Jumla Sh. 43,878,828,000

**e. Fungu 67: Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma**

i. Matumizi ya Kawaida Sh. 3,360,526,000  
Jumla Sh. 3,360,526,000

**f. Fungu 94: Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma**

Matumizi ya Kawaida Sh. 5,231,094,000  
Jumla Sh. 5,231,094,000

g. Matumizi ya Kawaida Sh.1,445,945,000  
Jumla Sh. 1,445,945,000

**Fungu 09: Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma**

**h. Fungu 04: Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa**

Matumizi ya Kawaida Sh. 2,564,368,000  
Miradi ya Matumizi ya Maendeleo Sh. 2,000,000,000  
Jumla Sh. 4,564,368,000

**95. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge**, Jumla kuu ya Bajeti ninayoomba kwa mafungu yote yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mwaka wa Fedha 2020/21, ni kama ifuatavyo:-

Matumizi ya Kawaida Sh. 517,131,499,000  
Matumizi ya Miradi ya Maendeleo Sh. 183,024,821,000  
Jumla Sh. 700,156,320,000

**96. Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge**, mwisho naomba kuwasilisha maombi haya ili muweze kuyajadili na kuyaidhinisha.

**97. Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa hoja.

*Kapt. (Mst.) George H. Mkuchika (Mb.)*

**WAZIRI WA NCHI – OFISI YA RAIS (MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA)**

**WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:**

Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na hoja imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora, Mheshimiwa Kapt. Mstaafu George Mkuchika. Ahsante sana kwa kuwasilisha hoja yako vizuri kwa

maelezo fasaha kabisa ambapo umeliomba Bunge likubali kujadili na kupitisha bajeti unayoipendekeza kwa mwaka wa fedha unaokuja 2020/2021. Ahsante sana.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, katika kuendelea kuboresha shughuli zetu, tunataka tu-*test* mitambo kidogo leo. Kwa hiyo, nitaomba msemaji anyefuata ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati wa Kamati ya Kudumu ya Utawala na Serikali za Mitaa, Mheshimiwa Dkt. Rweikiza awasilishe taarifa ya Kamati yake kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa Fedha 2019/2020, pamoja na maoni ya Kamati hiyo kuhusu Makadilio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021 kwa dakika 20, lakini sasa tumsikilize akituhutubia kutoka ukumbi wa Msekwa. Mheshimiwa Dkt. Rweikiza, endelea.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:**

Mheshimiwa Spika, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 fasili ya (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, vifungu vya 6 (4)(a) na 7 (1)(a) vya Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kimeipa Kamati hii majukumu ya shughulikia bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejementi ya Utumishi Umma na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi hii ya maendeleo katika Mikoa ya Singida na Manyara, iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha katika Mwaka wa Fedha 2019/2020 kuanzia tarehe 11 hadi 15 Machi, 2020. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa bajeti ya

Ofisi hii ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 16 na 17 Machi, 2020.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina mafungu nane ya bajeti kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa pili wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

(i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;

(ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa Mwaka wa Fedha, 2019/2020;

(iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021; na

(iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

Mheshimiwa Spika, Matokeo ua Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha kwa mwaka wa fedha 2019/2020. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa kiasi cha shilingi bilioni 198.4 kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu manne kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa nne wa taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, miradi ya maendeleo iliyotembelewa na kukaguliwa na Kamati hii inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii *TASAF*, mpango wa kurasimisha rasilimali na biashara za wanyonge (MKURABITA) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (*TPSC*). Ufafanuzi wa miradi hiyo inapatikana katika ukurasa wa tano hadi ukurasa wa 15 wa taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, maoni na jumla kuhusu utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inapenda kutoa maeneo yafuatayo:-

(i) Mpango wa Ruzuku wa Kaya Maskini umesaidia wasichana balehe na wanawake vijana kujipatia taulo za kike;

(ii) Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Maskini umesaidia kuboresha maisha ya wanufaika kwa kuwawezesha kumudu gharama mbalimbali za maisha;

(iii) Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Maskini umesaidia kuboresha mahudhurio ya watoto shuleni katika Vituo vya Afya;

(iv) Mpango wa Ruzuku kwa Kaya Masikini umechochea utamaduni wa Kaya masikini kujiwekea akiba na kupata elimu ya masuala ya fedha na uendeshaji wa biashara ndogo ndogo;

(v) Kituo cha Pamoja cha Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara kiwezeshe kuwa na wataalamu siku zote za kazi ili kiweze kuhudumia wafanyabiashara muda wote;

(vi) Bajeti finyu ya maendeleo kwa *MKURABITA* inaathiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha shughuli za urasimishaji;

(vii) Serikali ikiwezeshe Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida kujenga majengo yake katika eneo la Mungumaji na hivyo kuokoa gharama zinazotumika kwa ajili ya kodi ya pango; na

(viii) Serikali ikipatie Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida Watumishi wa kudumu na vitendea kazi ili kuboresha utendaji na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti na Uzingatiaji wa Mapendekezo ya Kamati kwa mwaka wa fedha 2019/2020. Uchambuzi wa Kamati katika Mapitio na Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa. Njia zilizotumika na Kamati wakati wa uchambuzi ni pamoja na kuangalia hali halisi, kwa kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. Uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kiasi kilichotolewa na Hazina, kwani:-

- (i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ukilinganisha na mpango wa upatikanaji wa Fedha (*cash flow plan*);
- (ii) Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo (Matumizi ya kawaida asilimia 70.9 na Maendeleo asilimia 44.8); na
- (iii) Fedha hazipatikani kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa Fedha zilizopokelewa na mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoka Hazina hadi kufikia mwezi Februari, 2020 ambayo ni robo ya tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020 na kiasi ambacho kilichoidhinishwa.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi zaidi umebainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Ofisi hii pamoja na mafungu hayo yaliyo chini yake ilikuwa imepokea shilingi



bilioni 832 .96 kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Maendeleo kiasi hicho ni sawa na asilimia 63.35 ya Fedha iliyoidhinishwa na Bunge. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa takribani shilingi bilioni 58.3 sawa na Asilimia 15.5 ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambacho kilikuwa ni Shilingi bilioni 374.7.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa fedha za Maendeleo uchambuzi umeonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari, 2020 Ofisi ya hii na mafungu yake ilikuwa imepokea shilingi bilioni 86.6 kutoka hazina sawa na asilimia 44.8 ya fedha yote iliyodhinishwa na Bunge kwa ajili ya Maendeleo. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa asilimia 9.25 ikilinganishwa na shilingi bilioni 82 zilizopokelewa kwa ajili ya maendeleo katika kipindi kama hicho cha mwaka wa fedha 2018/2019.

Mheshimiwa Spika, aidha uchambuzi wa jumla umebaini kwamba mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani asilimia 63 ya fedha zote zilizoidhinishwa. Vilevile, katika kipindi hicho jumla ya shilingi bilioni 343.3 zilikuwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia 71 ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Kiasi cha fedha kilichopokelewa kimeongezeka kwa asilimia 17.3 ikilinganishwa na shilingi bilioni 292.7 zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi kama hicho katika mwaka wa Fedha 2018/2019. Hali hiyo imeonesha kuwa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kinachotolewa na Hazina kimeendelea kuwa kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Mwenendo huu umeshuhudiwa katika miaka minne ya fedha mfululizo tangu mwaka 2016/2017 hadi 2019/2020.

Mheshimiwa Spika, mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati, wakati wa kupitia na kuchambua bajeti Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka 2019/2020. Kamati ilitoa maoni na ushauri katika mambo kumi na tatu (13) kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi. Uzingatiaji

wa maoni na ushauri huo ni kama inavyoonekana kwenye ukurasa wa 20, 21 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, Uchambuzi wa Mpango wa Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Taarifa ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora unajumuisha Mafungu Nane fungu namba 04, 09, 20, 30, 32, 33, 67 na 94 na umeandaliwa kwa kuzingatia:-

- (i) Mpango wa Maendeleo wa miaka Mitano;
- (ii) Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala;
- (iii) Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021; na
- (iv) Maeneo muhimu ya kuzingatia kama ilivyoaunishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Mheshimiwa Spika, aidha, Ofisi hii pamoja na Mafungu yake imepanga kutekeleza jumla ya Malengo 174 kwa mwaka ujao wa fedha, malengo hayo yameoneshwa katika ukurasa wa 22 – 25 wa Taarifa ya Kamati.

Mheshimiwa Spika, ili kutekeleza malengo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishwa jumla ya shilingi bilioni 699.69 kati ya fedha hizo shilingi bilioni 517.1 kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na shilingi bilioni 182.8 ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida Shilingi bilioni 39.2 sawa na asilimia 5.5 ni kwa ajili ya Mishahara na Shilingi bilioni 477.9 sawa na asilimia 68.2 ni kwa ajili ya matumizi mengineyo.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti iliyoombwa kuidhinishwa kwa mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa shilingi bilioni 16.4 sawa na asilimia 2.4 ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/

2020 ambayo ilikuwa shilingi bilioni 683.53. Aidha, kwa upande wa fedha za matumizi ya kawaida katika mwaka ujao wa fedha uchambuzi umebaini kwamba zimeongezeka kwa kiasi cha shilingi bilioni 33.4 ambacho ni sawa na asilimia 6.9 ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa shilingi bilioni 483.6.

Mheshimiwa Spika, vile vile Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kiasi cha Fedha za Miradi ya Maendeleo kinachoombwa kimepungua kwa shilingi bilioni 17 sawa na Asilimia 8.5 ilinganishwa na fedha za miradi ya Maendeleo zilizo dhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/2020 ambazo zilikuwa shilingi bilioni 169.8.

Mheshimiwa Spika, uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021. Uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021. Uchambuzi umelenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

(i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo ni shilingi bilioni 695.5 ni sawa na asilimia 2.01 ya Bajeti yote ya Serikali. Ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo ni shilingi trilioni 34.876;

(ii) Mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 unaonesha ongezeko la bajeti kwa asilimia 5.36 ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa 2019/2020 wakati Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021

imeongezeka kwa asilimia 2.4 ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa kwa mwaka wa fedha 2019/2020; na

(iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia 5.3 katika fedha za Maendeleo ambazo ni sawa asilimia 36.9 ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021; hili hali bajeti ya Maendeleo ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora ambayo ni asimilia 2.01 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa Asilimia 2.4 ikilinganisha na Mwaka wa fedha 2020/2021. Ufafanuzi zaidi unaoneshwa kupitia jedwali la chati mraba kama inavyoonekana kwenye taarifa hii.

Mheshimiwa Spika, Maoni na Ushauri wa Kamati, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo, taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha, Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iangalie namna ya kutatua changamoto ya upungufu wa watumishi wa umma haswa wa kada za Afya na Elimu ambayo kwa sehemu kubwa imechangiwa na watumishi wengi kuondolewa kazini baada ya kubainika kutumia vyeti vya kughushi;

(ii) Serikali iongeze mshahara kwa watumishi wa umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zimeongezeka mara kwa mara. Aidha, hali hiyo imechangia watumishi kukosa ari ya utendaji na kuishia kulalamika kuwa maisha yamekuwa ghali;

(iii) Serikali ichukue hatua ili kuondoa ucheleweshaji wa Watumishi wa Umma kupanda madaraja na kubadilisha Mishahara, hali ambayo imesababisha baadhi yao kustaafu bila kupata stahiki na haki zao za haki;

(iv) Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali kupitia Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) za kushughulikia Rushwa kubwa ambapo watuhumiwa

wamekamatwa na kushitakiwa katika vyombo vya Sheria. Hata hivyo Kamati inashauri juhudi hizi ziongezwe hasa katika kupambana na Rushwa ya Ngoni ambayo imekuwa ikilalamikiwa kushamiri katika Taasisi za Elimu, sehemu za kazi na maeneo mengine ya jamii;

(v) Serikali ihakikishe halmashauri zinawatumia kikamilifu Maafisa Maendeleo ya Jamii, na Maafisa Ustawi wa jamii kwa ajili ya kuwaelimisha na kuwasimamia wanufaika wa mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini ili kuhakikisha wanaelekeza sehemu za ruzuku wanazopata kwenye shughuli za kiuchumi ili kuondokana na umaskini;

(vi) Serikali ihakikishe inatumia kikamilifu fedha ilizozipata kwa ajili Utekelezaji wa Awamu ya II ya Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini kwa kuyafikia maeneo yote yaliyobaki (Vijiji/Mtaa/Shehia 5,693) ili kuwapa wananchi wa maeneo hayo fursa ya kunufaika na mpango;

(vii) *TASAF* iongeze wigo kwenye mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya Kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki), ili kuharakisha na kurahisisha malipo kumfika mlengwa moja kwa moja;

(viii) Serikali iongeze kiasi kinachoingia katika utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini, kwani bado mchango wake ni mdogo sana. Tangu mpango huu ulipoanza mwaka wa fedha 2013/2014, hadi taarifa hii inaandaliwa Serikali imechangia shilingi bilioni 8.12 tu kati ya shilingi bilioni 70 ilizopaswa kuchangia, sawa asilimia 11.5 kwa ufafanuzi ufuatao; Serikali ihakikishe halmashauri zote nchini zinashirikiana na Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) ili ziweze kuanzisha (*One Stop Business Formalization and Development Centre*) kwa ajili ya kusaidia kurahisisha urasimishaji na uendelezaji wa biashara kwa kupunguza gharama na muda;

(ix) Serikali ihakikishe Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inatoa mafunzo kwa Viongozi wa Umma

wanaoteuliwa katika nyadhifa mbalimbali kabla hawajaanza kutekeleza majukumu yao;

(ix) Serikali ikiwezeshe Chuo cha Utumishi wa Umma kujenga majengo yake katika eneo la Mungumaji – Manispaa ya Singida ili kuwezesha Kampasi ya Singida kuwa na majengo yake na hivyo kuokoa gharama nyingi zinazotumika kwa ajili ya kulipa kodi ya pango.

Mheshimiwa Spika, hitimisho, nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Mheshimiwa Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kufikia Taarifa hii. Kwa kutambua kuwa hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati katika Bunge hili la Kumi na Moja, nitumie fursa hii kuwatajia Wajumbe wa Kamati pamoja na Wabunge wengine wote kila la kheri katika uchaguzi ujao na Mwenyezi Mungu atujaalie turejee sote katika Bunge lijalo ili tuendeleze gurudumu la ujenzi wa Taifa letu kwa kutimiza wajibu wetu wa kikatiba wa kuwakilisha wananchi na kuisimamia Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu wao ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati hiyo kwa kuwataja majina yao. Hata hivyo kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe katika Kumbukumbu za Rasmi za Bunge *(Hansard)*.

Mheshimiwa Spika, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mheshimiwa Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb)...

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Rweikiza tunakushukuru, malizia hotuba yako.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha kwa Kamati.

**SPIKA:** Malizia hotuba yako.

**MHE. JASSON S. RWEIKIZA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Spika, nawashukuru pia Watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Laurean Ndumbaro (Utumishi), na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Dkt. Fransic Michael kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya Bajeti hii. Aidha, nawashukuru kwa dhati kabisa Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyopo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao na utekelezaji makini wa bajeti kwa mwaka wa fedha unaisha.

Mheshimiwa Spika, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge ndugu Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi, Ndg. Gerlad Magili, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima, Ndg. Asmin Kihemba na Ndg. Prosper Minja wakisaidiwa na Ndg. Kokuwaisa Gondo kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali. Naomba kuwasilisha na ninaunga mkono hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA KUHUSU UTEKELEZAJI WA BAJETI YA OFISI YA RAIS,  
MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALABORA  
KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020 PAMOJA NA MAONI  
YA KAMATI KUHUSU MAKADIPIO YA MAPATO NA MATUMIZI  
KWA OFISI HIYO KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021 –  
KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

---

**1.1 UTANGULIZI**

**Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Kanuni ya 99 (9) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kuhusu utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2019/2020, pamoja na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa Fedha 2020/2021.

Kifungu cha 6 (4)(a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, kimeipa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa jukumu la kusimamia shughuli za Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora.

Aidha, Kifungu cha 7(1) (a) cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kinatoa wajibu kwa Kamati zote za Kisekta kushughulikia bajeti za Wizara zinazozisimamia. Jukumu hili la uchambuzi wa bajeti ambalo hutekelezwa kwa mujibu wa Kanuni ya 98 (2) ya Kanuni za Bunge, hutanguliwa na jukumu la ukaguzi wa miradi ya maendeleo iliyotengewa fedha katika mwaka wa fedha unaoisha kwa mujibu wa Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Bunge.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa taarifa kwamba Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, ilifanya ziara za ukaguzi wa miradi ya maendeleo katika mikoa ya Singida na Manyara, iliyotengewa na kupokea fedha katika mwaka wa fedha 2019/2020 kuanzia tarehe 11 hadi 15 Machi, 2020. Kamati pia ilifanya uchambuzi wa Bajeti ya



Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora tarehe 16 na 17 Machi, 2020.

Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ina Mafungu Nane (8) ya bajeti kama ifuatavyo:-

- i) **Fungu 20:** Ofisi ya Rais, Ikulu;
- ii) **Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- iii) **Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
- iv) **Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- v) **Fungu 67:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- vi) **Fungu 94:** Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
- vii) **Fungu 09:** Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma; na
- viii) **Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa

**Mheshimiwa Spika**, taarifa hii inatoa maelezo kuhusu maeneo manne yafuatayo:-

- i) Matokeo ya Ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotembelewa na Kamati;
- ii) Mapitio ya Taarifa ya Utekelezaji wa Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2019/2020;
- iii) Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi hii kwa mwaka wa Fedha 2020/2021; na
- iv) Maoni na Ushauri wa Kamati.

## **2.1 MATOKEO YA UKAGUZI WA MIRADI YA MAENDELEO ILIYOTENGEWA FEDHA KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

### **2.2 Ufafanuzi wa Miradi ya Maendeleo iliyotengewa fedha na kukaguliwa**

**Mheshimiwa Spika**, katika mwaka wa fedha 2019/2020, Ofisi ya Rais , Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora ilitengewa kiasi cha Tsh **198,389,120,525/=** kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo kupitia mafungu manne (4) kama ifuatavyo:-

**i) Fungu 30:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri - Tshs **154,189,384,717/=**;

**ii) Fungu 32:** Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma - Tshs. **41,060,000,000/=**;

**iii) Fungu 33:** Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma – Tshs. **1,139,735,808/=**; na

**iv) Fungu 04:** Ofisi ya Rais, Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa – Tshs.**2,000,000,000/=**.

**Mheshimiwa Spika**, katika kuzingatia masharti ya Kanuni ya 98(1) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari 2016, Kamati ya Utawala na Serikali za Mitaa ilitembelea baadhi ya miradi iliyotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Miradi iliyotembelewa inahusu Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF); Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania (TPSC). Ufafanuzi wa miradi hiyo ni kama ifuatavyo:-

#### **2.1.1 Mradi Na.6220 – Support to Tanzania Social Action Fund (TASAF)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya Shilingi 76,626,997,721/= na ulipangwa kutekelezwa chini ya Kifungu 1003 cha Fungu 30 – Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.

Mfuko huu ambao unatekelezwa katika Mamlaka zote za Serikali za Mitaa Tanzania Bara na Wilaya zote za Zanzibar, uko katika sehemu ya pili ya utekelezaji wa awamu ya tatu ambayo umejikita katika kuzitambua kaya maskini kwenye Vijiji/Mitaa/Shehia zilizosalia kwa lengo la kuzisaidia kujimudu kiuchumi kwa kupunguza umaskini wa kipato; kuboresha maisha na ustawi wa jamii; na kushawishi wananchi kuwajibika katika ufanyaji wa kazi.

Taarifa ya Utekelezaji inaonesha kuwa kwa kipindi cha Julai, 2019 hadi Februari, 2020 TASAF iliweza kutoa ruzuku ya **shilingi bilioni 35.6** kwa kaya maskini **992,526** zilizoandikishwa zenye jumla ya watu **Milioni 5.2** kwa upande wa Tanzania Bara na Zanzibar katika Vijiji/Mitaa/Shehia **9,867**. Kaya hizo zilipata ruzuku hiyo kwa kuzingatia masharti ya lishe, afya na elimu.

Aidha, katika kipindi hicho kulikuwa na utekelezaji wa miradi 1,521 katika Vijiji, Mitaa na Shehia zipatazo 1,212 ambao uliwezesha kaya 161,416 kupata ajira za muda katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 42 na Wilaya zote za Zanzibar.

Miradi hiyo ambayo iligharimu **shilingi bilioni 6.4** ilihusu ujenzi na ukarabati wa malambo ya maji; uanzishaji wa vitalu vya miche ya miti; uchimbaji wa visima vifupi; uboreshaji wa barabara; uhifadhi wa vyanzo vya maji na hifadhi za mazingira.

Vilevile, TASAF iliandaa mfumo wa malipo kwa walengwa kwa njia ya kielektroniki kupitia mitandao ya simu na benki na kufanyiwa majaribio katika mamlaka za maeneo ya utekelezaji **16** za Tanzania Bara. Baadhi ya maeneo hayo ni Jiji la Arusha, Manispaa ya Ilala, Manispaa ya Temeke, Halmashauri ya Bahi, Mpanda Mji, Halmashauri ya Siha, Halmashauri ya Kisarawe, Manispaa ya Kigoma – Ujiji; Manispaa ya Songea; Halmashauri ya Urambo na Halmashauri ya Muheza. Aidha, Halmashauri zote za Unguja na Zanzibar zilihusishwa. Hadi kufikia mwezi Februari, 2020 jumla ya Walengwa **55,087** walipokea malipo yenye thamani ya **shilingi bilioni 2.14** kwa njia hiyo.

**Mheshimiwa Spika**, ili kujiridhisha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mpango huu Kamati ilitembelea na kukagua Mtaa wa Sokoine Manispaa ya Singida, na Mkoa wa Manyara.

### **2.1.2 Na.4921 – Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)**

**Mheshimiwa Spika**, mradi huu ulitengewa jumla ya shilingi 1,500,000,000/= na unatekelezwa chini ya Kifungu **1003** kiitwacho „**Policy and planing** cha **Fungu 30** – Ofisi ya Rais, Sekretarieti yaBaraza la Mawaziri.

Mpango huu unatekeleza jukumu la kuandaa na kusimamia mfumo wa kitaifa wa umiliki wa rasilimali na uendeshaji wa biashara nchini unaotambulika na kukubalika kisheria. Mpango huu umewezesha wanyonge kurasimisha ardhi na biashara na kuvitumia kukuza mitaji ya shughuli za kiuchumi.

Taarifa zilizowasilishwa kwenye Kamati zilibainisha kuwa, Wakulima **180** na Viongozi **22** wa vyama vya wakulima wamejengewa uwezo wa kutumia Hati za Haki Miliki za Kimila kupata Mitaji katika Benki na Taasisi zingine za Fedha katika Halmashauri ya Wilaya ya Kilosa. Aidha, mafunzo hayo yamewezesha Wakulima 48 katika Vijiji vya Mvumi na Magubike kufungua Akaunti katika Benki.

Aidha, huduma za urasimishaji wa biashara zimesongezwa kwa wananchi kwa kuanzisha vituo vya pamoja (**One Stop Business Formalization and Development Centre**) katika Halmashauri ya Manispaa ya Tabora na Halmashauri ya Mji wa Babati ambapo huduma muhimu hutolewa kama leseni za biashara, utoaji wa namba ya utambulisho wa mlipa kodi (**TIN**) kupitia **TRA**, usajili wa jina la biashara kupitia **BRELA**, huduma za benki na mifuko ya hifadhi ya jamii.

Aidha, Wafanyabiashara **1,529** wamepata mafunzo ya urasimishaji na uendeshaji wa biashara katika kipindi husika Vituo vimesajiliwa biashara **313** na Wafanyabiashara 420 wamefunga akaunti katika benki kwa ajili ya kuweka akiba na kukopa fedha ili kujiongezea mitaji.

Vilevile, zoezi la urasimishaji wa ardhi mijini kwa dhana ya Mfuko Endelevu wa Wilaya limeanza kwa kufanya utambuzi wa milki **200** kati ya **1,000** zilizopangwa katika Halmashauri ya Manispaa ya Iringa.

**Mheshimiwa Spika**, napenda kulijulisha Bunge hili kuwa Kamati ilitembelea Halmashauri ya Manispaa ya Singida, Mkoani Singida ili kujiridhisha kuhusu shughuli zinazotekelezwa na MKURABITA.

### 2.1.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)

**Mheshimiwa Spika**, chuo hiki kilianzishwa ili kutoa mafunzo, ushauri, kufanya utafiti tumizi na kutoa machapisho mbalimbali katika nyanja za uongozi, menejimenti na utawala. Aidha, chuo kinaendesha mafunzo ya muda mfupi na mrefu, na kutoa kozi za kitaaluma kwa ngazi za astashahada, stashahada na shahada katika nyanja za Uhazili, Utunzaji Kumbukumbu, Menejimenti ya Raslimali Watu, Utawala na Manunuzi ya Umma. Chuo kinatekeleza majukumu hayo kupitia Kampasi Sita (6) za Dar es Salam, Tabora, Mtwara, Singida, Tanga na Mbeya.

Aidha, utoaji wa mafunzo kwa watumishi wa umma umeendelea kuimarishwa ili kuwajengea uwezo katika utendaji kazi na kutoa huduma bora kwa wananchi. Hili limeimarishwa zaidi baada ya iliyokuwa Wakala ya Mafunzo kwa Njia ya Mtandao (**TaGLA**) kuunganishwa na Chuo cha Utumishi wa Umma Tanzania kupitia Tangazo la Serikali **Na.63** la Tarehe 31 Januari, 2020.

Ili kujiridhisha kuhusu utendaji wa chuo hiki Kamati ilipata fursa ya kutembelea Kampasi ya Singida ili kukagua utekelezaji wa chuo hicho pamoja na eneo la Mungumaji ambako majengo ya Kampasi hiyo yanatarajiwa kujengwa.

## 2.2 Matokeo ya Ukaguzi

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na ukaguzi wa miradi ya maendeleo hiyo inayotekelezwa na Ofisi ya Rais, Menejimenti

ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, katika mwaka wa fedha 2019/2020 naomba kutoa Taarifa kwa Bunge lako Tufuku kuhusu mambo ambayo Kamati iliyabaini kama ifuatavyo: -

### 2.2.1. Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini 'Support to Tanzania Social Action Fundi'

i. **Mheshimwa Spika**, katika Halmashauri ya Manispaa ya

Singida, Kamati ilitembelea na kukagua Mtaa wa Sokoine ambao una jumla ya kaya **2,824** zinazonufaika na mpango wa kunusuru kaya maskini ambapo hadi Februari, 2020 jumla ya shilingi bilioni **4.2** zilikuwa zimepelekwa kwa ajili ya ruzuku za msingi na utekelezaji wa shughuli zingine.

Manispaa ya Singida ni miongoni wa Halmashauri 10 za Tanzania zinazotekeleza Mpango wa Timiza Malengo wa kuwezesha wasichana balehe na wanawake vijana kutimiza malengo kielimu na kufikia ndoto zao (**Adolescent Girls and Young women - AGYW**) unaofadhiliwa na Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (**TASAF**) kwa kushirikiana na Tume ya kudhibiti UKIMWI (**TACAIDS**). Halmashauri nyingine zinazotekeleza mpango huu ni Kongwa, Mpwapwa, Bahi, Kilombero, Ulanga, Kondo Mji na Ifakara Mji.

Mpango wa **AGYW** unawahusu wasichana wote walio kwenye kaya zilizo kwenye mpango wa TASAF wa kunusuru kaya maskini katika Manispaa ya Singida na ulianza Juni, 2018 kwa kufanya utambuzi wa kuwatambua wasichana hao kutoka kaya zinazonufaika. Katika utambuzi huo jumla ya wasichana **2,250** walitambuliwa na kati ya hao **1,303** wanasoma katika shule mbalimbali na **947** hawasomi.

Utekelezaji wa Mpango wa Timiza Malengo (**AGYW**) uko katika maeneo mawili; utoaji wa ruzuku kwa wasichana balehe waliopo shuleni, na kwa wanawake vijana waliokosa fursa ya shule kwa kuendesha shughuli zao kwa kwa lengo la kukuza kipato.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilipata ushuhuda kutoka mnufaika wa ruzuku ya kaya maskini Bi. Edith Brayson Makala (miaka 55) ambaye anaishi katika Mtaa wa Sokoine ambaye ameamua kuitumia vyema kauli mbiu ya “Hapa Kazi tu” ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Pombe Joseph Magufuli ambayo imemuwezesha kuinua uchumi wa familia yake kupitia ruzuku ya kaya maskini kutoka **TASAF**.

**Bi. Makala** alianza kwa ajira ya muda chini ya mpango wa kunusuru kaya maskini mwaka 2016 ambapo alifanya kwa miezi minne (4) na kupata kipato kilichomuwezesha kununua cherehani na kuanza kujishughulisha na ushonaji, huku akimpatia mume wake mtaji wa biashara ya maji.

Mwaka 2018 alipata tena ajira ya muda ambayo ilimuwezesha kununua cherehani ya pili na hivyo kuongeza shughuli za ushonaji kwa kushirikiana na binti yake. Vyerehani hivyo vyenye thamani ya shilingi 400,000/= vinamuwezesha Bi. Makala kuendesha shughuli za ushonaji wa nguo mbalimbali ikiwa ni pamoja na sare za shule na mashuka.

“Tumejikita kushona sare za shule kwani ni biashara endelevu kwa kuwa watoto wanasoma kila siku na kila mwaka, hivyo itasaidia kuboresha maisha yangu na familia.” Alisema Bi. Makala na kuongeza kwamba, kipato anachokipata kimemuwezesha kusomesha watoto wake sekondari na mmoja amefikia elimu ya chuo kikuu.

**Mheshimiwa Spika**, mnufaika mwingine ni Bi. Ester Ikumbi ambaye alijikuta katika maisha magumu sana baada ya kutelekezwa na mume wake akiwa na watoto watano (5). Anaeleza kwamba, alifanya kazi katika ajira za muda za wanufaika wa mpango wa kunusuru kaya maskini na kupata kipato kilichomuwezesha kuboresha hali yake ya kiuchumi hadi kufikia hatua ya kununua kiwanja na kuanza ujenzi wa nyumba.

“Ninamshukuru sana Rais Magufuli kwa TASAF kwani imenirejeshea tumaini la kuishi, mimi na watoto wangu.

Nilikuwa nimekata tama kabisa, lakini sasa nafurahia maisha." Anasema Bi. Ikumbi na kuongeza kwamba, ameingia katika ujasiriamali kwa kuanzisha utengenezaji wa sabuni za maji na batiki ili kukuza kipato kitakachomuwezesha kulea na kusomesha watoto wake.

**ii. Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea na kujionea utekelezaji wa Mpango wa kunusuru Kaya masikini katika Halmashauri ya Mji wa Babati, ambao ulianza mwaka 2015 kwa kutambua na kuandikisha jumla ya Kaya **1,439**. Hata hivyo, baada ya uhakiki kwa lengo la kubaini na kuondoa kaya zisizo na sifa kaya hizo zilipungua hadi kaya **1,115**. Hadi kufikia Februari, 2020 malipo ya ruzuku yalikuwa yamefanyika kwa awamu 23 ambapo jumla ya **shilingi milioni 977.7** zimetumika kwa ajili ya uhawilishaji fedha kwa kaya masikini.

Utekelezaji wa mpango huu umesaidia kuboresha hali ya maisha kwa wanufaika kwa kuwawezesha kupata mlo wa uhakika, watoto kutoka kaya za wanufaika kuhudhuria masomo na wale walio chini ya miaka mitano kuhudhuria kliniki kikamilifu.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ilitembelea Mtaa wa Mrara uliopo kata ya Babati na kukutana na wanufaika wawili ambao kupitia ajira za muda zinazotolewa na mpango wa TASAF wameweza kuboresha maisha yao kwa kujiongezea kipato.

Bi. Albina Mathayo ambaye ni mjane aliyefanya kazi katika ajira za muda na kupata mtaji ambao umemuwezesha kuanzisha mradi wa kupasua kokoto, na ufugaji wa mbuzi, anasema kwamba TASAF imekuwa mkombozi wake kwani inamuwezesha kuendesha maisha bila wasiwasi.

" Kipato kutokana na ajira ya muda kiliniwezesha kupata mtaji wa kuanzisha shughuli ya kupasua kokoto, ambapo ninauza tipa moja kwa shilingi 80,000/= na maisha yanasonga." Anasema Bi. Alibina.

Mnufaika mwingine ni Rahabu Musa Samaki ajira ya muda imemuwezesha kuanzisha mradi wa ufugaji kuku na kupata



kipato cha kumuwezesha kusomesha watoto wake wawili hadi Sekondari na wawili ngazi ya stashahada, pamoja na kujenga nyumba ya vyumba vitatu kwa tofali za kuchoma.

**a) Mafanikio**

(i) Ugawaji wa taulo za kike zaidi ya 8000 kwa Wasichana waliopo shuleni kupitia AGYW;

(ii) AGYW imesaidia kutoa ruzuku kwa wasichana waliopo shuleni kwa ajili ya mahitaji yao (daftari, sare za shule, kalamu n.k);

(iii) Mafunzo kwa wasichana balehe na wanawake vijana 438 waliopo nje ya shule kupitia AGYW kuhusu namna ya kuandaa maandiko ya biashara;

(iv) Kaya 130 za walengwa zimejiunga na huduma za Mfuko wa bima ya Afya ulioboreshwa (iCHF);

(v) Wanufaika wameanzisha shughuli za kiuchumi kama vile kilimo, mifugo na biashara ndogo ndogo ili kujiongezea kipato na hivyo kujikwamua kiuchumi;

(vi) Mpango umsaidia kuboresha mahudhurio ya watoto shuleni na kliniki kwa walio chini ya miaka mitano.

**b) Changamoto**

(i) Idadi kubwa ya wasichana balehe na wanawake vijana kupenda matokeo ya haraka na hivyo kukimbilia kuolewa au kutafuta kazi za ndani badala ya kuandaa maandiko ya biashara ili wapatiwe mitaji;

(ii) Uhitaji mkubwa wa mpango wa AGYW kwa wasichana balehe na wanawake vijana walio nje ya mpango wa TASAF katika vijiji na mitaa ambayo haijafikiwa na mpango;

(iii) Baadhi ya Walengwa wa Mpango wa ruzuku kwa Kaya maskini kutumia fedha za ruzuku kinyume na malengo yaliyokusundiwa kama vile ulevi;

(iv) Kuchelewa kuanza utekelezaji wa baadhi ya shughuli zilizo katika mpango, kama vile ajira za muda mfupi, uboreshaji wa miundombinu ya afya, elimu, barabara, maji na mafunzo ya ujasiriamali.

### 2.2.2 Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA)

**Mheshimiwa Spika**, katika Halmashauri ya Singida ambayo Kamati ilitembelea na kukagua utekelezaji wa MKURABITA, yapo mambo kadhaa ambayo yalibainika ikiwa ni pamaoja na Mafanikio na Changamoto.

Katika mwaka wa fedha 2019/2020 MKURABITA kwa kushirikiana na Halmashauri ya Manispaa ya Singida, ilifanikiwa kufanya urasimishaji wa biashara za Wafanyabiashara **777** wa Halmashauri ya Singida na kuwajengea uwezo kwa lengo la kuwawezesha biashara zao kuwa kwenye Mfumo rasmi na unaotambulika Kisheria.

Aidha, pande hizo mbili zimejenga Kituo kimoja cha Urasimishaji na Uendelezaji Biashara (**One Stop Business Formalization and Development Centre**) kwa ajili ya kusaidia urasimishaji wa biashara kuwa wa haraka na wa gharama nafuu kwa mfanyabiashara. Kituo hicho kinawaleta pamoja wadau mbalimbali ili kumuwezesha mfanyabiashara kupata huduma zote muhimu anazozihitaji pale anapotaka kuanzisha biashara yake. Wadau hao ni pamoja na BRELA, TRA, Benki za CRDB na NMB, NSSF, SIDO, TCCIA, NIC na NHIF.

**Mheshimiwa Spika**, jengo linalotumiwa kwa kituo hicho awali **lilikuwa** ukumbi wa Manispaa ya Singida lakini baada ya pande mbili hizo kuona umuhimu wa kuwa na kituo cha aina hiyo, walikubaliana kubadili matumizi ya ukumbi huo kuwa kituo cha urasimishaji biashara kwa kufanya ukarabati uliogharimu **shilingi milioni 17.3** ambazo zilitolewa na MKURABITA na Manispaa iliweka uwekaji wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na ada na leseni. Aidha, MKURABITA ilichangia vitendea kazi kwa ajili ya kuwezesha shughuli za urasimishaji kutekelezwa kwa ufanisi

kwa kutoa Kompyuta moja, UPS, Scanner na Printer vyote vikiwa na thamani ya **shilingi milioni 4**.

**a) Mafanikio**

i. Kituo kimesaidia kupunguza usumbufu kwa wafanyabiashara kwa kuwawezesha kupata huduma za urasimishaji na uendelezaji biashara katika sehemu moja;

ii. Kuongezeka kwa mapato yanayotokana na ada za leseni ambapo tangu kuanzishwa kwa kituo hicho Disemba, 2019 hadi machi 2020 jumla ya shilingi milioni **52.3** zimekusanywa

iii. Ongezeko la Wafanyabiashara wanaofungua akaunti katika benki ya NMB;

iv. Wafanyabiashara 47 wamenufaika na mikopo yenye thamani ya **shilingi milioni 188** kutoka benki ya NMB na hivyo kuongeza mitaji ya biashara zao;

v. MKURABITA imeingia makubaliano na NMB ili wafanyabiashara **50** waliorasimishwa na MKURABITA katika Halmashauri waunganishwe **NMB Business Clubs** kwa ajili ya kuwapa mafunzo, mitaji na kuunganishwa na masoko;

**b) Changamoto**

i. Uhaba wa Watumishi wa kutoka kwenye Taasisi zinazohudumia kituo kwa muda wote;

ii. Wananchi wengi hawajapata elimu ya kutosha kuhusiana na shughuli na umuhimu wa kituo cha pamoja cha urasimishaji na uendelezaji wa biashara; na

iii. Huduma kutolewa kituoni hapo kwa siku chache (siku mbili) kwa wiki jambo linalowanyima wafanyabiashara wengi fursa ya kupata huduma za kituo.

**2.2.3 Chuo cha Utumishi wa Umma (TPSC)**

**Mheshimiwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma, kilianzishwa rasmi kama Wakala wa Serikali tarehe 17 Agosti, 2000 baada ya kuunganishwa kwa vyuo viwili; Chuo cha Watumishi wa

Serikali kilichokuwa Dar es Salaam (Civil Service Training Centre) na Chuo cha Uhazili Tabora (Tabora Secretarial College). Kwa sasa chuo kina kampasi sita (6) Dar es Salaam, Mtwara, Mbeya, Tanga, Tabora na Singida.

**Mheshimwa Spika**, Chuo cha Utumishi wa Umma kampasi ya Singida kilianza rasmi mwezi Julai, 2011 na kilipata usajili kamili wa Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE) wenye **Na.REG/BTP/038** mnamo mwezi Novemba, 2014. Chuo kinaendelea kutoa mafunzo ya muda mrefu kwa ngazi ya cheti na stashahada.

Katika ziara ya ukaguzi wa Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida Kamati ilibaini yafuatayo:-

**(a) Mafanikio**

- i. Chuo kimefanikiwa kudahili wanafunzi 1,380 tangu kilipoanzishwa;
- ii. Chuo kimeweza kujiendesha kwa kutumia mapato ya ndani;
- iii. Chuo kimefanikiwa kununua eneo lenye ukubwa wa ekari 76 katika eneo la Mungumaji, Kitongoji cha Sasu

**(b) Changamoto**

- i) Chuo hakina majengo yake na hivyo kulazimika kukodi majengo kwa mtu binafsi na hivyo kutumia fedha nyingi kwa ajili ya kulipa kodi;
- ii) Chuo kinakabiliwa na upungufu wa Watumishi wa kudumu na hivyo chuo kutumia fedha za mapato ya ndani kulipa watumishi wa muda;
- iii) Ukosefu wa hostel kwa wanafunzi;
- iv) Upungufu wa vitendea kazi na samani za ofisi.

## 2.3 Maoni ya Jumla kuhusu Utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2019/2020

**Mheshimiwa Spika**, kutokana na matokeo ya ukaguzi wa miradi ya maendeleo Kamati inapenda kutoa maoni yafuatayo:-

(i) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umesaidia wasichana balehe na wanawake vijana (Adolescent Girls and Young Women – AGYW) kujipatia taulo za kike;

(ii) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umesaidia kuboresha maisha ya wanufaika kwa kuwawezesha kumudu gharama mbalimbali za maisha;

(iii) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umesaidia kuboresha mahudhurio ya watoto shuleni na katika vituo vya afya;

(iv) Mpango wa ruzuku kwa kaya maskini umechochea utamaduni wa kaya maskini kujiwekea akiba na kupata elimu ya masuala ya fedha na uendeshaji wa biashara ndogondogo;

(v) Kituo cha Pamoja cha Urasimishaji na Uendelezaji wa Biashara kiwezeshe kuwa na wataalamu siku zote za kazi ili kiweze kuhudumia wafanyabiashara muda wote;

(vi) Bajeti finyu ya maendeleo kwa MKURABITA inaathiri utendaji wa mpango huo na hivyo kukwamisha zoezi la urasimishaji;

(vii) Serikali ikiwezeshe Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida kujenga majengo yake katika eneo la Mungumaji na hivyo kuokoa gharama zinazotumika kwa ajili ya kodi ya pango;

(viii) Serikali ikipatie Chuo cha Utumishi wa Umma, Kampasi ya Singida Watumishi wa kudumu na Vitendea kazi ili

kuboresha utendaji na hivyo kupunguza gharama za uendeshaji.

### **3.1 UCHAMBUZI WA TAARIFA YA UTEKELEZAJI WA BAJETI NA UZINGATIAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI KWA MWAKA WA FEDHA 2019/2020**

#### **3.2 Uchambuzi wa Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2019/2020**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Kamati katika Mapitio ya Utekelezaji wa Mpango wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2019/2020 ulijikita katika kuangalia mwenendo na upatikanaji wa fedha za matumizi kwa shughuli zilizopangwa. Njia zilizotumiwa na Kamati wakati wa uchambuzi huu ni pamoja na kuangalia hali halisi, kwa kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa vikao vya Kamati.

#### **3.2 Upatikanaji wa fedha kutoka Hazina**

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa Taarifa ya Utekelezaji wa Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, umebaini kwamba hakuna ulinganifu kati ya kiasi cha fedha kilichoidhinishwa na Bunge lako Tukufu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 na kiasi kinachotolewa na Hazina.

Kutokana na uchambuzi huo Kamati imebaini kwamba Njia kubwa zilizotumiwa wakati wa uchambuzi huu ni pamoja na kuangalia hali halisi, kuzingatia taarifa mbalimbali zilizowahi kuwasilishwa kwenye Kamati na mahojiano yaliyochangia upatikanaji wa taarifa muhimu wakati wa Vikao vya Kamati.

(i) Fedha zilizoidhinishwa zinatolewa kidogo ikilinganishwa na mpango wa upatikanaji wa Fedha (cash flow plan);

(ii) Fedha za matumizi ya kawaida zinatolewa kwa kiasi kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo (Matumizi ya kawaida asilimia **70.98** na Maendeleo asilimia **44.85**);na

(iii) Fedha hazipatikanaji kwa wakati na hivyo kuathiri utekelezaji wa malengo ya Bajeti ya Ofisi hii.

Maelezo hayo ni matokeo ya ulinganisho wa Fedha zilizopokelewa na mafungu yaliyo chini ya Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kutoka hazina hadi kufikia mwezi Februari ,2020 (robo tatu ya mwaka wa fedha 2019/2020) na kiasi cha fedha kilichoidhinishwa.

**Mheshimiwa Spika**,uchambuzi zaidi umebainisha kwamba hadi kufikia mwezi Februari,2020 Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora pamoja na mafungu yaliyo chini yake ilikuwa imepokea kiasi cha **Shilingi 432,987,967,686/=** kutoka Hazina kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na Maendeleo kiasi hicho ni sawa na asilimia **63.35** ya Fedha yote iliyoidhinishwa na Bunge. Kiasi hicho cha fedha kimeongezeka kwa takribani **Shilingi 58,281,023,829/=** sawa na Asilimia **15.55** ikilinganishwa na kiasi kilichopatikana katika kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019 ambacho kilikuwa ni **Shilingi 374,706,943,857/=**

Kwa upande wa fedha za Maendeleo uchambuzi umeonesha kwamba, hadi kufikia mwezi Februari,2020,Ofisi ya Rais,Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora na mafungu yake ilikuwa imepokea jumla ya **Shilingi 89,646,053,464.88/=** kutoka hazina sawa na asilimia **44.85** ya fedha yote iliyodhinishwa na Bunge kwa ajili ya Maendeleo. Kiasi hicho cha fedha kimeongeeeka kwa **asilimia 9.25** ikilinganishwa na kiasi kilichopokelewa kwa kipindi kama hicho katika mwaka wa fedha 2018/2019 kwa ajili ya Miradi ya Maendeleo ambacho kilikuwa **Shilingi 82,052,427,230/=**

Aidha Uchambuzi umebaini kwamba jumla ya mwenendo wa upatikanaji wa fedha haukuwa mzuri kwani fedha zilizopatikana zilikuwa ni takribani asilimia **63.35** ya fedha zote

zilizoidhinishwa .Kwa hali ya kawaida kiasi ambacho kilipaswa kiwe kinaenda asilimia **25** ya kila robo ya mwaka wa fedha hakikuweza kupatikana. Kwa kuzingatia kiasi cha fedha kwa kipindi hicho cha fedha zilizoidhinishwa kilipaswa kuwa kimepatikana na kutolewa kwa takribani **asilimia 75**.

Vilevile katika kipindi hicho jumla ya **Shilingi 343,341,914,222/=** zilikwa zimepokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida sawa na asilimia**70.98** ya fedha iliyoidhinishwa kwa ajili hiyo. Kiasi cha fedha kilichopokelewa kimeongezeka kwa asilimia **17.32** ikilinganishwa na **Shilingi 292,654,516,627/=** zilizopokelewa kwa ajili ya matumizi ya kawaida katika kipindi kama hicho katika mwaka wa Fedha **2018/2019**.

Hali hiyo inaonesha kuwa kiasi cha fedha za matumizi ya kawaida kinachotolewa na Hazina kimeendelea kuwa kikubwa ikilinganishwa na fedha za maendeleo. Mwenenendo huu umeshuhudiwa katika miaka minne ya fedha mfululizo tangu mwaka 2016/17 hadi 2019/20.

**Mheshimiwa Spika**, uchambuzi wa jumla wa Kamati umebaini kwamba, mtiririko wa fedha kutoka Hazina siyo mzuri ikilinganishwa na miaka iliyopita kwani kiasi kinachotolewa kimeendelea kupungua huku upande wa fedha za maendeleo ukiathirika zaidi ikilinganishwa na upande wa matumizi ya kawaida.

### **3.3 Mapitio ya Utekelezaji wa Maoni na Ushauri wa Kamati**

**Mheshimiwa Spika**, wakati wa kupitia na kuchambua bajeti Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kwaka 2019/2020 . Kamati ilitoa maoni na ushauri katika mambo kumi na tatu **(13)** kwa lengo la kuhakikisha bajeti hiyo inatekelezwa kwa ufanisi.

Napenda kulitaarifu Bunge lako Tukufu kuwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, imezingatia kikamilifu baadhi ya maoni na Ushauri wa



kamati na inaendelee kuzingatia yaliyosalia .Baadhi ya Maoni na ushauri vilivyozingatiwa ni kuhusu:-

(i) Serikali kupitia Taasisi ya Uongozi iendelee kutoa mafunzo ya uongozi na utawala kwa viongozi wanaoteuliwa ili kuwakumbusha juu ya umuhimu wa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji na hivyo kuepusha migongano isiyo ya lazima. Mafunzo hayo yameendelea kutolewa na matunda yake yameanza kuonekana ambapo vitendo vya ukiukwaji wa sheria, kanuni na miongozo ya kiutendaji vimepungua; na

(ii) Zoezi la kuhakiki na kuondoa kaya zisizo na sifa katika mpango wa ruzuku kwa kaya maskini litekelezwe kwa uangalifu ili kuepuka uonevu na malalamiko kutoka kwa waathirika. Zoezi hili limefanyika kwa umakini na kukamilika ambapo kaya zilizoondolewa ni zile zisizo na sifa.

**Mheshimiwa Spika**, licha ya baadhi ya maoni na ushauri wa Kamati kuzingatiwa na kufanyiwa kazi na Serikali, bado Kamati inaona kuna umuhimu wa kuendelea kuyasisitiza ili Serikali iyatekeleze kwa lengo la kuleta ufanisi katika utendaji. Baadhi ya maoni na ushauri hivyo ni pamoja:-

(i) Serikali iongeze mshahara kwa watumishi wa umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka kila kukicha. Serikali haijaongeza Mshahara kwa watumishi wa umma kwa miaka mitatu ya fedha iliyopita; na

(ii) Serikali iongeze bajeti ya maendeleo ya MKURABITA na kutoa kikamilifu na kwa wakati fedha inayotengwa ili kuongeza kasi ya upimaji na urasimishaji wa ardhi na biashara za Wananchi. Hadi mwezi Februari, 2020 MKURABITA ilikuwa hajapokea fedha yoyote ya maendeleo kati ya shilingi bilioni 1.5 zilizoidhinishwa na Bunge.

#### **4.1 UCHAMBUZI WA MPANGO WA MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI KWA MWAKA WA FEDHA 2020/2021**

#### **4.2 Uchambuzi wa Makadirio ya Mapato kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa ya Mpango na Bajeti kwa mwaka wa Fedha 2020/2021, kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora unajumuisha Mafungu Nane (04,09,20,30,32,33,67 na 94,) na Umeandaliwa kwa kuzingatia Mpango wa Maendeleo wa miaka Mitano (2016/17 -2020/21); Ilani ya Uchaguzi ya Chama Tawala ya mwaka 2015, Mwongozo wa Taifa wa kuandaa Mpango wa bajeti kwa mwaka wa fedha 2020/2021 pamoja na maeneo muhimu ya kuzingatia kama yalivyoanishwa na Serikali ya Awamu ya Tano.

Kwa ujumla Ofisi hii pamoja na Mafungu yake imepanga kutekeleza Malengo 174 kwa mwaka ujao wa fedha na Malengo hayo ni haya fuatayo:-

- i) Kutoa huduma kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na familia yake;
- ii) Kutoa ushauri kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania katika masuala ya Siasa, Uchumi, Jamii, Sheria, Diplomasia, Mawasiliano na Habari, Uhusiano wa Kikanda, Kimataifa na ushauri mwingine kwa lengo la kumsaidia Rais kufanya maamuzi;
- iii) Kufanya mafunzo na ufuatiliaji wa utekelezaji wa Mkakati Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III) na programu za maboresho katika ngazi za Wizara, Mikoa na Serikali za Mitaa;
- iv) Kuratibu na kusimamia Miradi ya Maendeleo ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF), Mpango wa Kurasimisha Rasilimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (MKURABITA) na Programu ya kujenga uwezo wa Taasisi za Serikali Kupambana na Rushwa (BSAAT);

v) Kukarabati majengo ya Ikulu ya Dar es salaam na Ikulu Ndogo za Mwanza, Arusha, Lushoto, Tabora na Shinyanga na Nyumba za Wafanyakazi zilizopo Dodoma;

vi) Kuendelea na uboreshaji wa Ikulu ya Chamwino;

vii) Kuandaa Taarifa za Utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu, na kukamilisha mfumo wa kielekroniki wa ufuatiliaji na tathmini ya utekelezaji wa Mkakati wa Taifa Dhidi ya Rushwa Awamu ya Tatu (NACSAP III);

viii) Kutoa mafunzo kuhusu utayarishaji na uwasilishaji wa Nyaraka za Baraza la Mawaziri na uchambuzi wa sera kwa Maofisa wa Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Waratibu wa shughuli za Baraza la Mawaziri wa Wizara;

ix) Kuratibu na kuendesha mikutano sita ya uratibu wa maboresho kwa Makatibu Wakuu na Waratibu wa Programu za Maboresho kwa lengo la kuimarisha usimamizi, uongozi na umiliki wa mchakato wa maboresho katika sekta ya umma nchini;

x) Kuratibu, kuandaa na kushiriki mikutano 60 ya Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri, mikutano 40 ya Kamati Maalum ya Makatibu Wakuu (IMTC) na mikutano 20 ya Baraza la Mawaziri;

xi) Kuandaa mkutano wa kimataifa na kikanda na mikutano saba ya kitaifa katika masuala ya Uongozi na Maendeleo Endelevu;

xii) Kuendelea na urasimishaji wa Wachimbaji wadogo wa Madini katika Mkoa wa Geita;

xiii) Miradi 2,390, katika sekta ya afya, elimu, maji, ujasiriamali nabarabara za vijiji itatekelezwa chini ya mpango wa kutoa ajira za muda katika Halmashauri 42 pamoja na Unguja na Pemba;

xiv) Kufanya mapitio ya pamoja baina ya Timu ya Serikali na wadau wa Maendeleo kuhusu maendeleo ya utekelezaji wa shughuli za Mpango wa Kunusuru Kaya Maskini;

xv) Kutoa huduma ya usafiri wa anga kwa viongozi wakuu wa kitaifa;

xvi) Kusimamia mikakati ya ukodishaji wa ndege kwa kampuni ya Ndege ya Taifa (ATCL);

xvii) Kupokea matamko ya Viongozi wa Umma kuhusu Rasilimali na madeni yanayopaswa kutolewa kwa mujibu wa Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma

xviii) Kufanya mapitio ya Sheria na Miongozo ya kiutumishi katika Utumishi wa Umma kwa lengo la kuboresha utendaji kazi;

xix) Kutoa mafunzo ya kujiandaa kufanya Mitihani ya Utumishi wa Umma kwa Watumishi 1,115;

xx) Kuendesha mafunzo kwa njia ya mtandao ili kusaidia Serikali kupunguza gharama, kuwa na mazingira rafiki katika kujifunza, kutoa fursa ya kuepuka muingiliano wa mafunzo na majukumu ya kazi, kupunguza safari nje ya mahali pa kazi na kuepuka kuwa mbali na familia;

xxi) Kusanikisha katika taasisi za umma, Mfumo Shirikishi wa Kusimamia shughuli za Rasilimali za Taasisi;

xxii) Kuwezesha mifumo ya TEHAMA ya kimkakati na ya kisekta kubadilishana taarifa;

xxiii) Kusimamia na kuendesha michakato ya ajira ili kuwezesha waajiri kupata watumishi wenye sifa zinazotakiwa kwa mujibu wa miundo ya utumishi husika;

xxiv) Kuimarisha Ofisi ya Sekretarieti ya Ajira iliyopo Zanzibar ili kurahisisha michakato ya ajira kwa ajiri za Muungano;

xxv) Kufanya mikutano ya Kisheria ya Tume ili kujadili na kutolea uamuzi rufaa na malalamiko, taarifa za ukaguzi na masuala mengine ya kiutumishi kadri yatakavyopokelewa;

xxvi) Kufanya utafiti kuhusu mazingira magumu ya kazi;

xxvii) Kukusanya taarifa, kumbukumbu, nyaraka na machapisho mbalimbali yanayohusu historia ya nchi yetu kutoka taasisi za Umma, taasisi na watu binafsi.

**Mheshimiwa Spika**, ili iweze kutekeleza malengo hayo yaliyokusudiwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, inaomba kuidhinishwa jumla ya **Shilingi 699,956,320,000**. Kati ya fedha hizo **Shilingi 517,131,499,000/=** ni kwa ajili ya Matumizi ya kawaida na **Shilingi 182,824,821,000** ni kwa ajili ya miradi ya Maendeleo. Aidha, katika fedha za matumizi ya kawaida **Shilingi 39,154,604,000** sawa na asilimia **5.58** ni kwa ajili ya Mishahara na **Shilingi 477,976,895,000/=** sawa na asilimia **68.29** ni kwa ajili ya matumizi Mengineyo.

Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba, bajeti inayoombwa kuidhinishwa kwa mwaka ujao wa fedha imeongezeka kwa **Shilingi 16,427,108,383/=** sawa na asilimia **2.4** ikilinganishwa na bajeti ya mwaka wa fedha 2019/2020 ambayo ilikuwa **shilingi 683,529,211,617/=**.

Aidha, kwa upande wa wa Fedha za Matumizi ya kawaida katika mwaka ujao wa fedha zimeongezeka kwa kiasi cha Shilingi **33,469,533,000/=** ambacho sawa ni asilimia **6.92** ikilinganishwa na mwaka wa fedha 2019/2020 ambapo matumizi ya kawaida yalikuwa **Shilingi 483,661,966,000/=**.

**Mheshimiwa Spika**, Vile vile Uchambuzi wa Kamati umebaini kwamba kiasi cha Fedha za Miradi ya Maendeleo kinachoombwa kimepungua kwa **Shilingi 17,042,434,617/=** sawa na Asilimia **8.53** ilinganishwa na fedha za miradi ya Maendeleo zilizoidhinishwa katika mwaka wa fedha **2019/2020** ambacho zilikuwa Shilingi **199,867,255,617/=**

#### **4.3 Uchambuzi wa Bajeti ya Wizara kwa kulinganisha na Mpango wa Maendeleo wa Taifa wa Mwaka 2020/2021**

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Kamati ulifanya ulinganisho wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi

wa Umma na Utawala bora na Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Uchambuzi umelenga kubaini ni kwa kiasi gani ongezeko la bajeti ya Taifa linaathiri mwenendo wa bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora katika mwaka ujao wa fedha. Ufafanuzi wa uchambuzi huo umetekelezwa kwa kutumia jedwali, asilimia, ulinganishaji na utofautishaji na ili kurahisisha maelezo Kamati imetumia Chati. Katika uchambuzi huo mambo yafuatayo yalibainika:-

(i) Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 ambayo ni **Shilingi 699.56** ni sawa na asilimia **2.01** ya Bajeti yote ya Serikali ambayo kwa mujibu wa Mpango wa Maendeleo wa 2020/2021 ni **Shilingi 34,876/=**

(ii) Mpango wa maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021 unaonesha ongezeko la bajeti kwa **asilimia 5.36** ikilinganishwa na Mpango wa Bajeti kwa mwaka wa 2019/2020 wakati Bajeti ya Ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 imeongezeka kwa **asilimia 2.4** ikilinganishwa na bajeti iliyoidhinishwa katika mwaka wa fedha 2019/2020; na

(iii) Mpango wa Maendeleo ya Taifa unaonesha ongezeko la asilimia **5.3** katika fedha za Maendeleo ambazo ni sawa asilimia **36.98** ya Bajeti ya Taifa kwa mwaka wa fedha 2020/2021; Hili hali bajeti ya Maendeleo ya ofisi ya Rais Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala bora ambayo ni sawa na asilimia 2.01 ya Bajeti ya Taifa, imeongezeka kwa Asilimia **2.4** ikilinganisha na Mwaka wa fedha 2020/2021.


**Jedwali Na. 1:** Ulinganisho wa Bajeti ya Ofisi ya Rais (UUB) dhidi ya Bajeti ya Taifa kwa Mwaka wa Fedha 2020/2021

BAJETI KUU YA TAIFA 2020/2021			BAJETI YA OFISI YA RAIS UUB 2020/2021		
Mgawanyo	Bajeti Kuu (Tsh. Milioni)	Asilimia ya Jumla ya Bajeti Kuu	Mgawanyo	Bajeti ya Wizara	Asilimia ya Jumla ya Bajeti ya
OC	3,741,137	10.73	OC	477,976,895,000	68.29
Deni la Taifa	10,476,834	30.4	-	-	-
Mishahara	7,762,389	22.25	Mshahara	39,154,604,000	5.59
Maendeleo	12,899,433.8	36.98	Maendeleo	182,824,821,000	26.12
<b>Jumla</b>	<b>34,879,793</b>	<b>100</b>	<b>Jumla</b>	<b>699,959,320,000</b>	<b>100</b>

**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa na Randama ya Ofisi ya Rais – UUB kwa Mwaka wa fedha 2020/2021.


Aidha, matokeo ya ulinganisho wa Bajeti ya Taifa, dhidi ya Bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora yanaoneshwa sawia kwa kutumia **Chati Mraba Na.01** na **Na. 02** kama ifuatavyo:-

**Chati Na. 01: Bajeti ya Taifa kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo, Maendeleo na Deni la Taifa kwa mwaka 2020/21**



**Chanzo:** Mpango wa Maendeleo wa Taifa kwa mwaka wa fedha 2019/20

## Chati Na.02 Bajeti ya OR-UUB kwa ajili ya Mishahara, Matumizi Mengineyo na Maendeleo kwa mwaka wa Fedha 2020/21



**Chanzo:** Randama ya OR – UUB kwa Mwaka wa fedha 2020/2021

### 5.1 MAONI NA USHAURI WA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia taarifa za ukaguzi wa Miradi ya Maendeleo ,taarifa za utekelezaji wa bajeti iliyopita na maombi ya makadirio ya mapato na matumizi kwa mwaka ujao wa fedha,Kamati inapenda kutoa maoni na ushauri kwa Serikali kama ifuatavyo:-

(i) Serikali iangalie namna ya kutatua Changamoto ya upungufu wa watumishi wa umma haswa wa kada za Afya na Elimu ambayo kwa sehemu kubwa imechangiwa na watumishi wengi kuondolewa kazini baada ya kubainika kutumia vyeti vya kughushi;

(ii) Serikali iongeza mshahara kwa watumishi wa umma ili kuwawezesha kumudu gharama za maisha ambazo zinaongezeka mara kwa mara. Aidha, hali hiyo imechangia watumishi kukosa ari ya utendaji na kuishia kulalamika kuwa maisha yamekuwa ghali;

(iii) Serikali ichukue hatua ili kuondoa ucheleweshaji wa Watumishi wa Umma kupanda madaraja na kubadilishiwa Mishahara, hali ambayo imesababisha baadhi yao kustaafu



bila kupata stahiki na haki zao. Aidha hali hiyo inasababisha maumivu kwa watumishi hao na baadhi yao kutafsiri kwamba, wanadhulumiwa na Serikali stahiki na haki zao;

(iv) Kamati inatambua na kupongeza juhudi za Serikali kupitia Taasisi ya kuzuia na kupambana na Rushwa (TAKUKURU ) za kushughulikia Rushwa kubwa ambapo watuhumiwa wamekamatwa na kushitakiwa kwenye vyombo vya Sheria.Hata hivyo Kamati inashauri juhudi zaidi ziongezwe hasa katika kupambana na Rushwa ya Ngono ambayo imekuwa ikilalamikiwa kushamiri katika Taasisi za Elimu,Sehemu za kazi na maeneo mengine ya jamii;

(v) Serikali ihakikishe halmashauri zinawatumia kikamilifu Maafisa Maendeleo ya Jamii, na Maafisa Ustawi wa jamii kwa ajili ya kuwaelimisha na kuwasimamia wanufaika wa mpango wa ruzuku wa kaya maskini ili kuhakikisha wanaelekeza sehemu ya ruzuku wanazopata kwenye shughuli za kiuchumi ili kuondokana na umaskini;

(vi) Serikali ihakikishe inatumia kikamilifu fedha ilizozipata kwa ajili Utekelezaji awamu ya pili ya mpango wa kunusuru kaya maskini kwa kuyafikia maeneo yote yaliyobaki ( Vijiji/Mtaa/Shehia 5,693) ili kuwapa wananchi wa maeneo hayo fursa ya kunufaika na mpango;

(vii) TASAF iongeza wigo kwenye mfumo wa malipo ya walengwa kwa njia ya Kielektroniki (kupitia mitandao ya simu na Benki), ili kuharakisha na kurahisisha malipo kumfika mlengwa moja kwa moja. Aidha, mfumo huo utasaidia kuondoa malalamiko kutoka kwa baadhi ya walengwa kwamba wamekuwa hawapati malipo kamili yanayostahili;

i) Serikali iongeze kiasi inachochangia katika utekelezaji wa mpango wa kunusuru kaya maskini, kwani bado mchango wake ni mdogo sana. Tangu mpango huu ulipoanza mwaka wa fedha 2013/2014, hadi taarifa hii inaandaliwa Serikali imechangia **shilingi bilioni 8.12** tu kati ya **shilingi bilioni 70** ilizopaswa kuchangia, sawa **asilimia** 11.58. Kwa ufafanuzi ufuatao: -

**Jedwali Na. 02:** Mchango wa Serikali na kiasi ilichotoa

Na.	Mwaka wa Fedha	Kiasi kilichoahidiwa (Tshs. Bilioni)	Kiasi kilichotolewa (Tshs. Bilioni)	Bakaa (Tshs. Bilioni)
01.	2013/14	18.50	3.00	15.50
02.	2014/15	14.00	0.00	14.00
03.	2015/16	14.00	0.60	14.00
04.	2016/17	14.00	0.00	14.00
05.	2017/18	3.00	0.75	2.25
06.	2018/19	3.00	3.00	0.00
07.	2019/20	3.5	1.01	2.5
	<b>Jumla</b>	<b>70</b>	<b>8.12</b>	<b>61.91</b>

(viii) Serikali ihakikishe Halmashauri zote nchini zinashirikiana na Mpango wa Kurasimisha Raslimali na Biashara za Wanyonge Tanzania (**MKURABITA**) ili ziweze kuanzisha (**One Stop Business Formalization and Development Centre**) kwa ajili ya kusaidia kurahisisha urasimishaji na uendelezaji wa biashara kwa kupunguza gharama na muda;

(ix) Serikali ihakikishe Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma inatoa mafunzo kwa Viongozi wa Umma wanaoteuliwa katika nyadhifa mbalimbali kabla hawajaanza kutekeleza majukumu yao. Hali hii itasaidia kuwakumbusha Viongozi hao kuzingatia maadili ya kiutendaji, kujjepusha na mgongano wa maslahi na kuishi kwa kuzingatia kiapo cha ahadi ya uadilifu;

(x) Serikali ikiwezeshe Chuo cha Utumishi wa Umma kujenga majengo yake katika eneo la Mungumaji – Manispaa ya Singida ili kuwezesha Kampasi ya Singida kuwa na majengo yake na hivyo kuokoa gharama nyingi zinazotumika kwa ajili ya kulipa kodi ya pango.

## 6.0 HITIMISHO

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kwa niaba ya Kamati kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na Wenyeviti wa Bunge, kwa jinsi ambavyo mmekuwa mkitimiza majukumu yenu kwa umakini wa hali ya juu na kuwezesha Bunge letu Tukufu kutimiza wajibu wake kwa ustadi mkubwa.

Aidha, nawashukuru kwa moyo wa dhati Wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Utawala na Serikali za Mitaa, kwa ushirikiano na jinsi walivyojitoa kikamilifu katika kipindi chote cha uchambuzi wa bajeti ya ofisi hii hadi kukamilika kwa Taarifa hii. Kwa kutambua kuwa hii ni taarifa ya mwisho ya Kamati katika Bunge hili la Kumi na Moja, nitumie fursa hii kuwatakia Wajumbe wa Kamati pamoja na Wabunge wengine wote kila lakheri katika uchaguzi ujao na Mwenyezi Mungu atujaalie turejee sote katika Bunge lijalo ili tuendeleze gurudumu la ujenzi wa Taifa letu kwa kutimiza wajibu wa kikatiba wa kuwakilisha wananchi na kuisimamia Serikali.

**Mheshimiwa Spika**, Kamati hii inashughulikia mafungu ya bajeti 36 ambayo ni mengi kuliko Kamati nyingine ya Bunge, na kwa kuzingatia muda mfupi uliotengwa kwa ajili ya uchambuzi, ni wazi Wajumbe walilazimika kufanya kazi kwa muda mrefu na wakati mwingine hadi jioni kabisa. Hata hivyo, mazingira hayo hayakuwa kikwazo kwa namna yoyote ile kwa Wajumbe kutekeleza jukumu la uchambuzi kwa moyo na weledi wa hali ya juu. Hii ni ishara tosha ya utayari wa Wabunge kuitumikia Bunge, Taifa na Wananchi.

**Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu wake ningetamani kuwatambua Wajumbe wa Kamati kwa kutaja majina yao. Hata hivyo, kwa kuzingatia ufinyu wa muda naomba majina yao yaingizwe kwenye Kumbukumbu za Taarifa Rasmi za Bunge (Hansard). Majina ya Wajumbe hao ni haya yafuatayo:-

1. Mhe. Dkt. Jasson Samson Rweikiza, Mb – Mwenyekiti
2. Mhe. Mwanne Ismail Mchemba, Mb - Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Margaret Simwanza Sitta, Mb

4. Mhe. Angelina Adam Malembeka, Mb
5. Mhe. George Malima Lubeleje, Mb
6. Mhe. Dkt. Mwigulu Lameck Nchemba, Mb
7. Mhe. Daniel Edward Mtuka, Mb
8. Mhe. Hamad Salim Maalim, Mb
9. Mhe. Innocent Sebba Bilakwate, Mb
10. Mhe. Mwatum Dau Haji, Mb
11. Mhe. Dkt. Saada Mkuya Salum, Mb
12. Mhe. Salum Khamis Salum, Mb
13. Mhe. Venance Methusela Mwamoto, Mb
14. Mhe. Anna Joram Gidarya, Mb
15. Mhe. Jerome Dismas Bwanausi, Mb
16. Mhe. Martha Moses Mlata, Mb
17. Mhe. Lusya Ursula Michael, Mb
18. Mhe. Rehema Juma Migilla, Mb
19. Mhe. Joseph Roman Selasini, Mb
20. Mhe. Joel Mwaka Makanyaga, Mb
21. Mhe. Philipo Augustino Mulugo, Mb
22. Mhe. Khatib Said Haji, Mb
23. Mhe. Njalu Daudi Silanga, Mb
24. Mhe. Hamidu Hassan Bobali, Mb
25. Mhe. Mansoor Hirani Shanif, Mb
26. Mhe. Ibrahim Hassanali Mohammedali Raza, Mb

**Mheshimiwa Spika**, nitumie fursa hii kumshukuru sana Mhe. Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika (Mb), Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Mhe. Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa (Mb), Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano mkubwa waliouonesha kwa Kamati katika kipindi chote cha utekelezaji wa majukumu yake.

Nawashukuru pia watendaji wote wa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora wakiongozwa na Makatibu Wakuu Dkt. Moses Kusiluka (Ikulu), Dkt. Laurean Ndumbaro (Utumishi), na Naibu Katibu Mkuu (Utumishi) Dkt. Fransic Michael kwa ushirikiano wao kwa Kamati wakati wote wa kuchambua Taarifa ya utekelezaji wa majukumu ya Ofisi hiyo kwa mwaka wa fedha 2019/2020

na Makadirio ya Mapato na Matumizi kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Aidha, nawashukuru kwa dhati kabisa Wakuu wa Taasisi, Idara na Vitengo vilivyopo chini ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa ushirikiano wao na utekelezaji makini wa Bajeti ya mwaka wa fedha unaoisha.

**Mheshimiwa Spika**, kwa namna ya pekee namshukuru Katibu wa Bunge Ndg. Stephen Kagaigai, Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge, Ndg. Michael Chikokoto, Mkurugenzi Msaidizi wa Kamati za Bunge, Ndg. Gerlad Magili, Makatibu wa Kamati Ndg. Chacha Nyakega, Ndg. Eunike Shirima, Ndg. Asmin Kihemba na Ndg. Prosper Minja wakisaidiwa na Ndg. Kokuwaisa Gonda kwa uratibu wao mzuri wa shughuli za Kamati ikiwa ni pamoja na kukamilisha maandalizi ya Taarifa hii kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, baada ya maelezo hayo, sasa naliomba Bunge lako Tukufu likubali kuidhinisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa mwaka wa fedha 2020/2021, kama yalivyowasilishwa na Mtoa Hoja hapo awali.

**Jasson S. Rweikiza (Mb)**  
**MWENYEKITI**  
**KAMATI VA KUDUMU**  
**VA UTAWALA NA SERIKALI ZA MITAA**  
15 Aprili, 2020

**SPIKA:** Asante sana Mheshimiwa Dkt. Rweikiza kwa kutuzindulia utaratibu mpya ambao unatuwezesha kumbi hizi mbili kuweza kuwasiliana na kusikilizana na tutaendelea kujaribu hapa na pale na kurekebisha yale madogo madogo ambayo yanahitaji kurekebishwa. Ikiwa ni pamoja na watakaokuwa kwenye ukumbi huo kuzingatia muda tutaweka utaratibu ambao tutahakikisha wanazingatia muda ule ule unaotakiwa. Sasa nimuite Msemaji wa Kambi

Rasmi ya Upinzani ambaye atawasilisha maoni ya Kambi hiyo kuhusu Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa muda wa dakika ishirini. (*Makofi*)

Mheshimiwa Ruth utakumbuka nimeshakubonyeza kifungu 11, 13 na 24 uyaache, vinginevyo mengine yote endelea tu.

**MHE. RUTH H. MOLLEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, *I hope summary* yangu itaenda na ya kwako.

Mheshimiwa Spika, kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa afya njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu utendaji kazi wa Serikali, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa 2020/2021.

Mheshimiwa Spika, kwa umuhimu mkubwa, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kuendelea kuniamini na kuiteua kuwa Waziri Kivuli wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, naamini nimejitahidi kutimiza wajibu wangu ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, hakuna mtu ajuaye kesho yake ila Mungu mwenyewe. Hivyo basi, katika hotuba yangu ya mwisho katika Bunge hili la 11, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Makamanda wenzangu kwa ushirikiano mkubwa walionipa. Hakika nimejifunza mengi kutoka kwenu na Baraka za Mungu ziambatane nasi popote tutakapokuwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa upekee napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa viongozi pamoja na wanachama wetu wa ngazi mbalimbali kwenye Kanda ya Pwani, na

hususan Wilaya ya Mkuranga kwa ukomavu wao katika kutambua haki zao za msingi wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kisiasa licha ya vitisho vingi kutoka kwa watendaji wanaolipwa kwa kodi za wananchi. Ninawatia moyo kwamba Tanzania inapita katika kipindi cha mpito kuelekea kwenye demokrasia ya kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika majukumu yangu haya ya Kibunge na kisiasa ya ambayo naendelea kujifunza. Nasema ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, baada ya miaka takribani minne na zaidi, katika nafasi hii ya Uwaziri Kivuli, Utumishi na Utawala Bora nimekuwa nikitoa ushauri kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali kupitia hotuba zangu za kila mwaka wakati wa kujadili bajeti ya ofisi hii. Kwa msingi huo nitajikita kwenye tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kambi Rasmi ya Upinzani kwa muda wote wa uhai wa Bunge lako tukufu.

Mheshimiwa Spika, hotuba hii iliyo mbele ya Bunge lako tukufu imejikita katika mafungu yafuatayo yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais; hayo mafungu yameainishwa yapo saba. Pamoja na mafungu hayo, Ofisi hii ya Rais inasimamia pia Taasisi ya Kupambana na Rushwa. Hata hivyo, nitazungumzia tu baadhi ya maeneo ambayo kwa maoni yangu yanahitaji msisitizo zaidi.

Mheshimiwa Spika, Utawala Bora ni pamoja na kuzingatia misingi ya Katiba, Sheria, Kanuni, Miongozo, Demokrasia na kuheshimu haki za binadamu katika kuliongoza Taifa.

Aidha Utawala Bora ni matumizi ya mamlaka yenye uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu na usawa unaofuata utawala wa sheria. Rasimu ya Pili ya Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba na Katiba pendekezwa inaainisha kwamba wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itawajibika kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, utawala bora ni dhana pana sana inajumuisha pia haki ya kuchagua na kuchaguliwa. Ili wananchi wawe na uwanja ulio sawa kuchagua viongozi wanaowataka wawakilishe katika kuisimamia Serikali, uwepo wa Tume Huru ya Uchaguzi nalo ni jambo ambalo haliepukiki ili kulinda haki za wananchi kuchagua viongozi wanaowafaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwepo wa Tume ni huru ni muhimu kwa sababu tarehe 22 Machi, huko Busokelo Mbeya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke ndugu Mwakibibi akiwepo kwenye harambee ya kujenga zahanati alionekana akiwa amevaa mavazi ya Chama cha Mapinduzi na bila hofu kujitangaza kuwa ni Mbunge ajaye wa Jimbo la Busokelo na alichangia mabati 100, huyu *DED* pamoja na mkewe ambaye pia ni *DED* wa Biharamulo Kagera walipiga kampeni kwa uwazi na kutoa rushwa kwa wananchi wa Busokelo.

Mheshimiwa Spika, viongozi hawa ni wasimamizi wa uchaguzi *Returning Officers* katika maeneo yao. Je, watatenda haki kweli kipindi cha uchaguzi wakati inaonekana waziwazi wameegemea upande wa Chama Tawala, sio hivyo tu ametumia gari la ofisi ya umma kwenda kwenye harambee ya kampeni. Huu si utawala bora na unatakiwa kupigwa vita kwa nguvu zote. Yu wapi Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma? Yu wapi Waziri wa Utumishi wa Umma? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, huyu *DED* ndugu Mwakabibi yeye amejitokeza wazi kwamba ni mwanachama wa CCM, wapo Wakurugenzi watendaji wengi ambao ni wanachama wa CCM, hivyo basi kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba uchaguzi utakuwa huru na wa haki itakuwa mashakani, hivyo basi Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri yafuatayo:-

(i) Tume ya Maadili imchukulie hatua ya kinidhamu Mtumishi wa Umma kwa kujinasibu hadharani kwamba ni mwanachama wa Chama Tawala kinyume na maadili ya Utumishi wa Umma.



(ii) Serikali ilete Muswada kwa masharti ya dharura Bungeni kurekebisha baadhi ya vipengele vya Katiba hususani Ibara ya 74 na 75 ili kuwezesha uundwaji wa Tume Huru ya uchaguzi ili kuhakikisha uhuru uchaguzi wa Oktoba unakuwa huru na wa haki. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, baada ya uchaguzi wa Oktoba CHADEMA itapata ridhaa ya kuongoza nchi endapo uchaguzi utakuwa huru na haki. Jukumu la Serikali yetu kwanza ni kurekebisha sheria zote kandamizi zinazozuia wananchi kutoa maoni yao kwa uhuru bila hofu yoyote, wananchi ndio watakuwa mamlaka ya juu ya Serikali yao, Serikali hii itakuwa ni ya demokrasia ya kweli; *Government of the people by the people and for the people.* *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, uwajibikaji ni sehemu ya utawala bora; Bunge lako Tukufu kwa muda wote wa miaka mitano limekuwa likipitisha bajeti ya Mapato na Matumizi kwa Wizara zote, hata hivyo uzoefu umeonesha bajeti ya matumizi kawaida na maendeleo haitolewi na Serikali kama Bunge linavyokuwa limepitisha na wakati mwingine yanafanyika matumizi nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge hili. Kwa muktadha huo ni dhahiri Serikali imeshindwa kuwajibika kabisa inakuwa ni vigumu kupima uwajibikaji kwa kuwa fedha zinazopitishwa zimetumika kwa jambo ambalo halikupangwa na kupitishwa na Bunge. Aidha, kama Serikali inashindwa kuwajibika ni kwa vipi wananchi watawajibika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali ijayo iwe inatayarisha makisio ya mapato na matumizi kufuatana na mazingira halisi ya nchi.

Pili iwasilishe Bungeni bajeti halisi kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi, ni afadhali kutotenga kabisa fedha za miradi ya maendeleo na kuzielekeza kwenye maeneo ya vipaumbele kuliko utamaduni uliojengeka wa kutenga fedha za maendeleo lakini hazitolewi kutokana na fedha kama ilivyopitishwa kunatia dosari uwajibikaji na *credibility* ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, sitapenda kujadili kuhusu utawala wa sheria kwa sababu ipo wazi kwa jinsi waliopewa dhamana wametumia Madaraka yao vibaya *with impunity* bila kuadhibiwa wananchi wamekuwa wahanga wakuu wa kubambikiwa kesi wangi wako mahabusu au wamefungwa tumeshuhudia baadhi ya ma-DC, ma-RC wanavyoweka wananchi au watumishi mahabusu kutoa maneno ya ukakasi mbele ya wananchi bila soni kwa sababu ya ulevi wa Madaraka. Wamesahau kabisa kwamba wao ni watumishi wa umma. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali kuhakikisha hadhi ya utumishi wa umma inalindwa kwa:-

(i) Kutoa mafunzo ya uongozi kwa wote wanaoteuliwa na Rais kabla ya kuanza kazi. (*Makofi*)

(ii) Viongozi wote wa kisiasa wafanyiwe upekuzi kabla ya kupewa madaraka. (*Makofi*)

(iii) Wanaopewa uongozi wasiwe na rekodi yoyote ya jinai/maadili; kwa kuzingatia ushauri huo, tutapata viongozi wanaojitambua na wasiotiliwa shaka. Chuo cha Uongozi "*Leadership College*" kipo, fedha zitengwe ili viongozi wote wa juu wapate mafunzo kabla ya kuanza kazi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Uchumi Imara ni Matokeo ya Utawala Bora pia. Toka Awamu ya Tano iingie madarakani haijwahi kuongeza mishahara ya watumishi wa umma, wamenyimwa hata zile nyongeza za kisheria kwa mujibu ya Kanuni ya Kudumu ya E(8), mishahara yao imedumaa kwa miaka minne na zaidi mfululizo ili hali gharama za maisha zikiendelea kupanda. Watumishi wanahisi kutothaminiwa na hivyo kukosa ari na ubunifu wa kutimiza majukumu yao, hivyo kurudisha nyuma maendeleo na kuongezeka kwa vitendo vya rushwa ndogo na kubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, licha ya ukikukwaji Kanuni zinazoainisha ongezeko la mishahara na kupandishwa kwa madaraja kwa watumishi wa umma, lakini hatujasikia vyama vya wafanyakazi kukemea na kutetea wafanyakazi, jambo hili linazidi tu kutupa mashaka zaidi juu ya viongozi wa vyama

hivyo katika utetezi wa wafanyakazi katika kuhakikisha wafanyakazi wanawajibika na pia wanapata stahili zao kulingana na sheria na kanuni.

Mheshimiwa Spika, nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena kuikumbusha Serikali kwamba bila rasilimali watu wenye furaha, ari na ubunifu miradi yote inayotekelezwa haitafanikiwa kwa kiwango kikubwa, mitambo hiyo haitajiendesha yenyewe bali inahitaji wataalam wa kusimamia, hivyo Serikali isipuze hata kidogo mchango wa rasilimali watu kwenye maendeleo ya nchi.

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kwamba kutokana na kupanda kwa gharama za maisha na mishahara ya watumishi kutopandishwa kwa muda mrefu, watumishi wa umma walipwe nyongeza zao za kila mwaka kwa mujibu wa sheria. Aidha, kwa Mamlaka aliyonayo mwajiri Mkuu Mheshimiwa Rais aruhusu watumishi wafanyiwe marekebisho ya mishahara na fedha zitengwe mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuwapunguzia makali ya maisha.

Katika hili la utumishi wa umma tunafahamu kuwa nafasi ya *RC* na *DC* kwa kiwango kikubwa ni utumishi wa kisiasa, lakini vilevile kwa kiwango kikubwa ni utumishi wa umma, hivyo wahusika wanapokuwa katika kutekeleza majukumu yao kwa wananchi ni vyema kutoegemea mlengo wa vyama. Tumeshuhudia mara kadhaa viongozi hawa wakiwa katika ukaguzi wa miradi au ufuatiliaji wa maendeleo ya Waziri Mkuu au maelekezo ya Waziri Mkuu au Mheshimiwa Rais wakiwa katika mavazi ya Chama cha Mapinduzi.

Mheshimiwa Spika, mfano mzuri ni kwa *RC* Lindi, wa Manyara na *DC* Hai. Jambo hili ni kinyume kabisa cha utumishi wa umma, kama Mheshimiwa Rais ndio Mwenyekiti wa Chama na Mheshimiwa Waziri Mkuu wake hawajahi kuonekana hadharani katika utendaji wao kuvaa nguo za chama inakuwaje wasaidizi wao wanavaa nguo za chama, au ni kutaka kuonesha kuwa wao ni wanachama zaidi ya viongozi wao? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Serikali inashauriwa irudi kwenye maadili ya utumishi wa umma inayoainisha kwamba Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na watendaji watambue dhamana waliyopewa ya Watanzania. Nafasi ya uongozi wa umma kupitia mkono wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kwa ajili ya kuwatumikia wananchi, watambue kwamba mishahara yao na stahili zao zote zinatokana na kodi za wavuja jasho wa nchi hii, hivyo waelekezwe kufundishwa kwamba katika majukumu yao ya umma hapaswi kuonesha mlengo wa siasa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mafunzo kwa Watumishi wa Umma; kutoa mafunzo ni jukumu la Serikali, hivyo kusomesha watumishi ni sawa na uwekezaji katika sekta ya miundombinu, nishati, afya na maji. Hivyo basi, umuhimu wa kuwaendeleza watumishi kila wakati haukwepeki. Unahitaji kutekelezwa ili kuwawezesha watumishi hao kuwa nguvu na injini ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia mazingira yaliyopo ya Waraka. Nimeainisha ni vitu gani ambavyo vinatakiwa kutekelezwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakwenda kwenye 36, kuzuia na kupambana na rushwa; pamoja na jitihada kubwa zinazofanyika dhidi ya rushwa bado hatujafanikiwa kwa sababu vita hii ni ya maeneo mawili ambayo ni rushwa ndogo ndogo ambayo ni *Systemic* na rushwa kubwa. Rushwa ndogo inagusa sana huduma za jamii afya, barabara, mahakamani, maeneo mengi ya kutoa huduma ambapo inabidi kutoa pesa ya soda au nauli vinginevyo unasota. Kwa hiyo Kambi Rasmi ya Upinzani tumetoa mapendekezo ambayo yapo *roman* (i) mpaka *roman* (iv).

Mheshimiwa Spika, naenda kwenye upande wa pili ambayo ni rushwa kubwa inayohusu uhujumu uchumi na utakatishaji fedha ambayo inasababisha upotevu mkubwa wa mapato ya Serikali. Hivyo, TAKUKURU inahitaji kuwezesha na kujipanga kuhakikisha mafisadi hao wanaohujumu uchumi na kutakatisha fedha wanakamatwa na kufikishwa kwenye vyombo vya sheria katika muda mfupi iwezekanavyo. Kumkamata mtuhumiwa na kumweka mahabusu kwa muda

mrefu kwa kisingizio cha upelelezi kutokukamilika ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna baadhi ya watumishi wamewekwa mahabusu kwa mwaka na zaidi baadaye wameachiwa kwa kusekana ushahidi wa kutosha. Je, Serikali itawajibika kwa madhira waliyoyapata ya kiuchumi kushindwa kuendesha maisha yao ya kujiongezea kipato au kisaikolojia? Serikali itawajibika na msongo wa mawazo uliowakumba kwa kuwa mbali na familia zao, au Serikali itafidiaje heshima ya wahusika iliyodhalilika mbele ya jamii? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, haya ni baadhi ya maswali Serikali inahitaji kuyajibu kwa kukamata watuhumiwa kabla ya upelelezi kukamilika. Kuweka *time frame* ya kuweka watumishi mahabusu itasaidia kwanza kuzuia viongozi wasiokuwa na hofu ya Mungu kutumia mwanya huu wa uhujumu uchumi na utakatishaji fedha kuonea wananchi, kulipiza visasi na hivyo kuweka mahabusu wananchi wasiokuwa na hatia kwa muda mrefu kwa kisingizio cha upelelezi unaoendelea.

Mheshimiwa Spika, pili ni kwa faida ya Serikali yenyewe endapo mtuhumiwa hatakuwa na hatia Serikali itaepuka kulipa fidia kwa wale wasiokuwa na hatia. Tunatambua kwamba kwa makosa yanayodhaminika mtuhumiwa kisheria anakaa mahabusu kwa muda wa siku 60; kwa ndugu zetu wa Zanzibar ni miezi tisa. Aidha, pendekezo letu sasa ni kwamba kwa maelezo niliyotoa hapo juu makosa ya jinai ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha yadhaminike ili haki itendeke na kuepusha wasio na hatia kuteseka bure mahabusu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzania inashauri yafuatayo:-

(i) Serikali ilete Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Uhujumu Uchumi na Utakatishaji wa Fedha ili makosa hayo yaweze kudhaminika.

(ii) Katika marekebisho hayo kuwepo na kipengele cha muda maalum wa mtuhumiwa kukaa mahabusu wakati upelelezi unaendelea, muda huo ukifika bila upelelezi kukamilika mtuhumiwa aachiwe huru kwa dhamana.

(iii) Vyombo vya Ulinzi na Usalama vihakikishe watuhumiwa wa makosa hayo wanapatikana na kupelekwa Mahakamani baada ya upelelezi kukamilika.

(iv) Vivyo hivyo Tume ya Kurekebisha Sheria (*Law Reform*) ifanye mapitio ya sheria mbalimbali ambazo baadhi ni tangu ukoloni na kuzifanyia marekebisho zierendane na mazingira ya uhuru, haki na demokrasia ya nchi yetu.

Mheshimiwa Spika, nitakwenda kwa ajili ya muda lakini naomba *speech* yangu yote iingie kwenye *hansard*. Ofisi ya Rais, ndio kila kitu katika utumishi wa umma, hivyo ofisi hii ikiwa na mfumo usioridhisha katika upatikanaji wa watendaji maana yake ni kwamba hata zao la kiutendaji litakuwa hafifu. Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri sana kuwa utumishi wa umma ndio wa kuiangusha Serikali au wa kuipaisha Serikali katika kufikia malengo iliyojiwekea. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Kambi Rasmi ya Upinzani inasisitiza jambo hili kutokana na ukweli kwamba watendaji wengi hasa wanaoteuliwa hawafanyiwi upekuzi wa kutosha kulingana na nafasi zao wanazopewa kiasi kwamba wanaiabisha Serikali. Baadhi yao wamewahi kutuhumiwa kwa kesi za jinai au maadili kwa vyovyote hawawezi kuwa viongozi wa mfano au kuaminiwa na wananchi wanawaongoza. Mifano ya wateule wa aina hii ipo aliyetia fora ni yule aliyefunguliwa shtaka la kujifanya mtumishi wa usalama wa Taifa, kiongozi aina hii hawezi kuzingatia utawala bora katika utekelezaji wake wa kazi. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana ni kengele ya pili malizia.

**MHE. RUTH H. MOLLEL - MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI KWA OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA**

**UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, ahsante naomba *speech* yangu yote iingie kwenye *hansard*. (Makofi)

**SPIKA:** Ahsante sana, *speech* yako yote kwenye *Official Hansard* itaingia isipokuwa yale mafungu 11,13 na 24 ambayo nakushukuru na wewe hukupoteza muda kuyapitia nakushukuru sana hotuba yako imekuwa *focused* imejielekeza kwenye mambo mahususi na mependekezo maalum yatafanyiwa kazi na Serikali. Umeonesha umahiri wako wa uzoefu wako na elimu uliyonayo katika masuala ya utumishi wa umma tunakushukuru sana. Ni matarajio yangu kwamba hotuba za upinzani zitaendelea kuwa zinaji-*focus* kama ilivyokuwa kwenye hotuba ya TAMISEMI, kama Mheshimiwa Ruth Mollel alivyojielekeza hivi sasa moja kwa moja.

Waheshimiwa Wabunge, haya mengine ya mahakamani, nyinyi wenyewe mnatuambia mambo yako mahakamani, mkitoka hapo mnayaandika nyinyi wenyewe, yaani ni mikanganyiko ambayo haina sababu, inatupa shida tu kila wakati, *politics* ambazo hazina maana lakini tuji-*focus* na hoja ambazo zinakuwa zimeletwa hapa, mtaona hatuna shida hata kidogo na mnaruhusiwa kupinga mnavyojisikia wala hakuna shida hata kidogo. (Makofi)

**HOTUBA YA MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI  
BUNGENI KATIKA OFISI YA RAIS – MENEJIMENTI YA UTUMISHI  
WA UMMA NA UTAWALA BORA, MHESHIMIWA RUTH HIYOB  
MOLLEL (MB), AKIWASILISHA BUNGENI MAONI YA KAMBI  
RASMI YA UPINZANI BUNGENI (KRUB) KUHUSU BAJETI YA OFISI  
HIYO, KWA MWAKA WA FEDHA 2020/21 - KAMA  
ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

*Yanatolewa chini ya Kanuni ya 99(9) ya Kanuni za Bunge,  
Toleo la Januari, 2016*

---

**A. UTANGULIZI**

**1. Mheshimiwa Spika,** kwa heshima kubwa napenda kuchukua nafasi hii kumshukuru Mungu kwa kunipa afya

njema na kuniwezesha kusimama mbele ya Bunge hili, kutoa maoni ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, kuhusu utendaji kazi wa Serikali, pamoja na makadirio ya mapato na matumizi ya fedha za Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

**2. Mheshimiwa Spika**, kwa umuhimu mkubwa, napenda kumshukuru Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo na Kiongozi wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni, Mheshimiwa Freeman Aikael Mbowe kwa kuendelea kuniamini na kunitewa kuwa Waziri Kivuli wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, naamini nimejitahidi kutimiza wajibu wangu ipasavyo.

**3. Mheshimiwa Spika**, hakuna mtu ajuaye kesho yake ila Mungu mwenyewe. Hivyo basi, katika hotuba yangu ya mwisho katika Bunge hili la 11, napenda kuchukua fursa hii kuwashukuru Makamanda wenzangu kwa ushirikiano mkubwa walionipa. Hakika nimejifunza mengi kutoka kwenu. Baraka za Mungu ziambatane nasi popote tutakapokuwa.

**4. Mheshimiwa Spika**, kwa upekee napenda kutoa shukrani zangu za dhiti kwa viongozi pamoja na wanachama wetu wa ngazi mbalimbali kwenye Kanda ya Pwani, na hususan Wilaya ya Mkuranga kwa ukomavu wao katika kutambua haki zao za msingi wakati wa kutekeleza majukumu yao ya kisiasa licha ya vitisho vingi kutoka kwa watendaji wanaolipwa kwa kodi za wananchi. Ninawatia moyo kwamba Tanzania inapita katika kipindi cha mpito kuelekea kwenye demokrasia ya kweli.

**5. Mheshimiwa Spika**, mwisho lakini kwa umuhimu mkubwa, naishukuru familia yangu kwa kunivumilia na kunipa moyo katika majukumu yangu haya ya Kibunge na kisiasa ambayo naendelea kujifunza. Nasema ahsante sana.

**6. Mheshimiwa Spika**, baada ya miaka takribani minne na zaidi, katika nafasi hii ya Uwaziri Kivuli, Utumishi na Utawala Bora nimekuwa nikitoa ushauri kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kwa Serikali kupitia hotuba zangu za kila



mwaka wakati wa kujadili bajeti ya ofisi hii. Kwa msingi huo nitajikita kwenye tathmini ya utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kambi ya Upinzani kwa muda wote wa uhai wa Bunge lako tukufu.

**7. Mheshimiwa Spika**, hotuba hii iliyo mbele ya Bunge lako tukufu imejikita katika mafungu yafuatayo yanayosimamiwa na Ofisi ya Rais;

- i. Fungu 20 - Ofisi ya Rais (Ikulu);
- ii. Fungu 30 - Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri;
- iii. Fungu 32 - Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma;
- iv. Fungu 33 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma;
- v. Fungu 67 - Ofisi ya Rais, Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma;
- vi. Fungu 94 - Ofisi ya Rais, Tume ya Utumishi wa Umma;
- vii. Fungu 09 - Ofisi ya Rais, Bodi ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma.

**8. Mheshimiwa Spika**, pamoja na mafungu hayo, Ofisi hii ya Rais inasimamia pia Taasisi ya Kupambana na Kuzuia Rushwa. Hata hivyo, nitazungumzia tu baadhi ya maeneo ambayo kwa maoni yangu yanahitaji msisitizo zaidi.

## **B. UTAWALA BORA**

**9. Mheshimiwa Spika**, Utawala Bora ni pamoja na kuzingatia misingi ya Katiba, Sheria, Kanuni, Miongozo, Demokrasia na kuheshimu haki za binadamu katika kuliongoza Taifa. Aidha Utawala Bora ni matumizi ya mamlaka yenye uwazi, uwajibikaji, ushirikishaji wa watu, ufanisi, tija, uadilifu na usawa unaofuata utawala wa sheria. Rasimu ya Pili ya Mheshimiwa Jaji Joseph Sinde Warioba na Katiba Pendekezwa inaainisha kwamba wananchi ndio msingi wa mamlaka yote na Serikali itawajibika kwa wananchi.

**10. Mheshimiwa Spika**, kwa msingi wa tafsiri hiyo, utawala bora una uhusiano wa moja kwa moja na maendeleo ya nchi kwa ujumla wake. Taasisi zinakuwa shirikishi na ushirikishwaji wa wananchi unakuwa chachu ya maendeleo.

Kama alivyowahi kusema Rais Mstaafu wa Marekani Barack Obama, kwamba nchi zetu zinahitaji "Taasisi na mifumo imara na si viongozi imara". Viongozi wanapita bali taasisi na mifumo imara ni vya kudumu.

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**12. Mheshimiwa Spika**, katika hotuba yangu Bungeni ya tarehe 14 Aprili, 2017 tulisema kwamba; *"Vyombo vya ulinzi na usalama vinapoilinda Serikali basi vinakuwa adui wa wananchi" na hicho ndicho kinachotokea sasa katika nchi yetu. Mtazamo wa kuilinda Serikali usipobadilika basi usalama upo mashakani, kwani ni dhahiri kwamba vyombo hivyo vinatagemea taarifa toka kwa wananchi. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri wahusika wajitafakari kwa amani ya nchi yetu".*

**[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**14. Mheshimiwa Spika**, kauli mbiu ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwa mwaka 2019/2020 ilikuwa ni " Ujenzi wa taasisi imara kwa maendeleo endelevu," ni dhahiri kwamba hatuna Katiba Mpya ambayo ni nguzo kuu ya ujenzi wa taasisi imara katika usimamizi na uendeshaji wa Serikali, lakini bado Ofisi ya Rais, hasa Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, kwa kutumia sheria zilizopo inatakiwa kuwa kioo cha jamii kwa kuhakikisha utawala bora unasimamiwa na kujenga utumishi wa umma uliotukuka, wenye ari na utashi wa kufanya kazi kwa msingi wa utu kwa kuzingatia sheria na kanuni zilizopo.

**15. Mheshimiwa Spika**, utawala bora ni dhana pana sana inajumuisha pia haki ya kuchagua na kuchaguliwa. Ili wananchi wawe na uwanja ulio sawa kuchagua viongozi wanaowataka wawakilishe katika kuisimamia Serikali, uwepo wa Tume Huru ya Uchaguzi nalo ni jambo ambalo haliepukiki ili kulinda haki za wananchi kuchagua viongozi wanaowafaa.

**16. Mheshimiwa Spika**, uwepo wa Tume Huru ni umuhimu kwa sababu tarehe 22/03/2020 huko Busokelo, Mbeya Mkurugenzi wa Manispaa ya Temeke Ndugu Mwakabibi akiwepo kwenye harambee ya kujenga zahanati, alionekana akiwa amevaa mavazi ya Chama cha Mapinduzi, na bila hofu kujitangaza kuwa ni Mbunge ajaye wa Jimbo la Busokelo, na alichangia mabati mia moja. Huyu DED pamoja na mkewe ambaye pia ni DED wa Biharamulo, Kagera walipiga kampeni kwa uwazi na kutoa rushwa kwa wananchi wa Busokelo. Viongozi hawa ni wasimamizi wa uchaguzi (**Returning Officers**) katika maeneo yao. Je, watatenda haki kweli kipindi cha uchaguzi wakati inaonekana waziwazi wameegemea upande wa Chama Tawala? Sio hivyo tu ametumia gari la ofisi ya umma kwenda kwenye harambee ya kampeni, huu si utawala bora na unatakiwa kupigwa vita kwa nguvu zote. Yu wapi Mwenyekiti wa Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma? Yu wapi Waziri wa Utumishi wa Umma?

**17. Mheshimiwa Spika**, huyu DED Ndugu Mwakabibi yeye amejitokeza wazi kwamba ni mwanachama wa CCM, wapo Wakurugenzi Watendaji wengi ambao ni wanachama wa CCM. Hivyo basi, kauli ya Mheshimiwa Rais kwamba uchaguzi utakuwa huru na wa haki itakuwa mashakani. Hivyo basi, Kambi Rasmi Upinzani inashauri yafuatayo:-

a. Tume ya Maadili imchukulie hatua za kinidhamu mtumishi wa umma kwa kujinasibu hadharani kwamba ni mwanachama wa Chama Tawala kinyume na maadili ya utumishi wa umma.

b. Serikali ilete muswada kwa masharti ya dharura Bungeni kurekebisha baadhi ya vipengele vya Katiba hususan Ibara ya 74 na 75 ili kuwezesha uundwaji wa Tume Huru ya Uchaguzi ili kuhakikisha uchaguzi wa mwezi Oktoba unakuwa huru, wa haki na wa amani.

**18. Mheshimiwa Spika**, baada ya uchaguzi wa Oktoba, CHADEMA itapata ridhaa ya kuongoza nchi hii, endapo uchaguzi utakuwa huru na wa haki. Jukumu la Serikali la kwanza ni kurekebisha sheria zote kandamizi zinazozuia

wananchi kutoa maoni yao kwa uhuru bila hofu yoyote. Wananchi ndio watakuwa mamlaka ya juu ya Serikali yao, Serikali hii itakuwa ya demokrasia ya kweli *“Government of the people by the people and for the people”*.

### C. UWAJIBIKAJI

19. **Mheshimiwa Spika**, uwajibikaji ni sehemu ya utawala bora. Bunge lako tukufu kwa muda wote wa miaka mitano limekuwa likipitisha bajeti ya mapato na matumizi kwa Wizara zote. Hata hivyo uzoefu umeonesha bajeti ya matumizi ya kawaida na maendeleo haitolewi na Serikali kama Bunge linavyokuwa limepitisha na wakati mwingine yanafanyika matumizi nje ya bajeti iliyopitishwa na Bunge hili. Kwa muktadha huo, ni dhahiri Serikali imeshindwa kuwajibika kabisa. Inakuwa vigumu kupima uwajibikaji kwa kuwa fedha zilizopitishwa zimetumika kwa jambo ambalo halikupangwa na kupitishwa na Bunge. Aidha, kama Serikali inashindwa kuwajibika ni kwa vipi watumishi watawajibika?

20. **Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kwamba Serikali ijayo iwe inatayarisha makisio ya mapato na matumizi kufuatana na mazingira halisi ya nchi, pili, iwasilishe Bungeni bajeti halisi kwa kuzingatia vipaumbele vya wananchi. Ni afadhali kutotenga kabisa fedha za miradi ya maendeleo na kuzielekeza kwenye maeneo ya vipaumbele, kuliko utamaduni uliojengeka wa kutenga fedha za maendeleo, lakini hazitolewi. Kutokutoa fedha kama ilivyopitishwa kunatia dosari uwajibikaji na “credibility” ya Serikali.

21. **Mheshimiwa Spika**, sitapenda kujadili kuhusu utawala wa sheria kwa sababu iko wazi kwa jinsi waliopewa dhamana wametumia madaraka yao vibaya “with impunity” bila kuadhibiwa. Wananchi wamekuwa wahanga wakuu kwa kubambikiziwa kesi. Wengi wako mahabusu au wamefungwa. Tumeshuhudia baadhi ya ma-DC, ma-RC wanavyoweka wananchi au watumishi mahabusu, kutoa maneno ya ukakakasi mbele ya wananchi bila ya soni kwa sababu ya ulevi wa madaraka. Wamesahau kabisa kwamba

wao ni watumishi wa umma. Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali kuhakikisha hadhi ya utumishi wa umma inalindwa kwa;

i. Kutoa mafunzo ya uongozi kwa wote wanaoteuliwa na Rais kabla ya kuanza kazi.

ii. Viongozi wote wa kisiasa wafanyiwe upekuzi kabla ya kupewa madaraka.

iii. Wanaopewa uongozi wasiwe na rekodi yoyote ya jinai/ maadili; kwa kuzingatia ushauri huo, tutapata viongozi wanaojitambua na wasiotiliwa shaka. Chuo cha Uongozi "Leadership College" kipo, fedha zitengwe ili viongozi wote wa juu wapate mafunzo kabla ya kuanza kazi.

#### **D. UCHUMI IMARA NI MATOKEO YA UTAWALA BORA**

**22. Mheshimiwa Spika**, ujenzi wa uchumi imara ni matokeo ya moja kwa moja ya utawala bora katika nchi au ukuaji wa uchumi ni lazima uende sambamba na utawala bora. Lakini katika nchi yetu kumekuwa na mambo yanayoifanya nchi yetu isiwe mahala salama kwa ajili ya uwekezaji. Mambo ambayo yanavutia uwekezaji ni pamoja na "**ujenzi wa taasisi imara na utawala wa sheria nchini.**"

**23. Mheshimiwa Spika**, utawala wa sheria na misingi ya utawala bora haitafanikiwa kama hatutaimarisha taasisi za kusimamia haki zilizoanzishwa kwa mujibu wa Katiba na Sheria za nchi yetu. Tukipuuza kuimarisha taasisi za kusimamia misingi ya sheria na haki tutaishia kutawaliwa na kauli za Wakuu wa Mikoa na viongozi wengine wa Serikali ambapo kauli zao kwa njia moja au nyingine zinafukuza au kuwatia hofu wawekezaji na kuifanya nchi yetu kuwa sio nchi salama kwa ajili ya uwekezaji.

#### **[MANENO YAMEONDOLEWA KWA MAELEKEZO YA KITI]**

**25. Mheshimiwa Spika**, lakini pia ikumbukwe kuwa ni kosa kutumia majukwaa ya Serikali kufanya shughuli za kisiasa au

kutumia mali na pia vyombo vya dola kukandamiza vyama vingine vya siasa. Haya yote yamekuwa yanafanyika wazi bila kificho na Serikali inaonekana kuyabariki yaendeleo huku wakijua mambo hayo yanajenga chuki miongoni mwa wananchi, na katika mazingira hayo ujenzi wa uchumi imara na endelevu utafikiwa lini?

**26. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inaishauri Serikali kutenganisha shughuli za Chama na Serikali, kodi za wananchi zitumike kwa shughuli za Serikali tu, kwa sababu kodi zinazokusanywa ni za Watanzania wote, wenye vyama na wasio na vyama. Matumizi yoyote ya rasilimali watu na fedha kunufaisha Chama Tawala ni sawa na matumizi haramu ya kodi za wananchi.

#### **E. UTUMISHI WA UMMA**

**27. Mheshimiwa Spika**, utumishi wa umma ndio nguzo na nyenzo kuu katika kuhakikisha utendaji wa Serikali unafikia viwango na kujikita katika utawala bora kwa muktadha wa misingi kumi ilivyonyumbulishwa katika Katiba Pendekezwa. Utumishi wa umma uliotukuka na wenye ari unazingatia sheria, kanuni na taratibu. Aidha, mbali ya sheria na kanuni pia kuna vyama vya wafanyakazi ambavyo ni daraja kati ya mwajiri na mwajiriwa, vyama vya wafanyakazi ni mdomo wa wananchi/wafanyakazi.

**28. Mheshimiwa Spika**, Tanzania ni nchi ya wakulima, wafugaji na wafanyakazi na ukweli ni kuwa toka awamu hii ya tano iingie madarakani vyama hivyo ni kama vimekufa na havifanyi kazi tena ya kuwatetea wanachama wao na badala yake, haijulikani viko upande gani. Kuna matukio kadhaa ambayo yametokea, pale watumishi wa umma wakisitishiwa ajira zao na wateule wa Rais kwenye mikutano au katika ziara za viongozi hao. Kadhaa hizo ziliwakuta walimu, madaktari, mainjinia na kadhalika, lakini hatukuwahi kusikia vyama vya wafanyakazi vikikemea udhalilishaji huo. Ni muhimu sana Vyama vya Wafanyakazi vikatekeleza majukumu ya kutetea wafanyakazi kwa mujibu wa sheria na kanuni za nchi.

**29. Mheshimiwa Spika**, toka awamu ya tano iingie madarakani, haijawahi kuongeza mishahara ya watumishi wa umma. Wamenyimwa hata zile nyongeza za kisheria kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu E 8. Mishahara yao imedumaa kwa miaka minne na zaidi mfululizo ilhali gharama za maisha zikiendelea kupanda. Watumishi wanahisi kutothaminiwa na hivyo kukosa ari na ubunifu wa kutimiza majukumu hivyo kurudisha nyuma maendeleo na kuongezeka kwa vitendo vya rushwa ndogo na kubwa.

**30. Mheshimiwa Spika**, inasikitisha kwamba pamoja na kunyimwa nyongeza za kila mwaka ambazo ziko kisheria, hata ile nyongeza ya May Day inayotolewa na Rais wakati wa kuadhimisha siku ya wafanyakazi duniani, kwa lengo la kuwasaidia watumishi kupunguza makali ya maisha na pia kama motisha haijawahi kutolewa na mwajiri namba moja. Watumishi wanasononeka na hawana raha.

**31. Mheshimiwa Spika**, ni rai ya Kambi Rasmi ya Upinzani kumkumbusha Mheshimiwa Rais kwamba ile kauli aliyoitoa kuwa hatapandisha mishahara hadi pale ujenzi wa (SGR) reli kwa kiwango cha standard gauge imefika Mwanza/Kigoma na umeme wa utakaokuwa umezalishwa katika Bwawa la Stiegler's umeingia kwenye gridi ya Taifa, aivunje na awaongeze watumishi mishahara kwani ahadi yake hiyo itachukua muda mrefu kutekelezeka na watumishi wa umma wataendelea kuumia.

**32. Mheshimiwa Spika**, licha ya kukiukwa kanuni zinazoainisha ongezeko la mishahara na kupandishwa kwa madaraja kwa watumishi wa umma, lakini hatujasikia vyama vya wafanyakazi kukemea na kutetea wafanyakazi. Jambo hili linazidi kutupa mashaka zaidi juu ya viongozi wa vyama hivyo katika utetezi wa wafanyakazi katika kuhakikisha wafanyakazi wanawajibika na pia wanapata stahili zao kulingana na sheria na kanuni.

**33. Mheshimiwa Spika**, nichukue fursa hii kwa mara nyingine tena, kuikumbusha Serikali kwamba bila rasilimali watu wenye furaha, ari na ubunifu, miradi yote inayotekelezwa

haitafanikiwa kwa kiwango kikubwa. Mitambo hiyo haitajiendesha yenyewe bali inahitaji wataalam wa kuisimamia. Hivyo Serikali isipuuze hata kidogo mchango wa rasilimali watu kwenye maendeleo endelevu ya nchi.

**34. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri Serikali kwamba kutokana na kupanda kwa gharama za maisha, na mishahara ya watumishi kutopandishwa kwa muda mrefu, watumishi wa umma walipwe nyongeza zao za kila mwaka kwa mujibu wa sheria. Aidha, kwa mamlaka aliyonayo kama mwajiri mkuu, Mheshimiwa Rais aruhusu watumishi wafanyiwe marekebisho ya mishahara (salary adjustment) na fedha zitengwe mwaka wa fedha 2020/2021 ili kuwapunguzia makali ya maisha.

**35. Mheshimiwa Spika**, katika hili la utumishi wa umma, tunafahamu kuwa nafasi za RCs na DCs kwa kiwango kikubwa ni utumishi wa kisiasa, lakini vilevile kwa kiwango kikubwa ni utumishi wa umma. Hivyo wahusika wanapokuwa katika kutekeleza majukumu yao kwa wananchi ni vyema kutoegemea mrengo wa kivyama. Tumeshuhudia mara kadhaa viongozi hawa wakiwa katika ukaguzi wa miradi au ufuatiliaji wa maelekezo ya Waziri Mkuu au Rais wakiwa katika mavazi ya Chama cha Mapinduzi. Mfano mzuri ni kwa RC wa Lindi na Manyara na DC wa Hai. Jambo hili ni kinyume kabisa cha utumishi wa umma. Kama Rais ambaye ni Mwenyekiti wa Chama na Waziri Mkuu wake hawajawahi kuonekana hadharani katika utendaji wao kuvaa nguo za chama, inakuwaje wasaidizi wao wanavaa nguo za chama? Au ni kutaka kuonesha kuwa wao ni wanachama zaidi ya viongozi wao?

**36. Mheshimiwa Spika**, Serikali inashauriwa irudi kwenye maadili ya utumishi wa umma, inayoainisha kwamba; Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya na Watendaji watambue dhamana waliyopewa na Watanzania ya kupewa nafasi za uongozi wa umma kupitia mkono wa Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ni kwa ajili ya kuwatumikia wananchi. Watambue kwamba mishahara yao na stahili zao zote zinatokana na kodi za wavuja jasho wa



nchi hii. Hivyo waelekezwe na kufundishwa kwamba katika majukumu yao ya umma hawapaswi kuonesha mrengo wa siasa.

## F. MAFUNZO KWA WATUMISHI WA UMMA

**37. Mheshimiwa Spika**, Mpango wa Pili wa Kukuza Uchumi na Kuondoa Umaskini Tanzania 2010/2011-2014 (MKUKUTA – II) uliopangwa kutekeleza Dira ya Taifa ya Maendeleo 2025, unasisitiza suala la kujenga uwezo, weledi, upangaji na matumizi mazuri ya rasilimali watu kuwa ni moja ya njia muhimu ya kuliwezesha Taifa kufikia Malengo ya Dira ya Maendeleo 2025.

**38. Mheshimiwa Spika**, kutoa mafunzo ni jukumu la msingi la Serikali, hivyo kusomesha watumishi ni sawa na uwekezaji katika sekta ya miundombinu, nishati, afya na maji. Hivyo basi, umuhimu wa kuwaendeleza watumishi kila wakati haukwepeki. Unahitaji kutekelezwa ili kuwawezesha watumishi hao kuwa nguvu na injini ya Serikali katika kutekeleza majukumu yake ipasavyo kwa kuzingatia mazingira yaliyopo. Waraka Na. 5 wa mwaka 2011 unasisitiza kwamba:-

i. Watumishi wanaojirwa kwa mara ya kwanza wapatiwe mafunzo elekezi (induction course) ya awali ndani ya kipindi cha miezi mitatu tangu kuajiriwa. Inashauriwa pia wapewe mitihani kutathimini uelewa wao, wale wanaoshindwa kufaulu wasiajiriwe. Mchujo huu utawezesha kupata watumishi wenye dhamira na utashi.

ii. Waajiri wote wahakikishe kwamba watumishi wapya wafanyiwe upekuzi (vetting) kwanza na kupatiwa mafunzo elekezi yanayohusiana na majukumu yao.

iii. Waajiri wote wanapaswa kutenga fedha kwenye bajeti ya kila mwaka kwa ajili ya mafunzo ya awali na ya kitaalamu kwa walio kazini. Vilevile Serikali ihakikishe bajeti hiyo inatolewa.

**39. Mheshimiwa Spika**, licha ya maelekezo hayo waajiriwa wamekuwa wakitenga bajeti kidogo au kutotenga kabisa kwa ajili ya mafunzo. Mafunzo yamekuwa hayapewi kipaumbele kabisa katika bajeti za Wizara mbalimbali, madhara ya kutotenga bajeti kwa ajili ya mafunzo yamekuwa dhahiri zaidi hasa kwa wateule wa Rais ambao hawajui wala kuelewa jinsi Serikali inavyoendeshwa au maadili ya kuzingatiwa katika utumishi wa umma.

**40. Mheshimiwa Spika**, tumeshuhudia baadhi ya wateule wa Rais, Mawaziri, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya wakitoa kauli ambazo hazistahili kutolewa na viongozi wa umma. Kuna mifano mingi, wa hivi karibuni ni wa tarehe 05/03/2020 kule Ngorongoro kwenye *Pass out parade* ya majeshi usu (*Parlamilitary*) ambapo Waziri wa Maliasili na Utalii, aliwadhalilisha Maaskari wa Wanyama Pori waliokuwa wanatunukiwa vyeo baada ya kuhitimu mafunzo. Aliwauliza maswali ambayo hayakuwa na uhusiano wowote na kazi zao. Wale waliokosea walidhalilishwa na mmoja wao walirushwa kichura mbele ya familia yake, wasaidizi (surbodinates) na wageni wengine waalikwa.

Tunalaani kitendo hicho cha udhalilishaji, ukiukwaji wa maadili, uonevu na matumizi mabaya ya madaraka. Tunaitaka Serikali kuliambia Bunge lako tukufu Waziri huyu amepewa mamlaka hayo chini ya sheria au kanuni gani? Hii inaonesha kwamba bado hawajitambui na hawajui dhamana kubwa waliyopewa. Ni muhimu sasa Serikali ikatengeneza mfumo wa mafunzo kwa viongozi wa kisiasa katika utumishi wa umma ili waelewe Serikali inavyoendeshwa (Government Administration), watambue dhamana waliyopewa, wajibu na mipaka ya kazi zao.

**41. Mheshimiwa Spika**, nimeendelea kushauri kuhusu mafunzo kwa wateule wa Rais kwa sababu naona bado Serikali haijachukua hatua madhubuti kuhusu mafunzo, bado baadhi yao hawatoi taswira nzuri ya Serikali. Hatua zingine za kuchukua ni kupewa onyo au hata kutenguliwa nafasi zao. Tunashauri Serikali itakayoingia madarakani itoe kipaumbele kwenye mafunzo ili kuwajengea uwezo.

## G. TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA (TAKUKURU)

**42. Mheshimiwa Spika**, pamoja na jitihada kubwa zinazofanyika dhidi ya rushwa bado hatujafanikiwa kwa sababu vita hii ni ya maeneo mawili:-

- Rushwa ndogo ndogo “Systemic” ambayo ni ya mifumo.
- Rushwa kubwa.

Rushwa ndogo inagusa sana huduma za jamii na inawaathiri sana wananchi wenye uchumi mdogo. Rushwa zipo sana upande wa afya, barabarani, mahakamani na maeneo yote ambayo wananchi wanapewa huduma. Ili upate huduma haraka inabidi kutoa pesa ya soda au nauli vinginevyo utasota. Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inapendekeza yafuatayo:-

(i) Serikali itenge fedha zaidi kupanua Mfumo wa **TEHAMA** ili huduma nyingi iwezekanavyo zitolewe kwa mtandao.

(ii) Kuendelea kutoa elimu wananchi wajue huduma wanayopata ni haki yao ni sio fadhila.

(iii) Serikali iwapatie **TAKUKURU** bajeti ya kutosha ili watelekeze wajibu wao.

(iv) Wapatiwe watumishi wa kutosha na Ofisi ziwepo hadi Wilayani na wajengewe uwezo ndani na je ya nchi ili wajifunze mbinu mpya.

(v) **TAKUKURU** iweke mfumo wa kuwepo motisha kwa raia wema wanaotoa taarifa kuhusu rushwa.

**43. Mheshimiwa Spika**, kwa upande wa pili kuna rushwa kubwa inayohusu kuhujumu uchumi na utakatishwaji fedha ambazo zinasababisha upotevu mkubwa wa mapato kwa Serikali. Hivyo basi **TAKUKURU** inahitaji kuwezesha na kujipanga kuhakikisha mafisadi hao wanaohujumu uchumi na kutakatisha fedha wanakamatwa na kufikishwa kwenye

vyombo vya sheria katika muda mfupi uwezekanavyo. Kumkamata mtuhumiwa na kumuweka mahabusu muda mrefu kwa kusingio cha upelelezi kutokukamilika ni ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu. Kuna baadhi ya watuhumiwa wamewekwa mahabusu kwa mwaka na zaidi, baadaye wameachiwa kwa kukosekana ushahidi wa kutosha. Je, Serikali itawajibika kwa madhila waliyoyapata ya;

i. Kiuchumi: kwa kushindwa kuendesha maisha yao ya kujiongezea kipato?

ii. Kisaikolojia: Serikali itawajibika na msongo wa mawazo uliowakumba kwa kuwa mbali na familia zao.

iii. Kadhalika: Serikali itafidiaje heshima ya wahusika iliyodhalilika mbele ya jamii.

Haya ni baadhi ya maswali Serikali inahitaji kuyajibu kwa kukamata watuhumiwa kabla ya upelelezi kukamilika.

**44. Mheshimiwa Spika**, kuweka “time frame” ya kuweka watuhumiwa mahabusu itasaidia kwanza kuzuia viongozi wasiokuwa na hofu ya Mungu kutumia mwanya huu wa uhujumu uchumi na utakatishaji fedha, kuonea wananchi, kulipiza visasi na hivyo kuweka mahabusu wananchi wasiokuwa na hatia kwa muda mrefu kwa kisingizio cha upelelezi unaoendelea.

Pili, ni kwa faida ya Serikali yenyewe endapo mtuhumiwa hatakuwa na hatia, Serikali itaepuka kulipa fidia kwa wale wasiokuwa na hatia. Tunatambua kwamba kwa makosa yanayodhaminika mtuhumiwa kisheria anakaa mahabusu kwa muda wa siku sitini, kwa ndugu zetu wa Zanzibar ni miezi tisa. Aidha, pendekezo letu sasa ni kwamba kwa maelezo niliyoyotoa hapo juu makosa ya jinai ya uhujumu uchumi na utakatishaji fedha yadhaminike ili haki itendeke na kuepusha wasio na hatia kuteseka bure mahabusu.

**45. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni inashauri Serikali yafuatayo:-

i. Serikali ilete Muswada wa Marekebisho wa Sheria ya Uhujumu Uchumi na Utakatishaji wa Fedha ili makosa hayo yaweze kudhaminika.

ii. Katika marekebisho hayo kuwepo na kipengele cha muda maalum wa mtuhumiwa kukaa mahabusu wakati upelelezi unaendelea, muda huo ukifika bila upelelezi kukamilika mtuhumiwa aachiwe huru kwa dhamana.

iii. Vyombo vya Ulinzi na Usalama vihakikishe watuhumiwa wa makosa hayo wanapatikana na kupelekwa Mahakamni baada ya upelelezi kukamilika.

iv. Vivyo hivyo Tume ya Kurekebisha Sheria "Law Reform Commission" ifanye mapitio (review) ya sheria mbalimbali ambazo baadhi ni tangu ukoloni na kuzifanyia marekebisho ziendane na mazingira ya uhuru, haki na demokrasia ya nchi yetu.

**46. Mheshimiwa Spika**, wahenga walisema, *"kuishi kwingi ni kuona mengi"*, kumezuka aina nyingine ya rushwa ambayo inaanza kuwa donda ndugu hapa kwetu, na aina hii ni mbaya na inayoifilisi nchi yetu, bila uelewa ni ile ambayo watu walioaminiwa na wapiga kura na kabla ya kumaliza muhula wao wa Kikatiba wanadai kwa hiari yao kuhama chama na kujiunga na chama kingine na kuruhusiwa kugombea nafasi ile ile bila mchakato wa ushindani ndani ya chama husika, ni aina mpya ya rushwa ambayo hajjawahi kutokea. Uchaguzi huo wa marudio haukuwa na tija yeyote kwa wananchi wetu, umaskini na shida zao ziko pale pale. Kodi yao ambayo ingetumika kuboresha huduma za jamii zimetumika kwa jambo lisilokuwa na faida yoyote kwao.

Wakati Jaji Warioba anafanya utafiti wake kuhusiana na rushwa na kuwasilisha taarifa yake ya Corruption and the State ya mwaka 1996 rushwa ya aina hiyo haikuwepo hapa Tanzania. Ni vyema kama TAKUKURU wangetuambia ni kiasi

gani cha fedha nchi imepoteza kwa mchezo huu wa rushwa katika siasa ili Watanzania waone jinsi gani rasilimali zao zinavyoangamizwa na hao wanaojiita wawakilishi wao. Msajili wa Vyama vya Siasa arekebishe sheria na kuainisha utaratibu sahihi wa kuhama vyama na kugombea nafasi za uongozi.

**47. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni imetoa maoni mara nyingi kwamba Taasisi hii haiko huru kwa jinsi inavyofanya kazi zake. Mosi, taasisi hii iko chini ya Ofisi ya Rais - Ikulu, na pili kushindwa kuendesha kesi bila kupata idhini ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) ambaye pia ni mteule wa Rais. Hivyo DPP kuwa na mamlaka ya kuamua kesi gani iende mahakamani au la.

**48. Mheshimiwa Spika**, kama ambavyo nimekwishaainisha, kukamata watuhumiwa bila ushahidi wa kutosha na mahabusu kukaa muda mrefu, kunatoa tafsiri kwamba uhuru na utendaji kazi wa taasisi umefinywa sana. Kambi Rasmi ya Upinzani katika hilo ikawa na hoja, je, ni sheria ya uanzishwaji wake ndio inainyima uhuru TAKUKURU au kukaa chini ya kivuli cha Ofisi ya Rais, Ikulu? Hivyo basi kwa vyovyote itakavyokuwa tunazidi kuishauri Serikali kuhakikisha uimara wa taasisi hii na uimara wa taasisi ni uhuru wake wa kufanya kazi bila ya kuingiliwa na mamlaka nyingine yoyote.

**49. Mheshimiwa Spika**, kuonesha kuwa kuna tatizo katika taasisi hii Vyama vya Upinzani vimetoa ushahidi mara kadhaa kuhusiana na makubaliano haramu ambayo yamekuwa yakifanywa baina ya wawakilishi wa wananchi toka Vyama vya Upinzani na Chama Tawala ili kujivua uanachama wao, lakini hatujawahi kuona taarifa ya TAKUKURU kuhusu jambo hilo. Hapo kuna ulakini mkubwa kwenye suala hilo, pia kumekuwepo na hisia hasi kuwa inakuwaje TAKUKURU inawakamata wafanyabiashara kuwa wameiibia Serikali bila ya watumishi wa Serikali kuhusika? Mapesa yaliyochotwa kwenye akaunti ya Escrow iliyo Benki Kuu, watumishi wa BOT na Hazina ni akina nani walioshirikiana na wale watuhumiwa walio Segerea na kesi zao zinasikilizwa wapi?

**50. Mheshimiwa Spika**, kama nilivyoainisha kwenye aya ya 23, kunahitajika taasisi imara. TAKUKURU ni kati ya Taasisi zinazotakiwa kuwa imara na kufanya kazi zake kwa uhuru. Uhuru huu utakuwepo tu endapo uteuzi wa Mkurugenzi Mkuu utatafutwa utaratibu mwingine, Rais ateue Mkurugenzi miongoni mwa majina aliyopewa na jopo la uteuzi na baadae athibitishwe na Bunge lako tukufu utaratibu wa kumtoa, vilevile ufanyiwe uchunguzi na jopo na mapendekezo ya kumtoa au la yapelekewe Rais. Utaratibu huu utamuwezesha Mkurugenzi kufanya kazi zake kwa uhuru na weledi, kuna usemi “You can not bite the hand that feeds you” ugumu wa kutolewa kwa Mkurugenzi utamuwezesha kufanya kazi zake bila kuogopa kutumbuliwa. Hivyo basi, miundo na mifumo ya Taasisi iangaliwe upya na kufanyiwa marekebisho kama Serikali ina dhamira ya kusimamia utawala bora.

#### **H. TUME YA MAADILI YA VIONGOZI**

**51.Mheshimiwa Spika**, kwa mujibu wa Katiba ya Tanzania Ibara ya 132(1) Tume ya Maadili ya Viongozi wa Umma imeanzishwa kwa Sheria Na. 13 ya mwaka 1995 na marejeo yake kwenye Marekebisho ya Sheria Na. 5 ya mwaka 2001, kwamba; *“kutakuwa na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma ambayo itakuwa na mamlaka ya kuchunguza tabia na mwenendo wa kiongozi wa umma yeyote kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba masharti ya Sheria ya Maadili ya Viongozi wa Umma yanazingatiwa ipasavyo.”*

**52.Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Tume ya Maadili ipo chini ya Ofisi ya Rais, japokuwa inasemekana kuwa ni ofisi huru, lakini kwa muktadha wa ofisi hiyo kuwa chini ya Ofisi ya Rais ni dhahiri kwamba uhuru wa ofisi hiyo katika utendaji wake unatia mashaka makubwa. Hili linathibitishwa na ukweli kwamba Ofisi ya Tume imeshindwa kuchukua hatua pale panapotokea malalamiko ya kimaadili dhidi ya wateule wa Rais.

**53.Mheshimiwa Spika**, Tume haijawahi kuchukua hatua zozote dhidi ya viongozi walioshtakiwa, mbali ya kufanya mahojiano na viongozi mbalimbali kuhusiana na mali zao

walizoandika kwenye fomu za Tamko la Maadili. Hili ni tatizo kubwa, kwani kuna malalamiko mbalimbali kuhusiana na maadili ya viongozi wa umma lakini hayafanyiwi kazi na taarifa zao kutolewa hadharani kama ambavyo waleta malalamiko wanavyofanya. Kuna malalamiko ya Mayor wa Ubungo dhidi ya Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, malalamiko dhidi ya aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Arumeru Mashariki na sasa Mkuu wa Mkoa wa Manyara, na pia kuna malalamiko dhidi ya Mkuu wa Wilaya ya Hai juu ya utendaji kazi wake. Wahusika waliowasilisha malalamiko yao hawajawahi kupata feedback wala umma kujulishwa hatua zilizochukuliwa.

**54.Mheshimiwa Spika**, wasiwasi wetu kuhusu utendaji wa Tume ya Maadili kukosa meno unatokana na utaratibu kwamba, hata baada ya uchunguzi na kiongozi kukutwa na kesi ya kujibu kwa mujibu wa Ibara 23(2) (a) - (b) ya Sheria ya Maadili Namba 13 ya 1995 inabidi Kamishna amtaarifu kwanza Rais au Spika kabla ya kuchukua hatua zaidi. Hatua hii ndipo kuna “discretionary powers” kama Kamishna aendelee na hatua zaidi au la Ibara ***“23(4) The Commissioner shall notify the President and Speaker of the allegation and shall offer consultation with the Attorney General and Chief Justice, appoint a tribunal to investigate the allegation”***.

**55. Mheshimiwa Spika**, urasimu wa kupata kibali cha Rais au Spika uondolewe na Kamishna baada ya kuridhika kwamba kuna kesi ya kujibu apewe madaraka ya kuwasiliana moja kwa moja na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Jaji Mkuu ili tribunal iundwe kuchunguza tuhuma hizo. Kamishna awe na utaratibu wa kutoa taarifa kila robo mwaka kwa Mheshimiwa Rais na Mheshimiwa Spika za kesi zilizoshughulikiwa. Utaratibu huu utaepusha utamaduni wa kulindana katika utumishi wa umma.

Kambi Rasmi ya Upinzani inapendekeza kwamba sasa ni muda muafaka kwa chombo hiki cha Kikatiba kuwa huru na kutoka katika bawa la Ofisi ya Rais, kwa kurekebisha sheria ya utendaji kazi wake ili kukidhi matakwa ya Kikatiba ya uanzishwaji wake. Aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri



Ili Tume ya Maadili iwe ni tume huru katika utendaji kazi wake ni vyema mapendekezo yaliyotolewa katika Katiba Pendekezwa kuanzia Ibara ya 228 hadi 234 pamoja na Rasimu ya Pili ya Katiba ya Jaji Warioba kuanzia Ibara ya 200 - 207 yazingatiwe.

## I. OFISI YA RAIS

**56. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais ndio kila kitu katika utumishi wa umma, hivyo ofisi hii ikiwa na mfumo usioridhisha katika upatikanaji wa watendaji maana yake ni kwamba hata zao la kiutendaji litakuwa ni hafifu. Vilevile Kambi Rasmi ya Upinzani inashauri sana kuwa utumishi wa umma ndio wa kuiangusha Serikali au kuipaisha Serikali katika kufikia malengo inayojiwekea.

**57. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi inasisitiza jambo hili kutokana na ukweli kwamba watendaji wengi hasa wanaoteuliwa hawafanyiwi upekuzi wa kutosha kulingana na nafasi zao wanazopewa kiasi kwamba wanaiabisha Serikali. Baadhi yao wamewahi kutuhumiwa kwa kesi za jinai au maadili kwa vyovyote hawawezi kuwa viongozi wa mfano au kuaminiwa na wananchi wanaowaongoza. Mifano ya wateule wa aina hii ipo aliyetia fora ni yule aliyefunguliwa shitaka la kujifanya mtumishi wa Usalama wa Taifa (impersonation). Kiongozi wa aina hii hawezi kuzingatia utawala bora katika utendaji wake wa kazi. Anasumbua sana watumishi wa umma na wafanyabiashara. Pamoja na madaraka makubwa aliyopewa ameshindwa kurekebisha tabia yake kukidhi matarajio na maadili ya utumishi wa umma.

**58. Mheshimiwa Spika**, vyombo vikuu vya kutafuta na kutoa taarifa mbalimbali za uchunguzi viko chini ya mamlaka ya Ofisi ya Rais. Madhumuni ya kuwa chini ya ofisi hiyo ni ili kumuwezesha Mheshimiwa Rais kupata taarifa sahihi na kwa wakati kumuwezesha kufanya maamuzi sahihi kwa ustawi wa Taifa. Maamuzi hayo ni pamoja na taarifa za watarajiwa kabla ya teuzi. Inakuwaje sasa Mheshimiwa Rais anateua

watumishi ambao rekodi zao ni mbaya na zinafahamika na umma?

**59. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani inaishauri Serikali kutathmini upya utendaji na mifumo ya ofisi hii ili iendane na teknolojia ya kisasa, ofisi hii ianze utaratibu wa kufuatilia mienendo ya watumishi waandamizi ambao ndio baadae wanateuliwa kushika nafasi za uongozi. Ufuatiliaji huu na kutengeneza kanzi data, utasaidia kupata taarifa sahihi kwa wakati inapohitajika.

**60. Mheshimiwa Spika**, Ofisi ya Rais ni ofisi nyeti sana ambayo haitakiwi kunyooshewa kidole au kutuhumiwa kwa jambo lolote. Utaratibu ulionzishwa wa kuhamishia shughuli za utendaji zinazohusisha manunuzi makubwa ya ndege na kadhalika kwenye ofisi hii litafakariwe kwa kina. Itakuwa vizuri shughuli hizi za utendaji hasa manunuzi zitabaki katika Wizara husika ili kukitokea makosa au ukiukwaji wa taratibu Ofisi ya Rais isihusike ili iwe na uhalali "moral authority" ya kukemea na kuchukua hatua stahiki.

## **J. BODI YA MISHAHARA NA MASLAHI KATIKA UTUMISHI WA UMMA**

**61. Mheshimiwa Spika**, chombo kilianzishwa kwa mujibu wa Ibara ya 36(1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Ibara hiyo inampa mamlaka Mheshimiwa Rais kuanzisha chombo hicho kupitia Waraka Maalum wa Rais uliochapishwa kwenye Gazeti la Serikali Na. 162 la Juni 3, 2011; kikiwa na jukumu kubwa la kufanya marekebisha ya mishahara ya watumishi mara kwa mara kulingana na madaraja yao na stahili zingine za watumishi (**kurekebisha mfumo mzima wa mishahara na marupurupu ya watumishi mara kwa mara**) na kumshauri Mheshimiwa Rais kuhusiana na mapendekezo hayo.

**62. Mheshimiwa Spika**, tangu Serikali ya awamu ya tano imeingia madarakani hadi sasa watumishi wa umma hawajapata stahili zao za nyongeza za mishahara hadi sasa, ila kwa kuwa huu ni mwaka wa uchaguzi hatutashangaa

nyongeza hizo zikatolewa sasa ili kuwafumba macho watumishi ambao wameishi kwa ukata mkubwa kwa kipindi chote hicho. Kama ikitokea hivyo ni dhahiri jambo hilo halitakuwa na nia njema katika muktadha wa utawala bora bali ni kuwarubuni watumishi ili waichague tena CCM ile ile iliyowatesa katika Uchaguzi Mkuu wa mwezi Oktoba.

**63. Mheshimiwa Spika**, aidha, Kambi Rasmi ya Upinzani inapata mashaka kama kweli Bodi hii ya Mishahara na Maslahi katika Utumishi wa Umma inatimiza majukumu yake, kwani watumishi hawaoni matokeo yake kwa kipindi chote hicho. Kama ndio hivyo, imeshindwa kuwajibika na kungoja huruma za Mheshimiwa Rais wakati wa Sikukuu ya Wafanyakazi Duniani, Mei Mosi ndio wapate ahueni. Hivyo basi chombo hiki kiwezeshe kwa fedha na rasilimali kiweze kutimiza wajibu wake kwa mujibu wa sheria. Ikiwa hakipewi fedha za kutafiti na kutoa mapendekezo ya mishahara kwa ngazi mbalimbali kwa kujibu wa miundo ya utumishi ni dhahiri kodi ya Watanzania haitumiki ipasavyo kwa tija basi kifutwe ili bajeti hiyo ielekezwe kwenye maeneo ya huduma za jamii.

## K. UTEKELEZAJI WA BAJETI

**64. Mheshimiwa Spika**, Kambi Rasmi ya Upinzani kama sehemu ya Bunge imepitia kasma mbalimbali kwa kila fungu chini ya Ofisi ya Rais ili kuelewa ni kwa jinsi gani Serikali inawajibika kwa Bunge, kwa kuzingatia yote ambayo yamepitishwa na Bunge kutekeleza miradi ya maendeleo.

**65. Mheshimiwa Spika**, baada ya kupitia utekelezaji wa bajeti kuu kwa mwaka wa fedha 2019/2020 inaonesha kwamba bajeti ya fedha za maendeleo zilizotolewa hadi sasa ni shilingi trilioni 6.22 sawa na asilimia 50.8 kati ya shilingi trilioni 12.24 za bajeti ya mwaka mzima.

**66. Mheshimiwa Spika**, Randama inaonyesha kwamba mwaka wa fedha 2019/2020 Ofisi ya Rais Fungu 30 linalojumuisha Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri na Taasisi zingine chini ya Ikulu waliidhinishiwa jumla ya **bilioni 564,312,423,717.00** kati ya fedha hizo **bilioni 154,169,384,717.00**

zilikwa ni kwa ajili ya miradi ya maendeleo zilizokuwa zimepokelewa hadi Februari, 2020 ni **bilioni 67,852,222,710.00** kwa kuwa taasisi kama TAKUKURU na Usalama wa Taifa nazo ziko chini ya Ofisi ya Rais, Kambi Rasmi ya Upinzani ingependa kupata ufafanuzi wa mgawanyo wa hizo fedha kwa Taasisi.

**67. Mheshimiwa Spika**, Fungu la 32 la Menejimenti ya Utumishi wa Umma pamoja na Wakala zake kwa mwaka 2019/2020 waliidhinishiwa jumla ya **bilioni 72,572,322,000.00** kati ya fedha hizo **41,000,000,000.00** zilikuwa za maendeleo. Hata hivyo hadi Februari, 2020 zilikuwa zimetolewa **bilioni 1,496,660,846.55** sawa sawa na asilimia 3.64 tu. Kwa mwaka wa fedha 2020/2021 wanaomba kuidhinishiwa jumla ya **bilioni 36,423,578,000.00** na kati ya hizo **bilioni 3,500,000,000.00** ni fedha za maendeleo.

**68. Mheshimiwa Spika**, kwa mtiririko wa utekelezaji wa bajeti ni dhahiri kuwa Serikali haitoi fedha kama zilivyoainishwa na Bunge lako tukufu hasa kwenye miradi ya maendeleo. Tunaishauri Serikali kwamba badala ya kutenga fedha za miradi ya maendeleo ambazo hazitolewi ni bora zisitolewe na kuelekezwa kwenye miradi ya kipaumbele na Bunge liidhinishe kwa ajili ya miradi hiyo, kuliko kuelekeza kwenye miradi ya maendeleo ambayo haitekelekezi.

## L. HITIMISHO

**69. Mheshimiwa Spika**, kwa miaka minne na zaidi mfululizo, Kambi Rasmi ya Upinzani, imeendelea kuishauri Serikali kuhusu ukiukwaji mkubwa wa haki za binadamu, uhuru wa kutoa maoni, uonevu kwa wananchi, uminywaji wa shughuli za kisiasa ambazo ziko kwa mujibu wa Katiba. Madhila haya yote yanaongeza chuki kwa Serikali. Kukosekana kwa uvumilivu wa itikadi tofauti za kisiasa umeligawa Taifa na hivyo kuhatarisha umoja wa mtangamano wananchi. Kwa mara nyingine tena tunaishauri Serikali kuongoza Taifa kwa mujibu wa Katiba, kanuni na taratibu tulizozitengeneza wenyewe. Uzingatiaji huo ndio utaliponya Taifa letu.

**70. Mheshimiwa Spika**, hakuna mtu wala chama kinachoshabikia ufnasidi au uhujumu uchumi. Wote tunataka kuona wahalifu hao wanachukuliwa hatua za kisheria bila kukiuka haki za raia. Serikali haitendi haki kuweka watuhumiwa mahabusu kwa miaka kwa kisingizio cha upelelezi kutokamilika. Kuna uwezekano mkubwa mwanya huu ukatumiwa na wenye mamlaka kuonea, kulipiza visasi dhidi ya wananchi wasiokuwa na hatia. Sheria hizo za Uhujumu Uchumi, Utakatishaji Fedha zifanyiwe marekebisho ili makosa hayo yadhaminike ili kunusuru wananchi wasio na hatia kuozea mahabusu.

**71. Mheshimiwa Spika**, rasilimali watu ndio injini ya maendeleo, bila watumishi wenye weledi, ari na ubunifu maendeleo ya nchi yatarudi nyuma sana. Serikali ichukue hatua za makusudi kuwalipa watumishi vizuri, kuwapatia mafunzo ya mara kwa mara, ndani na nje ya nchi na kuweka mifumo madhubuti ya kupima utendaji kazi ili kuongeza tija na uwajibikaji.

**72. Mheshimiwa Spika**, taasisi za usimamizi na uwajibikaji zinazomsaidia Rais, kwa maana ya TAKUKURU na Tume ya Maadili, zifanyiwe tathmini upya kuendana na mapendekezo yaliyotolewa kwenye Katiba Pendekezwa ili ziweze kufanya kazi zao kwa haki na uhuru bila upendeleo au woga. Waingereza wanasema, "*you can't bite the hand that feeds you*" kwa hakika wateuliwa wa Rais hawawezi kufanya kitu chochote kinyume na matakwa ya mwajiri wao ambaye ni Rais wa Jamhuri ya Muungano.

**73. Mheshimiwa Spika**, nihitimishe kwa kuishauri Serikali kwamba pamoja na tofauti zetu za kiitikadi, Tanzania ni yetu sote na kwamba tutaijenga au kuibomoa sisi wenyewe. Naishauri Serikali ifanyie kazi mapendekezo yetu ili utawala bora katika nchi yetu uwe chachu ya maendeleo.

**74. Mheshimiwa Spika**, kutokana na hali halisi kuwa Bunge linapitisha bajeti kwa ajili ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo na matumizi ya kawaida lakini mara zote takwimu za utekelezaji wa bajeti zinazoletwa Bungeni ni kwamba mara zote utekelezaji unakuwa chini ya asilima 60.

Tunatambua pia Sheria ya Fedha inampa mamlaka Mheshiwa Waziri wa Fedha kuhamisha fedha kutoka kasma moja kwenda nyingine, kutekeleza shughuli/miradi ambayo bajeti yake ilipitishwa na Bunge lako tukufu tu, si vinginevyo supplementary budget iletwe na kuidhinishwa na Bunge lako.

Uzingatiaji wa sheria na kanuni za fedha "*financial discipline*" ni sehemu ya utawala bora na uwajibikaji. Kutokana na utekelezaji hafifu wa bajeti hasa kwenye miradi ya mendeleo na tofauti kubwa iliyokuwepo kati ya makisio ya mapato na mapato halisi yanayopatikana kunaipa uhalali Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni kupiga kura ya **HAPANA** wakati wa kupitisha bajeti.

Ushauri wa Kambi Rasmi ya Upinzani Bungeni ni kwamba Serikali ipange bajeti kulingana na hali halisi ya upatikanji fedha. Uzoefu wa miaka iliyopita ni kigezo kizuri cha kufanya makisio ya mapato kwa mwaka unaofuata.

**75. Mheshimiwa Spika**, baada ya kusema hayo kwa niaba ya Kambi Rasmi ya Upinzani, naomba kuwasilisha.

.....  
Ruth H. Molle (Mb)

**MSEMAJI MKUU WA KAMBI RASMI YA UPINZANI-  
OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA  
UTAWALA BORA**

14 Aprili, 2020

**SPIKA:** Sasa katika uchangiaji wetu tunao wachangiaji wetu kidogo na muda hauko upande wetu, mitaanza namchangiaji wa *CUF* ambaye ni Mheshimiwa Hamidu Bobali yeye atachangia kwa niaba ya Mheshimiwa Suleiman Juma Bungara, kwa sababu Mheshimiwa Bungara nimefahamishwa hapa amepata msiba wa ghafla wa binti yake Bi. Salma Suleiman Bungara, binti yake wa miaka 35 ambaye amefariki leo saa saba mchana huko Kilwa Kivinje. Kwa hiyo imebidi Mheshimiwa Bungara aondoke ghafla kuelekea huko kwa ajili ya maandalizi ya mazishi,

tunamuomba marehemu kwa Mwenyezi Mungu ili aiweke roho yake mahali pema peponi.

Waheshimiwa Wabunge, kwa hatua hiyo sasa nikamkaribishe Mheshimiwa Hamidu Bobali dakika 10 tafadhali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ....

**SPIKA:** Attafuatiwa na Mheshimiwa Emmanuel Kingu Elibariki ambaye yeye atachangia kutoka Msekwa na nimwombe Mheshimiwa Upendo na yeye aelekee Msekwa baada ya muda sio mrefu nitamwita atachangia kutoka kule. Mheshimiwa Bobali tafadhali.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa fursa hii. Kwanza niendeleo na mimi kumwomba kijana wetu ambaye amefariki huko Kilwa, binti wa Mheshimiwa Bungara.

Mheshimiwa Spika, nianze na suala la watumishi wa umma na stahiki zao. Kumekuwa na changamoto ya watu wanaostaafu kucheleshewa mafao yao na haijulikani tatizo ni nini lakini kiukweli orodha sasa inaongezeka siku hadi siku. Mimi mwenyewe nilikuwa na mzazi wangu, baba yangu mkubwa, alistaafu mwaka 2010 mpaka mwaka jana mwisho 2019 tunamzika halikuwa hajawahi kupata kiinua mgongo chake. Tumefuatilia sana na jambo kama hili sasa hivi imekuwa ni *tendency* hata Walimu...

**SPIKA:** Alikuwa akifanya kazi wapi majina yake kwa sababu inasaidia.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Alikuwa anaitwa Mzee Mohamed Said Bobali, alikuwa mtumishi wa Idara ya Ujenzi pale Mkuranga na Mbunge wa Mkuranga anafahamu, hata Wizara inafahamu nilishawahi kusema sana kwenye Kamati kwa sababu bahati mimi ni mjumbe wa hii Kamati. Kwa hiyo jambo hili la watumishi

kucheleweshewa mafao yao naomba Serikali walichukue *serious*, walifanyie kazi kwa kweli ni jambo ambalo linakatisha tamaa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nina orodha pia ya Walimu takribani wawili wa Jimboni kwangu wamenitumia na taarifa zao wamestaafu mwingine miaka miwili iliyopita, mwingine miaka mitatu bado hawajalipwa mafao yake. Sasa ningepomba sana Mheshimiwa Waziri *senior* jambo hili analifahamu naomba alichukulie kwa umakini watumishi wanapostaafu wawe wanalipwa fedha zao.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa ni suala la mishahara, lakini mimi leo nitazungumza kwa upendeleo maalum kwa Madaktari. Watumishi wa umma wote wana umuhimu mkubwa kwenye jamii lakini umuhimu wa Madaktari tunaweza tukaupa ni umuhimu wa kipekee. Nilikuwa nasoma andiko moja juzi kuna mtu ameandika pale Uingereza, alikuwa anajuliza, hivi yale mabilioni wanaowalipa wachezaji wa mpira leo yako wapi yawasaidie kuokoa maisha ya watu wanaopotea kila siku kutokana na gonjwa hili la *corona*. Kwa hiyo kuna haja Madaktari kuongezewa mishahara wakafanya kazi wakiwa na morali, najua wana morali kubwa lakini tukiwaongezea motisha hasa katika kipindi hiki itakuwa ni jambo la msingi sana. Kama kuna bajeti maalum ikachukuliwa *specifically* ikapelekwa kwa Madaktari kuwaongezea motisha ni jambo la msingi sana, litatusaidia na wao kuwapa motisha na morali kubwa ya kufanya kazi ya kutuhudumia hasa katika kipindi hiki ambacho tunapitia kwenye mtihani mkubwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, *TASAF*. Kwanza nishukuru mapendekezo ya Kamati yetu, katika kipindi chote tulikuwa tukishauri Serikali ione umuhimu wa kwenda katika kila kijiji kwa sababu kumekuwa na malalamiko *TASAF* inagusa baadhi ya maeneo na maeneo mengine haigusi. Tunashukuru sana Wizara imelichukua pendekezo hili na *TASAF* awamu ya tatu imekuja na mkakati wa kwenda takribani karibu vijiji vyote. Jambo hili ni la msingi sana na niliona Mheshimiwa Rais alilizindua na akasisitiza ifikapo mwezi wa



Julai jambo hili likianza, basi niendeleo kusisitiza kwamba liwaguse watu wanaostahiki.

Mheshimiwa Spika, Kamati yetu imekuwa ikiigua ikipita kwenye miradi huko mbalimbali ya *TASAF*. Mfano mwezi huu uliopita tulikwenda Babati pale Manyara na bahati tulifuatana na Waheshimiwa Mawaziri, tunaona kabisa kwamba *TASAF* ikimkuta mtu mwenye malengo ya kujinasua inamnasua kweli na ule umasikini allonao, lakini ikikuta na mtu ambaye yeye anakusidia tu apate ile pesa aweze kutumia kwa siku ile inaleta changamoto pia.

Mheshimiwa Spika, jambo hili pia naweza kushauri, iandaliwe *modal*, kwa sababu unaona unatembelea mradi wa mtu A mnufaika mmoja unakuta umefanya vizuri, unakuta tena watu wawili, watatu wamefeli, nafikiri kungekuwa na haja ya kuandaa *modal* ya kuona kwamba ni kwa namna gani hawa wote wanaweza kunufaika katika mazingira sawa, aidha kwa kuwapa kupitia kwenye vikundi ama kuwa na miradi ya kimkakati inayo-*fit* kwenye maeneo yao husika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mfano, tulitembelea Babati tukakuta mama wa *TASAF* anauza kokoto, tulipiga mahesabu pale Waziri, Naibu Waziri na Wajumbe wote wa Kamati na Mwenyekiti wetu alikuwepo haimlipi yaani anachokiwekeza na muda wake ni kikubwa kuliko kile anachokwenda kukipata mwisho wa siku. Kwa hiyo, inaonekana bado Wizara inapaswa iangalie namna gani wanaweza kusaidia watu hawa wa *TASAF*.

Mheshimiwa Spika, nisisahau lazima na mimi niwaombe wale wananchi hasa kwenye Tarafa ya Mchinga kwenye Jimbo langu waliokosa ile *TASAF* I na II. Naomba vijiji vyote vile Mheshimiwa Waziri mvichukue; vya Kilorambwani, Maloho, Mvuleni, Kijiwani, Kilangala, Kitomanga na maeneo mengine kwa sababu wakati mwingine wanahisi kama wao wameachwa wakati wazee wenzao wa maeneo mengine wanaofanana nao kila kitu wanapata. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana, niliona nichangie hayo machache. (*Makofi*)

**SPIKA:** Nakushukuru sana Mheshimiwa Hamidu Bobali kwa kuzingatia muda.

Mchangiaji anayefuata ni Mheshimiwa Elibariki Kingu na atafuatiwa na Mheshimiwa Mwanne Mchemba. Mheshimiwa Elibariki Kingu dakika 10 kutokea Msekwa, zingatia muda tafadhali.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima nimshukuru sana Mungu kwa kunipatia nafasi ya kuweza kutoa mchango wangu katika Bunge lako Tukufu.

Mheshimiwa Spika, lakini kabla sijaanza, binafsi nianze kwa kukushukuru na kukupongeza sana wewe binafsi kwa hatua madhubuti ulizoweza kuzichukua katika kukabiliana na janga la virusi vya *Corona* katika kuhakikisha kwamba unawakinga Wabunge wako pamoja na watumishi wote wa Bunge. Tunakupongeza sana Spika wetu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kama wote tunavyojua tunapozungumzia suala zima la utawala bora, huwezi kuuzungumzia utawala bora bila uchumi. Wote kwa pamoja na tunajua dunia sasa hivi imepata *pandemic* ambayo imeleta madhara ulimwenguni kote na ime-*shake* uchumi wa dunia kwa ujumla na sisi kama Tanzania miongoni mwa nchi zilizopo katika ulimwengu huu hatuwezi kuji-*exempt* kutokana na madhara ambayo yanaweza yakajitokeza.

Mheshimiwa Spika, naomba nilipe taarifa Bunge lako Tukufu kwamba kwa mujibu wa machapisho na ripoti mbalimbali za dunia, mataifa kama Marekani, European Union pamoja na Japan yanatengeneza asilimia 50 ya *GDP* ya Dunia. Taifa la China ambalo ni *partner* mkubwa wa kibiashara na mataifa ya Afrika na sisi Tanzania tukiwemo anachukua asilimia 16 ya *GDP* ya dunia.

Mheshimiwa Spika, maana yangu ni nini? Maana yangu ni kwamba tunapoelekea katika kipindi cha miezi mitatu ama minne hasa katika upande wa *good governance* pamoja na *governance* kwa ujumla katika Taifa letu lazima tuchukue tahadhari kubwa kuhakikisha kwamba Taifa na Serikali yetu imechukua tahadhari zote kuhakikisha kwamba tunaulinda uchumi wa nchi yetu ili kusudi tuweze kufanikiwa. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nataka nikuhakikishie, Serikali yetu ya Tanzania asilimia 53 ya mapato tunayoyapata tunaya-*collect* kutoka kwenye *goods* na *service*. Kama tuna-*collect* mapato yetu asilimia 53 yanatoka katika *goods* na *service*, China wame-*lock down* nchi, Marekani wame-*lock down* nchi zao na mataifa mbalimbali yame-*lock down* nchi zao. Nazungumza hili nikiwa na maana kwamba *impact* ya *lock down* kwa mataifa makubwa itawafanya wafanyabiashara wetu wa Kitanzania ambao walikuwa na uwezo wa kusafiri na kwenda kuleta *goods* ambazo baadaye tunazi-*impose tax* ambayo inasababisha kupata *revenue* za kuendesha Serikali, lazima kama Serikali tufanye *projection*. Taifa letu kama Watanzania tunakwenda kuathirika ndani ya kipindi cha miezi mitano na hii itakwenda kuleta madhara makubwa katika mpango mzima wa bajeti kwa Serikali. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, nini ushauri wangu kwa Serikali yangu kwa ajili ya hii *pandemic* kubwa ambayo imeikumba dunia? Ntoa ushauri kama *package* ya *good governance*, tusaidie sekta ambazo zitakwenda kuathiriwa moja kwa moja na hii *pandemic*. Moja, rekodi zinaonyesha mataifa ya Tanzania, Kenya, Ethiopia pamoja na baadhi ya mataifa ya South Africa yanaajiri zaidi ya watu milioni mbili katika sekta ya utalii.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa sababu gani? Leo hii navyozungumza sekta utalii, inawezekana kabisa hakuna mtalii hata mmoja ameingia. Serikali yetu asilimia 18 ya *revenue* ya *GDP* ya nchi inategemea kutoka kwenye utalii. Zaidi ya *forex* inayotokana na utalii, tunapokea zaidi ya asilimia 50 ya fedha za kigeni kutokana na utalii, leo utalii

haupo. Leo tunapozungumza watalii hawaji kwenye nchi. Hii ina maana ya kwamba sekta ya utalii kwa upande wa mikopo waliyokuwa wamechukua katika kuendesha sekta hii biashara zitakwenda ku-*cease* kwa kipindi kisichopungua miezi sita naweza nikafanya projection.

Mheshimiwa Spika, ushauri wangu kwa Serikali; *BoT* pamoja na vyombo vingine vya mamlaka ya Serikali, hii ni *package* ya *governance* tutengeneze mikakati ya kuhakikisha kwamba sekta ambazo zinaathiriwa moja kwa moja tunazilinda. Wakati huo huo tuhakikishe kwamba Benki yetu Kuu ina *reserve* ya kutosha kuhakikisha kwamba uagizaji wa mafuta unapewa kipambeke ili kusudi nchi ya Tanzania isije ika-*stack* katika siku za usoni. Haya ni ya muhimu kuzingatiwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nayasema haya kwa sababu ni wazi kabisa ndani ya kipindi cha miezi sita inayokuja, dunia itakwenda kupata madhara makubwa. Watafiti wa kiuchumi wanaonyesha *projection* ya *fall* ya *economic* kwa dunia kwa ujumla itakwenda ku-*hit* kwa kiwango kikubwa na *slope* inaonyesha inashuka zaidi hasa kwa mataifa kama ya yetu yaliyo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Mheshimiwa Spika, tafiti zinaonyesha, wawezekezaji ambao walikuwa wanataka ku-*inject capital* katika *emerging new markets* zaidi ya mtaji wa bilioni 84 Dola za Kimarekani wametoa mitaji yao, kwa hiyo hata *FDI* zitakwenda kusimama. Ombi langu, tufanye *program* walivyofanya mataifa ya wenzetu, hili jambo ni kubwa, Benki Kuu, Wachumi wetu watoe ushauri wa namna ya kuweza kuokoa uchumi wa nchi kwa faida ya Taifa letu katika *crisis* inayokuja. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niende katika ushauri wangu; wengi wamezungumza na namuunga mkono Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Rweikiza. Ni wakati muafaka watumishi wetu wa umma, tumekaa katika kipindi kisichopungua miaka mitano, chini ya Jemedari wetu Rais Magufuli, tumefanyakazi kubwa katika kuokoa maisha ya Watanzania katika sekta

mbalimbali kama vile kilimo, afya na mambo mengine, sasa natoa raia na ushauri wangu tuwakumbuke watumishi wa umma katika kuwaongezea mishahara. Wamekuwa waaminifu na wameendelea kuipenda Serikali yao na kufanya juhudi zao katika kuitumikia Serikali ili kuboresha utawala bora, ushauri wangu, tuwaongeze mishahara. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, lakini nisiende mbali, utawala bora ni pamoja na kuzingatia nyenzo zingine ambazo sisi tunaweza tukazona kama ni nyenzo ndogo. Mimi kwa upendo kabisa nataka nitoe *recommendation*, napongeza sana kazi ambayo inafanywa na Mkuu wa wangu wa Wilaya ya Ikungi, Ndugu Edward Mpogoro pamoja na Justice Kijazi, Mkurugenzi wangu. Watu hawa katika utawala bora.

Mimi nilikuwa Mkuu wa Wilaya huenda nimejifunza jambo jipya kwa DC mwenzangu huyu; tulishindwa kuweza kuwafikia watu wa *local government* katika kuwapa *training* namna ya kuendesha Serikali za Mitaa. Mkuu wetu wa Wilaya hapa napozungumza ndani ya mwezi mmoja ameweza kuwafikia Watendaji wa Serikali za Mitaa na Serikali zote za vijiji zaidi ya watu 4,000 kuwafundisha namna ya ku-*operate*, kushirikiana na utawala bora katika ngazi za chini. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, jambo hili limeleta *impact* kubwa. Natoa ushauri kwa Serikali, msione aibu, chukueni *package* ya huyu Mkuu wa Wilaya, wapelekeeni Ma-DC wengine badala ya Ma-DC wengine kukaa na kutoa matamko ambayo hayana maana na tija kwa nchi wajifunze kwa DC huyu wa Ikungi, wakatoe *training* kwa wananchi na viongozi wa Serikali za chini ili kuweza kuwasaidia wananchi kuweza kujua wajibu wao hasa hawa wa Serikali za Mitaa ambao wamechanguliwa hivi karibuni. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba nijielekeze katika suala zima la kuokoa sekta ambazo nimezitungumza mwanzo. Sekta ambazo nimezitaja, utalii naomba tuokumbuke kwa jicho la karibu. Pia naomba tuangalie sekta za *transport* pamoja na sekta nyingine

ambazo zinaguswa moja kwa moja na suala la hii *pandemic* ambayo imekumba dunia.

Mheshimiwa Spika, navyozungumza hapa ni wazo kabisa *projection revenue* zote tulizoziweka, kwa mfano, suala la *corporate tax it is obvious* hatuwezi kuvuna kumi hata moja ya *corporate tax* kutoka katika sekta ya utalii. *The sector has been hit, the world has been hit, we are not isolated* askisiwa.

Mheshimiwa Spika, natoa wito hili jambo ni la muhimu sana, tukiacha kuchukua hatua sasa hivi, nachokwambia baada ya miezi nane, tisa *company* zote zita-*close* na baadaye tutakuja kushindwa kupokea watalii kwa sababu sisi kama Taifa tunategemea utalii sana katika kuendesha shughuli zetu za kila siku.

Mheshimiwa Spika, lakini kuna jambo moja limezungumzwa...

*(Hapa kengele illia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Ahsante sana.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono kabisa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati...

**SPIKA:** Ni kengele ya pili...

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Singida; Chuo kile cha Utumishi...

**SPIKA:** Tunakushukuru sana Mheshimiwa Elibariki Kingu.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Mheshimiwa Spika, sasa ni wakati muafaka wa Serikali yetu kujikita kuhakikisha kwamba chuo hiki kinajengwa. Chuo hiki kitakapoweza kujengwa kitasaidia kuokoa fedha nyingi ambazo tunazipoteza kama ilivyosema Kamati. Kwa hiyo, hilo naomba Wizara waweze kulizingatia.

Mheshimiwa Spika, lakini pia, moja ya *good governance* inapimwa kipindi cha *crisis*; limetokea jambo la *pandemic*, dunia yote imetikisika lakini nataka niwaambie...

**SPIKA:** Wale wa *Camera* ikishaisha *time* ambayo tumei-*allocate* mnapaswa kukata mawasiliano kutoka Msekwa na kuyarudisha kwenye Ukumbi hapa. (*Makofi*)

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** Uongozi tulloonayeshwa na Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kwa kutokuamua ku-*copy* mipango ya *Western policy* pamoja na mataifa mengine, ameamua kutokufanya *lock down* kwenye nchi, hii ina-*impact* gani katika masuala mazima ya *good governance*? Hapa leo tunapozungumza, ndani ya kipindi kifupi kinachokuja dunia itakwenda kukumbana na tatizo kubwa lingine litakalozalishwa, suala la *food security*.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Dkt. John Joseph Pombe Magufuli kuamua kutokuiweka *lock down* nchi yetu ni cha kijasiri na cha kishujaa. Mimi kama Mbunge wa CCM nampongeza sana Rais wetu na Baraza lake lote la Mawaziri kwa sabbau ndiyo washauri wazuri. Pia navipongeza sana vyombo vyetu vyote vya Ulinzi na Usalama wakiwepo *TISS* na mamlaka zingine zote za Serikali kwa kumpa Rais wetu ushauri mzuri. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, leo tunapozungumza, baadhi ya mataifa kama Kenya yameshaanza kuonja joto ya jiwe ya *lock down*. Sisi kama Taifa nchi yetu ni ya kufanya kazi na ku-*earn*. Unakwenda saa nane unafanya kazi unaleta mkate kwa familia. Tungeweza ku-*copy policy* ya ku-*lock down* nchi lakini hapa ndipo tunaposema ya kwamba...

**MBUNGE FULANI:** Dakika.

**MHE. ELIBARIKI E. KINGU:** *Good governance* its all about kuwa *stable* kipindi cha *crisis*. Rais na Serikali yetu ya CCM mmeonyesha ushujaa mkubwa kipindi hiki cha *crisis*.

Watu wametukana, wametoa kejeli lakini msimamo wa Rais umeendelea kuwa *stable*. Nina imani kabisa kwamba kipato kidogo kinachopatikana kuwafanya Watanzania waweze ku-*sustain...*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Elibariki Kingu. Ame-*perform the best* kabisa, hata ningekuwa mimi ningefanya hivyo hivyo. (*Kicheko*)

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea kurekebisha ndiyo maana tumesema tuna-*test* mitambo ili tuweze kujua *hiccups* ndogo ndogo ziko wapi. Nawahakikishia tunavyokwenda tutazidi ku-*improve*. (*Makofi*)

Waheshimiwa Wabunge, naomba niwakumbushe kwamba leo ni siku ya kupiga kura na ukipiga kura ndiyo mahudhurio yako. Kwa hiyo, tusisahau kupiga kura Waheshimiwa kila mmoja mahali pake. Baadhi wameshapiga, baadhi bado, kwa hiyo tuendeleo na zoezi la kupiga kura.

Nilishakuita Mheshimiwa Mwanne Mchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza ambaye yuko huko huko Msekwa. Kwa hiyo, watu wangu wa mitambo mjitahidi kukata kwa *time* inayotakiwa, tunawapa mihani mwingine huo. Baada ya Mheshimiwa Mchemba atafuata Mheshimiwa Upendo.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi jioni hii nichangie Wizara ya Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu kuniwezesha kusimama leo kwenye bajeti ya tano. Namshukuru Mungu, nasema ahsante Mwenyezi Mungu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, baada ya kumshuru Mwenyezi Mungu sasa nichangie kwa kutoa pongezi zifuatazo. Naomba nichukue nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, Dkt.



John Pombe Magufuli kwa kazi nzuri anayoifanya, kwa kusimamia Ilani na utekelezaji wa Ilani ya uchaguzi ya CCM. Pia nimpongeze Makamu wa Rais kwa kazi nzuri anayofanya ya kumshauri Rais na nimpongeze pia Mheshimiwa Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nichukue nafasi kidogo kukupongeza wewe kwa kazi nzuri unayofanya kwa kuendesha Bunge hili. Wewe ni mzoefu na uzoefu wako ndiyo umewezesha kufanya kazi nzuri ambayo tunaiona sasa. Siyo hilo tu, katika Bunge la 2015 mpaka sasa karibuni asilimia 83 ni wageni lakini umeweza kuonyesha umahiri wako na sasa hivi Bunge limetulia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini nimpongeze Mheshimiwa Naibu Spika kwa kazi nzuri inayoifanya. Unapokuwa haupo kazi yote inakwenda akisaidiana na Wenyeviti ambao wanafanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Waziri wa Wizara hii Capt. George Mkuchika, Naibu Waziri, Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Katibu Mkuu, Naibu Makatibu Wakuu na Taasisi zote ambazo ziko chini ya Wizara hii kwa kazi nzuri wanayofanya. Wameonyesha ushirikiano mzuri sana kwenye Kamati yetu na ndiyo maana sisi tumeridhika kwamba kazi wanayoifanya ni nzuri. Wizara hii pia ni watu makini kwani hakuna jambo ambalo Kamati imependekeza hawakulifuatilia, wamefuatilia na wamefanyakazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini pia katika nafasi hii nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Fedha. Mimi kama Makamu Mwenyekiti nimeona fedha zilizokwenda kwenye maendeleo ya Tanzania hii. Kwenye kila Mkoa Wakurugenzi pamoja na Wakuu wa Mikoa wamefanya kazi nzuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nimpongeze Naibu Waziri wa Fedha kwa sababu Naibu Waziri wa Fedha naye pia ni msimamizi mzuri na Wizara pia ya Fedha. Kwa sababu bila kupatiwa fedha maendeleo hayatapatikana. Wizara ya

Fedha ndiyo inayokusanya na makusanyo ni mazuri ambapo yameweza kufanya maendeleo yamekuwa juu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nichukue nafasi hii kumpongeza rasmi Mkurugenzi wa TAKUKURU. Mkurugenzi huyu amefanya kazi nzuri sana. Amefanya kazi nzuri akiwa Kaimu; kwenye zao la korosho kafanya kazi nzuri sana, usimamizi mzuri na fedha zimerudishwa lakini siyo hilo akaenda kwenye utumishi. Nimuombe sana maana ni msikivu na muelewa sana; Mkurugenzi Mkuu nakuomba angalia watu wako wa chini bado kuna matatizo makubwa baadhi siyo waadilifu. Maana ya TAKUKURU ni kusimamia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hivi karibuni sisi kumetokea mtafaruku mkubwa. Mtu labda amepewa kitu kidogo au kutokuelewa ikawa wanakamatwa watu ambao hasa Viti Maalum tunateseka sana kukamatwakamatwa na TAKUKURU. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kama ni Mbunge wa Jimbo katoa baiskeli au katoa kitu chochote TAKUKURU hawamfuatili lakini Mbunge wa Viti Maalum akifanya kazi hiyo atakamatwa, atafuatwa mpaka chooni. Mkurugenzi tunakuamini bado kuna miba midogo midogo, sisi hatuna sauti, tunabughudhiwa ajabu na baadhi ya watumishi wako. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, sisi Wabunge wa Viti Maalum tuna haki, sisi ni Wabunge ambao tunatetea utekelezaji wa Ilani ya Uchaguzi kwenye maeneo yetu lakini hatuna amani. Sasa tunakwenda kwenye uchaguzi tunaomba hili suala ulisimamie, tutendewe haki vinginevyo utakuwa unapewa taarifa za uongo mezani wakati siyo kweli. Kwa hiyo, niombe uwaangalie sana watendaji wako wa chini ili haki iweze kutendeka. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini lingine ambalo nataka kuchangia kwenye Wizara hii ni suala zima la watumishi kukaimu. Hata alipokuja Mkurugenzi wa TAKUKURU tulimuuliza kwa nini unakaimu? Namshukuru Mwenyezi Mungu akasiliza

maswali yetu hatimaye Rais akamteua, hongera sana. Ni mchapakazi mzuri siyo mbabaishaji lakini tunaomba yafuatilie haya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, suala lingine katika Wizara hii upandishaji wa madaraja ni tatizo; mtu anapandishwa daraja lakini mshahara ni ule ule, anastaafu mshahara ni ule ule hakuna kitu chochote. Kwa hiyo, tuombe sasa hivi vitu viwili viende pamoja kwamba anapandishwa leo daraja kesho anaongezewa mshahara wake ili akistaafu basi mshahara wake uweze kwenda sambamba. Kwa hiyo, hilo nalo naliona kwamba lazima tulifanyie kazi. *(Makofi)*

Pia lingine wenzangu wameongea kuhusu Chuo cha Utumishi Mungumaji – Singida; wanapanga kwa gharama kubwa sana. Kwa bahati nzuri Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri tulikwenda wote mpaka *site* wamepata kiwanja, wao wenyewe wana shilingi milioni 400 ambazo ni *own source* zao lakini hazitaweza kuanzia msingi.

Kwa hiyo, niombe Serikali kwa sasa itenge fedha ili waweze kusaidiwa angalau kupandisha au kujenga jengo dogo hata kama ni madarasa au chuo kidogo ili wanafunzi waweze kuhamia pale kuliko fedha ambayo inalipwa kwa mwenye nyumba ambapo wamepanga. Kwa hiyo, naomba sana hii fedha iokolewe ili tuweze kufanya mambo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lingine ni suala zima la *TASAF*. *TASAF* inafanya kazi nzuri sana.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Mwanne dakika kumi ni chache, nakushukuru sana kwa mchango wako malizia.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, kwa heshima na taadhima, naomba niunge mkono hoja, ahsante sana, nashukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Tunarudi tena Msekwa kwa jaribio lingine, Mheshimiwa Upendo Furaha Peneza, dakika kumi. Watu wangu wa mitambo, dakika kumi zikiisha, unakata unarudisha kwenye ukumbi. Mheshimiwa Upendo.

**MHE. UPENDO F. PENEZA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Pia namshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ameniwezesha kufika leo na kuweza kuchangia katika bajeti hii ya Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwanza naomba niseme kwamba ninatambua kwamba Serikali inafanya jitihada kupitia Ofisi ya Waziri Mkuu na Wizara husika katika kudhibiti ugonjwa wa *Corona*. Ni jambo ambalo nasema tunatambua na ninawapongeza kwa kazi ambayo imeshafanyika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo ni lazima tutambue kwamba suala hili siyo dogo kwamba tulipuuze, ni suala kubwa sana kwa kuzingatia jinsi ambavyo tatizo linaendelea kukua; hata nchi nyingine ambazo walianza na tatizo dogo tatizo liliendelea kukua na likawa kubwa zaidi na hatimaye kusababisha hara ndani ya nchi kufa watu 2,000 kwa siku; saa nyingine wanakufa watu 600 kwa siku. Ni tatizo kubwa ambalo kama tukifikia huko, nchi yetu itakuwa imeingia kwenye hatari kubwa sana.

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, nimesikia kauli mbalimbali ambalo viongozi wetu wanatoa ambalo ni jambo jema. Mheshimiwa Rais ametuhakikishia Watanzania kwamba uchaguzi utakuwepo mwezi wa Kumi. Sina haja ya kupingana na hilo wala kuliongelea kwa sababu ni takwa la kikatiba; siyo Rais anayepanga, ni takwa la kikatiba kwamba uchaguzi ufanyike kipindi hicho.

Mheshimiwa Spika, cha kwanza ambacho inabidi tuwahakikishie wananchi wa Kitanzania ni kwamba je, watakuwa salama kiasi gani ili waweze kushiriki huo uchaguzi ufikapo Oktoba? Kutuhakikishia kwamba uchaguzi kwamba utafanyika, haitoshi bila kuonyesha ni jitihada gani na mazingira gani ambayo yamewekwa kuhakikisha kwamba

uchaguzi utafanyika, wananchi watatoka kwenda kupiga kwa amani, wananchi wa wataenda kupiga bila hofu ya ugonjwa wa *Corona* katika maeneo yao?

Mheshimiwa Spika, kwa kuzingatia hilo, nadhani ingekuwa hata ni busara kwa viongozi wetu kutoa kauli ya kwanza kama nchi tunajitahidi kwa kiasi kikubwa kwamba ugonjwa usifike katika hali mbaya ili hatimaye yale yote ambao tumepanga kufanya yaweze kufanyika.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi, tunapozungumzia utawala bora napenda nizungumzie zaidi kwa kuzingatia ugonjwa huu wa *Corona* kwa sababu ndiyo suala mimi naona ni la msingi. Tukiongelea leo kupanda mishahara na tatizo hili bado tunahitaji pesa kukabiliana na tatizo. Tukiongelea masuala ya uchaguzi, ni vyema lakini ni kujizingatia sisi zaidi ambao tunagombea na kuchaguliwa bila kuzingatia haki na matatizo ya Watanzania.

Mheshimiwa Spika, naomba kwamba kuwe na suala zima la uwazi katika suala hili wa *Corona*. Serikali itupe picha halisi kwa sababu kumekuwa na wagonjwa ambao wanazidiwa katika maeneo mbalimbali, wanapelekwa katika hospitali za kawaida. Tumepata kusikia wagonjwa ambao wanatibiwa kupitia Hospitali za Aga Khan, wengine Masana, Hospitali nyingine za *private* na baadaye ugonjwa unajulikana siku tatu, siku mbili kabla ya kifo cha huyo mtu na wanakuwa wanahamishiwa siku mbili kabla katika Hospitali za Mloganzila.

Mheshimiwa Spika, maana yake ni kwamba hakuna utambujaji mzuri wa awali. Kuna Madaktari au Manesi ambao inawezekana wakapata huo ugonjwa katika hizo hospitali nyingine kwa sababu bado hawajagundua kesi wanayo-*dea/nayo* ni kesi ya namna gani na hatimaye mtu anatolewa hapo anapelekwa Mloganzila na ndiyo maana unaona watu wanakufa na taarifa ya kifo inayotolewa, mtu amekufa siku mbili, siku tatu baada ya taarifa zake kujulikana kwamba anaumwa *Corona*. Maana yake ni kwamba hata upimwaji wake unacheleweshwa.

Mheshimiwa Spika, tumepata taarifa kwamba kuna watu wanatumia siku saba ili matokeo ya vipimo halisi yaweze kutoka. Maana yake ni kwamba tunaendelea kuhatarisha hata Madaktari ambao wanatibu hao watu, tunaendelea kuhatarisha jamii, tunaendelea kuhatarisha familia hizo husika. Tunahitaji suala la uwazi lakini pia Madaktari katika hospitali hizo za Serikali ziwe za *private* waandaliwe kikamilifu kutambua na kufanya *isolation* mapema kabla hata ya tatizo lenyewe halijaweza kugundulika kwa mapana yake.

Mheshimiwa Spika, vile vile, tunahitaji Serikali ituambie wao wana makisio gani ya magonjwa? Kwamba sasa hivi tuna wagonjwa inasemekana 59, kadri tunavyoenda makisio yako kiasi gani? Inawezekana tukafikia wapi? Maandalizi ni yapi? Upungufu ni upi? Ukiangalia hata katika nchi nyingine, wanasema inawezekana tukafikia *peak* katika kipindi hiki cha mwezi. Inawezekana tukawa na wagonjwa wengi katika kipendi hiki. Kutoa *predictions* au makisio kama hayo, yanatusaidia kuweza kujiandaa kikamilifu kukabiliana na matatizo na magonjwa katika maeneo ya hao watu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia hatujui tatizo hili ndani ya nchi yetu liko kwa kiasi gani? Hatujuwi tuna *ventilators* kiasi gani? Hatujui tuna vitanda kiasi gani vya kuweza kuhudumia kama tatizo linakuwa kubwa? Tunahitaji Serikali ituambie ukweli ili kama wananchi tunaamua kuchangia, tuchangie tukijua ukubwa wa tatizo na Serikali iweze kuwajibika kikamilifu kuhakikisha ya kwamba inaweza kukabiliana na hilo tatizo la Corona.

Mheshimiwa Spika, suala lingine ni suala la ushirikishwaji. Katika maeneo yetu tuna watu wanafanya biashara mbalimbali; tuna watu ambao ni akina mama wa masoko, kuna magulio kuna maeneo ambayo watu wanafanya minada; Serikali haifanyi ushirikishwaji wa wananchi. Wanawaambia fanya *isolation*, jitengeni, kaeni mbali, lakini hawaambiwi na hawasaidiwi namna gani ya kujipanga ili wakae mbali kwa kiasi hicho.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, pamoja na hayo, tufanye ushirikishwaji wa maeneo hayo, tufanye ushirikishwaji wa masuala ya kibishara. Kuna watu wanaomiliki shule, leo wamefunga shule, hawana hela; kuna masuala ya kikodi; kuna watu wanaofanya biashara mbalimbali ikiwemo dhahabu kama Geita. Sasa hivi imekuwa ni ngumu kusafirisha dhahabu kupeleka nje ya nchi, imekuwa ni gharama kubwa, wanalazimika kutoa mpaka *ten thousand US Dollars* kusafirisha mzigo mdogo. Sasa Serikali inasaidiaje biashara iendeleo, watu waendeleo kupata mapato kwa njia nyingine lakini huku huku tunaendeleo kujikinga na suala nzima la ugonjwa la Corona? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la lingine watu wana haki ya kusambaa kutoka kwenye eneo moja kwenda kwenye eneo lingine. Kama hatutazingatia, ugonjwa huu utasambaa.

Naomba watu wa Dar es Salaam, sehemu ambayo kuna maeneo mengi, watu wasiruhusiwe kutoka kwenda maeneo mengine. Huduma za muhimu tu ndiyo ziwe zinaenda kama chakula na mengineyo ndiyo yaweze kwenda Dar es Salaam lakini watu wasiruhusiwe kuchangamana na maeneo mengine kwa sababu hatuna uwezo wa kukabiliana na tatizo tuisababishie tatizo likawa kubwa zaidi.

Mheshimiwa Spika, nina ombi moja la mwisho kwamba Serikali imetangaza, baada kupitisha bajeti ya Waziri Mkuu wametangaza kurudia zoezi la uandikishaji wa wapigakura. Tusipoangalia, zoezi hili inawezekana ikawa ni chanzo la usambazaji wa magonjwa katika maeneo ambayo hatuna *Corona* hivi leo.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejipanga vipi kuhakikisha kwamba watu wanaoenda kuandikisha wapigakura katika maeneo husika hawawi chanzo cha kusambaza ugonjwa Geita, Chato, Shinyanga na kwingineko ambako magonjwa hajaenda? Kwa sababu tunatambua kwamba hawa ni watumishi ambao watatoka sehemu moja wanahama, wanahama, wanahama. Leo Serikali imetangaza kwamba

wanapunguza mikusanyiko mingi iwezekanavyo, wametangaza kwamba kutakuwa na kituo kimoja tu kila Kata.

Mheshimiwa Spika, sasa watu wanaokusanyika kutoka kwenye Kata nzima kuja kujiandikisha ni wengi sana. Ni lazima tu hiyo mikusanyika itakuwepo katika maeneo husika. Sasa kama wanataka kufanya uwandikishaji uendeleo, ni lazima tutenge vituo vingi, siyo katika Kata, lakini katika vijiji ili kuhakikisha kwamba watu wanaenda na hiyo *distance* inakuwepo na zoezi linafanyika taratibu. Ubaya zaidi, Serikali imeweka siku tatu tu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, kama Serikali kweli ina nia thabiti ya kusema tunazuia hili gong'wa la *Corona*, tuwe wazi, lakini pia tushirikishe wananchi, tutambue changamoto walizonazo, tutambue changamoto za kibiashara tulizonazo ambazo zinaenda kuathiri hata kodi na mapato ndani ya nchi na tujuwe namna gani tunaweza kusaidia na tukafanya biashara ikawa rafiki.

Mheshimiwa Spika, pia kama tunakwenda kwenye uchaguzi, hebu kuanzia sasa kwenye zoezi la uandikishwaji, tunawalindaje wananchi kuhakikisha ya kwamba wanajiandikisha, wanakuwa salama na Serikali yenyewe kwa kuanzisha hili zoezi leo hawawi chanzo cha kusambaza ugonjwa huu kutoka sehemu moja kwenda sehemu nyingine.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana. Nakushukuru sana kwa kutumia muda wako vizuri. Tunakushukuru sana. Sasa Mheshimiwa Martha Mlata na atafuatiwa na Mheshimiwa Mansoor Sharif Hirani.

**MHE. MARTHA M. MLATA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia kwenye hotuba ya Wizara hii. Mimi ni Mjumbe wa Kamati katika Wizara hii pia, lakini nakupongeza kwanza kwa



teknolojia ambayo sasa hivi tunaendelea kuishuhudia chini ya uongozi wako. Nakumbuka siku moja ulisema kwamba unatamani kutokusikia mtu anatamka mwongozo au taarifa, zaidi atabonyeza tu pale mezani, wewe utamwona anataka nini. Naamini unatupeleka huko. Mungu akubariki sana, hongera sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba nimpongeze sana Mheshimiwa Mkuchika ambaye ni Waziri wa Wizara hii, ambaye kwa kweli amekuwa akifanya kazi nzuri sana, kwa sababu sisi tuko kwenye Kamati tumemwona akichapa kazi na wakati mwingine tukiwa kwenye ziara tunaongozana naye. Vile vile nampongeza Naibu Waziri, Mtumishi wa Mungu Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, mnyenyekevu, ambaye naye amekuwa akichapa kazi nzuri sana, mwanamke shupavu. Tumemwona akienda vijijini huko akitumbukia kwenye nyumba za watu ambao walitoka kwenye nyumba za udongo wameingia kwenye nyumba za bati kwa ajili ya TASAF. Kwa kweli nawapongeza sana. Nampongeza Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu na Watendaji wote wa Wizara hii. Kwa kweli kazi imefanyika.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu muda ni mdogo na mambo ya kuzungumza ni mengi, nitaweza kuzungumza yale machache ambayo naweza nikayasema. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa sababu ameonyesha ushupavu na ujasiri wa hali ya juu sana katika kusimamia suala la utumishi hasa utumishi na utawala bora. Nikisema hivyo ni kwa sababu tumeona mambo mengi ambayo yamekuwa yakifanyika kwa uadilifu mkubwa sana hasa ukienda kwenye nidhamu ya watumishi.

Mheshimiwa Spika, wakati wa awamu nyingine, ukienda Ofisini ukifika unaulizwa unataka nini? Ukifika tu pale, unaulizwa unataka nini? Sasa hivi ukifika unaulizwa, tukusaidie nini? Unapokelewa vizuri sana sana. Kwa hiyo, naomba nipongeze sana katika sehemu hii ya watumishi kwenye nidhamu, wamekuwa watumishi wazuri, wenye nidhamu na wanaosimamia maadili ya kazi zao. Ni lazima tuwapongeze kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia kwenye suala la uadilifu hasa kwenye matumizi ya pesa kwanza kwenye kukusanya lakini bado na kwenye matumizi. Tumeona fedha hata kama tukisema kwamba labda zilipelekwa kidogo; zamani ukipeleka kidogo na kidogo hizo hizo zinapotea, lakini sasa hivi hata zikipelekwa kidogo, zikipelekwa nyingi unaona ni namna gani wanavyoweza kusimamia matumizi ya fedha hizo na ndiyo maana maendeleo yameweza kuonekana. Kama ni Zahanati, tumeziona watumishi wamesimamia; kama ni shule tumeziona, wamesimamia fedha vizuri kwa sababu ya uadilifu na matumizi mazuri ya fedha ambayo Mheshimiwa Rais kwa kweli tunampongeza sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, pia naomba nizungumzie suala la *TASAF*. Katika Mkoa wangu wa Singida namshukuru Mheshimiwa Waziri amesoma kwenye eneo la Mkurabita, *TASAF* na tuna *One Stop Center* ambayo iko pale amelezea vizuri. Nampongeza Mkuu wa Mkoa wangu, Dkt. Rehema Nchimbi, *Canon* pamoja na *RAS* wake na watendaji wote ambao waliweza kusimamia na kuweka utaratibu wa wa *One Stop Centerya* kuwasaidia watu ambao wanataka kuanzisha biashara zao ndogo ndogo wasisumbuliwe. Akiingia pale, benki ipo pale na kila kitu kipo pale. Hata kama kuna mtu amemnyanyasa, kuna sehemu ya kushitaki. Kwa hiyo, ninaipongeza *TASAF* kwa sababu imefanya kazi nzuri sana katika Mkoa wangu wa Singida.

Mheshimiwa Spika, bado kuna maeneo ambayo nilikuwa naomba, kuna mitaa hasa pale mjini 27 ambayo ilishaingizwa pamoja na vijiji, lakini bado 45. Tulikuwa tunaomba ile iingie. Vile vile kwenye maeneo mengine, ukienda Mkalama, Iramba, Ikungi, Manyoni, Singida Vijijini kote kule kuna maeneo ambayo kwa kweli yamebaki. Naomba na wale waweze kuingizwa kwa sababu wamefanya vizuri. Anayeteteleza vizuri, basi apewe zawadi ya kuongezewa hiyo.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naona pia hawa watu wa *TASAF* ambao tumewaona wametoka katika hali ya chini bado wanaendelea kufanya shughuli zao za maendeleo,

lakini shughuli za maendeleo bila miundombinu, haisaidii. Kwa hiyo, naomba kuwe na miundombinu inayowawezesha hawa kupeleka mazao yao na vitu vyao vidogo vidogo.

Mheshimiwa Spika, kwa mfano, ukitoka Singida kama unaenda Iramba hakuna barabara; ukitoka Singida kwenda Sepuka, uende Ndago, uende mpaka Kizaga, uende mpaka Mtekente uende Urugu, ukitoka pale uende labda Kinampanda hivi, yaani barabara zile, wale watu ambao wamewezeshwa na *TASAF*, vitu vyao wanataka kuleta mjini wanashindwa kwa sababu ya ile miundombinu ambayo sasa hivi imearibika sana. Kwa hiyo, tunapowawezesha tuangalie na miundombinu ili waweze kutekeleza vizuri shughuli zao za kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nampongeza sana Mkurugenzi Mkuu wa TAKUKURU. Ni kweli unaweza na unatosha. Zile fedha unazoziokoa, endelea kuokoa. Mimi najua ziko nyingi mikononi mwa watu, endelea kuokoa lakini angalia na kwenye mashirika mbalimbali, kwenye zabuni mbalimbali, kuna fedha ziko kule ambazo zinavuja, nenda kazitafute uokoe ili zije sisi tupeleke kwenye Zahanati kwa ajili ya madawa.

Mheshimiwa Spika, napongeza kwa kuajiri Madaktari 1,000; hebu naomba tujitahidi kuajiri na Manesi pia. Maana yake Mheshimiwa Rais ametupatia nafasi ya Madaktari 1,000, basi tuangalie Manesi hasa vijijini kule bado tunahitaji, tuna vituo vingi sana tumevijenga, tunahitaji pia Manesi waende kule. Tena ukizingatia na janga hili la *Corona* tunahitaji sana watumishi hawa waweze kwenda kule.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu kengele imegonga, naomba tu niseme naunga mkono hoja, nawatakia heri na Mungu awabariki sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Martha Mlata. Mheshimiwa Mansoor Shanif Hiran, atafuatiwa na Mheshimiwa Joseph George Kakunda akituhutubia toka

Msekwa. Mheshimiwa Kakunda awe Msekwa. Mheshimiwa Mansoor!

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi nami nichangie hoja ambayo iko mbele yetu. Kwanza kabisa naomba nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa afya njema niweze kusimama kwenye Bunge letu leo kuzungumza hoja ambayo iko mbele yetu.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii kwanza kabisa kuipongeza Serikali yangu kwa kazi nzuri ambayo inafanya dhidi ya janga la *Corona* kwa kuelimisha wananchi vizuri na pia Wizara ya Afya kwa kuhakikisha kwamba hatupati vifo vingi. Tunashukuru sana wamesimamia vizuri, tuna vifo vitatu, tunawapongeza sana Madaktari wanafanya sana kazi nzuri ya kupunguza na kusimamia angalau maambukizi yasiongezeke.

Mheshimiwa Spika, natambua leo ni Mkutano wa Kumi na Tisa na ni Mkutano wa mwisho kabla ya Bunge kuvunjwa tarehe 30 Juni. Nafikiri ni muda muafaka wa kupongeza na kushukuru.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi ya kwanza kabisa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa utekelezaji mzuri sana wa Ilani ya Chama cha Mapinduzi. Naomba nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa miradi mingi sana ya kimkakati ambayo ametekeleza ndani ya miaka minne hii na huu mwaka wa tano. Nitakuwa sijamtendea haki kama sitasema machache.

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa ni kuhamisha Serikali kutoka Dar es Salaam kuja Dodoma. Hayo maamuzi yalikuwa ni mazito sana. Serikali ya Awamu ya Tatu ndiyo ilitoa maamuzi ya kuhamia Dodoma, lakini Serikali ya Awamu ya Tano chini ya Mheshimiwa Dkt. John Pombe Magufuli ndiyo imetekeleza azma hiyo. Kwa kweli anastahili pongezi ya kipekee. Hilo ni suala la kihistoria kabisa kwa Mheshimiwa Rais kuhamisha Serikali kuja Dodoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, la pili, ni elimu bila malipo. Mheshimiwa Rais alipoapishwa katika hotuba yake ya kwanza hapa Bungeni mwezi Novemba akasema, naagiza Mheshimiwa Waziri Mkuu apange bajeti ya kutoa elimu bila malipo kutoka Januari, 2016. Ni maamuzi ya ujasiri. Ni fedha nyingi aliamua kuzitumia ndani ya muda mfupi.

Mheshimiwa Spika, nataka nichukue nafasi hii kumpongeza na pia wananchi wa Jimbo la Kwimba wamenituma nimshukuru sana.baada ya kutoa elimu bila malipo watoto wetu wengi ambao walikuwa hawana uwezo wa kwenda kusoma, wamepata elimu na ndani ya miaka mitano hii watoto wengi sana wamejiunga kwenye Shule za Chekechea. Kwa hiyo, nashukuru sana kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba kwa kupata elimu bila malipo.

Mheshimiwa Spika, lingine ningependa kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa kujenga reli ya kati kuanza kujenga bwawa la Julius Nyerere ambalo nayo ilikuwa ni maamuzi ya Awamu ya Kwanza, Awamu ya Tano ndio imetekeleza mradi huo, kwa kweli nampongeza sana Mheshimiwa Rais. Pia kufufua shirika la ndege la *ATC* ndani ya miaka minne kununua ndege nane kwa kweli ni sifa ni heshima ametuletea nchi ya Tanzania.

Mheshimiwa Spika, baada ya miradi ya mikakati ambayo Mheshimiwa Rais ameteteleza haya ni machache nimesema, naomba niseme pia kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kwimba nishukuru. Kwenye Jimbo langu la Kwimba tumepata miradi mingi ya mkakati ndani ya miaka hii minne, tumepata chuo cha *VETA* ambacho sasa hivi kinajengwa mwezi wa sita kitakuwa kimekamilika. Tumepata hospitali ya wilaya mpya inajengwa sasa hivi, tumepata kituo cha afya cha Mwamashimba ambacho kimeshaamilika, tumepata barabara ya lami kilometa 1.2 na bado tumeahidiwa mwaka huu kwenye orodha; barabara tumepata kilometa 5 ya lami ambazo *TARURA* wametuahidi bajeti ya mwaka huu pia wanatujengea, madawa sasa hivi yanapatikana ya kutosha kwenye zahanati na hospitali zetu.

Mheshimiwa Spika, suala la maji wakati nimechaguliwa Jimbo la Kwimba tulikuwa tunatumia maji ya madimbwi na visima sasa hivi leo baada ya miaka mitano naomba irekodiwe kata 13 zina maji ya Ziwa Victoria tumebakiza kata mbili tu ambazo hazina maji ya Ziwa Victoria na bado tuna miradi saba za maji zinatekelezwa sasa hivi mpaka mwezi wa sita zitakuwa zimekamilika. Mungu akitujalia mwakani tukirudi hizo kata mbili tutahakikisha zinapata maji maana yake Jimbo la Kwimba kata zote *center* zote zitakuwa na maji ya Ziwa Victoria ya mabomba. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kwenye suala la umeme tumepata mafanikio makubwa sasa hivi nilipochaguliwa tulikuwa hatuna umeme, tulikuwa na umeme kwenye *center* ya Ngudu peke yake tuna kata 15, baada ya miaka minne na nusu tuna umeme kwenye kata 14, tumebakiza kata moja tu. *(Makofi)*

**SPIKA:** Jamani mnasikiliza mafanikio hayo, haya makofi natumaini hayatoshi hayo eeh !

**MHE. MANSOOR S. HIRAN:** Mheshimiwa Spika, tunashukuru sana tumepata miradi mingi umeme unawaka *center* zote, sasa hivi tunaelekeza miradi ya maji kupelekwa kwenye vitongoji kwenye *center* zote umeme unawaka na mwezi wa sita tutahakikisha maeneo mengine yamekamilika tunabakiza kata moja tu ambayo ni ya pembezoni.

Mheshimiwa Spika, naomba nichukue nafasi hii pia nimesema miradi mingi zimefanikiwa kwenye Jimbo la Kwimba naomba niseme pia Mheshimiwa Rais hajakosea Mheshimiwa Waziri wa Utumishi, Mheshimiwa George Mkuchika na Naibu wake Mheshimiwa Dkt. Mwanjelwa, Mheshimiwa Rais hajakosea kuwachagua kwanza hawa ndio wamesimamia ndio maana watumishi leo wameteteleza miradi yote hii ya kitaifa na wilaya kwa sababu sasa hivi uadilifu umeongezeka kwa hali ya juu sana chini ya uongozi wa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, pia naomba kabla sijamaliza nichukue nafasi hii ya kipekee kukushukuru wewe na Naibu Spika miaka mitano umetuongoza vizuri sana, umetuvumilia, umetuelimisha mara nyingi umetushauri kama wadogo zako kwa kweli Mheshimiwa umekuwa mvumilivu sana kwenye masuala haya, tunakushukuru sana kwa sababu huu ndio muda muafaka wa kushukuru na kupongeza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia hoja hii, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mansoor Shanifu Hirani nakushukuru sana kwa shukrani. Nimeshakutaja Mheshimiwa Joseph George Kakunda kwamba utachangia kutoka Msekwa, Mheshimiwa Kakunda tafadhali na atafuatiwa na Mheshimiwa Godbless Lema kutoka humu ukumbini.

**MHE. JOSEPH G. KAKUNDA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana naomba nimpongeze Mzee George Huruma Mkuchika kwa jinsi ambavyo amewasilisha hotuba yake vizuri sana kwa weledi mkubwa pia kwa ulezi ambao amekuwa ananipa malezi tangu alipokuwa mkuu wa wilaya nilikuwa afisa mtendaji wa kata hadi tulipokuwa kwenye baraza pamoja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lengo kuu la kuanzisha wizara hii ilikuwa ni kusimamia ufanisi wa watumishi na kuboresha utawala bora katika kuwahudumia wananchi. Majukumu makuu ya wizara hii nitataja matatu kusimamia ajira na michakato yake, kusimamia maadili ya watumishi, kusimamia uwajibikaji au *accountability* na uwazi (*transparency*) ndani ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, majukumu hayo ukiangalia taarifa ya Mheshimiwa Waziri kwenye hotuba yake wameyasimamia vizuri sana napenda kuchukua nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Waziri na timu yake yote ikiongozwa na Katibu Mkuu Dkt. Ndumbaro. Kwa mfano katika eneo la ajira wametoa vibali 6975 wameajiri watumishi 2968,

wamepandisha vyeo watumishi 290,625, wamelipa madeni bilioni 33.3 kwa watumishi 14,761 ndani ya miezi hii minane tu tangu mwaka huu uanze hii ni kazi kubwa sana wamefanya wanastahili kupongezwa sana.

Mheshimiwa Spika, nachokiomba kwa Mheshimiwa Waziri kupitia kwako ninaomba sana sana zoezi la kulipa madeni yaliyobaki liharakishwe vilevile uhakiki ambao unaendelea nao uharakishwe ili madeni yote ya watumishi yawe yameliywa ifikapo wakati wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, eneo la pili katika eneo la kusimamia maadili vyombo vinavyosimamia maadili vinafanya vizuri sana hadi sasa isipokuwa naomba Serikali iendeleo kuviimarisha kwa mafunzo na bajeti, vyombo vyote vya uchunguzi na ukaguzi ili kuondoa mianya yote ambayo bado inasumbua maadili. Kwa mfano kuimarisha Idara ya Upelelezi ya Jeshi la Polisi ambayo ndio idara mama, kuimarisha TAKUKURU, kuimarisha Idara ya Usalama wa Taifa, kuimarisha Idara ya Kupambana na Utakatishaji wa Fedha, au *money laundering* Tume ya Kuratibu, Udhhibiti wa Dawa za Kulevya, Tume ya Haki za Binadamu na Utawala Bora, Tume ya Kudumu ya Uchunguzi.

Mheshimiwa Spika, vyombo hivi vikiimarishwa kwa mafunzo na bajeti inawezekana tukapata tija zaidi katika utendaji wao. Vilevile ushirikiano wa vyombo hivyo uongezwe ili kuboresha ufanisi katika maeneo wanayosimamia. Kwa mfano tutapata faida zaidi ya vyombo hivi kama vitaongezewa majukumu ya kufatilia na kusimamia utekelezaji wa mapendekezo ya CAG anayoyatoa kwenye taarifa yake ya kila mwaka badala ya kuishia tu kwenye mijadala ya Bunge na Mapendekezo ya Bunge ningependa kuona kwamba mapendekezo ya CAG yanachukuliwa hatua za dhati baada ya mijadala ya Bunge kukamilika. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, eneo la uwajibikaji na uwazi ipo haja ya kurejesha mfumo wa kila wizara kila idara ya Serikali na kila Serikali ya Mtaa kuhakikisha kwamba tunarudisha



*strategic plans*, hizi *strategic plans* zilisaidia sana kuboresha utendaji wa watumishi kwa sababu ndani yake kulikuwa na eneo la viashiria na eneo la ufuatiliaji na tathmini. Kwa hiyo, kama tutarudisha *strategic plan* ambayo sasa hivi kama zimeachwa hivi ninaomba sana zitaboresha sana utendaji wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, eneo lingine la kuboresha mifumo ya ununuzi, mifumo ya uhasibu na mifumo ya uhandishi kwenye hasa kwenye mikataba ya miradi ya ujenzi. Ninaomba sana iunganishwe ili kuboresha ufanisi wa Serikali.

Mheshimiwa Spika, mwisho naomba wizara isimamie ajira nchi nzima kuna maeneo mengi kata hazina watendaji wa kata wenye sifa, kuna maeneo mengi vijiji vingi havina watendaji wa vijiji wenye sifa. Hili eneo naomba litiliwe mkazo sana na Mheshimiwa Waziri ili kuhakikisha kwamba wananchi wanaboreshewa huduma wanazopata kutoka Serikali kwa sababu hawa watendaji ndio wako karibu kabisa na Serikali. Sasa kama hawapo na maeneo mengine kama halmashauri yangu wanatumia watendaji wa vijiji wa kujitolea ambao kwa kweli wanaishi katika mazingira magumu sana. Ninaomba halmashauri yangu ipewe kipaumbele katika kutoa vibalii vya ajira vya watendaji wa vijiji ili watendaji wa vijiji waajiriwe katika vijiji vyote nchi nzima.

Mheshimiwa Spika, nadhani kwa sababu mambo mengi yameelezwa vizuri na Mheshimiwa Waziri, nachukua nafasi hii tu kusema kwamba naunga mkono hoja ya Wizara hii na Mungu amabariki sana Mheshimiwa Waziri aendelee kuchapa kazi ahsante sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Joseph George Kakunda kwa kuzingatia muda na kwa hoja nzuri ambazo umeziwasilisha. Sasa Mheshimiwa Godbless Lema na atafatiwa na Mheshimiwa Abdallah Majura Bulembo.

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, pia nakushukuru sana. Mambo ni mengi na muda ni mchache na jana angalau nilipewa dakika tano nikaongelea *issue* ya

Corona kidogo leo sitaiongea sana ila nisisitize hali ni mbaya kuliko maelezo tunayopewa na wizara.

Mheshimiwa Spika, nikuombe kiti chako kichukue *leadership* kiliombe Bunge litenge siku nzima kujadili madhara na bahati mbaya kwa sababu siku hizi kusema ni kesi watu wengi hawasemi, hawaongei lakini kama hali itaendelea hivi hali itakuwa ni mbaya sana, nikuombe tafuta siku hata kama ni *weekend* Bunge lije lijadili upana na kina wa jambo hili ili tuweze kuwasaidia Serikali namna gani ya kwenda mbele. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, kwanza kabisa niseme nimesoma kitabu cha Mheshimiwa Waziri Mzee wangu katika ukurasa wa 17, kesi ambazo zilifikishwa mahakami na *TAKUKURU* ambazo zinahusiana na mahujumu uchumi pamoja na utakatishaji fedha zilikuwa ni kesi 352 na kesi 143 watu hawa waliachiwa huru, na 196 walikutwa na hatia. Maana yake ni ukipata kesi ya utakatishaji fedha hama uhujumu uchumi kesi hiyo haina *bail* maana yake kuna kuna kesi ambayo ni watu ama ni kampuni zenye watu 143 walikuwepo mahabusu waliishi mahabusu baada ya muda kwa sababu ya hatuna sheria yenye kikomo cha upelelezi watu hawa wakaja wakaambiwa wako huru. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, utawala bora huu tunaopigia kelele sio kwa ajili ya maslahi ya CHADEMA ni kwa ajili ya maslahi ya Taifa hili na watoto wa Taifa hili. Tukiongea habari ya magereza ama watu kukaa mahabusu muda mrefu wenzetu mna bahati nzuri hamuwezi kuelewa *pinch* ina maana gani. Kukaa magereza wiki moja ama siku moja au unakaa miaka mitatu, minne mitano kama ilivyokuwa kesi ya Mediam Ally miaka nane upelelezi unakwenda mahakamani haujakamilika, haujakamilika, huwezi kusema nchi ina utawala bora wakati watu wanalala mahabusu. (Makofi)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri leteni sheria bungeni tubadilisha sheria tuliwekee Jeshi la Polisi kikomo cha upelelezi huwezi kumweka mtu mahabusu zaidi ya miaka

mitano, sita halafu baadaye unamwachia huru hana kosa lolote halafu mmeona ni jambo la kawaida.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri watu walioko magereza wengi siku ya mwisho wanaka miaka mitano, sita upelelezi haujakamilika, na siku upelelezi ukikamilika ndio hiyo anafutiwa mashtaka. Kuna mtu mmoja alifukuzwa kazi alifunguliwa mashtaka baada ya muda ni Mkurugenzi wa *TPDC* amefukuzwa kazi na wengine wakapewa mashtaka, mashtaka ya kutosha zaidi ya 100 baada ya muda *DPP* akaenda akaita *null* yule mtu akarudishwa kazini na Rais lakini mtuu huyu alishachafuliwa, huyu mtu alishaitwa muhujumu uchumi na huyu mtu tayari kama angekuwa amekwenda ama alikuwa magereza maana yake tayari amesha-*suffer*. Niombe sio kwa ajili yetu ni kwa ajili ya sisi wote hakuna aliye salama katika masuala haya ya kushutumiana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, katika kesi hizi ambazo zinaendelea nimesoma gazeti diwani mmoja amefungwa miaka 20 kwa kesi ya uhujumu uchumi wa shilingi milioni nne.

Mheshimiwa Spika, najiuliza hizi sheria wakati tunazitunga na nilikuwemo Bungeni na kama nilikuwa Bungeni siku hiyo nilikuwa nimefanyaje mbona hata sikufanya fujo Spika anipe adhabu, ilikuwaje tunatunga sheria kwamba mtu ana kesi ya milioni mbili, nne anahukumiwa kwenda jela miaka 20. Mtu ana kesi ya milioni saba anahukumiwa kwenda jela miaka 20 kuna sababu na haja ili kuimarisha *sense* ya utawala bora ya kuleta mabadiliko ya sheria katika Bunge hili. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nasema haya kwa sababu gani unapooonelea utawala bora cha kwanza kabisa katika utawala bora ni maisha ya watu.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga taarifa.

## T A A R I F A

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, nataka nimpe taarifa shemeji yangu Mheshimiwa Lema kuwa uhujumu uchumi sio kuangalia kiwango cha hela uhujumu uchumi ni kuangalia athari zinazoipata jamii kutokana na upotevu wa hela hiyo. Kwa mfano Maleria inaua, dawa ya Maleria ni shilingi 2000 tu mtu akikosa anakufa ahsante sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Lema pokea taarifa ya Shemeji yako

**MHE. GODBLESS J. LEMA:** Mheshimiwa Spika, ni bahati mbaya sana dada yangu alikosea mlango lakini *anyway* ana bahati mbaya sana dada yangu alikosea mlango kwamba huyu ni shemeji yangu, hata wewe mwenyewe unanionea huruma lakini tutawafundisha migombani huko *Christmas* tukienda. *(Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri nikupongeze kwa jambo moja tu umekuwa ukitoa kauli nzuri kuhusu mamlaka ya ma-DC na ma-RC kuweka watu ndani. Nimeona umerudia zaidi ya mara moja mara mbili kiburi cha ma-RC na ma-DC kimezidi Mawaziri hata wewe Spika katika nchi hii. Mfano ni juzi hapa Waziri Mkuu anatoa maelekezo namna ya ku-*combat issue* ya *corona* na anasema wanaopaswa kutoa taarifa na kwenda mbele anasema ni Waziri Mkuu, Makamu wa Rais, Waziri ama Rais mwenyewe. Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam yaani Waziri Mkuu hajapanda gari kufika nyumbani kwake akanywe chai Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam anaita watu anafanya *mocking* na aliyetoa kauli hapa ni Waziri Mkuu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ukienda huko mitaani Mkuu wa Mkoa wa Mwanza Mongela anakusanya watu tena kwa dhihaka anasema hii *issue* ya *corona* hii haipo kwanza mkikaa ndani mtakula nini unaweza ukalala na mama ukawa mbegu hazina nguvu ukazaa mtoto taira, unajjuliza hawa ma-RC na ma-DC mbona ni tofauti na wale mimi nilikuwa nawajua

zamani. Zamani ulikuwa ukionyeshwa *DC* ama *RC* wakati nakuwa ukiambiwa yule ni *RC* ama *DC* unaenda kuomba kupiga naye picha. Hawa wa sasa hivi ni aibu hata kupiga nao picha ya bahati mbaya kwa sababu hawana nidhamu.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri hawa vijana wako huko mitaani huko hawana nidhamu wanaonea watu, wame-*create uncertainty* kubwa ya kutosha kabisa, wanaweka watu ndani wafanyabiashara hawana amani hawachukui maelekezo ya mawaziri unajjuliza ni utawala gani bora huu. Leo *RC* ama *DC Arusha* juzi siku hizi siongei mambo ya Arusha naacha wanyukane kwa sababu Octoba nataka nipite kiraisi. Siku hizi Arusha wakinyukana siongei kabisa najifanya hata sioni tena nikiona wananyukana nachukua picha ya *wife* na-*twitter* nahama kabisa.

Mheshimiwa Spika, juzi amekamatwa Kaimu Mkurugenzi wa Jiji alhamis TAKUKURU wamekwenda pale wanataka *document* ya mwaka 2011 wa Arusha Miji, akasema sikuwepo nina miaka miwili tu hapa na Mkurugenzi hayupo naomba niwaandalie hizo nyaraka mnazotaka niwape siku ya jumanne kwa sababu kesho ni *good Friday* hakuna kazi, jumamosi na jumapili ni Pasaka wakampeleka wakamweka ndani. *DC* wake na *DSO* wakaenda polisi wanamwomba *OCD* wamwekee dhamana Mkurugenzi, *OCD* anamkatalia *DC* wake ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ya Ulinzi wa Usalama. Mnaua tachi ya utawala katika Taifa hili mnaua mamlaka, hamuuwi kwa sababu yale mambo mlikuwa mnatufanyia sisi yanahama yanahamia kwenu na yakihamia kwenu kwa sababu nyie mnazijua hizi mamlaka vizuri ninyi hamtapelekana magereza kama sisi nyie mtasubiriana kwenye mageti. Hakuna *discipline* kabisa ma-*DC* wamekuwa ni miungu watu wanachukua rushwa wanaonea watu anasema hapa Waziri, anasema Waziri Mkuu hakuna chochote kinachofanyika. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, niombe sana kwenye suala la nidhamu ya viongozi ma-*DC* na ma-*RC* Mheshimiwa Mkuchika hawa sasa hivi hawa hawajengi *image* ya chama na sisi tumegundua siku hizi kwa sababu nyie hampangiwi

na mlishasema hampangiwi siku hizi tukiona mnafanya mambo ya hovyotunakaa kimya kwa sababu tukiwasema wana-*shift liability* wanasema hawa CHADEMA wanapiga vita ndio sababu mmeona napigwa vita.

Mheshimiwa Spika, huyu hapa Waziri, Mheshimiwa Dkt. Kigwangalla, amekwenda kuvisha watu nishani. Waziri ana-*humiliate* wale *Soldiers* wa Wanyamapori hadharani, wale watu wamekuja na ndugu zao, anawa-*humiliate* kabisa. Wewe njoo hapa, ruka kichura, fanya nini; nani amempa hayo mamlaka? Mnadhaliisha nafasi zenu, achene kiki zisizokuwa na msingi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kuwa Waziri sio kwamba unajua kila kitu. Sasa unajiuliza na huyu ni Waziri ukimwangelia kwenye *twitter* unaweza ukashangaa.

*(Hapa kengele iligonga kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**SPIKA:** Dakika zako zimekwisha Mheshimiwa Lema, nakushukuru sana. (*Makofi*)

Mheshimiwa Waziri, Kapteni Mkuchika, hili la Arusha endapo ni kweli nadhani linahitaji kufuatilia kwa karibu, kwa sababu vyombo vya dola ikifika mahali vinavutana hadharani katika mazingira hayo, nasema endapo ni kweli, itakuwa inasikitisha sana. Kwa sababu Mheshimiwa Lema mambo mengi hajui, kwa hiyo sasa ndiyo maana nasema endapo ni kweli. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Bulembo nilikutaja, atafuatiwa na Mheshimiwa Mchungaji Msigwa dakika tano, halafu Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Nami nitumie nafasi hii kwanza kumpongeza Mheshimiwa Dkt. Mary Mwanjelwa, Naibu Waziri, kwa kazi nzuri anazofanya; Katibu Mkuu Dkt. Ndumbaro, Dkt. Francis, lakini mwisho nimpongeze shemeji

yangu anayependa Yanga sana kwamba Simba akifungwa goli moja yeye anaona raha kuliko ubingwa, basi awe anacheza *friendly match* anaacha kucheza ligi.

Mheshimiwa Spika, nianze kwenye elimu mtandao. Kuna jambo zuri limeanzishwa katika eneo hili; sisi tunaohangaika na biashara siku hizi tenda unatafuta kwenye mtandao. Sasa nataka kumwomba Mheshimiwa Waziri; kuna kijambo kimeanza hapo ndani na ni mapema kinaweza kuharibu maana yake yote.

Mheshimiwa Spika, tenda inavyotangazwa kwenye mtandao inakuwa na siku ya mwisho ya kurudisha *document*. Mnaingia pale kuomba, labda watu 15 au 20, kwenye urudishaji labda ni kesho saa sita mchana, kwenye urudishaji kwenye tenda sio lazima ulete siku ya mwisho, unaweza kuleta siku mbili kabla, siku moja kabla, ikishafika yale maeneo ambayo watu wana *interest* nayo, mtandao unaanza kucheza, kila mkipeleka haiendi, saa sita inapita wanafungua waliokwisha peleka wale wengine wanaambiwa mtandao ulikuwa na matatizo, hawa wanakwenda wapi kukata rufaa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo ombi langu katika eneo hili; wale viongozi wa taasisi husika tenda ikitangazwa wawe na mamlaka ya kusimamia ile mpaka saa ya mwisho, lakini tukiwaachia hawa vijana wanaocheza na *IT* watakuwa wanachagua kampuni wanazozitaka kwenye *competition* na ndiyo zitapata kazi, zile zingine siku zote mtandao umecheza mambo yameishia palepale. Kwa hiyo natoa ushauri kwenye eneo hilo la mtandao, imeanza kwa nia njema lakini imeshaanza kuleta matatizo.

Mheshimiwa Spika, suala la pili, sina mengi, nina machache sana, la pili niende TAKUKURU. Kwanza nimpongeze Mheshimiwa Rais kwa kumteua Kaimu Mkurugenzi wa TAKUKURU kuwa Mkurugenzi Mkuu, nampongeza sana, sana, sana. Pamoja na pongezi hizi nimwambie kwenye eneo lake kuna kazi moja ngumu. Ndugu zangu, TAKUKURU hawa wanafanya kazi kubwa sana, lakini kuna maeneo gari hawana. TAKUKURU amepewa *information*

anakwenda kukamata mtu gari unaambiwa *carburetor* imefanyaje wanaanza kusukuma; hivi watakamata? Watamkuta kweli?

Mheshimiwa Spika, TAKUKURU hawana usafiri, hawana vitendea kazi. Nchi hii pesa nyingi zimepelekwa kwenye maeneo mpaka chini; afya, elimu na huko ndiyo kuna rushwa. Taarifa ya rushwa imekuja lakini eneo hili sasa wanakwendaje. Mheshimiwa Kepteni Mkuchika kwenye utawala bora wanakwendaje hawa? Kwa sababu hawa ndio wanaangalia *value for money* lakini hawawezi kufika kwa sababu magari ni mabovu.

Kwa hiyo namuomba Mheshimiwa Kapteni Mkuchika; watu hawa wapeni vitendea kazi. Mwaka huu ni mwaka wa uchaguzi ndiyo kuna vurugu sana ya rushwa; watafikaje? Kama magari hayawezekani wapeni basi hata pikipiki.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo namwambia Mkurugenzi hongera kwa kuteuliwa, lakini pole kwa changamoto iliyopo mezani kwake, kwa sababu kuna mahali litatokea tukio, uwezekano wa kufanya kazi hiyo itakuwa ni ngumu kwa sababu kuna tatizo la usafiri. Kwa hiyo naiomba Serikali yangu na chama change, hebu wawaangalieni hawa ili uchaguzi uwe sawa kwa sababu tuko mlangoni.

Mheshimiwa Spika, niende kwenye hili lingine ambalo nimeliona. Mimi si mwanasheria lakini kwenye kuangalia ilivyoandikwa hapa nimeona jambo moja, sipendi kumuunga mkono Mheshimiwa Lema, lakini inafananafanana. Jambo hili ni kwamba TAKUKURU wamefanya uchunguzi wa kesi 183, wamepeleka kwa *DPP*, kesi zilizopelekwa mahakamani ni 47, sijui kama wanaiona hiyo.

Sasa chombo hiki kwa nini hakipewi meno, kwa nini hakiruhusiwi kufanya kazi yake moja kwa moja? Kwa sababu ukienda kusema kuna rushwa atakayekwenda kumata ni TAKUKURU, atakayepeleleza ni TAKUKURU, atakayekwenda mahakamani ni TAKUKURU, lakini hapa katikati kuna mtu anaitwa *DPP*. Hapana, Bunge ndiyo hili hili.



Mheshimiwa Spika, nimefanya utafiti kidogo kwa wenzetu wanafanyaje. Ukienda Rwanda kiongozi wa TAKUKURU kwa *system* ileile, akishachunguza akapeleleza, anakwenda mahakamani moja kwa moja, hapiti kwa mtu mwingine. Ukienda Uganda wanafanya hivyo hivyo, ukienda *South Africa* wanafanya hivyo hivyo, Botswana wanafanya hivyo hivyo na Ghana wanafanya hivyo hivyo.

Mheshimiwa Spika, lakini tujiulize, Manispaa yangu ya Ilala pale amekwenda mtu amekamatwa na rushwa, hana ujanja ameshakamatwa. Faili linafanyiwa uchunguzi wanamaliza ndani ya wiki moja, wanapeleka kwa *DPP*, faili lile linakaa miezi tisa. Hivi hao wengine wanaofanya mchezo ule pale wataona shida? Kwa nini wataalam wa sheria wasilete sheria, *DPP* huyu wakamwacha akafanya mengine aliyonayo mengi, TAKUKURU akapewa nafasi yake ya kuwajibika? Ndiyo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, maana yake hapa tunaona amepongezwa, amefanya nini, lakini 183, zilizokwenda mahakamani 47; inaumiza na haileti maana. Kwa sababu maana ya TAKUKURU kumkamata mtu akaenda kufungwa yule aliyeko chini yake aogope. Mmemkamata mwaka mzima, hajawahi kwenda watu wanaona ni vitu vya kawaida. Kwa hiyo naomba sana wenye sheria; Waziri wa Sheria hapa simwoni...

**WAZIRI WA KATIBA NA SHERIA:** Niko hapa.

**MHE. ALHAJ ABDALLAH M. BULEMBO:** Mheshimiwa Spika, samahani, Mheshimiwa Balozi Mahiga, Mheshimiwa Profesa Kabudi wanafanya sheria, hebu wamwambie *DPP* abakize kazi ndogo. Kwa nini wanamlazimisha kuwa na vitu ambavyo haviwezi? Huyu mtu wa TAKUKURU kama wanamwamini wapeni mamlaka kwa sababu mahakamani anakwenda yeye, Mwakili wake ndio wanakwenda; kukamata ni yeye, kupeleleza ni yeye; kwa nini kwenda mahakamani wanaweka mtu mwingine mwenye kazi nyingi huyu? *Effectiveness* yake haionekani. Kwa hiyo mimi hapa nawapongeza TAKUKURU kwa kazi wanayofanya lakini

nasema kama bado kuna *DPP* katikati siwezi kusema uongo Bungeni, nchi tano nimewatajia, waende wajifunze wenzetu wamefanyaje mpaka wakafikia hatua hiyo.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja ya Mheshimiwa Kepteni Mkuchika. Simba ndio anakuwa bingwa, Yanga imeambulia kushinda ushindi huu. Ahsanteni sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Bulembo kwa mchango wako mzuri. Hii hoja muhimu sana lakini ina utata.

Unajua bahati mbaya *DPP* naye, labda watu wa Katiba na Sheria siku zijazo hizo ikitokea kwa Wabunge watakaorudi, mje mpate nafasi ya kumsikiliza. Wakati mwingine mnaweza mkamtuhumu wakati kumbe ni mamia ya kesi tu, kumbe kesi zenyewe, maana yake naye ni mtaalam anayeangalia, vinginevyo ni usumbufu kupeleka watu mahakamani mpaka mahakama ikaanze kuchunguza yaani hapo ni pagumu sana kusema kwamba tatizo liko kwake, ni vizuri mkakaa mkasikiliza na *DPP* naye afunguke kidogo aina ya kesi. Wakati mwingine huenda mkaletewa kesi zilivyo hovyo hovyo mkashangaa, kwa hiyo mkajikuta kuna umuhimu wa chujio linaloitwa *DPP*. Mimi sijui lakini tusimlaumu moja kwa moja, hatujui kuna nini, iko haja ya kujua huyu *DPP* anakutana na mambo gani. Simtetei lakini nadhani *there must be a problem somewhere*.

Mheshimiwa Mchungaji Msigwa, dakika tano.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi. Wenzangu wamezungumza na mimi nimezungumza vilevile masuala ya ugonjwa huu, lakini nirudie tena mimi kwa mara ya kwanza walivyotangaza ugonjwa huu kwamba ni *pandemic* niliomba mwongozo humu wa Spika lakini bahati mbaya tulifanya mambo mengine ya kuhusu Mheshimiwa Zitto, naomba Serikali bado itupe mkakati maalum namna gani tunatoka katika jambo hili.

Mheshimiwa Spika, ninalotaka kuzungumza utawala bora ni jambo la msingi sana, lakini kwa bahati mbaya tunamaliza Bunge. Mimi niliyekwenda gereza ni wenzangu kuna unyanyasaji wa hali ya juu sana ndani ya magereza yetu. Wengine kweli ni mahabusu, wengine ni wafungwa.

Mheshimiwa Spika, nazungumza haya kwa sababu nime-*experience*. Kwa bahati mbaya sheria ile ya magereza ilitungwa wakati wa mkoloni wakati kuna *oppressor* na *oppressed*. Sasa bado *practice* ni ileile kama vile tuna *oppressor* na *oppressed*. Kuna mambo ya hovyoyote na ya aibu sana ndani ya magereza. Nimepata *experience*, mimi silaumu askari magereza kwa sababu ndiyo hali iliyopo na sheria inavyotokea, lakini watu kuvuliwa nguo hadharini mbele ya watu mia na kitu, mia mbili, mnapanga foleni mko uchi kuna kagunia tu kamezibwa kwa kisingizio cha kufundisha adabu, nadhani inaleta shida ndani ya magereza.

Mheshimiwa Spika, hakuna hata *privacy*, watu wanapimwa UKIMWI mnaambiwa panga foleni hapa mnapimwa UKIMWI, nyie msio na UKIMWI kaa huku mlio na UKIMWI kaa huku, yaani hakuna ubinadamu. Nadhani utawala bora ni pamoja na kuangalia watu.

Mheshimiwa Spika, kitu ambacho ni *paramount* kwenye Serikali yoyote ni uhai wa watu na maisha ya watu. Naomba haya masuala bahati mbaya tunamaliza muda wetu, wengine tunapozungumza magereza hivi wanaona kama hawatatembea, hata sisi wengine hatukuamini kwamba kuna siku tutakwenda magereza. Kwa hiyo hili suala la gereza sio suala la *Opposition* na nani, mtu yeyote anaweza kwenda magereza. Mimi sitetei wahalifu wala siwapiganii wahalifu kwamba watetewe, lakini nataka nizungumzie ile *privacy* ya watu, heshima ya watu, ubinadamu wa watu.

Mheshimiwa Spika, kwa sababu wengine wamekaa mule ndani amezungumza Mheshimiwa Lema wale watu wa *money laundering* wengine wamekaa miezi tisa, mwaka; kuna mtoto mmoja alifungwa na miaka nane sasa hivi ana

miaka 19 yuko ndani mle na kesi haijaanza kusikilizwa. Kwa hiyo kuna maonezi ya hali ya juu sana yako kule ndani, tunaweza tusijue kitu kinachoendelea.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri, kwa hiyo tunapozungumza utawala bora hebu tuangalie utawala bora katika maeneo mengi na mapana. Kuna watu wanaamini kwamba haya mambo hayatawakuta, lakini kuna siku meza zinaweza zikageuga hapa unaweza ukashangaa wengine hamjaona ile hali na wengine tunaamini labda Mungu alitupeleka kwa makusudi ili tuwe na nafasi ya kuweza kuwatetea wengine.

Mheshimiwa Spika, naomba suala hilo la magereza la uonezi wa watu, wanapigwa watu kama ng'ombe. Nimeshuhudia watu watatu wamefungwa pingu, anakuja mtu na kirungu anawabonda kama ng'ombe, binadamu ambao wengine ni mahabusu, hawajahukumikiwa lakini wanapigwa. Sikatai, inawezekana wengine labda ni wakorofi, lakini ile hali ni hali ya *oppressor* na *oppressed*, hii ni *republic*, tulipata uhuru. Haya mambo lazima kwa pamoja tukiwa *sober* tuyazungumze na tuyajadili kwa ajili ya vizazi vinavyokuja kwa faida ya Taifa letu. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, hii inasababisha vijana wengi wakitoka magereza wanakuwa wabaya zaidi, hakiwi chuo cha mafunzo, hawafundishwi, wanakuwa wabaya zaidi kwa sababu wako *treated* vibaya sana, kwa hiyo hawajifunzi chochote. Naomba tuwe na fikra za kufanya *reformation*, tu-*transform*, tubadilishe hii dhana ya wafungwa ili kiwe chuo, watu wakitoka magereza wawe na tija kwenye maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, mtu anafungwa anapewa faini na hakimu amefungwa miezi nane anakosa 50,000 inabidi atumikie miezi nane ndani ya gereza, gharama ya kumlisha ndani ya gereza ni kubwa sana kuliko 50,000. Sasa tunaangalia wanasema tupunguze watu magereza, wanajazana mle ndani, kwa hiyo hivi ni vitu vya kupanua

ubongo tu namna gani tunaweza tukasaidiana kama Taifa kwa sababu kuna changamoto na gharama zingine tunaziingiza bila sababu.

Mheshimiwa Spika, vijana wengi waliojaa magerezani ni wale ambao wana vimakosa vidogovidogo ambapo hata wangepewa nafasi za kufagia, kufanya usafi huko mitaani, lakini wamejazana magerezani tunatumia pesa nyingi kuwalisha, kuwatunza na kuhakikisha ulinzi wao ambazo hazina hata sababu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo naomba kwa masuala ya utawala bora hebu twende kwa upana zaidi, tusiji-*limit* tu kwenye masuala madogo. Mambo mengine wamezungumza lakini kuna maeneo mengine ambayo tunaliingiza Taifa kwenye shida na matatizo bila sababu, ni masuala ya kufikiri na kubadilisha sheria na kuzirekebisha ili magereza yenyewe iwe chuo cha mafunzo badala ya kuwa sehemu ya *torturing*. Kuna mateso ambayo yanawapata wengine mle ndani ya magereza hata wakoloni hawakufanya hivyo. Kwa hiyo ni vizuri tukayatafakari kwa pamoja ili tuweze kubadilisha mambo.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mchungaji Msigwa. Anatupa uzoefu wake kule sehemu sehemu kule, ile nyumba ya wanaume ile, nyumba ya wote ile, kwa hiyo hoja yako ni muhimu sana, tunakushukuru sana.

Labda nikumbushe kwamba wale watakaokuwa na maswali ya kiseru kwa Mheshimiwa Waziri, wote watayaulizia wakiwa Msekwa, kwa hiyo wawahi kule, majina yote ambayo nimepewa na *Chief Whips* wa vyama wawe kule Msekwa, Waziri atakuwa hapa.

Mheshimiwa Mwanne Mchemba, Mheshimiwa Venance Mwamoto, Mheshimiwa Mlinga, Mheshimiwa Mabula, Mheshimiwa Ruth Mollel, Mheshimiwa Khatib Haji Kai na Mheshimiwa Ally Keissy, endapo tutapata muda wa wote, lakini kila atakayetaka awe Msekwa Waziri atakuwa hapa.

Mheshimiwa Mnzava, atafuatiwa na Mheshimiwa Mlinga.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nami niweze kuchangia hotuba hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora. Kwanza kabisa niungane na wenzangu kumpongeza sana Mheshimiwa Rais, lakini pia kumpongeza Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri na Makatibu Wakuu na watendaji wote wa taasisi zote waliokuwa chini ya ofisi hii kwa kazi kubwa na nzuri ambayo wameifanya.

Mheshimiwa Spika, kipekee nitumie nafasi hii kuwapongeza sana TAKUKURU, wanafanya kazi kubwa, wanafanya kazi nzuri. Huu ndiyo mwelekeo ambao kama Taifa tunatamani kwenda huko, kwamba vyombo vyetu vya ulinzi na usalama pamoja na kazi kubwa na nzuri wanayoifanya lakini watusaidie sana kuhakikisha kwamba kwa kiasi kikubwa tunasaidia kuzia athari zinazoweza kujitokeza kabla hazijitokeza.

Mheshimiwa Spika, kitendo cha kusaidia kuokoa fedha za umma, kusaidia kuokoa fedha za wananchi, ni kitendo kizuri sana. Pamoja na kwamba tunalo jukumu pia la kuchukua hatua yanapokuwa yametokea matatizo, lakini ni jambo zuri tukijitahidi kuzuia lakini pia kuokoa fedha za umma kabla matatizo hayajatokea na kuweza kutuathiri sana kama Taifa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kazi kubwa na nzuri ambayo inafanywa na Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, lazima tukubaliane kwamba bado tuna changamoto kubwa kwa upande wa utumishi. Tunao uhaba mkubwa wa watumishi kwenye maeneo yetu, tunaomba sana ofisi hii ijitahidi kuwa na mkakati madhubuti wa namna ya kutusaidia kutatua changamoto hii.

Mheshimiwa Spika, juzi TAMISEMI wametuahidi kutoa fedha za zahanati tatu kwa kila halmashauri. Sasa halmashauri 185, zahanati tatu zikikamilika kwa *standard* ya

Wizara ya Afya zahanati inatakiwa kuwa na watumishi wasiopungua 15, unaweza kuona tunakuwa tuna uhitaji kiasi gani wa watumishi kwa ajili ya kuleta maendeleo kwenye maeneo yetu. Ni vyema tukajipanga vizuri na mapema kuwa na mipango ya namna gani ya kutatua tatizo la changamoto ya watumishi. Hata hivyo, pamoja na kazi kubwa tuliyofanya tuendelee kuangalia namna gani ya kuboresha maslahi na stahiki za watumishi wetu.

Mheshimiwa Spika, nimewapongeza TAKUKURU na kama walivyotangulia kusema wachangiaji wengine ni kweli unaweza kuona kwamba wanafanya uchunguzi wa majalada mengi, mashauri mengi lakini mwisho wa siku yanayokwenda mahakamani ni machache. Jambo hili sio jipya, miaka ya nyuma tumewahi kuwa na mvutano mkubwa sana kati ya Ofisi ya *DPP* na Ofisi ya TAKUKURU na mvutano ulikuja mpaka ukaenda hadharani ukaenda mpaka kwenye vyombo vya habari. Kama ulivyosema ni kweli unaiona haja ya kuharakisha angalau mashauri yanayofanyiwa kazi TAKUKURU yaweze kwenda mahakamani mapema na ikiwezekana yote ambayo yanachunguzwa yakikamilishwa yakipelekwa kwa *DPP* wapate kibali cha kwenda mahakamani.

Mheshimiwa Spika, yapo mambo ambayo lazima tukubaliane kama nchi; kwanza ni jambo la msingi na la muhimu kuwa na mamlaka inayotambuliwa, yenye mamlaka na kibali cha kusema shauri lipi liende mahakamani kwa sababu ya kuangalia mambo mengi yakiwemo maslahi ya Taifa. Kwa hiyo bado upo umuhimu wa kuyapitisha kwa *DPP*.

Mheshimiwa Spika, kinachoweza kufanyika hapa ni namna tu ya kufanya, taasisi hizi zote ni taasisi ya Serikali, ziangalie namna gani ya kuwasiliana na kuwekeana kanuni ikiwezekana za muda lakini pia za kupeana taarifa. Kama uchunguzi umekamilika jambo hili haliwezi kwenda mahakamani basi TAKUKURU apate taarifa mapema kwamba jambo hili haliwezi kwenda kwa sababu moja, mbili, tatu, nne, lakini pia kuwe na angalau mawasiliano ya muda;

namna gani unaweza ukawekwa muda wa kuzingatiwa kabla shauri halijapelekwa mahakamani.

Mheshimiwa Spika, nitumie nafasi hii kuzungumza kidogo, huu mwaka ni wa uchaguzi na kama taifa tunajiandaa Mwenyezi Mungu akitujalia kwenda kwenye uchaguzi mwezi Oktoba. Kumekuwa na malalamiko na maneno mengi hususan kuhusu Tume ya Taifa ya Uchaguzi. Leo humu ndani nimesikia pia ukitolewa mfano wa Wakurugenzi wa Halmashauri ambao ndiyo wasimamizi wa uchaguzi.

Mheshimiwa Spika, kwanza lazima tukubaliane Tume yetu ya Uchaguzi Tanzania ni huru. Ni huru kwa mujibu wa Katiba, muundo wake na kwa namna inavyofanya kazi. Ukisoma Sheria ya Taifa ya Uchaguzi imeeleza taratibu za uchaguzi kuanzia hatua ya kwanza ya uandikishaji, kampeni, upigaji kura, uhesabuji wa kura na utangazaji wa matokeo. Kwa tafsiri yake ni kwamba hakuna msimamizi wala mtu anayejiamulia mwenyewe kipi cha kufanya na kwa wakati gani kwa sababu mambo yote yanayopaswa kufanyika yamewekwa kwa mujibu wa sheria. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hili la Wakurugenzi, inasemwa kwamba wako Wakurugenzi ni makada wa Chama cha Mapinduzi. Lazima tukubaliane ni watu wachache sana ambao hawana vyama kwenye nchi zetu lakini tunapokwenda kwenye uchaguzi kuna viapo vya kukana huo uanachama, hilo ni jambo la kwanza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo la pili lazima Tanzania tujipongeze tuna sheria nzuri sana ya uchaguzi. Ukisoma Kifungu cha 7(1) cha Sheria ya Taifa ya Uchaguzi ndicho kinachosema kwamba Wakurugenzi wa Halmashauri za Miji, Manispaa na Halmashauri watakuwa wasimamizi wa uchaguzi. Ukisoma Kifungu Kidogo cha (2) cha hicho Kifungu cha 7 kinaeleza kwamba anaweza akateuliwa mtu mwingine yeyote. Ukisoma Kifungu cha 3 kinaielekeza Tume kama yako mazingira ambayo tunaona kwamba siyo rafiki huyu Mkurugenzi ataachwa atateuliwa Afisa mwingine yeyote wa



Serikali Mwandamizi aweze kuwa msimamizi wa uchaguzi.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, sheria haijatufunga na mfano upo. Mwaka 2017 Novemba tulikuwa na uchaguzi mdogo wa Madiwani kwenye kata sita kwenye Mkoa wa Arusha, tano zikiwa Halmashauri ya Wilaya ya Meru na tano zikiwa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Meru alilalamikiwa na viongozi wa CHADEMA kwamba anaonekana kuwa na *element* za kukipenda Chama cha Mapinduzi. Tume ya Taifa ya Uchaguzi ikamteuwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Arusha awe Msimamizi wa Uchaguzi kwenye Wilaya ya Meru na Halmashauri ya Arusha, akiitwa Dkt/ Charles Mahela ambaye sasa hivi ndiye Mkurugenzi wa Tume ya Taifa ya Uchaguzi.  
(*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, mwaka jana kwenye Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kulikuwa na malalamiko kuhusu Wakurugenzi. Kwa sehemu kubwa Wakurugenzi hawakutumika kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa, Serikali ilika chini kwa mujibu wa sheria na kanuni wakateuliwa watu wengine wakaenda kusimamia uchaguzi wa Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Spika, ni vibaya kusema kwamba sheria au Katiba yetu inaifanya Tume kulazimika kusaidia kupendelea chama kimoja kwa mazingira hayo ambayo wanayo. Hata kule kwingine ambako wanapigia kelele kama Korogwe, walipolalamika kwamba wameonewa wakaambiwa haki ipo nendeni Mahakamani wakaenda Mahakamani mambo yalipokuwa magumu wakakimbia wenyewe na kesi wakaamua kuifuta wenyewe. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sheria yetu iko vizuri. Tuko vizuri na Tume yetu inafanya kazi nzuri na Mungu akitupa neema na uzima tunaamini Tume itafanya kazi nzuri tena mwaka huu mwezi Oktoba kwa mujibu wa kalenda na utaratibu utakaokuwa umepangwa na Tume.

Mheshimiwa Spika, nimalizie na *TASAF*. Niipongeze sana Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora, *TASAF* wanafanya kazi nzuri. Ombi langu mtusaidie yale maeneo ambayo bado watu wetu hawajafikiwa na huduma hii angalau watu wetu nao waweze kuipata, iweze kufika kwenye vijiji vyote ikiwemo vijiji vilivyokuwa vimbakia ili watu wetu waweze kunufaika na kujikwamua kutoka kwenye hali duni za maisha na kuwa na hali nzuri.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi. Naunga mkono hoja hii kwa asilimia 100, endeleeni kuchapa kazi na tunawatakia kila la kheri. Nakushukuru sana. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Mnzava. Nilishakutaja Mheshimiwa Mlinga na Mheshimiwa Lusinde utafuatia.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Naomba nianze kwa upande wa Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi.

Mheshimiwa Spika, labda sijui ufahamu wangu ni mdogo, bado sijaelewa, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma, leo hii ni ajabu sana anasimama Mbunge Bungeni anatoa *experience* ya jela. Leo hii sijaelewa wajibu wa Tume ya Maadili Mbunge anaenda kuvamia jela, Tume ya Maadili imekaa kimya. Sijaelewa wajibu wa Tume ya Maadili leo hii Mbunge anasababisha mauaji, Tume ya Maadili wajibu wake ni nini? Maana yake wanaishia kwenye mali na madeni tu lakini hapa inasema maadili ya viongozi wa umma. Mheshimiwa Waziri nitashika shilingi kwenye kipengele hiki, nakupa taarifa kabisa. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, hili siyo naliongea mimi tu, Msemaji wa Kambi Rasmi ya Upinzani amesema tuwe tunawafanyia *vetting* viongozi kabla hatujawateuwa na hii ni hatari sana. Nataka nikupe mfano mmoja, Wizara moja nyeti sana ambayo *PCCB* na Usalama wa Taifa wako chini ya Wizara hiyo aliyekuwa Katibu Mkuu wake baada ya kustaafu tu

akawa Mbunge wa Upinzani, hii ni hatari. Sasa jilize Katibu Mkuu huyo watu ambao aliteuwa mikononi mwake ni watu wa namna gani? Ndiyo maana leo hii tunalalamika viongozi lazima wafanyiwe *vetting*. Naaamini katika Serikali ya Awamu ya Tano hilo halipo.

Mheshimiwa Spika, tunapoongelea utawala bora...

**SPIKA:** Nilikuwa bado natafakari Mheshimiwa Mlinga kwamba yaani Mbunge anatoa uzoefu wa jela?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Aah, hebu endelea Mheshimiwa. (*Kicheko*)

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hotuba ya Waziri, Kambi Rasmi ya Upinzani hili wamelleleza vizuri sana, nguzo ya utawala bora ni uwazi na uwajibikaji, sehemu linapotokea jambo ikatokea minung'uniko ina maana uwazi haupo. Wiki mbili zilizopita lilituuliwa Baraza Kivuli la Mawaziri la Upinzani, minung'uniko ilikuwa mingi sana. Mbaya zaidi wakasema wameteuliwa wanawake watupu, wengine wakasema waliokuwa karibu zaidi, wengine wakasema utawala wa kisultana. Uwazi na uwajibikaji ni muhimu sana katika uongozi wetu. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, wewe ni shahidi kuna Wabunge humu wanakatwa michango shilingi milioni moja, shilingi laki tano kuchangia chama. Ikafika kipindi wewe Meza yako ilisema hapana, hawa Wabunge wanaonewa sikati, nawalipa wenyewe muende mkalipe, wale Wabunge walikaa miezi nane hawakulipa zile hela wakasema hatuwezi tukalipa hizi pesa kwa sababu hakuna uwazi katika matumizi ya hizi hela lakini juzi wakatishiwa kufutwa chama kwa hiyo, wanalazimika saa hizi kulipa madeni.

Kwa hiyo, uwazi na uwajibikaji usiishie tu Serikalini ushuke hadi kwenye vyama. Sisi Chama cha Mapinduzi sasa hivi ukitaka kutoa mchango kuna *control number* unapewa,

Bashiru anaiona kule, lakini wenzetu hilo halipo. Matumizi ya ruzuku hamna uwazi katika hilo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Yaani bado wanabanwa kutoa mamilioni ya shilingi?

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ndiyo.

**SPIKA:** Kwa sababu miaka ya nyuma hili jambo lilikuwa linafanyika kupitia Ofisi ya Bunge kwamba Wabunge wamekubaliana zikatwe hizi, tukawa tunafanya lakini baada ya muda tukapata malalamiko sana kwamba hii ni uonevu tukaacha, tunampelekea kila Mbunge kwenye akaunti yake. Sasa kumbe hukohuko mnarudisha tena, shauri yenu, mimi niliwasaidia. Endelea Mheshimiwa Mlinga. (*Kicheko*)

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante. Unajua Sheria yetu ya Vyama vya Siasa inabidi iletwe tena Bungeni ifanyiwe marekebisho kwa sababu wale Wabunge cha kusikitisha zaidi wameambiwa watafutwa uanachama na hakuna *option* nyingine. Sasa kwa sababu wengine umri wao mdogo wanapenda kuendelea kuwa Wabunge wakashindwa, kwa hiyo, bado wanaendelea kuzikusanya na kuzipeleka.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo nataka kuliongelea kubwa na baya linaloendelea sasa hivi katika nchi yetu, kuna viongozi wanaitumia vibaya hii vita dhidi ya *Corona*. Hivi navyoongea kuna baadhi ya maeneo wameweka mageti katikati ya miji kuwa ukija na gari lako unashuka unanawa, unarudi tena kwenye gari ndiyo unaendelea na safari, katikati ya miji.

Mheshimiwa Spika, kuna mwananchi mmoja leo amehukumiwa kwenda jela miezi sita ama kulipa *fine* shilingi elfu hamsini kwa sababu hajashuka kwenye gari kwenda kunawa. Hili jambo ni baya, vita dhidi ya *Corona* inatumika vibaya. Naomba watu kama madaktari watumike kwenye

hili tusiwaachie askari, askari hawajui taratibu nyingine za kiafya.

Mheshimiwa Spika, la mwisho nataka niongelee suala la wafanyakazi *vis-à-vis Corona*. Nataka nitoe mfano wa rafiki yangu mmoja ni mwalimu *graduate* ambaye anapokea mshahara Sh.716,000, makato ya mshahara huo ni 37%. Naomba Serikali iondoe baadhi ya makato kwa kipindi hata cha miezi mitatu.

Mheshimiwa Spika, rafiki yangu huyu anayepokea shilingi 716,000 anakatwa kodi ya 12% ambayo ni shilingi 86,000; Bodi ya Mikopo 15% ambayo ni shilingi 107,000; *pension* 5% ambayo ni shilingi 35,000; *NHIF* 3% ambayo ni shilingi 21,000; na *CWT* 2% ambayo ni shilingi 14,000. Matumizi yake, mfanyakazi huyu anatuma kijijini kila mwezi shilingi 30,000; umeme analipa shilingi 20,000; maji analipa shilingi 10,000; king'amuzi cha bei ya chini kabisa shilingi 15,000; nauli yake shilingi 80,000; chumba shilingi 50,000; *sanitizer* shilingi 20,000; na vocha shilingi 10,000. Mfanyakazi huyu anatumia shilingi 800,000 kwa mwezi, anakwepaje *Corana* hii? (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, nashauri tuwapunguzie mzigo wafanyakazi. Napendekeza Bodi ya Mikopo kwa sababu wanafunzi hawako chuo saa hizi hiki kipengele kingeondolewa *atleast* kwa miezi mitatu. Mifuko ya *pension*, haya makato ya *pension* 5% yangesimamishwa sasa hivi ili kumsaidia mfanyakazi kwa sababu tunajua Tanzania mfanyakazi mmoja anategemewa na familia zaidi ya tano. Kwa hiyo, tukianza kwa wafanyakazi tutawarasisia hata wafanyabiashara.

Mheshimiwa Spika, hivi Vyama vya Wafanyakazi na wenyewe wangesimamisha makato. Vyama vya Wafanyakazi sasa hivi ni wakati muafaka wa kumsaidia mfanyakazi kupambana na hii *Corona*. Kuna *CWT*, *TUCTA*, wamekaa kimya hawamsaidii mfanyakazi chochote. Kwa hiyo, naomba Bunge lako liridhie upunguzwaji wa makato kwa mfanyakazi ili aweze kupambana na *Corona* vizuri.

Mheshimiwa Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Goodluck Mlinga. Mheshimiwa Livingstone Lusinde atakuwa ndiyo mchangiaji wetu wa mwisho.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, namshukuru Mungu kupata nafasi ya kuchangia Wizara ya Utawala Bora. Kwa namna ya pekee nikushukuru wewe kwa kunipa nafasi hii, ili nitoe mchango wangu mdogo.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Waziri, Kapteni Mstaafu George Huruma Mkuchika pamoja na Naibu wake Dkt. Mary Machuche Mwanjelwa, Katibu Mkuu na Watendaji wote katika Wizara hiyo.

Mheshimiwa Spika, tunaipongeza Serikali kwa hatua kubwa ambazo imechukua kukabiliana na *Corona*. Maneno yote yaliyosemwa na Waheshimiwa Wabunge juu ya namna bora ya kujikinga na ugonjwa huu ni sahihi kabisa ambayo Serikali ikiyachukua na kuyafanyia kazi yanaweza kuwa muafaka.

Mheshimiwa Spika, lakini nina nyongeza kidogo; kuna vitu vya lazima kama masoko, uwekwe utaratibu mzuri wa watu kupata bidhaa. Hata hivyo, mimi sielewi ni kwa namna gani baa inakuwa kitu cha lazima? Ni kwa namna gani mtu aliyelewa anaweza kufuata masharti ya kujikinga na *Corona*? Hapa mimi napata tabu sana, mtu ameshakunywa, yuko mbwii, halafu anaambiwa akae hatua ngapi kutoka mhudumu, atawezaje kukubali huyu mnywaji? Hivi mtu akinywea nyumbani kwake hawezi kulewa mpaka awe baa? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, hizi baa zote zimeachwa wazi, hivi kweli zinatusaidia kujikinga na *Corona*? Wale wahudumu wa baa mtu akishakolea kinywaji anataka amkumbatie, akikataa anafukuzwa kazi, watakuwa na usalama kiasi gani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kuna haja gani ya kucheza *disco* katika hali ya ugonjwa kama huu? Kwa nini majumba ya *disco* yasifungwe na baa ukawekwa utaratibu na kama tunaona vipi kwa nini tusuzuie hata hizo baa Serikali ikasema basi tusubiri watu watakuonywa wakati tumekabiliana na Corona. Kuliko sasa hivi mtu amelewa saa 5:00 usiku halafu unamwambia fuata masharti nawa hapa, nani atakubali? Napata tabu kidogo kwenye jambo hilo. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, lakini imezungumzwa namna ambavyo *TASAF* natusaidia na mimi sina ubishi kabisa. Mimi ni Mbunge ninayetoka kwenye vijiji, *TASAF* inasaidia sana watu vijijini. Juzi Mheshimiwa Rais alisema kuna malipo hewa kwenye *TASAF*, hatua kali zichukuliwe na zionekane kwa wale watu ambao wanapenda kuchafua jambo hili ambalo linasaidia sana watu maskini wa vijijini. Tusipuuze, kama Mheshimiwa Rais anasema kuna matumizi hewa kwenye *TASAF*, hapo sasa ndiyo pakutolea macho kabisa ili kuweza kunusuru kaya maskini ambazo zimekuwa zikinufaika na mchango huu.

Mheshimiwa Spika, kuna mambo yamezungumzwa hapa kuhusu utawala bora. Hapa naomba nitoe darasa kidogo, unajua watu tunaposema utawala bora uanzie kwenye vyama sijui kwa nini hatuelewani. Chama cha siasa ndicho kinachopambana kupata Serikali.

Kwa hiyo, chama chenyewe cha siasa kisipokuwa na demokrasia pana, kisipokuwa na utawala bora chenyewe ndani ya chama maana yake kikishika Serikali ni hatari zaidi. Kwa hiyo, tunaposema utawala bora uanzie ndani ya vyama tunamaanisha kwamba vyama ndiyo baadaye vitashika Serikali, ndiyo vinavyotafuta dola.

Mheshimiwa Spika, nguvu kubwa inayotumiwa na Wabunge wa Upinzani, angalia alivyozungumza rafiki yangu Mheshimiwa Lema na Mheshimiwa Msigwa hivi wangekuwa wanazungumza hivyo kwenye Kamati Kuu ya CHADEMA wanataka haki itendeke hivyo kwa nguvu hiyo, leo CHADEMA ingekuwa na madudu kama tunayoyaona? Yasingekuwepo!

Wanangojea kuja kusema tu humu Bungeni lakini ndani ya chama chao hawasemi. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, kwa mfano mtu anasema kwa nini sheria zinatungwa za kukandamiza watu? Kumfukuza mtu uanachama kwenye chama chochote cha siasa duniani ni kumuua kisiasa. CHADEMA wameshamuua Mheshimiwa Zitto, Kafulila, wanaona ni utawala bora tu na ni adhabu sawasawa. Linapokuja suala la uzoefu wa gerezani, hivi Mheshimiwa Msigwa siku mbili gerezani kweli huo ni uzoefu? Siku mbili wewe unaweza ukayajua mambo ya jela jamani? Tusidanganyane hapa jamani, siku mbili, unaingia leo, kesho umelipiwa umetoka, unaita *press* unazungumza ndiyo unatuambia uzoefu wa jela? Acheni kutudanganya humu bwana, hakuna mtu mwenye uzoefu wa jela hapa.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali mwanasiasa yeyote sasa hivi akikosea hapana kufungwa jela za Dar-es-Salaam wanakunywa chai, wapelekwe gereza linaitwa Kingulungundwa, liko Kusini huko, hilo ndiyo kiboko. Wewe unaenda unakaa pale eti Keko unakuja unasema nilikuwa jela, jela Keko, kuna chai, watu wanakuja kukuona, unaletewa mswaki, sasa hivi watu wakifanya makosa wapelekwe Kingulungundwa, kule ndiyo kuna shughuli iliyokamilika. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, nasema hivyo kwa sababu nina uzoefu. Wakati napigania CHADEMA mimi nilikaa mahabusu siku 20, kwa hiyo, nina uzoefu mkubwa kuliko huo wa siku mbili wa hawa, wanapiga kelele bure tu hapa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, jela zimewekwa kurekebisha tabia za watu. Kama mtu nje ni mkorofi, halafu na jela nako ukamlee chai ya maziwa, si itakuwa hatari kubwa zaidi?

## TAARIFA

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, taarifa.



**SPIKA:** Mheshimiwa Lusinde unapewa taarifa na Mchungaji.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Spika, nilitaka nimpe taarifa kwamba sijakaa jela siku mbili. Nilikaa kwanza mahabusu siku tisa ukajumlisha na siku tatu. Kwa hiyo, nina uzoefu kidogo ndiyo maana ninaweza kuzungumza. *(Kicheko)*

**SPIKA:** Taarifa hiyo Mheshimiwa Lusinde.

**MHE. LIVINGSTONE J. LUSINDE:** Mheshimiwa Spika, yaani shemeji ana uzoefu wa siku 12, bado mimi zile 20 nimemzidi tu, kwa hiyo, unisikilize mimi mwalimu sasa nikueleze. Ukipenda kachumbari upende na pilipili. Ukiendesha vitu bila kufuata sheria yale yata kayokupata ni sehemu ya ule uvunjifu wa sheria.

Mheshimiwa Spika, tusichanganye mambo, kuvunja sheria ukaadhibiwa kwa sababu ya kosa la kuvunja sheria huwezi ukasema ile adhabu unayopewa unateswa, hapana. Wewe unatumikia adhabu kama ambazo hata wao kwenye chama wameshawahi kutoa; walimpa Mheshimiwa Komu adhabu hapa, wametoa adhabu kwa Wabunge wengi tu, lakini sisi hatukuwahi kusema kwamba wanakiuka haki za binadamu, wanawanyanya watu, hapana. Kwa hiyo, kama ukikosea na ukapewa adhabu unatumikia ile adhabu kwa haki kulingana na kosa ulilolifanya.

Mheshimiwa Spika, wao wanakosa sifa kwa sababu tabia yao siyo ya kufuta sheria. Hata kwenye huo uchaguzi tunaousema, tunasema tutafanya uchaguzi wa haki kama kila mwanasiasa atatii sheria na kanuni za uchaguzi lakini kama hutatii sheria na kanuni za uchaguzi ni lazima utakutana na dola na ukikutana na dola huwezi kusema unaonewa maana dola kazi yake ni kumrekebisha mtu.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, tusikae hapa tukaanza kusema ooh, wanavuliwa nguo. Sisi Wabunge tulikwenda jeshini na wa upinzani wengine wako hapa, tuliyoyaona kule

mengine yalikuwa ni kwa ajili ya *discipline* za kikamanda, hatuyasemi humu. Kwa hiyo, kama ulivua nguo ukaruka kichura kidogo yale ndiyo yanakuweka vizuri siku nyingine utaogopa kwenda jela kwa sababu unajua ukienda jela utavuliwa nguo, utaruka kichura halafu badaye utaingia kwenda *lock up*, utajirekebisha.

Mheshimiwa Spika, juzi Mheshimiwa Rais ametoa msamaha wa wafungwa elfu moja na kitu, wote tuliona hapa, lakini ndani ya wiki moja waliokuwa wafungwa zaidi ya 10 waliiba tena wakarudi jela, sasa jela ukiweka maziwa watarudi wangapi? Kama katika hali ambayo Mheshimiwa Msigwa katuambia jela kunatisha lakini mtu kasamehewa leo kesho anaenda kuiba makusudi ili arudi jela akaendeleo na maisha ya jela, je, tukianza kuweka pipi na soda hizo jela zitakaa watu wangapi? (*Kicheko*)

Kwa hiyo, mimi nashauri kwamba jela ziendeleo kuwa jela za kurekebisha tabia za watu. Kusema kwamba eti mtu akitoka jela anakuwa mbaya zaidi, anatushauri kwamba sasa tuongeze makali zaidi kwenye jela ambayo yataendeanana na huyu mtu anayekuwa mbaya zaidi mpaka atakapojirekebisha. Hatuwezi tukaigeuza jela ikawa hoteli, isipokuwa ni lazima watu wetu wakitoka jela wajirekebisha.

Mheshimiwa Spika, tumeona kati ya 1,200 waliorudi 10, maana yake wengine wote elfu moja na kitu wamejirekebisha. Tunakutana nao wengine wahubiri wa injili, wengine wanaswali, wengine wamekuwa wazee wa Kanisa.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja ya utawala bora, tuendeleze nchi yetu, tusimamie sheria na uchaguzi wa mwaka huu Mungu akitusaidia tukapambana na Corona kisawasawa tutaufanya kwa huru na haki. Ahsante sana, naunga mkono hoja. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Lusinde. Ni kweli. Hii ya mabaa kuendelea kuwa wazi, Mheshimiwa Jenista ushauri huo mkauangalie. *Barhata* kama itakuwa wazi, basi iwe *take away*, mtu afungashe aondoke na bia zake. (*Makofi*)

## MICHANGO KWA MAANDISHI

**MHE. ORAN M. NJEZA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuwashukuru na kuwapongeza Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Samia Suluhu Hassan, Makamu wa Rais wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Mheshimiwa Kassim Majaliwa Majaliwa, Waziri Mkuu wa wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania; Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Utumishi na Utawala Bora, kwa uongozi wao na utendaji uliotukuka wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, napenda pia kutumia fursa hii kukupongeza wewe binafsi, Naibu Spika na uongozi wote wa Bunge kwa uongozi wenu mahiri na wenye ubunifu wa hali ya juu katika kuongoza mhimili wa Bunge.

Mheshimiwa Spika, katika kipindi cha miaka minne, Serikali kupitia Wizara ya Utumishi na Utawala Bora imesimamia kwa uadilifu na ufanisi mkubwa masuala yote ya utumishi na hasa kurudisha uwabikaji kazini iliopelekea ufanisi mkubwa hasa kwenye utekelezaji wa miradi. Jimbo la Mbeya Vijijini limenufaika kupitia miradi ya *TASAF* ambapo imebadilisha maisha ya wananchi katika vijiji husika. Pia kwa kusimamia vizuri, rushwa na upendeleo umepungua kwa kiasi kikubwa kupelekea ufanisi mkubwa sehemu za kazi na hata miradi kukamilika kwa ufanisi mkubwa.

Mheshimiwa Spika, pamoja na mafanikio hayo makubwa, napendekeza upanuzi wa Chuo cha Watumishi Mbeya na eneo muafaka kwa ujenzi wa chuo kipya na cha kisasa ni Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya ambapo kuna maeneo mazuri ikiwemo yaliyokuwa mashamba ya *Tanganyika Packers* Mbalizi.

Mheshimiwa, Spika, napendekeza pia kuboresha mfumo wa *TASAF* ikiwemo msukumo wa miradi ilenge maeneo yatakayochochea uzalishaji wa mali ili zisaidie jamii kwa upana mkubwa. Pamoja na maeneo ya uzalishaji, msukumo ujumuishe kuimarisha masoko ya bidhaa

zitakazozalishwa katika maeneo ya mradi. Miradi ilenge kuboresha elimu na hata kusomesha watoto wanaotoka kwenye kaya maskini ya maeneo husika. Serikali iboresha taratibu za kupata maeneo ya miradi ya *TASAF* ili kupunguza malalamiko.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARIAM N.KISANGI:** Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja asilimia mia moja, kwa kweli ni ukweli usiopingika kuwa utumishi wa umma umetukuka.

Mheshimiwa Spika, nampongeza sana Mheshimiwa Rais kwa mipango mizuri aliyotuwekea katika utumishi wa umma. Nampongeza pia Mheshimiwa Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na Mheshimiwa Waziri wa Wizara pamoja na Katibu Mkuu na Naibu Katibu Mkuu kwa utendaji uliotukuka. Kwa kweli imeiweka Wizara hii katika mfumo ambao umewapunguzia watumishi kuwa na uwazi wa taarifa zao. Watumishi wa umma wanafanya kazi na mishahara inatolewa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, changamoto kubwa ni kwa baadhi ya watumishi kama walimu kukosa stahiki yao ya kulipwa nauli na mizigo yao pale wanapostaafu. Tatizo limekuwa kubwa, ni vyema Serikali wakatoa maelezo kama haki hiyo ipo au tuifute, vinginevyo malimbikizo yatakuwa makubwa na imani yao ni kulipwa. Serikali yangu ikibidi sasa tuangalie nini la kufanya.

Mheshimiwa Spika, naipongeza sana Serikali kwa kuwezesha kaya maskini kupitia *TASAF*. Kwa kweli mpango huu umezisaidia kaya masikini katika nyanja mbalimbali. Nimeshuhudia katika Mkoa wa dar es Salaam jinsi kaya mbalimbali zilivyofaidika na *TASAF*. Naunga mkono hoja kwa kumpongeza Mwenyekiti wa Kamati ya TAMISEMI, Makamu wake na wajumbe wote wa Kamati kwa kazi nzuri. *TASAF* imetekeleza llani ya Chama cha Mapinduzi kuwezesha kaya masikini. Mbarikiwe watendaji wote kwa kazi nzuri.

**MHE. ENG. RAMO M. MAKANI:** Mheshimiwa Spika, kwanza natoa pongezi kwa Mheshimiwa Rais, Makamu wa Rais, Waziri Mkuu na timu nzima ya Serikali akiwemo Waziri mtoa hoja hii *Comrade* Mkuchika.

Pili, natoa pongezi nyingi sana kwa CCM kwa utekelezaji wa ilani ulioweka rekodi.

Mheshimiwa Spika, naomba MKURABITA waongezewe fedha katika bajeti ili watekeleze majukumu yao ipasavyo kwani utekelezaji huo unawaongezea wananchi uwezo wa kuchangia uchumi wao na wa Taifa zaidi kupitia biashara zao.

Mheshimiwa Spika, *TASAF* inafanya kazi nzuri sana. Hata hivyo wanayo nafasi ya kufanya vizuri zaidi. Hivyo warekebishe kasoro zilizopo sasa katika utekelezaji wa majukumu yao ikiwa ni pamoja na kuwafikia walengwa badala ya watu wajanja.

Mheshimiwa Spika, kuhusu mpango wa kurithishana madaraka (*succession plan*) ni muhimu sana kwa kuboresha na kuimarisha ikama ya watumishi Serikalini kwa namna endelevu.

Mheshimiwa Spika, Wilaya ya Tunduru ina upungufu wa watumishi kama ilivyo katika Wilaya zingine. Hata hivyo, naiomba Serikali iingalie Halmashauri ya Wilaya ya Tunduru kwa jicho la ziada kutokana na kuwa mbali pembezoni. Ni ombi langu kuwa sekta za afya, elimu, kilimo na ardhi zipewe umuhimu wakati wa kuzingatia maombi yangu.

Mheshimiwa Spika, ahsante naomba kuwasilisha na naunga mkono hoja.

**MHE. BERNADETHA K. MUSHASHU:** Mheshimiwa Spika, nampongeza Waziri na Naibu Waziri kwa hotuba nzuri.

Mheshimiwa Spika, nampongeza Mheshimiwa Rais kwa juhudi zake na kuwezesha kupunguza rushwa Tanzania.

Naipongeza kwani Wizara hii imefanya kazi nzuri sana kuwakwamua watu wengi waliokwama kwenye lindi la umaskini kupitia Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

Mheshimiwa Spika, wapo baadhi ya walengwa ambao wakipata fedha za TASAF wanakula, zinaisha na kungoja nyingine au wengine wanazitumia kulewea pombe. Napendekeza hawa walengwa wasimamiwe, waelimishwe ili waweze kutumia fedha wanazozipata waweze kuanzisha miradi midogo midogo ili kujiongezea kipato na hii itapunguza utegemezi.

Mheshimiwa Spika, watumishi wa umma wamekaa muda mrefu bila kupanda madaraja na bila kupandishiwa mishahara. Hali ya maisha imepanda sana. Ili waweze kuyamudu maisha naomba watumishi wa umma wapandishiwe mishahara na waajiri wote wahakikishe watumishi wanapandishiwa madaraja kama wanavyostahili.

Mheshimiwa Spika, sekta nyingi zina upungufu mkubwa wa watumishi wa umma hasa katika elimu na afya. Tunaomba Serikali ijiri watumishi wa kutosha hasa katika afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. SOPHIA H. MWAKAGENDA:** Mheshimiwa Spika, nianze na TAKUKURU; kuelekea uchaguzi naomba Wizara isimamie rushwa kwa karibu na kuondoa malalamiko ya kiutendaji hasa kwa kutochukua hatua mapema ya kukamata wale wanaoshukiwa na bila kusahau vitendea kazi vya kisasa.

Mheshimiwa Spika, polisi hasa Kitengo cha Upelelezi kimekuwa kililalamikiwa sana, tunaomba TAKUKURU ifaanye uchunguzi wa ofisi na kiutendaji kuhakikisha haki ya watuhumiwa inafanyika.

Mheshimiwa Spika, kuhusu watumishi kupanda madaraja; kwa wafanyakazi imechukua muda mrefu sasa,

wafanyakazi hawajafanyiwa upandishwaji wa madaraja ambao ni haki yao Katiba.

Mheshimiwa Spika, kuhusu ajira, ni muda sasa hakuna ajira kwenye kada muhimu kama afya na elimu, naomba Wizara iweke kipaumbele cha kuajiri kwani ni muhimu sana kwa maeneo hayo ya kimkakati, tunao vijana wengi kwa muda sasa hawana ajira na hii kuweka nchi ya watu wenye mawazo.

Kwa upande wa Vyama vya Wafanyakazi; tunaomba Wizara ifanye kazi kwa pamoja hata kama mishahara na nyongeza havipo, ni vyema kuongea kabla na viongozi hao wawakilishi wao ili kuwaandaa wananchi.

**MHE. ANGELLAH J. KAIRUKI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi hii kuchangia hoja hii ya bajeti ya Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora. Aidha, napenda kueleza haya na kwanza naiunga mkono bajeti hii.

Napenda pia kupongeza uongozi mzima wa Ofisi ya Rais, Utumishi na Utawala Bora kupitia kwa Mheshimiwa Waziri, Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Wakurugenzi na Wakuu wa Taasisi zilizo chini ya ofisi hii.

Mheshimiwa Spika, Serikali imejitahidi kuboresha utoaji wa huduma za umma, hata hivyo bado ni eneo linalohitaji kupewa mkazo ili kuondokana na changamoto ya utoaji wahudumu hafifu kwa umma. Ni vyema Serikali ikaanzisha na kutekeleza dhana ya vituo vya huduma kwa umma (*huduma centres/one stop shops*). Vituo hivi vitasaidia kuongeza uwazi, uhakika wa upatikanaji wa huduma, kuondoa vitendo vya rushwa, kumpunguzia mwananchi mzigo wa kutembelea maeneo mengi/ofisi nyingi ili kupata huduma. Tunaweza kuzitumia Ofisi za majengo ya Posta au maeneo/ /majengo mengine ambayo Serikali itaona inafaa. Huduma mfano za *BRELA, NIDA, NECTA, Uhamiaji, TRA* na taasisi nyingine wanaweza kuwemo katika *huduma center's* hizo.

Mheshimiwa Spika, niendelee kupongeza kazi nzuri inayofanywa na kuwatakiya kila la heri na mafanikio.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Spika, nianze kwa kutoa pongezi kwa hotuba nzuri ya Ofisi ya Rais, Utumishi. Hata hivyo ninaombi moja tu la uhaba mkubwa wa watumishi katika Halmashauri yetu ya Wilaya ya Mbinga. Kwa ujumla Halmashauri ya Wilaya ya Mbinga ina jumla ya uhaba wa watumishi wapatao 2,264 kwa mchanganuo ufuatao; Utawala na Utumishi upungufu ni watumishi 66; Ukaguzi wa Ndani upungufu ni watatu; Sheria uhaba ni mmoja; Mipango na Ufuatiliaji 0; Fedha na Biashara watano; Manunuzi watatu; Ardhi na Maliasili 29; Nyuki saba; Maendeleo ya Jamii 147; TEHAMA watano; Elimu Msingi 748; Elimu Sekondari 420; Afya 530; Ujenzi 12; Maji watano; Mifugo/ Uvuvi 164; Kilimo na Ushirika 115 na Usafi na Mazingira wanne hivyo kufanya jumla ya upungufu kuwa ni 2,264.

Mheshimiwa Spika, hilo ni pengo kubwa sana. Naomba Serikali iangalie namna ya kupunguza pengo hili.

Mheshimiwa Spika, nitaleta maombi maalum ya wataalam hususani katika sekta za afya na elimu.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**MHE. BALOZI ADADI M. RAJAB:** Mheshimiwa Spika, naomba kuchangia hoja hii kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza naunga mkono hoja na kuwapongeza Waziri, Naibu Waziri na viongozi wote wa Wizara.

Mheshimiwa Spika, mimi hoja yangu ni moja tu, pamoja na kazi nzuri ya Wizara na vitengo vyake inavyofanya lakini kuna upungufu mkubwa sana wa wafanyakazi kwenye sekta mbalimbali hususan afya na elimu. Kuna upungufu mkubwa kwenye Jimbo langu la Muheza wa walimu na



madaktari na wauguzi, upungufu huo ni mkubwa na unaathiri ufanisi katika sekta hizo. Upungufu huo ni huu; walimu wa sekondari 64; walimu wa msingi 540; Madaktari 19 na Wauguzi 335. Upungufu huo Wizara ya TAMISEMI inaujua naomba Wizara yako inisaidie sana.

Mheshimiwa Spika, pili, naomba kuchangia kwenye Ofisi ya TAKUKURU kwa kumpongeza Mkurugenzi Mkuu kwa kupandishwa cheo, aidha, naomba wapewa vifaa vya kisasa ili waweze kufanya kazi zao kisayansi na kuweza kupata ushahidi mzuri ambao utakubaliaka mahakamani, aidha, nawombea gari Ofisi ya TAKUKURU Wilaya ya Muheza ambao naona wanafanya kazi bila ya kuwa na gari la uhakika.

Mheshimiwa Spika, vinginevyo nawapongeza sana kuwa kazi nzuri mzifanyazo.

**MHE. ZAINAB M. AMIRI:** Mheshimiwa Spika, awali nimshukuru Mungu kunipa afya njema ili na mimi kuweza kuchangia katika taarifa ya bajeti ya Wizara hii.

Mheshimiwa Spika, maoni, naishauri Serikali iongeze mishahara kwa watumishi ili kuweza kujikimu kimaisha hususan walimu.

Pia naishauri Serikali kwa wale watumishi ambao walienda kusoma na kuongeza ujuzi mara warudipo katika vituo vyao vya kazi, Serikali ione haja ya kuwaongeza mishahara yao ili kuweza kuwapa motisha ya kufanyakazi kwa weledi pia kuwashawishi watumishi wengine kwenda kuongeza ujuzi katika fani zao.

Pia naishauri Serikali kwa wale wastaafu wote katika taasisi mbalimbali waweze kupewa kiinua mgongo kwa wakati ili waweze kukitumia mara tu baada ya kustaafu.

Mheshimiwa Spika, naishauri Serikali kwa wale watumishi wanaostahili kupandishwa madaraja muda wao ukifika wapandishwe na mishahara yao pia iboreshwe kulingana na madaraja yao.

Mwisho, nashauri watumishi ambao ni wateule wa Rais wakiwemo Wakuu wa Mikoa, Wilaya na Wakurugenzi wafanye kazi zao kwa weledi kwa kuzingatia miongozo ya watumishi ya umma na siyo kufanyakazi kisiasa zaidi maana wananchi wanaowaongoza wanatokana na vyama tofauti na siyo Chama Tawala.

**MHE. STEPHEN L. KIRUSWA:** Mheshimiwa Spika, pamoja na kuipongeza Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu, Dkt. John Pombe Joseph Magufuli na Wizara ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kazi nzuri wanazozifanya. Naomba na mimi nichangie hoja iliyoko mezani kwa kutoa maoni na kuishauri Serikali kwa maandishi kama ifuatavyo:-

Kwanza naunga mkono maoni yote ya Kamati na nazidi kulisitiza haja ya Serikali kuhakikisha kuwa watumishi wanapopandishwa madaraja marekebisho ya mishahara yao ifanyike sawia pasipo kuchelewesha.

Mheshimiwa Spika, pili Serikali isitishie utaratibu unaoendelea sehemu mbalimbali nchini ya kuwakaimisha watumishi wa umma kwa muda mrefu jambo ambalo linaathiri ufanisi wao wa kiutendaji na ufanyaji maamuzi. Kwa mfano, katika Wilaya yangu ya Longido tumekuwa na tatizo la muda mrefu sasa la kuwa na Watendaji wengi wa Vijiji, Kata na hata Halmshauri wanaokaimishwa nafasi zao miaka mingi bila kuajiriwa. Baadhi ya *VEOs* na *WEOs* wapo wanaokaimu nafasi hizo kwa zaidi ya miaka mitano sasa. Nashauri Serikali watenge fedha na kutoa vibali vya watumishi wale wenye sifa kuajiriwa au waajiriwe wenye sifa kwa wakati.

Mheshimiwa Spika, tatu, Serikali iwekeze katika kununua na kusambaza kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali zote nchini vifaa vya kupima na vya kudhibiti usambaaaji wa virusi vya homa ya corona ili kuwakinga watoa huduma na wale ambao watalazimika kuwapokea na kuwahudumia watu wanaopatwa na maambukizi ya gonjwa hili na kupelekea kwenye vituo hivyo. Wilaya za mipakani kama Longido naomba zipewe kipaumbele kutokana na

kuweka kwa muingiliano mkubwa wa watu toka nchi jirani zilizoathirika.

Mheshimiwa Spika, nne, kutokana na hali halisi ya kuwa Wabunge wengi wanaendelea kusafiri mikoani ama majimboni na kurudi wakati huu wa Vikao vya Bunge la Bajeti vinavyoendelea na huku tukikabiliwa na tishio la kusambaa kwa virusi vya Corona nchini, nashauri Serikali iimarisha mikakati ya kuwabaini na ikibidi kuwatenga Wabunge wanaokwenda na kurudi toka maeneo yenye maambukizo kama Arusha, Dar es Salaam, Mwanza na Zanzibar.

Aidha, Serikali iweke barakoa za viwango bora na za kutosha kwenye Kliniki ya Bunge na kila Mbunge alazimike kuchukua na kuvaa wakati wote awapo Bungeni na hata nje ya Bunge ili pamoja na hatua zingine zinazochukuliwa kama kunawa mikono na *keeping of social distance*; tuendeele kudhibiti uwezekano wa Corona kuzidi kusambaa. Mungu apishilie mbali *corona virus* isije kutuingilia hapa Bungeni kwa sababu ya sisi kutochukua tahadhari za kutosha.

Mheshimiwa Spika, kwa haya machache, naunga mkono hoja.

**MHE. JUMA OTHMAN HIJA:** Mheshimiwa Spika, napenda kuchukua nafasi hii kukushukuru wewe kwa kunipatia fursa hii ya kuchangia katika hotuba hii.

Pili napenda kumpongeza Mheshimiwa Waziri wa Wizara hii pamoja na wafanyakazi wake wote kwa kutayarisha na kuiwakilisha kwa ufasaha na umakini wa hali ya juu sana.

Mheshimiwa Spika, katika kuchangia hotuba hii napenda kuchangia katika maeneo yafuatayo:-

Kwanza ni kuhusu Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Taasisi hii ni muhimu sana katika nchi kama yetu ambayo imepania kuleta maendeleo kwa wananchi wake. Taasisi hii imekuwa ikifanya kazi katika

maeneo mengi katika nchi hii bila ya woga. Huu ni ujasiri mkubwa ambao unafanywa na wafanyakazi wa taasisi hii.

Ushauri wangu katika taasisi hii ni kwamba ipanue zaidi maeneo ya ufanyaji kazi. Mfano , Waheshimiwa Wabunge tumekuwa tukilalamikia sana utendaji wa Halmashauri zetu juu ya matumizi ya Mifuko ya Wabunge ya Kuchochea Maendeleo. Baadhi ya Halmashauri zetu zimekuwa zikitumia vibaya mifuko hiyo. Hivyo naomba taasisi hii iangalie jambo hili kwa madhumuni ya kuzuia matumizi mabaya ya mifuko hii.

Mheshimiwa Spika, naunga mkono hoja.

**MHE. ZACHARIA P. ISSAAY:** Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kuungana na Waheshimiwa viongozi wa Taifa letu, Watanzania wote kumshukuru sana Mwenyezi Mungu kwa majaliwa yake kwetu sote. Nasema ameipenda sana nchi yetu.

Hata hivyo tuendeleo kumwomba sana Mwenyezi Mungu atuepushie janga hili la Corona katika nchi yetu na dunia nzima kwa ujumla. Hata hivyo naipongeza sana Serikali kwa jinsi inavyokabiliana na maambukizi ya ugonjwa wa Corona hapa nchini kwa kweli tusijadili janga la Corona kama suala la kisiasa. Mimi nasema Corona ni ugonjwa hatari sana. Hivyo basi sote tunakiri na kuwekeza wananchi wetu ugonjwa huo ni hatari sana tuungane kupambana nayo kwa kupokea maelekezo, maagizo ya Serikali.

Mheshimiwa Spika, hivyo basi nachukua nafasi hii kuviomba vyombo vya habari kama vile televishen, redio mbalimbali za jamii kutumia nafasi zao kuhabarisha umma kupitia vipindi vyao.

Mheshimiwa Spika, nachukua nafasi hii kumpongeza sana Mheshimiwa John Pombe Magufuli, Rais wetu mpendwa, Mheshimiwa Makamu wa Rais, Mheshimiwa Waziri Mkuu, uongozi wa Bunge letu na waandamizi wengine wote

Serikalini kwa jinsi walivyoiongoza nchi yetu mpaka leo, hakika nchi imepiga hatua kubwa sana kimaendeleo.

Mheshimiwa Spika, kwanza niipongeze sana Serikali yetu kwa jinsi ilivyotekeleza Ilani ya CCM ya mwaka 2015 - 2020, mfano halisi huko Jimbo la Mbulu Mjini nasema hongera sana Mheshimiwa Rais wetu.

Mheshimiwa Spika, sasa naomba kuishauri Serikali yetu ifanye mapitio ya nafasi zote za ajira kutoka mwaka 2016 hadi 2020 na kutoa taarifa hizo kupitia mifumo yake kuhabarisha umma. Kwa kuwa Serikali yetu imeajiri nafasi nyingi kwenye sekta zake, taasisi na mashirika ya umma ili kufuta upotoshaji wa wapinzani kwa vijana wetu kote nchini.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia *TASAF* Awamu ya Tatu ifanye mapitio ya mapungufu, changamoto, mafanikio ili kupata mkakati wenye tija, kuepuka orodha ya walengwa hewa, kuepuka wasiostahili kuingizwa kwenye orodha, kwa kuwa *TASAF* ya awamu hii ilikuwa mapungufu.

Mheshimiwa Spika, kwa upande wa TAKUKURU naomba kuishauri Serikali ipunguze muda wa upelelezi wa mashaka mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, mwisho, naomba kuwasilisha na naunga mkono 100%.

**MHE. DKT. SUSAN A. KOLIMBA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuchangia kwa maandishi. Awali ya yote naomba kumpongeza Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kuiongoza nchi yetu na kuwa mfano bora katika kuonesha njia na kuongoza katika misingi ya utawala bora ambapo amekuwa mfano wa kuigwa ndani na nje ya nchi yetu.

Pili, naipongeze Wizara ya Ofisi ya Rais, Utawala Bora chini ya Waziri Mheshimiwa George Mkuchika na Naibu Waziri, Katibu Mkuu, Naibu Katibu na watendaji wote kwa kufanya

kazi kwa weledi mkubwa na kufanikisha usimamizi, utekelezaji wa Ilani ya CCM iwe na mafanikio.

Tatu, natumia nafasi hii ya pekee kukupongeza wewe binafsi kwa maono mazuri ya kuona umuhimu kwa kulifanya Bunge lako liendeshe kwa mtandao maamuzi ambayo matunda yake tunayaoona sasa katika kipindi hiki chenye changamoto kubwa ya Taifa na dunia ya ugonjwa wa *Covid 19*, kwa sehemu kubwa imetoa ufumbuzi na mfano wa kuigwa. Hongera wewe Mheshimiwa Spika na timu nzima ya Naibu Spika, Katibu na watendaji wake.

Mheshimiwa Spika, ombi na ushauri; pamoja na kazi nzuri iliyofanywa na Wizara hii kwa heshima kubwa naomba maombi yafuatayo yafanyiwe kazi:-

Kwanza, ombi la kupewa watumishi wa kada ya afya, elimu ya msingi na sekondari hasa katika Wilaya ya Ludewa ambayo mazingira yake kijiografia ni magumu . Mfano katika ikama ya mwaka 2019/2020 Wilaya ya Ludewa ilitarajiwa kuwa na walimu wa shule za msingi 844 lakini mpaka sasa kuna jumla walimu 627 na kufanya upungufu wa walimu 217; katika Idara ya Elimu Sekondari walimu 530 na waliopo ni walimu 460 na kufanya upungufu wa walimu 70. Wakati Idara ya Afya watumishi wanaohitajika ni 590 na waliopo ni 473 na kufanya upungufu wa watumishi 117.

Ombi langu naiomba Wizara iweze kufanyia kazi upungufu huu ili kusaidia huduma husika iwafikie Watanzania hawa wanaoishi katika mazingira magumu sana kijiografia.

Mheshimiwa Spika, la mwisho naiomba Wizara iweze kuziba nafasi ya watumishi waliostaafu au kuhamia katika maeneo mengine kuendeleza utumishi wa umma hasa katika Wilaya hii yenye mazingira magumu na uhitaji mkubwa wa watumishi.

Mheshimiwa Spika, naomba kuunga mkono hoja hii ya Ofisi Rais, Utumishi na Utawala Bora.

**MHE. AMINA S. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, napenda nichangie kuhusu mambo mawili; kwanza ujumuishaji wa watu wenye ulemavu kwenye ajira na pili, mwongozo wa huduma kwa watumishi wenye ulemavu.

Awali ya yote, naomba itambulike kuwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu ya mwaka 2010 kifungu cha 31(2) inamtaka kila mwajiri mwenye wafanyakazi kuanzia 20; asilimia tatu wawe ni watu wenye ulemavu. Tangu sheria hii itungwe hakuna taasisi ya umma ambayo imeshafikia asilimia hii, hii ni kutokana na kutokuwepo na mkakati wa makusudi wa kutimiza takwa hili la kisheria.

Mheshimiwa Spika, tunaomba Wizara ije na mkakati wa kuhakikisha kwa kuanzia taasisi na mamlaka mbalimbali za umma zinatekeleza hili. Mbali na mkakati Wizara itusaidie kuwasilisha takwimu ya watu wenye ulemavu ni wangapi ambao wameajiriwa katika utumishi wa umma na asilimia ngapi kwa kila taasisi. Hii itasaidia kila taasisi kujitathmini inawajibika kiasi gani kuhakikisha watu wenye ulemavu wanajumuishwa kwenye utumishi wa umma.

Mheshimiwa Spika, pia tunaomba Wizara itoe agizo kwa taasisi zote zinazotangaza ajira zinaweka *caption* ya kuhimiza watu wenye ulemavu kuomba, kwa kufanya hivyo itawaamsha taasisi zinazoajiri kujiandaa kuwapokea watu wenye ulemavu katika mchakato mzima wa ajira kuanzia maombi, usaili pamoja na vituo vya kazi. Maana ipo mifano viziwi ambao walilalamikia kufika kwenye usaili lakini mahitaji yao ya ukalimani hayakuzingatiwa.

Mheshimiwa Spika, suala la pili ni menejimenti ya utumishi wa umma iliandaa Mwongozo wa Huduma kwa Watumishi wa Umma Wenye Ulemavu wa 2008.

Hadi sasa mwongozo huu una zaidi ya miaka kumi na uliangaliwa kabla ya kutungwa kwa Sheria ya Watu Wenye Ulemavu, hivyo unahitaji kuhuishwa (kufanyiwa marekebisho) ili uweze kukidhi haki na mahitaji yote ya watu wenye ulemavu, hasa yale ambayo hayakujumuishwa kwa wakati

huu husasani ushirikishaji wa watu wenye ulemavu katika kuamua namna na njia muafaka za kumuhudumia; kupanua wigo wa matumizi ya lugha ya alama na ukalimani na huduma kwa watumishi wenye watu wenye ulemavu kipindi/nyakati za dharura ambapo kipengele hiki hakikuguswa kabisa katika mwongozo.

Mheshimiwa Spika, hivyo tunaomba Waziri aueleze umma wa Watanzania wenye ulemavu, ni lini mwongozo huu utahuishwa!

Mheshimiwa Spika, mwisho, vilevile kutokana umuhimu watu wenye ulemavu, taasisi binafsi kuhitaji mwongozo kama huu, tunaomba Waziri aangalie namna ya kuweka kipengele katika mwongozo kikielekeza kuwa mwongozo huu unaweza kutumika kuwahudumia watu wenye ulemavu katika taasisi binafsi.

**SPIKA:** Sasa nimwite Mheshimiwa Waziri ambaye ni mtoa hoja ili aweze kupitia hoja mbalimbali za Waheshimiwa Wabunge mliochangia kwa maandishi, kwa kusema na baada ya hapo, ahitimishe hoja yake na tutafuatiwa na ile *session* ya maswali maalum ya kisera kama yapo. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kepteni Mstaafu George Mkuchika. Karibu sana.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza nichukue nafasi hii kuwashukuru Wabunge wenzangu wote waliochangia. Najua tumepata tatizo tu la muda lakini mchango wenu wote mliochangia humu ndani ni mchango uliokuwa makini sana. Sisi tunapenda kukosolewa. Mwalimu alisema, kujisahihisha. Unapojisahihisha, unajijimarisha. Kwa hiyo, nasi tumewasikiliza Waheeshimwia Wabunge kwa makini, tuko tayari pale ambapo hatukufanya vizuri kujirekebisha ili tufanye vizuri zaidi.

Mheshimiwa Spika, la pili nataka niseme kwa sababu hoja zimekuwa nyingi na muda umekuwa mfupi. Nitagusia tu maeneo machache na yale ambayo sitagusia



yatakuwemo kwenye majibu; na kila mtu aliyetoa hoja yake itajibiwa na Serikali.

Mheshimiwa Spika, suala moja ambalo nataka kulisema ambapo hata kwenye Kamati tulishauriwa ni kwamba katika nchi yetu hii hakuna mtu anayepata shida kupata malipo yake kama mstaafu. Kwamba, anafanya kazi, anathaminiwa, analipwa kila mwezi lakini akishastaafu, wako watu wanakaa miaka miwili, mitatu na wengine hata wanafariki kabla hawajalipwa mafao yao. Nimeshauriwa na Kamati nichukue hatua.

Mheshimiwa Spika, nataka niahidi mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba Wizara yangu itaandaa Mkutano Maalum wa Watumishi wanaoitwa Maafisa Utumishi wa Serikali nchi nzima na nilishatoa waraka huko nyuma kwamba masuala ya kufuatilia mafao ya mstaafu, mfuatiliaji siyo mstaafu. Kazi ile inatakiwa ifanywe na Afisa Utumishi pale alipokuwa anafanya kazi ili mtu asistaafu Bukoba akaambiwa nenda Dodoma; alistaafu Lindi, Mtwara au Ruvuma, nenda Dodoma.

Mheshimiwa Spika, katika mkutano huo nitakaoitisha, pale nitakapokuwa napata malalamiko kwamba mstaafu hajapata, mimi nitashughulika na Afisa Utumishi aeleze kwa nini hakuandaa mapema Taarifa za Utumishi? Kinachochelewesha watu wengi ni kukosekana tu taarifa muhimu, hilo tu. Ila kama Wizara, nilitoa mfano mwingine hapa; kwa mfano, majeshi yetu, kama huko ndani ya majeshi kuko shwari, mambo kama haya hayapo, kwa nini uraiani tusiige majeshi ili na watu wetu walipwe mapema?

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, hili naliahidi hili Bunge. Siyo kama nitafanya wakati huo, maana sina uhakika baada ya 2000 na ngapi? Hiki kipande cha miezi iliyofika, nitakutana nao, tutafanya marekebisho hayo ili kazi ya kufuatilia mafao ya watumishi ifanywe na Maafisa Utumishi na yule ambaye hatatekeleza wajibu wake, wanisikie huko waliko, nitaagana nao vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, jambo lingine lililozungumzwa hapa ni maombi kwamba *TASAF* ifike maeneo yote. Nadhani nimeeleza kwenye hotuba yangu na siku ya uzinduzi tumeleza pale *Mwalimu Nyerere International Convention Centre* kwamba *TASAF* awamu iliyopika tulifika asilimia 30. Sasa hivi tunafika asilimia 100 kwa maana ya Wilaya zote, Vijiji vyote na Shehia zote kama nilivyosema Tanzania Bara, Unguja na Pemba. Kwa hiyo, msiwe na wasiwasi, tutafika maeneo yote. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, suala la kujenga *Tanzania Public Service College* Singida, nadhani nilieleza kwamba tumejipanga kujenga Singida, ndiyo maana tumetafuta kiwanja. Kwa hiyo, niwatoe hofu ndugu zangu wa Singida, sijui nilikuta tu kule imeenea kwamba tunahama Singida kuja Dodoma; Dodoma hapa kuna kila kitu. Imekuwepo Ofisi ya Uratibu na kadhalika, lakini kwa maana ya *campus* ya Singida itaendelea kuwepo Singida. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limeelezwa kwenye Kamati na humu ndani Wajumbe mmieleza ni suala la Watumishi wa Umma kwenda kusoma katika Vyuo vya Utumishi wa Umma. Mheshimiwa Waziri Kivuli pale Mheshimiwa Mollel anafahamu kwamba zamani huanzi kazi Serikalini mpaka umepata *induction course*. Unafundishwa kujua jinsi Serikali inavyofanya kazi.

Mheshimiwa Spika, sasa Chuo cha Utumishi wa Umma, kazi yake ni hii. Kinachotokea sasa ni kwamba tunaajiri, lakini watu hawaendi kusoma Chuo cha Utumishi wa Umma. Tumeshauriwa na Kamati na kwa bahati nzuri tulishazungumza ndani ya Wizara, tutaweka utaratibu, Wizara itatoa waraka ambao sasa wewe uliyepata watumishi wapya hutakuwa na uhiari (*option*) wa kuwapeleka watumishi wako wapya kusoma au kutokwenda kusoma Chuo cha Utumishi wa Umma.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine, ndugu yangu Mheshimiwa Bobali pale, wastaafu walipwe mapema, nadhani nimelielezea.

Mheshimiwa Spika, sikuambiwa ni dakika ngapi, nami naogopa kutokuwa na nidhamu...

**SPIKA:** Muda usiozidi nusu saa. Kwa hiyo, bado una dakika kama 20 hivi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, sawa.

Mheshimiwa Spika, suala la Chuo cha Utumishi wa Umma Singida, tumeshalisema.

Mheshimiwa Spika, namshukuru Mheshimiwa Mwanne Mchemba alisema baadhi wa watumishi wa Umma kutokuwa waadilifu kwa mfano Tabora. Nataka nichukue nafasi hii, kipindi hiki tunapoelekea kwenye uchaguzi; maelekezo yameshatolewa kwa watumishi wa TAKUKURU kwamba Mbunge aliyepo madarakani kama mlivyo wote nyie ni ruhusa kutoa misaada mbalimbali katika Jimbo lake. Nataka nirudie, ni ruhusa kushiriki harambee, anachangia mabati ya Shule, mabati ya Kanisa, mabati ya Msikiti, Zahanati, huyu ndiye Mbunge aliyepo madarakani. Kwa hiyo, humwulizi kwa nini unatoa msaada? Ni kwa sababu mimi ni Mbunge niliyepo madarakani.

Mheshimiwa Spika, ila yule anayefanya mazoezi kwenda kuchukua Jimbo, marufuku kuzunguka na kuanza kutoa zawadi kwa sababu hapo tunakukamata kwa rushwa. Tena Chama ninachotoka mimi kinaitwa CCM, inapofika wakati wa uchaguzi, inatoa ratiba tarehe fulani kuchukua fomu, tarehe fulani hivi, wewe unazunguka leo unagawa shilingi mbili mbili, shilingi elfu tatu tatu kabla ya wakati, tutakushughulikia, tutakushitaki kwa kutoa rushwa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa yaliyotokea Tabora, nataka nimpungeze Mkurugenzi Mkuu wangu. Nasi ni wastaarabu, ma-*gentlemen*. Kilichotokea ni kwamba mtu aliyetakiwa afuatiliwe siye. Kwa hiyo, mtu mmoja akaenda kuwafuatilia Viti Maalum waliopo madarakani Tabora. Kwa nini

umewagawia *UWT* cherehani? Tena wametoa siyo kwa mtu mmoja mmoja; wametoa *UWT* Wilaya nzima, siyo mtu mmoja mmoja. Sasa makosa yale yalifanyika, wale wanaohusika tumewachukulia hatua, wamekemewa.

Mheshimiwa Spika, kikubwa kabisa, nataka nimpongeze Mkurugenzi Mkuu wangu, aliwapigia simu Wabunge wa Viti Maalum Tabora kuwaomba radhi kwa tukio la kwenda kumfuata mtu ambaye hakukusudiwa. *That is good governance*, ndiyo utawala bora huo. Ndiyo maana tuko hapa. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, sasa habari ya watumishi kukaimu tumeisikia, lakini nataka nitoe ufafanuzi juu ya watumishi kukaimu. Jamani, taratibu zinasema hivi, kama unamtaka huyo ateuliwe kuwa Mkuu wa Idara, iwe Halmashauri, iwe Wizara au wapi, mkaimishe mtu ambaye akipanda cheo ana-*qualify* hapo anapokaimu.

Mheshimiwa Spika, tatizo lililopo unaenda mahali unamkuta Mkuu wa Ofisi amempenda mtu fulani katika ofisi yake ama kwa utendaji, sasa anamkaimisha bila kujali yule mtu ni *junior* kiasi gani? Hilo la kwanza. La pili, ili umkaimishe mtu kwenye Halmashauri, Ofisi mbalimbali, unaomba kibali kwetu sisi Utumishi. Sasa unakuta mtu amekaimu miaka minne, hana kibali cha Utumishi, hajaombewa kibali, lakini unamkuta yule mtu yuko *very junior*, yaani yuko mbali mno na pale anapokaimu.

Mheshimiwa Spika, kazi yetu ni kuhakikisha kwamba tunatenda haki. Ukituletea yule mtu wa cheo cha chini sana, tunaanza kuuliza: Je, hawa wote waliopo juu yake hawafai? Sisi kwenye utawala bora tunayazingatia hayo ili isionekane kama kuna kubebana.

Mheshimiwa Spika, jambo lingine ambalo limezungumzwa hapa; tunapokea pongezi zote ambazo zimetolewa kwa Mheshimiwa Rais, kwa sisi watumishi tunaomsaidia katika Wizara, tunashukuru kwa pongezi

mlizotupa, mmetutia moyo tutaendelea kuchapa kazi.  
(Makofi)

Mheshimiwa Spika, suala la ulipaji wa madeni kwa watumishi, sema muda tu, ila takwimu zipo. Tumewalipa watumishi madeni waliyokuwa wanatudai na matarajio. Hata Mheshimiwa Rais alisema, acheni kuhamisha watu mpaka tutakapomaliza kuwalipa madeni wale watumishi ambao wanatudai. Hilo zoezi linafanyika.

Mheshimiwa Spika, tumepokea ushauri kwamba tuimarisha vyombo vya ulinzi na usalama ili viweze kufanya kazi nzuri zaidi na sisi tunaamini kwamba hayo ndiyo malengo yetu.

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mheshimiwa Godbless Lema, namshukuru. Ndiyo uzuri wa Bunge hili bwana! Ukifanya mambo mazuri unapongezwa bila kujali huyu yupo upande gani. Ndugu yangu Mheshimiwa Lema tena ametoka, ila namshukuru, amenipongeza kwamba nimekuwa nakemea watu wanaotumia madaraka vibaya. Nitaendelea kufanya hivyo.

Mheshimiwa Spika, nataka nikwambie, wako wengine hawasikii. Wale wachache ambao hawakusikia tumewachukulia hatua kwa mujibu wa taratibu za kazi, siyo lazima kila kitu kitangazwe. Wengine wamekemewa na wengine wameondolewa kimya kimya.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, nataka kusema tu kwamba nawashukuru kwamba Waheshimiwa Wabunge hili jambo wameliona kwamba tunajitahidi kukemea, lakini niseme kwamba nilitumia maneno ya Kiswahili siku ile kwamba "maji yametulia katika mtungi." Hali ilivyo sasa ya kamatakamata siyo kama ilivyokuwa huko zamani.

Mheshimiwa Spika, suala la Elimu Mtandao Mheshimiwa Bulembo tumesikia. Nitalifikisha kwa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Serikali Mtandao.

Mheshimiwa Spika, kuhusu TAKUKURU kupewa usafiri, tumelisikia. Nataka niseme kwamba mwaka 2019 tulimwomba Mheshimiwa Rais atupe ruhusa tufungue Ofisi za TAKUKURU Wilaya 21 mpya ambazo hazikuwa na Ofisi.

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Rais alitukubalia mwaka 2019, tumefungua ofisi katika Wilaya zote, tumetoa magari mapya wilaya zote. Tatizo tulilionalo sasa la usafiri wa TAKUKURU siyo wilaya hizi mpya, maana wana magari mapya, tatizo ni zile ofisi za zamani; nyingine zina magari madogo madogo hata kwenye matope haziwezi kutembea, nyingine zimechakaa lakini tuna matarajio kwamba mtatuwezesha. Mkituwezesha tutatekeleza.

Mheshimiwa Spika, kwamba TAKUKURU wapeleke na kushtaki bila kibali cha *DPP*; naomba hili niwaachie wenzangu watu wa sheria. Nataka nikwambieni, kwa dunia nzima, hili jambo lina ubishi mkubwa sana. Watu wa nchi za *Commonwealth* kuna kitu wanaita *check and balance*. Kwa mfano, *argument* inayotolewa hapa kwetu, *check and balance* kwamba TAKUKURU wasikamate na kupepeleza na kupeleka Mahakamani. Lazima apatikane mtu anayesema peleka au usipeleke.

Mheshimiwa Spika, Polisi wanakamata, wanapeleleza, na wanapeleka Mahakamani. Vile vile *check and balance* ni kwamba wewe unayeshtaki usitoe hukumu. TAKUKURU wakishitaki, anayetoa hukumu *you are guilty of an offense* au hapana, siyo TAKUKURU, yuko mtu anayekaa pale kusikiliza.

Mheshimiwa Spika, sasa kama alivyosema Mwenyekiti, mjadala huu nafikiri hata mpaka Bunge la Katiba ulikuwa mgumu sana. Kwa hiyo, naomba niachie hapo, wataalam waliobobea katika hili wanapatikana Wizara ya Sheria, nitawaomba, siku yao ni kesho kutwa. Basi wao pengine tukiwaomba wanaweza wakatufafanulia zaidi.

Mheshimiwa Spika, nimwambie ndugu yangu Mheshimiwa Mch. Msigwa, ametoka. Aah, yupo. Magereza

hakuna utawala bora. Sasa nataka niseme hivi, dhana ya Utawala Bora kama mlivyosema, nchi hii vinavyoshughulika na Utawala Bora siyo vyote vipo kwangu. CAG, ni Utawala vyombo Bora, Polisi ni Utawala Bora, TISS ni Utawala Bora, Mamlaka ya Manunuzi ni Utawala Bora, Bunge ni Utawala Bora. Hili neno Utawala Bora linakumbatia mambo mengi. kila jambo linalofanywa ili nchi yetu itawaliwe kwa mujibu wa sheria, taratibu na kanuni ni Utawala Bora.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, katika shughuli zangu za mgawanyo wa kazi siingii Magerezani. Huko ni Wizara nyingine, ni chombo kingine lakini basi ndugu yangu Mheshimiwa Mch. Msigwa ameeleza mambo aliyoyaona huko. Basi, unajua Waingereza bwana lugha yao wanaipenda kweli. Mtu aliyewahi kufungwa Waingereza wanamwita *Prison Graduate*, yaani amehitimu.

Mheshimiwa Spika, sasa Mheshimiwa Mchungaji Msigwa ukionana naye anakwambia siyo *Prison Graduate* wa siku mbili. Ndiyo maana hapa ameeleza siku zimekuwa nyingi kuliko watu wanavyodhani. (*Makofi/Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, ndugu yangu Mnzava nakushukuru sana. Wewe ni Mwanasheria, nimekusikia ulivyochambua, umeeleza vizuri, mambo ya TASAF yanajirudia, Tume ya Maadili.

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nataka niwe na nidhamu, nisizidishe muda ulionipa. Kwa hiyo, baada ya ufafanuzi huo, naomba kutoa hoja. (*Makofi*)

**WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**SPIKA:** Hoja imetolewa na imeungwa mkono. Tunakushukuru sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Kepteni Mstaafu George Huruma Mkuchika. Hoja nyingine amejibu, hoja nyingine hakujibu. Hoja ya Mheshimiwa Bulembo haikujibiwa hapa, lakini bado tunao muda wa ufafanuzi.

Sasa tunaanza na yale masuala ya sera. Basi tuliona Waziri Kivuli yeye abaki hapa hapa, lakini wachangiaji wengine wote wa masuala ya sera watakuwa wako Msekwa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ataanza Mheshimiwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Ruth Mollel na afuata Mheshimiwa Ally Keissy endapo yuko kule Msekwa na atafuata Mheshimiwa Mwanne Ismail Mchemba endapo yupo huko.

Kwa hiyo, tuanze na Mheshimiwa Ruth Mollel. Uulizaji dakika zisizozidi tatu, masuala ni ya kisera ya ufafanuzi na jambo ni moja tu.

#### HOJA ZA KISERA

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante, ningependa Mheshimiwa Waziri anipe *sense of comfort* hasa linapokuja swali hili la elimu na kupata mafunzo viongozi wa kisiasa kwa sababu kwa kweli hili jambo binafsi ninaona ni changamoto kubwa na haileti taswira nzuri kwa Serikali. Na najua kunai le *Leadership College* pale Oysterbay ambayo inaweza ikatumiwa kutoa mafunzo kwa ajili ya viongozi hawa wa kisiasa baadhi ambao wanatuaibisha Serikali. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Waziri utakuwa na mkakati gani kuhakikisha kwamba kwa kweli mwaka ujao ama baada ya *elections* wale watakaopata bahati ya kuteuliwa wawe *immediately* wanakwenda kwenye mafunzo. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri!

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika,



nakushukuru Mheshimiwa Mollel kwa ushauri wako mzuri. Moja, unazungumza elimu na mafunzo ya viongozi wa vyama vya kisiasa hapa unakusudia vyama vyote, mimi nataka niseme kwamba chuo chetu kile pale cha *Uongozi Institute* kipo wazi kwa kila mtu. Kwa hiyo, wale viongozi mnaotaka kuleta watu wenu kuja kusoma mnakaribishwa na pia nataka nitoe ushauri kwamba bahati nzuri wenzetu vyama vya siasa vyote vilivyoandikishwa nchi hii wana baraza lao, kuna mahali pao wanapokutana kushauriana; naomba ajenda hii iwe moja wapo ya kupeleka watu kwenda kusoma. (*Makofi*)

Mheshimiwa Spika, b) yake amezungumzia kwamba je, tunatoa ahadi gani kwa viongozi watakaoteuliwa kuhakikisha kwamba wanapewa mafunzo. Ushauri nimeupokea, nia yako wewe ni kwamba yale mafunzo yasichelewe, wakishateuliwa wapate mafunzo mara moja, ushauri umepokelewa. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana, Waziri Kivuli kama hukuridhika wewe tu nakupa nyongeza.

**MHE. RUTH H. MOLLEL:** Mheshimiwa Spika, ahsante, nimemuelewa Waziri mwenzangu, nafikiri mwezi wa 11 nitakuwa nimekaa hapo. (*Kicheko*)

Mheshimiwa Spika, lakini swali langu nimekubali ushauri wako wa viongozi wa kisiasa kwa ujumla lakini nazungumzia viongozi wa kisiasa ambao wanateuliwa na Mheshimiwa Rais kama ma-*RC, DC* na Mawaziri *in particular*. Kwa hiyo, nilitaka tu nisisitize hapo, ahsante. (*Makofi*)

**SPIKA:** Katika kujibu Mheshimiwa Waziri unaweza pia ukasaidiwa na Naibu Waziri wako kadri mtakavyoona inafaa, Mheshimiwa Naibu Waziri umesimama.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru ingawa naona ulinisahau kidogo katika kuchangia lakini maadam Mheshimiwa Waziri wangu amesimama yote ni heri.

Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu yake mazuri ya Mheshimiwa Waziri wangu aliyomjibu Waziri Kivuli naomba niongezee kidogo hapo katika *query* ya Mheshimiwa Waziri Kivuli wa ofisi hii ni kwamba Taasisi yetu ya *Uongozi Institute* tumejipanga kisawasawa. Na tunapozungumzia masuala ya utawala bora, Serikali ya Awamu ya Tano ipo makini, ina uadilifu na ni ya uchapaji kazi.

Mheshimiwa Spika na Waheshimiwa Wabunge, hii taasisi yetu ya *Uongozi Institute* ni kwamba tumeweka mkakati maalum, sio kusubiri mpaka ma-RAS, ma-DC, Wakuu wa Mikoa ama Wakurugenzi waje, sisi mkakati wetu ni kwamba tutawafuata wao kwenye maeneo yao iwe ni Kimikoa ama Kikanda kuhakikisha kwamba kwasababu semina elekezi hazipo na *technology* huwa zinabadilika kwa hiyo, tutakuwa tunawafuata kule kwenye maeneo yao ya kazi kuwafanyia semina kwa sababu pia hilo linapunguza hata gharama ya kuwaita wote kuja Dodoma au Dar es salaam, huo ni kakati mmojawapo wa kuhakikisha hili tunalitekeleza.

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy, endapo yupo Msekwa.

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana. Kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Waziri Mheshimiwa Mkuchika kwa hii hasa *TASAF* imesaidia sana kusema ukweli na hivi itakuwa sasa ni asilimia 100.

Mheshimiwa Spika, nakumbuka kwamba mimi nilitoa wazo kwamba kuna hali mbaya sana kwenye timu yetu ya wananchi Yanga mpaka juzi mgogoro ndio maana sasa Yanga inashindwa hata kuchukua ubingwa kwa sababu hiyo hali ni mbaya kiuchumi.

Mheshimiwa Spika, namshauri Waziri kwamba akali-*share* waingize nayo katika Mfuko wa *TASAF* lakini naona kwenye randama hamna. Sasa sijui Waziri anafikiriaje sisi timu ya wananchi.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri, swali muhimu sana hili Yanga kuingizwa katika *TASAF* kuna mpango gani Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba nimjibu ndugu yangu Mheshimiwa Keissy hoja yake kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, *TASAF* ipo tofauti kidogo na Wanachama wa Yanga. *TASAF* wanasaidiwa na mfuko maalum, Wanachama wa Yanga wanajisaidia wenyewe. Kwa hiyo, mpaka mnyama anapigwa, michango ya wanachama wenyewe. *(Makofi/Vigelegele)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Ally Keissy kule Msekwa una swali la nyongeza?

**MHE. ALLY K. MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, yeye asizungumzie habari ya Simba kupigwa, hali ya mwenendo wa Yanga kwa sababu kweli ni mbaya mpaka juzi wamesikia mgogoro na mfadhili wenyewe wanasikia. Kulipa mishahara imekuwa tatizo, sasa hapa anasema michango ya Yanga, michango ya Yanga Mheshimiwa Waziri haikidhi kabisa mishahara ya wachezaji wetu. Waingize Mheshimiwa Waziri, hali ni mbaya.

Mheshimiwa Spika, na mfadhili mwenyewe nasikia juzi tu ametoa masharti magumu magumu wewe mwenyewe unafahamu, hali ni mbaya; mwenendo wa wachezaji hali ni mbaya na mishahara yenyewe wanalalamika hata usajili wenyewe ulikuwa sio mzuri, Mheshimiwa Waziri unafahamu hicho kitu. Kwa hiyo, nakuomba kama nilivyoomba mara ya kwanza usiseme wanachama wanachangia, wanachama wapo dhoofu bin hali. *(Makofi/Kicheko)*

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri Wabunge wamekuwa wakipiga kura hapa wanaounga mkono hoja hii ni wengi kwamba Yanga waingizwe *TASAF*, tunaomba majibu yako Mheshimiwa Waziri. *(Kicheko)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nimtoe hofu ndugu yangu Mheshimiwa Keissy, unajua kwenye mambo ya ushindani ya timu huchukui mchele ukamwaga mbele ya kuku, sasa wanaosikiliza hapa ni wanachama na wasiokuwa wanachama. Kwa hiyo, mambo ya undani ya klabu hatuyasemi lakini kikubwa ni kwamba hakuna mchezaji aliyekimbia na tulipoona yule Morrison watu fulani wanataka kumviziavizia tukamsajili saa hiyohiyo, walipotaka kumfuatilia Tshishimbi tukamsajili saa hiyohoyo. Sasa subirini dirisha dogo maana mchezaji ukimuona anasajiliwa dirisha dogo, anatisha kama tulivyomsajili Morrison, dirisha dogo lile. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, lakini labda niseme tukiondoa haya ya utani wetu wa Simba na Yanga nataka niwatoe mashaka wanachama wa Yanga, mwezi Mei, mwezi ujao tutafanya mkutano mkuu wa kufanya mabadiliko makubwa ya Katiba ya Yanga tuuze hisa kwa watu wamiliki Klabu ya Yanga lakini hatutafanya makosa waliyofanya watu fulani kumrundikia mtu mmoja hisa zoote! Kwa hiyo, pamoja na kwamba wale wameenda kwenye kampuni lakini mmiliki wa klabu ile sasa hivi ni huyu mmoja, wale jamaa wale tuliowafunga juzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, nakushukuru. *(Makofi)*

**SPIKA:** Kwa kweli Mheshimiwa Mkuchika lazima tukupongeze maana juzi ulipotufunga bwana, daah! Aaha! Ulituweza hatuna la kusema lakini tunajipanga. Mheshimiwa Mwanne Mchemba atafuatiwa na Mheshimiwa Venance Mwamoto, Msekwa.

**MHE. MWANNE I. MCHEMBA:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi nipate ufafanuzi wa kina.

Mheshimiwa Spika, awali ya yote nimshukuru sana Mheshimiwa Waziri amejibu hoja zangu zote, nampongeza na namshukuru sana kwa kweli hoja yangu imejifuta yenyewe. Lakini pia nimshukuru sana Mkurugenzi wa TAKUKURU kwa

utekelezaji alioufanya, kwa kweli ametekeleza yale ambayo na mimi nilikuwa nimepeleka malalamiko. Kwa hiyo, naomba sana nimshukuru Mheshimiwa Waziri, ahsante kwa majibu yake mazuri.

**SPIKA:** Ahsante sana kwa kuwa hoja zako zote zimejibiwa, tunaendelea kumshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu mazuri. Sasa Mheshimiwa Venance Methusela Mwamoto na atafuatiwa na Mheshimiwa Goodluck Asaph Mlinga.

**MHE. VENANCE M. MWAMOTO:** Mheshimiwa Spika, ahsante kwa kunipa nafasi hii. Hoja yangu nilikuwa nataka Mheshimiwa Waziri anifafanulie hapa jambo na kama sitaridhika nitakamata shilingi yake.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba haya mambo yote ambayo tunayafanya sasa hivi ya kupitia bajeti, tunategemea sana bajeti ziende vizuri na fedha zile ziwafikie wananchi na zisiliwe. Lakini tunategemea sana wenzetu wa TAKUKURU katika hayo mambo. Pamoja na kujibu Mheshimiwa Waziri kwamba baadhi ya ofisi wamepewa magari na ofisi zimejengwa, kuna baadhi ya wilaya zile za zamani majengo ni mabovu, wafanyakazi wanakaa kwenye hali mbaya na ukichukulia Kilolo wenyewe wanakaa kwenye godauni kabisa.

Mheshimiwa Spika, sasa nilitaka nipate ufafanuzi kwa Mheshimiwa Waziri aniambie hapa ni lini hizi Wilaya ambazo hazina ofisi kabisa kama Kilolo ambao wanakaa kwenye godauni lini zitajengwa.

**SPIKA:** Ufafanuzi wa swali hilo muhimu Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, naomba kumjibu ndugu yangu Mheshimiwa Mwamoto, Mbunge wa Kilolo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nimefika Kilolo, nikienda Wilayani huwa nakagua ofisi zangu zinazonihusu, kweli ofisi ile hairidhishi na tukizingatia kwamba Kilolo ni Wilaya mpya. Kwa hiyo, naomba tu nimuahidi ndugu yangu na Mkurugenzi Mkuu anakusikia, mwaka huu tumejenga Ofisi za TAKUKURU za Wilaya 10. Tukipata tena mwaka huu basi maombi yake tutayazingatia kama tulivyozingatia ya ndugu yangu mmoja anaitwa Mheshimiwa Lubeleje anatoka Mpwapwa na maeneo mengine, ahsante.

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri, usisahau na Kongwa pia. Mheshimiwa Goodluck Mlinga atafuatiwa na Mheshimiwa Khatibu Haji Kai, Msekwa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana.

Mheshimiwa Spika, bado sikuyaona majibu yangu ambayo yanaridhisha kama niliposema kuhusiana na Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi. Tuna viongozi katika nchi hii lakini viongozi hao wamekuwa mfano mbaya kwa Taifa letu. Mifano michache Wabunge wa CHADEMA ambao walihukumiwa hivi karibuni kutokana na kesi ya kusababisha mauaji na vurugu lakini leo hii tumeona Tume ya Maadili imekaa kimya. Kwa hiyo, nilikuwa naomba ufafanuzi wajibu wa Tume ya Maadili juu ya hili.

**SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nchi, ufafanuzi.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru. Naomba nijibu hoja ya ndugu yangu Mheshimiwa Mlinga kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, ukichukua Sheria ya Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi kuna majukumu waliyopewa. Majukumu haya aliyoyasema ya kushughulikia na watu ndani ya vyama ambao labda wanatumia vibaya fedha za watu, hiyo ni kesi ya Polisi. Kwa hiyo, Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi ukichukua ile sheria kwa kunusuru tu muda kuna

mambo yameainishwa. Sheria tunapoianza huku Bungeni tunasema hiki chombo kitafanya kazi hii na hii, sasa kwa mfano kama watu wamesababisha mauaji hiyo ni kesi ya Polisi sio kesi ya Sekretarieti ya Maadili. Kwa hiyo, ndugu yangu Mheshimiwa Mlinga amesaidia tu kukemea kwamba vizuri viongozi tukawa na tabia nzuri, nadhani ujumbe umefika, nashukuru.

**SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, Mheshimiwa Waziri anapata tabu kufafanua mambo yanayokuhusu, unaweza kujitetea dakika mbili maana wewe *Chief Whip*.

**MHE. ESTER A. BULAYA:** Mheshimiwa Spika, sina cha kujitetea tu ila inaonesha ni namna gani baadhi ya Wabunge wetu walioingia ni namna gani hawajapata muda wa kusoma sheria mbalimbali, ndio maana nilikuwa nacheka. (*Makofi*)

**SPIKA:** Mheshimiwa Mlinga huko ulipo swali la nyongeza, Msekwa.

**MHE. GOODLUCK A. MLINGA:** Mheshimiwa Spika, haipendezi kiongozi kuvamia jela yaani kusikia kiongozi amevamia jela vitu hivi tulikua tunavisikia Amerika ya Kusini kwenye zile nchi ambazo wanauza sana madawa ya kulevya lakini Tanzania viongozi wanafanya hivyo ndio maana nilikuwa nataka ufafanuzi mzuri. Kama sheria zimekaa vibaya basi nilikuwa naomba Mheshimiwa Waziri atusaidie kuleta sheria ili tufanye mabadiliko, haiwezekani viongozi wakawa mifano mibaya, kiongozi wa kike anavamia jela.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha.

**SPIKA:** Hilo ni pendekezo Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, MENEJIMENTI YA UTUMISHI WA UMMA NA UTAWALA BORA:** Mheshimiwa Spika, kwa ruhusa yako, ninaomba hoja hii iletwe wakati wa Wizara ya Mambo ya Ndani kwa sababu magereza yapo Wizara ya Mambo ya Ndani. (*Makofi*)

**SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Waziri Khatibu Haji Kai endapo yupo kule Msekwa na atafuatiwa na Mheshimiwa Mabula. Mheshimiwa Khatibu kama hayupo basi Mheshimiwa Mabula moja kwa moja, Mheshimiwa Stanslaus Shing'oma Mabula hii inaelekea wote wawili hawapo, ahsante sana.

**Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Serikali kwa Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kw Mwaka 2020/2021 yalipitishwa na Bunge kama ifuatavyo:-**

Fungu 20 – Ikulu.....	Sh. 24,049,003,000/=
Fungu 30 – Ofisi ya Rais na Sekretarieti ya Baraza la Mawaziri.....	Sh. 439,935,875,000/=
Fungu 32 – Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma.....	Sh. 32,923,578,000/=
Fungu 33 – Sekretarieti ya Maadili ya Viongozi wa Umma.....	Sh. 7,621,110,000/=
Fungu 67 – Sekretarieti ya Ajira katika Utumishi wa Umma.....	Sh. 3,360,526,000/=
Fungu 94 - Tume ya Utumishi wa Umma.....	Sh. 5,231,094,000/=
Fungu 09 - Bodi ya Mishahara na Masilahi katika Utumishi wa Umma.....	Sh. 1,445,945,000/=
Fungu 04 - Idara ya Kumbukumbu na Nyaraka za Taifa .....	Sh. 2,564,368,000/=

**SPIKA:**Basi tunaendelea na shughuli zilizopangwa hapa mezani, nashukuru sana orodha ya Waheshimiwa Wabunge ambao walikuwa wameomba wapate fursa ya kupata ufafanuzi wa Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Utumishi na Utawala Bora kuhusu masuala ya kisera orodha hiyo imekamilika kwa vyama vyote na kwa kuwa sasa ufafanuzi huo umeshatolewa kwa umakini mkubwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, sasa hatua tuliyoifikia ni ya kufanya maamuzi ya Bunge kuhusu hoja ambayo Mheshimiwa Mkuchika kwa ujumla wake alikuwa ameiweka mbele ya Bunge na tumeijadili toka asubuhi ya leo.

Sasa nimesimama ili kuwatangazieni kuhusu hoja hii ya kupitisha makadirio ya mapato na matumizi ya Ofisi ya



Rais, Utumishi na Utawala Bora kwa mwaka wa fedha 2020/2021 na kura tayari zimekwishakupigwa na kura ni zaidi ya nusu na nyingi kabisa zinasema ndiyo, kwa maana hiyo nitangaze rasmi kwamba Bunge limekubali, limejadili na limepitisha Makadirio hayo ya mapato na matumizi ya Ofisi ya Rais (Utumishi na Utawala Bora) kwa mwaka wa fedha 2020/2021.

Hongereni sana Ofisi ya Rais, hongera sana Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Mheshimiwa Mkuchika, Mheshimiwa Naibu Waziri Mheshimiwa Mwanjelwa, Waheshimiwa Makatibu Wakuu Ofisi ya Rais wote mliopo katika ofisi hiyo na wasaidizi wenu wote pamoja na ofisi mbalimbali ambazo zipo chini ya Ofisi hii ya Mheshimiwa Rais (Utumishi na Utawala Bora) ikiwemo TAKUKURU, Mkurugenzi Mkuu tunakupongeza.

Kama Spika kwa niaba ya Bunge zima tukupongeze kwa imani ambayo Mheshimiwa Rais ameonesha kwako na umewasikia Waheshimiwa Wabunge wakionesha imani kubwa sana kwako, tunajua kazi uliyonayo ni ngumu lakini sisi Wabunge tutakupa kila aina ya ushirikiano na tunaamini kabisa utapata ushirikiano mkubwa sana kutoka sehemu mbalimbali za utumishi na utawala wa nchi yetu, wizara zote kila mahali kwa sababu chombo hiki ni muhimu sana katika kuhakikisha kwamba panakuwa na utawala bora katika nchi yetu. *(Makofi)*

Tunawatakia kila la heri,tunajua fedha tulizowapa si nyingi kihivyo, mnahitaji fedha zaidi, lakini ndiyo sungura tuliyenaye kwahiyo tunaamini kabisa mtatekeleza majukumu yenu vizuri. Kwa mwaka wa fedha unaokuja, tukumbuke kabisa kwamba Ofisi hii ni ya Mheshimiwa Rais,kwahiyo tunawatakia kila la heri kabisa kwasababu ndiyo ofisi kioo ambayo ofisi nyingine zinaangalia huko.

Baada ya hayo, kuna matangazo kidogo, lakini kabla ya matangazo Mheshimiwa Mkuchika na Ofisi ya Rais kwa ujumla na hasa TAMISEMI na yenyewe nayo ni Ofisi ya Rais. Sasa hili langu mimi kama mimi, ukisafiri katika nchi yetu kila

mahali unakuta mabango ya Shule za Msingi, ofisi za Watendaji wa Kijiji wa Kata, Ofisi za Wakuu wa Wilaya nakadhalika nakadhalika. Sasa ukikuta bango Mtendaji wa Kijiji tuseme Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji unakuta bango kitu cha kwanza limeandikwa Ofisi ya Rais, sasa unashuka, Kongwa kule milimani Ofisi ya Rais, Tandahimba huko Ofisi ya Rais, sijui wapi Ofisi ya Rais, Shule ya Msingi Ofisi ya Rais, mimi huwa najjuliza sana sasa kwa maoni yangu mimi inavunja hadhi na heshima ya Ofisi ya Rais.

Waheshimiwa Wabunge, nasema hivi kwasababu, madhumuni ya bango lile ni nini? Ni kusema Shule ya Msingi Kongwa mtu yeyote anayepita aone niShule ya Msingi Kongwa, tena tangazo au bango linapaswa kuwa na maneno machache iwezekanavyo, ndiyo kawaida. Ofisi ya Mkuu wa Wilaya Kongwa yeyote anayepita anaona,Ofisi ya Mtendaji wa Kata mahali fulani, hivyo, lakini kila bango yenyewe yamepauka, hayana maana, Ofisi ya Rais, Ofisi ya Rais, Ofisi ya Rais. TAMISEMI jamani hebu kaliangalieni hili jambo.

Waheshimiwa, mimi nimewahi kuuliza kwenye halmashauri yangu, hivi hii mmetoa wapi hii Ofisi ya Rais, Mwenyekiti wa Kitongoji Ofisi ya Rais,sasa Ofisi ya Rais haiwezi kuwa hivi,andika Ofisi ya Mwenyekiti wa Kitongoji mahali fulani, Mwenyekiti wa Mtaa Salasala yaani jina la mahali liendane na unachotaka kumwambia mwananchi anayepita pale hiki ni kitu gani *as such*. Sasa wao wanaandika anuani ya barua, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, sijui nini na nini na nini Halmashauri ya Wilaya ya Kongwa, halmashauri ya Kijiji X, Sanduku la Posta 12 Kongwa, namba ya simu, sasa hii ni barua. Watu wanachotaka kujua hapa wapi basi akitaka hayo mengine atafanya utaratibu mwingine wa kutaka kuyajua. Chuo Kikuu cha Dodoma umemaliza, haina haja kutuandikia sijui Wizara gani sasa hii nini? *University of Dar es Salaam* umemaliza mtu yoyote akipita anasema mahali fulani, mahali fulani.

Waheshimiwa Wabunge, mkitaka mifano mtaona kwenye *National Parks*, Waziri wa Utalii anajua haya mambo.

Kwenye *National Parks* mabango yote yanaelezea kivutio kilichoko kile kile haianzi na Wizara ya Maliasili na Utalii, hapana, Hifadhi ya Taifa Serengeti, mstari huo hapo, mshale unaonyesha hifadhi iliko, inatosha. Anayetaka kujua hiyo ni Wizara gani atatafuta kwa wakati wake yeye mwenyewe, kwasababu Wizara zinaweza zikabadilika. Kwa mfano Mheshimiwa Rais akiamua kitu fulani kihame, kwahiyo mabango nchi nzima yaanze tena kufuta lakini ikiandikwa Shule ya Msingi X ni Shule ya Msingi X nakadhalika.

Kwahiyo huu ni ushauri tunatoa muungalie kwa kweli yaani mabango yetu ni machafu na wanaopita na gari huwezi kusoma, sijui wanaowezaga kusoma hayo mabango labda upige picha utasoma baadaye, lakini vinginevyo yaani lazima usimame uanze kusoma maana yake ni *heading* ya barua, bango hilo. Tuliangalie hili jambo mabango yetu yaeleze hiki ni kitu gani, basi bila nyongeza hata kuandika sanduku la posta siku hizi wala haina maana, ni jina la mahali tu basi tumemaliza, inasaidia sana.

Kuna Mbunge amepoteza ufunguo wa gari yenye nembo ya Toyota, funguo hiyo iko hapa mezani kwahiyo popote pale alipo huyo Mbunge au mtumishi wa Bunge kwa vyovyote vile, basi ujue funguo ya gari yako iko hapa meza kuu.

Halafu tumepata ushauri kuhusu barakoa kuwa hazipatikani madukani, kwahiyo tumeshauriwa kwamba Bunge tuangalie uwezekano wa kupatikana kwa hizo barakoa. Watu wangu wanawasiliana na *MSD* kuona kama jambo hili linawezekana ingawaje sijui hata ugawaji wake unawezekanaje na akiweka kwenye mikoba mwingine akija atachukua 50 mtu mmoja, 30 mtu mmoja, sasa sijui kama ita-*work*, lakini Katibu wa Bunge alitazame aone hali inavyokuwa.

Waheshimiwa Wabunge kwa ujumla tunaendelea kusubiri Serikali walitoa ahadi kwamba iko siku watakuja kutupatia maelezo kuhusiana na suala la *corona*, naamini bado wanajipanga.

Waheshimiwa Wabunge, suala hili la *corona* ni jambo kubwa zito, ni vizuri wakati kwa wakati baadhi ya taarifa muhimu ambazo Serikali inazitoa ikazitolea hapa Bungeni na hasa zinazotoka Dodoma, ni vizuri na Watanzania wanathamini zaidi habari ambayo imetolewa Bungeni na Bunge limeambiwa yaani wanachukulia kwa uzito wake,muhimu sana. Kwahiyo fursa hii tusiipoteze wakati wowote mnapokuwa na jambo tuta-*twist* ratiba yetu kadri itakavyokuwa ili hata kama ni tamshi la dakika tatu, la dakika tano, mambo kama shule kufungwa na hivi na hivi, ni vizuri zaidi kama yangetolewa ndani ya Bunge kwasababu Bunge lipo, tupo na mambo haya yanakipaumbele kikubwa kuliko yakitolewa nje ya hapa wakati Bunge lipo na hawa ndiyo wawakilishi wa wananchi wa Tanzania. Kwahiyo tujitahidi kukumbushana, matamko yote muhimu muhimu wakati huu ambayo hasa yanatoka hapa Dodoma ni vizuri zaidi Mheshimiwa Waziri wa Nchi yakatolewa kupitia Bunge hili la wananchi, maana *corona* ni tatizo kubwa.

Waheshimiwa Wabunge, pia niendeleo kuwakumbusha Waheshimiwa Wabunge wengine wanaonekana baa, wengine wanaonekana kwenye madisko huko Dar es Salaam nakadhalika. Sasa mambo haya ambayo tunaambiana hapa sisi ndiyo tuwe wazingatiaji wa mambo haya wa kwanza kabisa,*social distance very important*, lazima *social distance* iongezeke. Kwahiyo sasa Mbunge sijui uambiwe lugha gani uweze kuelewa kwamba nyakati hizi ni nyakati tofauti kabisa na lazima tuendane na hali halisi,tena nakumbuka wale wenye *sanitizer* basi tuendeleo kukumbuka na mimi hapa kidogo *sanitizer* na nyinyi mlionazo huko tukumbuke mara kwa mara na masharti mengine yote ambayo Serikali wanatuambia na wataalam wa afya wanatuambia mara kwa mara,*this is not a joke*, hatuna nia ya kumpoteza yoyote kati yetu wala yeyote katika wapiga kura wetu. Kwahiyo tuzingatia sana, wageni wasio muhimu sijui nyumbani kwako hata Mawaziri maofisini huko *cut down* wageni *unless it is a very important issue*.

Waheshimiwa, niliwahi kueleza siku moja hapa mambo ya mafaili faili sijui utafanyaje huko *you have to cut*

*down* waje wasaidizi na mafaili yao, yaani hii *corona* inatuletea *transformation* kubwa sana katika utendaji kazi wetu. Hatuna nia na wala hatupendi kabisa, tunajiombea sana Mwenyezi Mungu *at least* atuweke salama mpaka tumalize shunguli zetu tarehe 30 Juni, Mungu akipenda na hata baada ya hapo basi tuwe salama na uchaguzi wetu mkuu uweze kuendelea kama ilivyopangwa, itakuwa ni jambo la neema sana na taifa letu liweze kuendelea na mambo yake kadri ilivyopangwa.

Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo kuishauri Serikali hapa na pale, kuliko ushauri mwingine mwingine huo ambao ni wa *Prophets of doom* kwamba mtaona baada ya wiki tatu mtaona, yaani inaonekana kama kuna watu wengine wanaombea yaani liharibike hivi, kitu ambacho si sawa. Ugonjwa huu ni ugonjwa wa kutisha, ukiombea hivyo kwa mfano umegusa familia yako, ukabaki mwenyewe itakuwaje. Hiki ni kitu hatari, tuendeleo kuliombea Taifa letu kama Mheshimiwa Rais alivyotuasa, Mungu atatunusuru maana ndiyo tegemeo letu kubwa, hatuna tegemeo lingine.

Wataalamu wa *TASAF* mpo, mnaifanya kazi nzuri sana Makao Makuu na hasa hii *TASAF* inayokuja ni nzuri sana kwasababu baadhi ya fedha zitaenda katika miradi ya maendeleo moja kwa moja, ni kitu kizuri sana. Hata hivyo, huku chini baadhi ya maeneo ugawaji wake wa fedha pangukuwa na hali kidogo si nzuri sana Mheshimiwa Waziri na katika Mkoa wetu wa Dodoma mfano ni wa majuzi juzi tu hapa kwa *TASAF* iliyopita hii katika Wilaya ya Bahi, ningewashauri kabla hamjaondoka *TASAF* Makao Makuu, mpote pale Bahi Wilayani muweze kupata uzoefu tu nini ambacho kimekuwa kikitokea. Ni vitu vya aibu kabisa, wale wagawaji kwenye vijiji vile vinakwenda vibibi vya watu vinaazima mikoba ya mabinti zao ili kwenda kupokelea hela ya *TASAF*, mwenye sijui elfu ngapi ngapi anapewa elfu 10, elfu saba, elfu moja moja anaweka kimkoba niwekee mwanangu anawekewa anafunga, anafikiri kafanyiwa haki, kumbe alichosainishwa kwa dole kule kingine, alichowekewa kingine, yaani *vivid examples*. Wamewashika wagawaji wale wame-*tack* fedha kwenye mifuko yao, bahati nzuri

wamechukuliwa hatua wakiwemo Watendaji wetu wa Kata baadhi yao Maafisa Tarafa, wakiwa katika mnyororo huo huo wa vitu vya ajabu kabisa.

Sasa hao waliokamatwa wakati huo je huko nyuma wamefanya hivyo mara ngapi na je, hii ni *isolated case*? Ina maana huu mchezo ulikuwa ukiendelea katika sehemu mbalimbali nchi nzima. Kwahiyo, sasa bahati nzuri kwasababu tunaanza awamu mpya ya *TASAF*, tuna nafasi ya kutosha kabisa ya hilo nalo kuliziba, hilo la mwananchi anapopewa fedha ya *TASAF* iweje. Hata kama ni hela ndogo bora hata warushiwe kwa *M-pesa* au sijui hata sijui iwekwe benki au vipi, itafutwe namna ambavyo hawa watu hela itawafikia, usimamizi wa kuhakikisha kabisa ile *cash* inapomkuta mtu pale kuna mthani bado, iweze kukaa sawasawa na pale ina maana hela ni hela ilimuuzwa hata bwana Yesu, fedha mthani na yalikuwepo na majina, piteni Bahi mtapata uzoefu, ni *one case study* lakini *very important*, inaonesha mchezo ambavyo umekuwa, ninyi juu mmejipanga vizuri, lakini hapa chini kumbe kuna mchwa. Naomba tulitazame sana hilo.

Baada ya hayo, niseme tu Kamati ya Uongozinawaomba mbaki wale ambao mpo na wale ambao wapo Msekwa warudi hapa. Kamati ya Uongozi nijambo la muda mfupi sana tuweze kushirikishana ili tuweze kuweka mambo yetu sawasawa.

Waheshimiwa Wabunge, kwa vile shughuli zilizopangwa kwa siku ya leo zimekamiliwa zote, naomba nichukue fursa hii tena kuwashukuru sana Waheshimiwa Wabunge, kuwashukuru wataalam wetu wa *IT* waendeleo kuboresha mfumo tumeu-*test* tumeuona kwamba tunaweza tukawashirikisha wenzetu wa ukumbi wa Msekwa maana walikuwa wanakaa peke yao, wanajihisi kama wametengwa, *they are not part of the discussion that is going on here*. Kwahiyo sasa angalau tunaweza tukashirikishana vizuri zaidi na kwa maana hiyo mijadala yetu inaendelea kuwa na maana zaidi tuendeleo kushirikiana Waheshimiwa Wabunge, tuendeleo kuiunga mkono Serikali, wamekuwa

wakifanya kazi nzuri kwa kweli. Mheshimiwa Mansoor ameeleza baadhi ya mambo ya Jimboni kwake unajisikia kuisimka jinsi ambavyo Serikali hii ya Awamu ya Tano imeweza kutekeleza mambo yake vizuri, ni maajabu sana. Ni jambo la kushukuru sana. *(Makofi)*

Baada ya mambo hayo kukamilika, naomba sasa niahirishe shughuli za Bunge hadi kesho, saa nane kamili mchana.

*(Saa 11.55 Jioni Bunge liliahirishwa mpaka Siku ya Alhamisi, Tarehe 16 Aprili, 2020 Saa Nane Mchana)*